



**EQUIPPING CHURCH LEADERS  
• EAST AFRICA •**

# **TAFSIRI YA BIBLIA**

**Mwandishi**

**Jonathan M. Menn**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**

**J.D., Cornell Law School, 1977**

**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders East Africa, Inc.**

**714 S. Summit St., Appleton, WI 54914**

**+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)**

**[jonathanmenn@yahoo.com](mailto:jonathanmenn@yahoo.com)**

**[www.ecla.net](http://www.ecla.net)**

Januari 2008, toleo la Mei 2013; toleo la Julai 2014; toleo la Machi, 2015; toleo la Septemba 2015; toleo la Septemba 2016; na toleo la Machi 2017

Maelezo na ufanuzi wa kanuni za namna ya kuelewa Biblia na kutafsiri kwa usahihi na ukweli.

Ikihusisha asili ya Biblia, nadharia ya tafsiri za Biblia, fafanuzi za tanzu kuu za Biblia, kanuni za hamenutiki na eksejesia, na tukilenga juu ya matumizi ya kifungu cha Biblia leo. Mifano ya kanuni za tafsiri na matumizi yanetolewa kwa wazi.

## **YALIYOMO**

<b>I. Biblia na Hitaji la Kutafsiriwa .....</b>	<b>3</b>
A. <i>Biblia Takatifu ni ufunuo maalum wa Mungu kwa mwanadamu.....</i>	3
B. <i>Ulivyo mtazamo wa Mtu kuhusu Biblia ndivyo ulivyo kuhusu Kristo.....</i>	3
C. <i>Mambo kadhaa yanayoshurutisha uwepo wa kanuni za kuelewa na kutafsiri Biblia.....</i>	3
<b>II. Maana, Matakwa, na Makusudi ya Tafsiri Biblia.....</b>	<b>4</b>
A. <i>Muundo na maana.....</i>	4
B. <i>Uhusiano uliopo kati ya muundo na maana katika tafsiri ya Biblia.....</i>	4
C. <i>Tafsiri ya Biblia ya "halisi kimsingi" dhidi ya "ulinganifu mtambuka"</i> .....	5
D. <i>Hemenutiki na eksejesia.....</i>	5
E. <i>Kusudi la kutafsiri Biblia ni kulelewa Biblia na kutii mamlaka yake na kufanya maagizo yake.....</i>	6
<b>III. Kanuni kuu za Hamenutiki za kuelewa Biblia.....</b>	<b>6</b>
A. <i>Biblia yenye ni mamlaka kuu kwa ajili ya imani na maisha.....</i>	6
B. <i>Biblia inajitafsiri yenye.....</i>	6
C. <i>Muktadha ni ufunguo wa kuelewa na kutafsiri kifungu chochote cha Biblia.....</i>	8
D. <i>Maelezo dhidi ya maelekezo.....</i>	11
E. <i>Kanuni zilizopo hapo juu zinaonyesha umuhimu wa kuelewa maandiko kwa usahihi .....</i>	13
<b>IV. Tanzu za fasihi katika Biblia.....</b>	<b>13</b>
A. <i>Simulizi.....</i>	14
B. <i>Mashairi.....</i>	15
C. <i>Vitabu vya Hekima.....</i>	16
D. <i>Unabii na Apokaliptiki.....</i>	17
E. <i>Mifano na mafumbo.....</i>	25
F. <i>Nyaraka.....</i>	27
<b>V. Kanuni za eksejesia za kutafsiri kifungu cha Biblia.....</b>	<b>27</b>
A. <i>Mambo ya msingi ya kuzingatia katika mchakato wa eksejesia.....</i>	27
B. <i>Eksejesia sahihi na uelewa wa kifungu chochote cha Biblia unazingatia vipengele vitatu— uchunguzi; tafsiri; na matumizi .....</i>	27
C. <i>Kuelewa muktadha.....</i>	28
D. <i>Andika dondoo za kitabu, sehemu na kifungu cha maandiko .....</i>	30
E. <i>Soma kwa njia ya kuijuliza maswali.....</i>	31
F. <i>Zingatia maelezo ya kina ya kihistoria na ya kitamaduni .....</i>	31
G. <i>Zingatia mambo halisi yaliyopo kwenye kifungu.....</i>	31
H. <i>Angalia kwa makini matumizi ya lugha .....</i>	34
<b>VI. Maana ya Maneno na Aina za Semi.....</b>	<b>36</b>
A. <i>Tafsiri maneno kulingana na muda na muktadha.....</i>	36
B. <i>Tafsiri maneno kulingana na nahau au aina za semi .....</i>	37
<b>VII. Matumizi ya Kifungu.....</b>	<b>41</b>
A. <i>Matumizi ya Biblia kimsingi yanahusiana na uelewa wake.....</i>	41
B. <i>Matumizi hatimaye yameweka mizizi yake katikalengo la kufanana na Kristo.....</i>	41
C. <i>Matumizi sahihi yanatokana na hemenutiki sahihi na eksejesia .....</i>	42
D. <i>Matumizi yasiyo sahihi yanatokana na hemenutiki isiyo sahihi na eksejesia.....</i>	42
E. <i>Maadili, mafundisho, na mifano ya kibiblia.....</i>	43
F. <i>Sheria, amri, na masharti ya kibiblia.....</i>	44
G. <i>Kuna "umahususi na pengo la jambo" kati ya jambo ambalo linaelezwa na Biblia na lile tunalokutana nalo, kwani Biblia haiongelei moja kwa moja au kimahususi kila jambo ambalo tunaweza kukutana nalo.....</i>	47
H. <i>Kuna "pengo la kitamaduni" kati ya utamaduni wa Biblia ikihusisha—sheria, amri, na sheria kulingana na tamaduni hizo—na tamaduni tofauti za siku tunazoishi leo .....</i>	47

<b>I. Sababu zinazotusaidia kuelewa vifungu vya Biblia vilivyofungwa katika utamaduni fulani na vile vya tamaduni zote .....</b>	<b>50</b>
<b>J. Hatua tano za kuweka daraja kuziba pengo la kitamaduni ili KUWEZA kutumia sharia, amri, na masharti ya kibiblia katika mazingira ya sasa.....</b>	<b>54</b>
<b>K. Kutumia hamenutiki ya “mchakato wa ukombozi/nia ya ukombozi” kuziba pengo la jambo na la kitamaduni pale amri za kiblia, sheria na masharti yanapokuwa HAYAWEZI kutumika kama yalivyo kwa kuwa hayakuwa maagizo makamilifu ya Mungu kwa watu wote na tamaduni zote.....</b>	<b>56</b>
<b><u>REJEA ZILIZOTUMIKA</u>.....</b>	<b>60</b>
<b><u>MWANDISHI</u>.....</b>	<b>63</b>
<b><u>NYONGEZA A:</u> Gregory Koukl, “Kamwe Usisome Mstari wa Biblia”.....</b>	<b>63</b>
<b><u>NYONGEZA B:</u> Mahubiri ya Kibiblia kwa Njia ya Kujifunza kwa Maswali .....</b>	<b>67</b>
<b><u>NYONGEZA C:</u> J. Daniel Hays, “Kutumia Sheria za Agano la Kale Leo”.....</b>	<b>69</b>
<b><u>NYONGEZA D:</u> T. Wayne, Dye, “Utamaduni na Dhamiri: Kweli za Biblia na Tofauti za Tamaduni”.....</b>	<b>77</b>
<b><u>NYONGEZA E:</u> Chimbua Utambue Kanuni za Hamenutiki: Kanuni za Msingi.....</b>	<b>87</b>

## **TAFSIRI YA BIBLIA**

### **I. Biblia na Hitaji la Kutafsiriwa**

#### **A. Biblia Takatifu ni ufunuo mahususi wa Mungu kwa wanadamu**

1. Waandishi wa Maandiko hudhihirisha kwamba Biblia ni ufunuo maalumu wa Mungu amba waliutoa na kuuandika(tazama, mfano, **Kutoka 17:14; 20:1; 24:4, 7:34:27, Neh 9:13-14; Yer 1:4, 9; Luka 3:2-4; 1 Wakor 7:10, 11:21; 1 Wath 2:2-9; 2 Tim 3:16-17; 2 Pet 1:20-21; 3:14-16**).
2. Baraza la Kimataifa la Mwandani mwa Biblia (ICBI) katika “tamko lake la Chicago kuhusu mwandani mwa Biblia” (1978: n.p.) walitoa muhutasari kuhusu asili ya Biblia, kama ifuatavyo:
  1. Mungu ambaye ni Kweli na kwamba husema yaliyo kweli tu, ameyavuvia maandiko Matakatifu ili kwa hayo ajifunue kwa mwanadamu aliyepotea kwa njia ya Yesu Kristo kama Muumbaji na Bwana, Mkombozi na Hakimu. . . .
  2. Maandiko Matakatifu, ambayo ni Neno lake Mungu, lililoandikwa na watu walioandaliwa na kuvuviwa na Roho wake, ni mamlaka halisi ya kiungu isiyo na makosa kwa kila eneo ambalo linagusa: linapasa kuaminiwa, kama Maelekezo ya Mungu, kwa yote inayofafanua: kutiwa, kama amri ya Mungu, kwa yale inayohitaji kutekelezwa, kushilikiliwa kwa matarajio; kama nadhiri za Mungu kwa yote inayoaahidi. . . .
  4. Likiwa kamili na limetolewa katika kinywa cha Mungu, maandiko hayana makosa wala mapungufu katika mafundisho yake, hayajapungua neno lolote katika kueleza matendo ya Mungu katika uumbaji, matukio katika historia ya uumbaji wa dunia, na chanzo chake kiujuzi chini ya mamlaka yake Mungu, na katika ushahidi wake wa Neema ya Mungu iookoayo kwa maisha ya mtu binafsi.

#### **B. Ulivyo mtazamo wa Mtu kuhusu Biblia ndivyo ulivyo kuhusu Kristo**

Kutokuiamini Biblia husababisha kutomwamini Yesu. Kushindwa kuamini kwa usahihi Biblia kunasababisha kushindwa kumwamini Kristo kwa usahihi.

1. Kristo Mwenyewe aliyaaamini maandiko yote (Yoh 10:35). Aliamini matukio ya kihistoria ya AK na wahusika wake kuwa ni halisi wala si mambo yaliyotungwa (**Mat 12:39-41; 19:4-5; 24:37; 24:37-39; Luka 10:12; Yoh 3:14**). Aliamini miujiza ya AK (**Mat 12:39-40; Luka 4:25-27; Yoh 6:49**). Alifundisha kwa dhati kuwa unabii katika AK ultoka kwa Mungu (**Mat 24:15; Luka 24:25-27, 44-45; Yoh 5: 39**).
2. Yesu aliitambua Biblia kama mamlaka (Mat 4:1-11; Luka 4:1-13; Yoh 17:17). Alithibitisha kwamba Biblia imevuviwa neno kwa neno yakiwa yameandikwa katika wakati uliopo au ujao kwa kila tendo lililoandikwa (**Mat 5:17-19; 22:31-32, 43- 45; Luka 16:17**). Alikiri kwamba Mungu alinena kupitia watu (**Mat 22:43; 24:15**); wakati huo huo alitofautisha tamaduni za watu na na Biblia (**Mat 15:6; Yoh 5:46-47**).
3. Alisema kila alichonena Yeye ni neno la Mungu(Yoh 8:28-29; 12:44-50). Alisema Biblia itatimizwa kupitia Yeye (**Mat 5:17; 26:56; Luka 4:21; 22:37**).
4. Alichukizwa na kukemea kushindwa kwa mwanadamu kuelewa maandiko (Mat 22:29; Luka 24:25; Yoh 3:10).

#### **C. Mambo kadhaa yanayoshurutisha uwepo wa kanuni za kuelewa na kutafsiri Biblia**

Biblia ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu na ipo ili sisi tusome na tuelewa. Hata hivyo zipo sababu za kuwa na kanuni za kuzifahamu ili kutusaidia sisi kuelewa Biblia. Kweli hizo huhusisha yafuatayo:

1. Biblia ni mkusanyiko wa kweli za kiungu kwa mwanadamu. Mungu ambaye hana mwisho huwasiliana na mtu ambaye si wa milele. Alichagua kuwatumia watu 40 walio waandishi, kwa muda zaidi ya 1300 – 1500 miaka (c.1400-1200 KB-BK 70 au 95). Katika kujidhihirisha Yeye kwa mwanadamu, Mungu amechagua kutumia njia ya lugha za wanadamu. Kwa hiyo tunahitaji kujua jinsi lugha inavyofanya kazi.
2. Dhambi, ikihusianishwa na nguvu ya dhambi ikaaayo ndani ya waamini imetia giza na kuharibu fahamu na uelewa wa watu (tazama **Mwanzo 5:1-3; Zab 51:5; Yoh 8:31-34; Warumi 3: 9-18; 6:6, 20-21; 7:14-25; Wafeso 2:1-3; Tito 3:3; 2 Pet 2:18-19**).
3. Kuna mwachano wa kiutamaduni baina ya tamaduni za watu na matukio yaliyomo katika Biblia na tamaduni nyingi za ulimwengu wa leo. Desturi nyingi, utaratibu wa kuishi, miiko ya kijamii, mapokeo ya kidini, likizo, na matukio mengine yalikuwa na misingi inayofanana na kueleweka vema kwa wale walioandikiwa Biblia. Ingawa kuna tofauti kubwa au haileweki kabisa kwa watu wa siku za leo.
4. Kuna mwachano wa kihistoria kati ya watu wa leo na matukio yaliyoandikwa kwenye Biblia.

Kumbukumbu za kihistoria, Mashirika ya kijamii, watu, vita, siasa, mambo ya kiuchumi na ya kijamii yalikuwa yanaeleweca kwa watu amba Biblia imeandikwa kwao. Hata hivyo kuna tofauti kubwa au kutoeleweca kabisa kwa watu siku za leo.

5. Kuna umbali wa kijiografia kati ya maeneo na matukio katika Biblia na wale wanaosoma Biblia leo. Kutembelea maeneo hayo ya kiblia kunaweza kuongeza uelewa wetu zaidi. Hata hivyo maeneo mengi ya kiblia hayapo tena au hayana mwonekano uliokuwepo wakati matukio yanatokea na kuandikwa kwenye Biblia.

6. Kuna tofauti kubwa ya lugha kati ya ile iliyotumika katika Biblia na yetu sisi leo. AK iliandikwa kwa lugha ya kiebrania mwanzoni (na baadhi Kiaramu); AJ lilikuwa limeandikwa kwa lugha ya kigiriki (baadhi Kiaramu). Hizo lugha zilibadilika kutoka karne hadi karne. Pia lugha hizo zina maneno, nahau, maelezo na misemo ambayo hayana maana ya moja kwa moja katika lugha ya kiingereza au lugha nyingine yejote.

7. Kuna tofauti ya maendeleo ya elimu ya uandishi wakati Biblia inaandikwa na uandishi wa siku za leo. Waandishi wa Biblia walitumia matoleo mbalimbali ya Biblia pamoja na vielelezo vyta hotuba, nahau, na mbinu za uandishi ambayo ni ya kawaida katika tamaduni zao. Baadhi ya mifano hiyo yanayoelimisha ni tofauti kabisa na hotuba za siku hizi pamoja na mitindo ya uandishi wa siku zetu.

## **II. Maana, Matakwa, na Makusudi ya Tafsiri ya Biblia**

### **A. Muundo na maana**

1. Ngazi ya Muundo wa lugha (pia inajulikana kama “muundo wa msingi”) huhusika na lugha yenewe (Maana ya kiwango cha Muundo wa maneno, virai na vishazi)
2. Ngazi ya uelewa ya lugha (pia inajulikana kama kiwango cha “muundo wa maana” au “kina cha muundo”) ni ujumbe wa wenye nguvu sana amba unaelezwa katika mfumo wa uandishi. Tafsiri ya Biblia hatimaye inahusu utambuzi wa maana ya kile kinachoelezwa na Biblia. Lakini maana imechukuliwa kutoka kwenye mtindo.

### **B. Uhusiano uliopo kati ya muundo na maana katika tafsiri ya Biblia**

Katika kuchunguza maana ya ujumbe unaotolewa na Biblia, ni lazima tuzingatie mambo matatu kama ifuatavyo:

1. Mwandishi. Ili kuelewa Biblia—kwa usahihi au waraka wowote ule au kazi yejote ya fasihi—swali la kwanza tunalopaswa kuijuliza linatakiwa liwe: “*Mwandishi* alikuwa na maana gani alipoandika aya au habari hii?” Geisler alitoa pendekezo lake katika hili kama ifuatavyo: “Kinachomaanishwa au maana inayotolewa na ujumbe ni kile tu kilichomaanishwa na mwandishi na haipaswi kubadilishwa na msomaji. Hii haimaanishi kwamba ufunuo zaidi hauweza kumfanya mtu aelewe kwa ukamilifu, lakini hii ina maana kwamba maana ya aya haibadiliki kwa sababu ya kweli ya ziada iliyofunuliwa. Maana pia ina mipaka yake na kwamba kuna mipaka kutokana na mipaka ya uelewa wa mwandishi katika lugha, muundo na mtindo pamoja na dhana ya kiutamaduni. Maana inamtegemea mwandishi na inavumbuliwa na wasomaji.” (ICBI 1982: Art. VII)
2. Mpokeaji wa kwanza wa ujumbe. “Mungu mara zote haongei na patupu bali anawasiliana na watu maalum wa aina Fulani akiwapa ujumbe maalumu kulingana na mazingira yao. Mambo yaliyowasilishwa kwao kwa njia ya maandishi huwa kwa lugha yao na kwa kutumia maelezo yanayoelweka kwao kwa muundo unaokubalika kwao.” (Volvaardt 2005:19) Kwa vile vitabu vyta Biblia mwanzoni vilikusudiwa kuwafikia watu Fulani maalumu, yatupasa kuijuliza, “Maandiko yalikuwa yana maana gani kwa Yule aliyekusudiwa kuyapokea?”
3. Kifungu chenyewe. Zaidi ya mwandishi na wasomaji, “upo umuhimu mkubwa zaidi ambaou husababishwa na ujumbe wenye kama chanzo cha maana ya ujumbe” (Ryken 2002: 116). Sababu ni, “Hatuna mwandishi mwanadamu ambaye tutamwuliza kuhusu alichomaanisha kwa jambo maalumu aliloandika. Wala hatuna wale waliandikwa ujumbe huo kwa mara ya kwanza ili watufahamishe maana ya ujumbe wakati walipoandikiwa.” (Volvaardt 2005:47) Kwa hiyo, “changamoto hizi za kufahamu ukweli halisi zimetufanya tuwe na tahadhari za kihekima ili tusifanye kosa la tafsiri la kukusudia na kupotoa ukweli, yaani kosa la kudhani kuwa mwandishi alikuwa na maana fulani badala ya kuzingatia yale alioandika” (Caird 1980: 61).
4. Muhutasari.
  - a. Maana inayoelezwa na kifungu kimoja cha Biblia moja, haita uatata, na haibadiliki.
  - b. Namna sahihi na kudhibiti badiliko la maana ni kuzingatia maana ya ujumbe katika mazingira yake ya asili.

c. Maana ya ujumbe wa biblia inategemea muundo wake.

### C. **Tafsiri ya Biblia ya “halisi kimsingi” dhidi ya “ulanganifu mtambuka”**

Kwa vile ujumbe ni msingi wa kutafuta maana, toleo la Biblia tunayotumia (ikiwa tunatumia toleo lililotafsiriwa) ni muhimu sana. Kuna nadharia mbili za msingi katika kutafsiri biblia: (1) “halisi kimsingi” kama vile NASB, ESV, NKJV na RSV; na (2) “ulanganifu mtambuka” kama vile NIV, Good News Bible, New Living Traslation, na Contemporary English Version

#### 1. Nadharia iliyopo nyuma ya Tafsiri za Biblia (Ryken 2002: 85-91).

- a. “*Halisi kimsingi*” hujielekeza katika ngazi ya *muundo* wa kifungu. Kimsingi wanafanya *tafsiri ya lugha* (i.e., maamuzi hufanyika kwa kuzingatia maneno [Kiingereza] mazuri zaidi kuelezea maneno ya Kiebrania na ya Kigiriki ya kifungu cha Biblia cha asili)
- b. *Tafsiri ya “ulanganifu mtambuka”* pia hushughulika na muundo lakini hujielekeza katika “wazo” au ngazi ya maana. Huhusika na *tafsiri ya maudhui* ya kifungu (i.e., *tafsiri ya maana ya kitheolojia* ya maana ya kifungu cha asili). Hilo husababisha mpangilio na matumizi ya maneno na muundo ambaeo haufanani na maneno ya asili ya kiebrania na kigiriki, ingawa hakuna awezaye kueleza mabadiliko yamefanya wapi. Katika kutekeleza, wahariri wa tafsiri ya ulanganifu mtambuka wamefanya tafsiri ya Biblia kwa ajili ya msomaji, ingawa msomaji hawezi kujuua wapi lilitokea. NIV na NRSV hazibadiliki kabisa (i.e., inakaribia tafsiri ya maana halisi ya lugha ya asili) kuliko tafsiri za Jerusalem Bible au Good News Bible.
- c. *Vifupisho*. Kwa upande mwininge wa Tafsiri ya ulanganifu mtambuka (i.e., ikiachana sana na uhalisia) ni vifupisho kama vile Living Biblia. Vifupisho vinatafsiriwa kwa kufuata “ulanganifu mtambuka lakini wakati mwininge huenda mbali kwa kuweka daraja kati ya baadhi ya tofauti za kitamaduni na za kihistoria kati yetu na nyakati za biblia” (Wolvaardt 2005:54). Hivyo, “msomaji hypokea tafsiri kiasi Fulani cha theology ya mtafsiri (na inapaswa ijulikane hivyo)” (Ibid.) Hayo matoleo ni mazuri kwa ajili kutupatia maana halisi na ya msingi katika kupata tafsiri ya kifungu cha Biblia, tahadhari ni lazima ichukuliwe na ni muhimu kulinganishwa na tafsiri za maneno halisi toka lugha ya asili ikiwa zinapatikana.

#### 2. Mapungufu yaliyomo kwenye matumizi ya tafsiri ya ulanganifu mtambuka. Tafsiri zote za ulanganifu mtambuka husumbua “usomaji” wa tafsiri kwa msomaji wa siku za leo akilinganisha na kifungu halisi alichoandika mwandishi. Kibaya zaidi hubadili kabisa kifungu cha asili kwa namna ambayo haiwezi kuvumilika kama ingelifanyika kwa riwaya au tamthiliya. Huwa zinaondoa maneno mengi ya kitheolojia yaliyotumiwa na mwandishi wa asili. Hivyo tafsiri sahihi hufanya kuwa ngumu zaidi—hususan katika kuelewa tofauti ndogo vichwa vidogo vya kifungu, ukizingatia kwamba maudhui huwa yanapatikana katika baadhi ya maneno, nukuu na dhana, na kulinganisha vifungu vya maneno tofauti tofauti—wakati mtu anapotumia tafsiri ya ulanganifu mtambuka badala ya tafsiri halisi zaidi. Tafsiri sahihi ya biblia hatimaye ni ile inayotokana na yale aliyosema mwandishi wa asili na si vinginevyo (i.e., “maana ya lugha”), badala ya kile anachowaza mhariri wa siku za leo kuwa ndicho alichomaanisha mwandishi wa asili (i.e., “maana ya kimaudhi”) (Ryken 2002: 117, 147).

### D. **Hemenutiki na eksejesia**

1. Hemenutiki inaelezea mchakato unaotumiwa na watu kuelewa jambo fulani linamaanisha nini na lina maana gani kwa maisha yetu.
2. Eksejesia ya kanuni za tafsiri ya biblia kwa kuzingatia maana ya lugha ya asili ya neno, hutumia kanuni hizo kwa uangalifu katika kujifunza kwa mtiririko wa maandiko ili kugundua maana ya asili iliyokusudiwa.
3. Kanuni hizo na eksejesia yake zinahusiana hivi: [Kanuni ya tafsiri ] husimama kama kitabu cha sheria katika michezo. . . Sheria siyo mchezo, na michezo haina maana bila ya sheria. Hemenutiki sahihi siyo tafsiri lakini matumizi ya eksejesia ni kanuni katika matumizi” (Ramm 1970: 11).
4. Hemenutiki na eksejesia huanzia alikoishia mwandishi na kuhitimisha na alikoanzia mchakato wake. “Tunapotafsiri kifungu cha maneno tunaanza kuyaangalia maneno na sentensi zilizoko mbele yetu na kuishia na alichomaanisha mwandishi. Kiuhalisa tunaenda kinyume cha mtiririko alioufuata mwandishi wakati anaandika kifungu cha maneno au habari. Mwandishi huanza na kile alichotaka kuwasilisha (maana) na kukiweka katika muundo, yaani katika maneno, sentensi, aya na muunganiko wa aya mbalimbali” (Wolvaardt 2005: 46)

### E. **Kusudi la kutafsiri Biblia ni kuelewa Biblia na kutii mamlaka yake nakufanya maagizo yake**

1. Kusudi halisi la kuelewa na kutafsiri Biblia ni ili kufanya kazi yale yanayosemwa ndani yake.

Kujitiisha kwenye mamlaka ya Biblia na kuyatii mafundisho yake, yote mawili ni malengo ya kuilewa Biblia, na hivyo tunalazimika kupata uelewa sahihi (tazama **Zab 111:10; 119:98-100; Mat 7:24-27; Luka 6:46-49; Yoh 7:16-17; Warumi 2:13; 1 Wakor 13:2; 1 Tim 1:5; Waeb 4:12-13; Yak 1:22-25**).  
2. Ingawa Biblia iliandikwa kwa watu maalumu na katika matukio maalumu, lakini imeandikwa na kutunzwa kama ujumbe kwa matumizi ya watu wote wa nyakati zote (tazama Kumb 31:9-13; Neh 8:1-8; Yoh 17:20; Warumi 15:4). Hivyo, Osborne anaelezea tafsiri ya biblia “kama ngazi ya kuzunguka inaanza na kifungu cha maneno na mazingira yaliyosababisha kifungu hicho kuandikwa kutoka katika maana ya asili katika lugha ya mwanzo na kuhusianishwa na mazingira ya sasa kwa kanisa la leo” (Osborne 1991: 6). Ingawa kifungu cha maneno huwa na *maana moja* au *tafsiri* lakini inaweza kuwa na matumizi mbalimbali (tazama ICBI 1982: Art. VII). Baada ya kumaliza kutafsiri sehemu ya maandiko na kuelewa maana yake yafaa kuijiliza, “Sehemu hii ya maandiko inatumikaje kwangu?” Kwa umuhimu zaidi ni vema kuijiliza, “Je sehemu hii ya maandiko *inanikataza* nini?”

### **III. Kanuni kuu za Hamenutiki za kuelewa Biblia**

Kanuni zifuatazo za hemenutiki mara zote zinatumika wakati mtu anasoma na kutafsiri kifungu chochote cha Biblia. Kanuni nane za msingi zimetolewa kwa muhutasari katika **NYONGEZA E: Chambua na Gundua kanuni za Hemenutiki: Kanuni za Msingi**.

#### **A. Biblia yenewe ni mamlaka kuu kwa ajili ya imani na maisha**

Kwa vile Biblia ni Neno la Mungu, ni mamlaka ya mwisho. Kanisa kama taasisi, desturi yake, historia yake, wasomi wanaoheshimika, uzoefu binafsi, na sababu zote zilizo muhimu zinapaswa kusikilizwa na kuheshimiwa. Pamoja na hayo yote Biblia inayo mamlaka juu ya hivyo vyote. Ikiwa mtu, fikra yake, uzoefu, taasisi, au desturi zina mamlaka juu ya Biblia, hiyo ina maana kwamba mtu amejiweka juu ya Mungu. Hii ndiyo maana kanuni sahihi za hemenutiki na eksejesia ni munhimu sana—pale tu zinapotumika kwa umakini mkubwa tunapolitafsiri Neno la Mungu ili kuleta uelewa sahihi wa kile kinasemwa na Neno la Mungu.

#### **B. Biblia inajitafsiri yenewe**

Biblia ni ufunuo wa simulizi ya ukombozi upatikanao kwa imani katika Kristo (tazama **Luka 24:27, 44-47; Yoh 5:39**). Ingawaje, ufunuo wa Mungu ni *jambo la kuendelea*—i.e., unajifunua katika Biblia nzima. Kanuni kadhaa hutokana na kweli hii.

##### **1. Maandiko kamwe hayawez i kujipinga.**

- a. *Biblia nzima inakubaliana katika ujumla wake*. Kwa hiyo sehemu mbili za maandiko zinazoonekana kупingana zinapochambuliwa vema hugundilika kwamba hazipingani. Sehemu moja ya maandiko inaweza kuboresha nyingine, au kuipa usahihi zaidi lakini haitaipinga.
- b. *Wakati mwingine kweli mbili au zaidi hufundishwa kwa uwazi katika Biblia, lakini hutokea kukinzana*. Kwa mfano Ukuu wa Mungu na wajibu wa mwanadamu ni vigumu kupatana ingawa bado Biblia inafafanua hayo mawili. Katika hali kama hizo kumbuka kwamba Biblia ni mkusanyiko ya kweli za kiungu kwa akili za mwanadamu zenye mipaka. “Wakati kweli mbili au zaidi zinafunazofundishwa kwa uwazi katika Biblia zinakinzana kumbuka kwamba unao ufahamu wenye mipaka. Usiyachukue mafundisho katika hali ya kuzidi kile ambacho Mungu hakusema ile kubaki kuwa sahihi katika ufahamu wako. Mwache Mungu asema alichosema bila kujaribu kumsahihisha au kumfafanua Mungu. Kumbuka yeye ni Mungu na wewe ni mtu. Nyenyekeza moyo wako kirahisi kwa imani na amini alichosema hata kama huwezi kuelewa au hakiendani na ufahamu wako vizuri”. (Arthur 1994: 62)

##### **2. Hatua ya ukombozi kwa pamoja na “shauri zima la Mungu” (**Matendo 20:27**) ni lazima izingatiwe kwa utaratibu maalumu ili kuelewa kwa usahihi kifungu maalumu cha maneno.**

Biblia ni kitabu kinachoeleza simulizi moja inayoelezea habari inayokubaliana. Ingawa ukweli wote wa Biblia haujafunuliwa kwa wakati mmoja, lakini ulifunuliwa kwa mwendelezo kwa muda mrefu. **AK** ni maandalizi ya Injili; **Injili zote** katika Agano jipyaa ni udhihirisho wa Injili; **Matendo ya Mitume** ni upanuzi wa Injili; **Nyaraka** ni usafanuzi ya Injili; na **Ufunuo** ni matumizi ya Injili. Maana kamili ya kifungu chochote cha maneno haiwezi kueleweka vema kama haijazingatia Biblia nzima na hatua ya historia ya ukombozi. “Kusoma Biblia kwa kuzingatia mazingira halisi ya ujumbe *kama Neno la Mungu* ni lazima kuhusisha maandiko yote yaliyokubaliwa kama mazingira hitimisho ya kifungu husika cha maneno” (Johnson 2007: 156).

##### **3. AJ inatafsiri AK.** Imesemekana kwamba “Jipyaa ipo ndani ya Kale ikiwa imefichwa; Kale imefunuliwa ndani ya Mpya.” “Kuja kwa Bwana wetu kumebadilisha sana uelewa wa Agano la Kale. Mitume walielewa canono katika nuru ya huduma ya Yesu, ujumbe wake, na kuinuliwa kwake. Uelewa

wa asili wa maneno ya Musa na Manabii ilipasa ibadilike sana katika mtazamo wake wa kumgoja Bwana ajaye.” (VanGemeren 1990: 83) Yesu na waandishi wa AJ kwa namna moja kwamba AK ni kitabu kuhusu Yesus. Yeye kiini cha maandiko na maudhui yaliyochanganuliwa na maandiko (**Luka 24:25-27, 44-45; Yoh 5:39-40, 46; Matendo 3:18, 24; 10:43; 26:22-23; 2 Wakor 1:20; Waeb 1:1-3; 1 Pet 1:10-12**). Kuelewa AK inatusaidia kumwelewa Yesu alivyosema kuhusu Yeye mwenyewe, Waisraeli wa AK na sheria zake, maadhisho, na desturi zingine, zilikuwa “mifano,” “vivuli,” au “vielelezo” vya uhalisia wa AJ (**1 Kor 10:1-6; Wakol 2:16-17; Waeb 8:1-10:22**). Shelia za AK, maadhisho, na desturi zingine zimekamilishwa na kutimilizwa katika Kristo (**Mat 5:17; 2 Wakor 3:12-16; Wagal 3:23-4:7**). Kuna yote mawili mwendelezo na kukosa mwendelezo kati ya AK na AJ. AJ hujenga kwenye dhana za AK, mara kadhaa kwa namna ya kushangaza sana. Kwa hiyo “siku zote soma maandiko ya Agano la Kale kwa miwani ya maandiko ya Agano Jipy” (Lehrer 2006: 177). Mifano ya hili huhusisha yafuatayo:

- a. *Sheria ya chakula. Mambo ya Walawi 11:1-23* inakataza wana wa Israeli kula aina mbalimbali za wanyama. Katika **Marko 7:19, Matendo 10:9-15, Wakol 2:16-17**, na **1 Tim 4:1-5** hayo makatazo hayahusiki tena (isipokuwa katazo dogo kwa nyama zilizotolewa sadaka kwa sanamu imetolewa katika **2 Wakor 8**).
- b. *Maana ya ndani au ya kweli katika AK, unabii, na mambo huwa wazi katika nuru ya mafundisho ya AJ.* “Agano Jipy” iliyotangazwa na Yeremia katika **Yer 31:31-34**, ambapo kwake ilitumika kwa ajili ya ufalme wa Israeli na wa Yuda na kwa hakika ilitimia katika Kristo na kwa wafuasi wake (tazama **Luka 22:20; 1 Wakor 11:25; 2 Wakor 3:6; Waeb 8:6-9:15**). Vile vile katika siku ya pentekoste, katika **Matendo 2:29-36**, Petro alifafanua kwa wazi ufufuo wa Kristo Yesu ambaa ulishaelezwa katika **2 Samweli 17** (i.e. “Agano la Daudi”) wakati Mungu alipomwapia Daudi kuwa mmoja wa uzao wake ataketi katika kiti chake enzi.

#### **4. Vifungu vya maandiko vinavyoileweka vinatakiwa vitafsiri vifungu vya maandiko ambavyo haviko wazi.**

- a. *Baadhi ya vifungu vinaweza kuwa tata na hivyo vikahitaji vifungu vingine kuvifafanua.* Katika **Isaya 7:14** Neno la kiebrania “bikira” laweza pia kumaanisha “mwanamke mdogo” kwa umri. Pamoja na hayo Mathayo ananukuu katika lugha ya kigiriki (**Mat 1:23**), analitumia kuelezea kuzaliwa kwa Yesu alimaanisha maana moja yaani “bikira.”
- b. *Baadhi ya vifungu vya maneno huonekana kuwa vinaeleweka kwa kuvitazama tu lakini si kamili; vifungu vingine ni muhimu ili kuelewa vizuri kinachofunzwa.* Kwa mfano, **Mat 21:22** husema “*kila unachoomba katika maombi ukiamini unapokea.*” Baadhi wametumia mstari huu wakijadili, theolojia ya “kipe jina na dai”—i.e., waaminio wanaweza kupokea chochote watakachoomba, sababu pekee ya kutokupokea ni ukosefu wa imani. Ingawa kuna vifungu vingine vinavyoilezea zaidi kuhusu maombi. Yakobo anasema, “*Mwaomba lakini hampokei kwa sababu mwaomba vibaya ili mvitumie kwa tamaa zenu wenyewe*” (**Yak 4:3**). **1 Yoh 5:14-15** hutuambia maombi yaletayo majibu hutegemea tunavyoomba “*kulingana na mapenzi yake*” (si mapenzi yetu). Zaidi, Mungu alikataa kujibu maombi ya wote wawili Paulo (**2 Wakor 12:7-9**) na Yesu Kristo mwenyewe (**Luka 22:41-42**)—lakini hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa “hana imani.”
- c. *Kifungu tata ni kile ambacho maana yake haiko wazi au haieleweki kirahisi.* Vifungu tata mara nyingi ni vile vyenye maelezo yaliyojitenga—i.e., yanaweza kutokea mara moja na yenye ufanuzi kidogo toka kwa mwandishi kuhusu anachomaanisha. Kwa sababu maana ni tata hatupaswi kutengeneza fundisho katika vifungu hivyo pamoja na maelezo yake

##### **(1) Katika hili tuzingatie mambo mawili:**

- (A) *Tazama vifungu vinavyoileweka katika funzo hilo hilo katika “mazingira mapana zaidi” ya kitabu chote, agano zima, au Biblia katika ujumla wake* Jaribu kutafuta ulinganifu wa maana kwa kutumia vifungu vilivyo wazi. Vifungu vinavyoileweka wazi vitatueleza ingawa kwa uchache kile ambacho kifungu tata hakimaanishi.
- (B) *Zingatia “mtiririko wa kimantiki” na kusudi la msingi la “mazingira ya karibu.”* Mazingira ambayo kifungu tata kimetolewa yanaweza kueleza kile ambacho kifungu kinamaanishi au hakimaanishi.

##### **(2) Vifungu tata vya maneno vyaweza kubakia katika hali ya utata.** Kwa kuyafahamu maandiko mengine vile vitu ambavyo *vipo wazi* na ukweli ambaa haujipindi wenyewe, tunaweza kusema kile ambacho kifungu tata *hakimaanishi*. Pia tunaweza kusema kile ambacho kifungu kinaweza kumaanisha au kinamaanisha hata kwa uchache.

(3) Kwa mfano kifungu mojawapo tata cha maneno ni 1 Wakor 15:12 ambacho kinaelezea watu “kubatizwa kwa niaba ya waliokufa.” Hakuna maelezo mengine yanayogusia “ubatizo” au “wafu” ambacho kinadokeza tendo hilo. Jambo la wazi zaidi kinachosaidia kufafanua maelezo ni mazingira ambayo maelezo yalitolewa. Maelezo ya Paulo yapo wazi na wala “hayatoi agizo” (i.e haagizi watu kubatizwa kwa niaba ya wafu amba ni rafiki zao au ndugu). Muktadha wa **1 Wakorintho 15** ni kwamba Paulo anahoji wale waliodai kwamba hakuna ufufuo wa wafu (**1Wakor 15:12**). Ingawa asili na maana ya ubatizo wa wafu haijulikani, msukumo wa hoja ya Paulo upo wazi: “Ikiwa wafu hawafufuliwi kuna maana au haki gani ya kubatizwa kwa niaba yao? Wale wafanyao desturi hiyo hawaonekani kama wapumbavu ikiwa kweli wafu hawafufuki? . . . Kiini cha utetezi wao kiukweli ni kinzani kati ya imani yao na matendo yao. Waliyamini kuwa hakuna ufufuo wa wafu huku wakitenda kinyume na kile walichoamini.” (Kaiser, et al. 1996: 617)

### C. *Muktadha ni ufunguo wa kuelewa na kutafsiri kifungu chochote cha Biblia*

*Muktadha ni muhimu sana katika kuelewa kifungu cha maneno ya Maandiko.* Muktadha ni yale “yote yanayoambana na kifungu cha maneno”. Kuna *muktadha wa aina mbili*, nayo huathiri kifungu cha maneno: *muktaadha wa kifasihi na muktadha wa kihistoria (wa kitamaduni)*. Muktadha wa kifasihi unajifunzwa kutoka kwenye Biblia pekee. Muktadha wa kihistoria unadai kujifunza au kupata habari nje ya Biblia.

#### 1. Muktadha halisi

- a. *Muktadha wa kifasihi ni “maneno, sentensi, aya au zinazozunguka na kuhusiana na kifungu”* (Doriani 1996: 31). Muktadha wa fasihi hutuonyesha namna aya au visehemu vingine vinavyoingia katika eneo kubwa zaidi la maandiko. Inatupa muono mkubwa zaidi kuhusu maana hata kama hatujui chochote kuhusu mwandishi na wale aliowaandikia.
- b. *Sura katika Biblia na mistari hazikuwepo katika vifungu vya asili.* Mgawanyo wa sasa wa sura haukuwepo hadi kufikia miaka ya 1200; namba katika mistari ya AK haikuwepo hadi kufikia mwaka 1400; namba ya mistari iliyopo sasa katika AJ ilianza kutumika miaka 1551 (Metzger na Coogan 1993: 105-07). Kwa sababu sura na namba katika mistari ni kwa ajili ya kufanya rejea “*mara zote hazikubaliani na mwendelezo wa wazo la asili katika kifungu*” (Ibid.: 105). Namba ya mistari huleta sintofahamu ya kwamba mstari mmoja “husimama peke yake” katika kutoa maana lakini hazifanyi hivyo.
- c. “*Vipimo vya mawazo*” katika *Biblia ni aya na wala, siyo mistari.* “Ufunguo wa kuhakikisha hatubadili maana ya mstari ni aya siyo neno moja moja” (Koukl 2001: n.p.). Hii ni kwa sababu “muktadha huunda mstari na kuupa maana maalumu. . . . Hii hufanya kazi kwa sababu ya ni sheria ya msingi ya mawasiliano yote: Maana siku zote hutiririka toka juu kuja chini, kutoka vifungu vikubwa kuelekea kwenye vifungu vidogo na siyo kinyume chake”. (Ibid) Kwa maelezo zaidi, “aya huzingatia maadhui maalumu. Ingawa maudhui hayo yanaweza kuundwa na vipengele tofauti tofauti, vyote hivi, hata hivyo huungana na kushughulikia maudhui yanayoelezwa na aya hiyo” (Wolvaardt 2005: 99). Maneno ni nyenzo anazotumia mwandishi aeleze wazo kubwa na maudhui aliyonayo katika ufahamu wake. Neno “kamwe halitumiki peke yake bali hutumiwa pamoja na maneno mengine kuunda sentensi(isipokuwa katika sentensi ya neno moja ambayo hutegemea moja kwa moja sentensi zinazoizunguka ili kuelewa maana yake” (Ibid.: 48).
- d. *Ingawa neno moja moja na mistari ni muhimu katika kutafsiri Biblia kwa usahihi, wazo la msingi ni kuanzia na vifungu vikubwa kuelekea kwenye vifungu vidogo.* Maneno yatakiwa kueleweka kwa kuzingatia mazingira ya mstari ambayo maneno hayo yanapatikana, Mistari inatakiwa kutafsiriwa, kwa kuzingatia nuru itolewayo na aya zenye mstari hiyo; aya hutafsiriwa kwa nuru ya aya inayozunguka aya hizo; yote haya huitiraji uelewa wa maudhui ya sura, sehemu ya maandiko, na kitabu kizima. Hii ni muhimu sana, Koukl analisemea kama ifuatavyo: “Sheria ya msingi” ni “*Kamwe Usisome mstari wa Biblia*. Badala yake, soma angalau aya. Mara zote angalia muktadha. Angalia mtiririko wa mawazo. Kisha jielekeze kwenye mstari. . . . Ni uzoefu wa somo la kivitendo ambalo nimewahi kujifunza . . . na ni jambo moja muhimu ambalo nimewahi kukufunza”. (Koukl 2001: n.p.; chapisho hili limeambatanishwa kama **Nyongeza A**)
- e. *Muktadha wa kifasihi ni kama ngazi ya mawazo.* “Vifungu cha Biblia huwasilisha fundisho, hatua moja kwa wakati, katika utaratibu maalumu kwa kuwa kila wazo huelekea kwenye hatua nyingine. Kama ambavyo ni vigumu kutoka ngazi namba moja na kurukia ya saba, kisha

kurukia ya tatu na kurukia ya name, hivyo ni upumbavu kuruka ruka ndani ya Biblia, bila kujali ngazi zake za mawazo na matukio.” (Doriani 1996: 32)

f. *Muktadha wa kifasihi ni kama bwawa.* Ni lazima kuzingatia “upana” mazingira ya kifasihi (i.e., sehemu, kitabu, na maelezo ambayo yana kifungu cha maneno), na “wembamba” au “iliyokaribu” mazingira ya kifasihi (i.e., sentensi na aya zilizo karibu na kifungu cha maneno kinachoshughulikiwa) unapotaka kuja kusudi na maana ya kifungu cha maneno. “Mtu akitupa jiwe kwenye bwawa la maji mahali pale jiwe lilipoangukiwa itatokea miduara inayoambatana ikizunguka hapo mahali. Mahali jiwe linapokutania na maji ni kama kifungu cha maneno unayojifunza na ile miduara inayoanzia kwenye eneo lililoangukia jiwe ni ni mfano wa kitabu chote chenye kifungu cha maneno hayo. Kwa kadiri mduara ulivyo karibu na mahali jiwe limeangukia ndivyo ulivyo na athari kubwa kwa kifungu cha maneno unachoshughulikia.” (Doriani 1996: 33)

g. *Ni vema zaidi kusoma kitabu chote moja kwa moja kabla ya kuanza kufanya kazi kifungu cha maeno katika kitabu hicho.* “Kwa vile mwandishi aliwasilisha ujumbe wake wote katika kitabu kimoja, ni muhimu mchakato wa kupata maana ya kifungu fulani cha maneno ni lazima uzingatie muktadha wa kitabu ambacho kifungu hicho cha maneno hayo kimetokea” (Wolvaardt 2005: 90). Kwa kusoma kitabu chote unapata “picha nzima.” Unafuatilia mtiririko wa wazo la mwandishi tangu mwanzo hadi mwisho wa kitabu. Jaribu kupuuza mgawanyo wa sura na mistari. Kipekee kwa vitabu vifupi, soma kitabu chote kwa mara moja na katika wakati mmoja. Kwa hakika kusoma kitabu zaidi ya mara moja ni faida kubwa. Unaanza kuona maudhui na mambo ambayo mwandishi anayazingatia. Unaanza kuona jinsi aya zinavyohusiana kwa pamoja. Kwa kifupi unaanza kuona jinsi ambavyo mazingira ya karibu na yale ya jumla ya kifungu cha maneno unachojifunza.

h. *Karibu kila mstari huonyesha umuhimu wa kuutafsiri kwa kuzingatia muktadha wake kifasihi.* Wakati mwagine maana ya mstari ipo wazi kabisa, lakini mazingiza yanatupa kweli ya ziada katika mstari huo. Hapa kuna mifano miwili:

(1) Mara nyingine rafiki wakristo, au mchungaji anapowekwa wakfu anaweza kunukuu maneno katika Mwanzo 31:49 kama ishara ya kujaliana na urafiki—“Mungu avizie kati ya mimi na wewe, wakati tusipoonana.” Japokuwa muktadha unaoonyesha matamshi hayo aliyatoa Labani kwa Yakobo. Muktadha mzima wa **Mwanzo 29-31** unaonyesha chuki na kutoaminiana kati yao wawili. Muktadha unaofuata kwa karibu katika **Mwanzo 31:22-55** hudhihirisha kuwa hilo lilitokana na uchungu na kutoamini.

Kutokana na hilo Labani anasema, “Mungu akutazame kwa jicho lake akuangushe chini ikiwa utavuka mstari huu au ukiwaumiza binti zangu.” Kwa hiyo muktadha unaeleza kuwa tamko lile lina maana tofauti na ile ambayo siku zote watu humaanisha linapotumiwa (ikiwa litatumika nje ya muktadha).

(2) Katika Luka 17:5 wanafunzi wakamwambia Bwana, “Tuongezee imani!” Katika kutazama tu hilo laonekana ombi zuri sana. Pamoja na hayo muktadha kifasihi hulipa picha ya tofauti kabisa. Katika **Luka 17:3-4** (muktadha waa karibu kabisa) Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wasameheane mara saba kwa siku moja. Katika mazingira haya “Tuongezee imani” inaweza kumaanisha “Tungetaka kukutii, basi tafadhali tusaidie kwa katuongezea imani,” au “Hatutaweza na hatutakutii vinginevyo utuongezee imani.” Yesu akajibu katika **Luka 17:6-10** (muktadha wa karibu unaofuata) walikuwa na hatia kwa kusema waliyoyasema. Maelezo yake alipotoa mfano wa mbegu ya haradali (**17:6**) ulionyesha kwamba tayari walikuwa na imani ya kutosha. Mfano aliota kuhusu mtumishi Yule (**17:7-10**) pia ulionyesha tendo la kusamhe ndugu siyo huduma ya ajabu na kwamba haihitaji—imani ya ajabu bali ni wajibu wa mtumishi. Kwa hiyo katika muktadha huo “kilio cha, ‘Tuongezee imani’ si tu haitakiwi bali ni kisingizio cha kukosa utii. . . . Ingawa vipo vifungu vinavyotutia moyo tuombe lakini Luka 17:5 siyo mojawapo. Hakuna la zaidi isipokuwa tunaonywa tusitumie maneno mazuri kuficha kutotii kwetu.” (Doriani 1996: 34)

i. *Nukuu toka AK au rejea katika AJ.* “Kuna nukuu zisizopungua 257 na zaidi ya rejea 1,100 (kulingana kitabu cha Kigiriki cha Nestle-Aland ) za Agano la Kale katika Jipyä” (Osborne 1991: 277). Rejea [i.e humaanisha, au rejea isyo ya moja kwa moja] “imekuwa na msisitizo mkubwa kwa kuwa mwandishi amedhani kuwa msomaji wake anajua anachokisema” (Ibid: 135). Hizo rejea na nukuu zinaffaa zifuatilie na kutathminiwa. Hizo nukuu au rejea *mara kwa kadhaa lakini si Mara zote hujikita katika mazingira ya AK katika uhalisia wake au mazingira*

*ya rejea zenyewe.* Mazingira ya AK yanaweza kuongeza kina au utajiri katika mazingira ya kifungu cha AJ. Katika kutathmini nukuu za AK au rejea katika AJ, au ikiwa muktadha wa AK nyuma ya nukuu au rejea unafaa kutumika, “yatupasa kutafuta kutambua (katika msingi wa uhusiano kati ya mazingira ya AK na AJ) misingi ya mwingiliano kati ya vigezo vya maana vilivyoonyeshwa katika Agano Jipyä na namna mwandishi wa Agano Jipyä alivyoelewa kifungu cha maneno katika Agano la Kale” (Ibid.: 136).

## 2. Muktadha wa kihistoria (kitamaduni).

- a. *Mauktadha wa kihistoria (kitamaduni)* ni “*desturi, lugha, imani, na historia ya mwandishi na wale watu aliowalenga*” (Doriani 1996: 31). Muktadha wa kihistoria hutupa namna ambavyo sehemu ya Biblia inavyoingia katika ulimwengu wake. Inatupa maelezo ya awali ambayo yataelezea umuhimu wa yale maneno, misemo, desturi, watu, maeneo, na matukio ya kibiblia ambayo mwandishi ameyarejea.
- b. *Kwa kadiri tunavyoufahamu ulimwengu wa Biblia ndivyo tunavyoifahamu Biblia.* Maisha na muda wa watu wa Biblia na tamaduni zao zaweza kutupa habari za thamani ambazo zinatusaidia kuelewa maana ya maelezo yaliyomo katika Biblia. Muktadha wa kihistoria haukutajwa kwenye Biblia kwa sababu miiko ya kitamaduni na matukio ya kihistoria yalifahamika vema na waandishi na wale waliokuwa wakiandikiwa. Ndiyo maana vyanzo vilivyo nje ya Biblia kama vile itifaki, atlasi, kamusi ya Biblia, ensaklopidia, na vitabu vingine vya rejea vyawenza kutumika.
- c. *Tafuta muktadha wa kihistoria kwa kutumia Biblia pekee.* Tukisoma kwa ufahamu wa utafiti, vidokezo vya maneno yaliyotamkwa humo vinatupa kushangazwa na matukio ya kihistoria na tamaduni zilizokuwapo. Hii inaweza kutusukuma zaidi kuendelea kujifunza au kutafiti. Biblia pekee pia inaweza ikatupa mwanga juu ya historia ya kale.
- d. *Muktadha wa kihistoria unaweza kutupa kina au kubadili ufahamu juu ya kifungu cha maneno.* Mifano ifauatayo huonyesha jinsi ambavyo ufahamu wetu juu ya muktadha wa historia unatusaidia kuleta uelewa:

(1) Ufahamu wetu kuhusu mavazi ya Wafilisti na desturi zao hutupa kina katika kuelewa baadhi ya vifungu vya maneno. Mavazi yalikuwa ghali sana, na idadi kubwa ya watu walikuwa na nguo chache sana. Hivyo, Yesu aliposema “*Mtu akikunyang’anya kanzu yako mwachie na joho pia*” (**Mat 5:40**), alikuwa akidai sadaka inayoleta maumivu sana. Hata nguo zilizotumika zilikuwa na thamani kubwa. Vibarua walipewa nguo za watu waliokufa kama ujira kwa kazi zao (tazama **Mat 27:35**; mstari ule na maelezo mengine ya ziada nje ya Biblia yanatueleza kuwa Yesu alisulubiwa akiwa uchi kabisa akiwa hana kabisa nguo, hata ile ya kiunoni kama wengine wanavyoonyesha katika picha). Kuongeza, katika mfano wa mwana mpotevu (**Luka 15:11-32**), “kwa kuchomeka kanzu yake na kukimbia angeonyesha baadhi ya nguo zake za ndani, baba alijali zaidi mwanaye kuliko mali. Alipompa kanzu, pete, viatu, wale wasikiasi wa mwanzo waliweza kujuu kuwa sasa amepokelewa tena kwenye familia.” (Doriani 1996: 46)

(2) Maarifa kuhusu Wana wa Isrseli na historia ya Rumi hupanua uelewa wetu kwa baadhi ya vifungu. Yesu kuingia kwa shangwe Yerusalem (**Yoh 11:13-15**), watu kupepea matawi ya mizeituni, na Yesu kuwa juu ya punda, wala siyo farasi, Matawi ya mizeituni ilikuwa alama ya Taifa la Israeli. Pia yalitumika kwenye sarafu na hata wakati askari wa Taifa la Kiyahudi wakipigana na Rumi AD 66-70 na 132-35. Kwa hiyo, kupepea kwa matawi ya mizetuni “ilikuwa ishara ya matumaini ya kitaifa kwamba utawala wa masiha unaanza kwa kufika kwake Yesu” (Carson 1991: 432). Ingawa, Yesu “hakuングia Yerusalem akiwa amepanda farasi wa vita . . . ambaye angeibua shauku za kisisa za watu wengi ambazo zingezua uasi na hasira, lakini alichagua kujionyesha kama mfalme ajaye kwa amani, ‘mpole akiwa amempanda punda’” (Ibid.: 433). Hii hii ya kihistoria hutuonyesha tofauti kati ya ujio wa kwanza na wa pili. Biblia hutumia lugha ya alama kusema kwamba Yesu ajapo mara ya pili hatakuja akimpanda punda lakini atakuwa juu ya “*farasi mweupe*” akiwa na jeshi likiwa limepanda “*farasi weupe*”, “*kuhukumu na kufanya vita*” (**Ufunuo 19:11-14**). Katika Rumi ya kale, mashujaa walioshinda vita vikubwa huwa na maonyesho kwenye hadhara ambapo waliingia kwa gari lililovutwa na farasi weupe wanne, wakiwa na majeshi yao yaliyoshinda yakiwafuata nyuma (Ramsay 1875: 1163-67).

(3) *Maarifa ya jiografia ya kale husaidia kuondoa dhana potofu kwa baadhi ya vifungu.* Katika **Ufunuo 3:15-16** Yesu analiongelea kanisa la Laodikia kwamba “*si baridi wala moto*” na kusema kwamba “*kwa sababu u vuguvugu . . . nitakutapika utoke katika kinywa changu.*” ‘Laodikia kuwa na sura ya ‘kutokuwa baridi wala moto’ lakini vuguvugu, katika desturi yao ilijukana kama alama ya wao kukosa usahihi wa kiroho na kujitoa kwao hakukuwa sawa sawa mbele zake Kristo. Tatizo la hili ni kwamba Kristo anatamani kuona wakiwa “baridi au moto” hayo yote yakiwa ni chanya. Mtazamo wa asili, ingawaje, unaonyesha baridi kuwa ni hali hasi, wazo la Yesu lilikuwa anawataka wasomaji wa Neno lake au wawe wamejaa wivu kwa ajili yake (‘moto’) au wasishughulike naye kabisa (‘baridi’) lakini siyo kuwa katikati ya barabara. Lakini hatudhani kwamba Kristo anashauri watu wakose uaminifu kabisa (bado 2 Pet. 2:21). Tafsiri ya hivi karibuni sana huchukulia muundo wa namna hii kwa jinsi ya tofauti sana. Taswira ya maji kuwa moto, baridi na vuguvugu huonekana kama sifa ya kipekee katika Laodikia na maeneo ya jirani katika karne ile ya kwanza. Maji ya moto ya Hierapolis yalikuwa ni dawa na maji ya baridi ya Kolosai yalikuwa safi, yanafaa kunywa, na yalikuwa mazuri kwa afya. Pamoja na hayo Laodikia imefahamika kwamba walikuwa na uwezo wa kupata maji ya vuguvugu tu ambayo hayakuwa na ladha nzuri na yalikuwa yakisababisha kichefuchefu. Ni kweli kuwa Laodikia ilikuwa mji uliondelea kwa vile ulikuwa na mazingira mazuri ya kibashara, lakini ulikuwa mbali na maji mazuri. Mji ulipojaribu kuvuta maji kwa watu ulifanikiwa kupata maji ya vuguvugu na yenye kutapisha. ‘Mwitikio wa tabia na mwenendo wao kwa Kristo ulifanana na mwitikio wa maji yao kwao’—Kristo ‘akataka kuwatapika watoke katika kinywa chake.’” (Beale 1999: 303)

#### D. Maelezo dhidi ya maelekezo

*Maelezo* ni mfano au msemo unaotoa taarifa kuhusu mtu fulani, kitu fulani au tukio lilitokea. *Maelekezo* ni amri (“agizo”) ambayo inatueleza jinsi ya kufanya au namna itupasayo kuishi. Mifano katika Biblia hazionekani kama amri isipokuwa pale inapoelekezwa kuwa ni amri. Kutofautisha maelekezo na maelezo katika Biblia ni muhimu sana inapofikia wakati wa *kutendea kazi* Neno la Mungu.

1. Aina za mijadala. Aina zote za maandishi huwa katika mfumo *wa kawaida au shairi*. Mwandishi anapokuwa ameamua ni mtindo gani anataka kuutumia, ni lazima apange habari yake kutokana na kile anachotaka kuwasilisha. This will lead to the selection of the four major types of discourse Hii inatufikisha katika hatua ya kuchagua kati ya aina nne ya uwakilishaji wa makala anaotaka kuutumia (Makala ni mjadala mrefu kuhusu jambo fulani): Fafanuzi; Kanuni; maelezo; and kutia moyo (kwa ujumla kuna mwingiliano wa aina za mijadala katika Biblia, kwa hiyo kwa ujumla hazipo kwenye mfumo “safi”). Aina hizi za makala zinazingatia mwunganiko wa sifa mbili: *mpangilio* (matukio hufuatana hatua kwa hatua kwa muda mrefu) na *maelekezo* (mjadala fafanuzi hueleza nini kifanyike) (tazama Wolvaardt 2005: 87-88):

	Iсио-еlekeза	Maelekezo
<b>Mpangilio wenye mipaka:</b>	<i>Masimulizi</i>	<i>Kanuni</i>
<b>Mpangilio usio na mipaka:</b>	<i>Maelezo</i>	<i>Kutia moyo</i>

2. Mifano ya aina nne za makala ni kama ifuatavyo:

- Masimulizi*—Kitabu cha **Ruthi**. Kina mipaka ya kimpangilio (kinaelezea tukio moja baada ya jingine katika maisha ya Naomi na Ruthi), lakini hakitoi maelekezo ye yeyote (ingawa kinatupa ujumbe lakini hakitoi maelekezo kwa msomaji). Masimulizi, kimsingi unahusika na wakati uliopita na unalenga watu maalumu, matendo yao, mahali, na vitu.
- Kanuni/utaratibu*—**Hesabu 8:5-14**. Mungu alimpa Musa maelekezo ya jinsi ya kuwaweka wakfu walawi. Inaelekeza (kwa Mungu alikuwa akimfanulia Musa nini akifanye), pia kina mpangilio (kwa sababu jambo moja linatakiwa lifanyike baada ya lingine). Kanuni/utaratibu kimsingi ni maelekezo yaliyo katika mpangilio unaonyesha jinsi jambo linavyotakiwa kutekelezwa au kukamilishwa hatua kwa hatua.
- Maelezo*—**Wakol 1:1-2:5**. Ingawa kuna mpangilio maalumu wa kile Paulo anachosema (i.e., anajenga fundisho moja juu ya jingine), maoni yake hayana (mpangilio wa muda) mpangilio maalumu (hivyo-hakuna mpangilio). Zaidi ya hayo, katika sehemu hii ya kitabu Paulo maelezo yenye ufanuzi kuhusiana nini cha kufanya au jinsi ya kuishi (kwa hiyo hakuna maagizo au amri). Ufanuzi kimsingi, huhusika na kutoa maelezo kuhusu wazo, nadharia, au hoja.
- Kutia moyo/ari*—**Wakol 2:6-4:6**. Katika sehemu hii ya kitabu Paulo anatoa maelekezo ya

jinsi wakristo wa Kulosai wanavyotakiwa kuishi (kwa hiyo inaagiza), lakini si katika mpangilio wenyewe mipaka (i.e., maelekezo yake hawezi kufuatiiliwa katika mitiriko maalumu). Kutia moyo kimsingi ni mazungumzo yenyenye mantiki kuhusu jinsi ya kuweka kwenye vitendo nidhamu na kanuni za kiroho.

3. Kosa moja la kawaida ni kugeuza maelezo ya Biblia na kuyabadili kuwa maagizo au amri, au kudai kuwa mfano wa kibiblia au matendo yafanywe kwa lazima kuwa ndiyo msisitizo wa mwenendo wa kanisa la leo. Kosa mara zote hutokea wakati mtu anapochukua mfano wa Biblia, na kufanya moja au zaidi ya yafuatayo:

- a. *Kushindwa kuzingatia “aina ya hotuba” (tazama hapo juu).*
- b. *Kushindwa kuona maudhui yaliyomo kwenye kifungu cha maneno yenyenye mfano huo, au vinginevyo huukuza mfano nje ya muktadha wake wa kifasihi.* Kwa mfano, watu wengi humpa Mungu masharti—ambayo huyaita “kujiondoa katika uwezekano wa kuamini uongo”—kujaribu kuvumbua mapenzi ya Mungu. Wanayafanya haya kwa kutumia **Waamuzi 6:36-40**. Pamoja na hayo, Biblia haituruhusu kufanya majaribio hayo au kuweka masharti yetu wenywewe au sheria ambazo Mungu anapaswa kuzifuata ili sisi tufanye kwa namna Fulani au tuvumbue mapenzi yake. Zaidi ya hayo, maudhui au jambo lililopo katika **Waamuzi 6 siyo** “namna ya kujua mapenzi ya Mungu.” Kwa hakika **Waamuzi 6:1-24** Mungu alimtokea Gideon kibinagsi, akamwambia yampasayo kufanya, na kumwambia “*hakika nitakuwa pamoja na wewe*”. Kwa hiyo majaribio ya Gideoni, hasa hasa yalidhihirisha *kukosa kwake imani na utii*.
- c. *Chagua mifano baadhi tu, au baadhi ya mambo katika mfano, lakini puuza baadhi ya mambo ambayo ni kinyume na huo “ukweli wa msingi” au desturi.*

(1) Katika kuutafuta somo kwenye mfano uliopo kwenye maelezo ya kibiblia ni lazima tuangalie maeneo yaliyo na maana zilizo wazi, na siyo mifano iliyo na maana iliyojitenega na kweli. Kwa mfano baadhi ya vikundi husema “*kujazwa Roho*” ina maana ni lazima unene kwa lugha mpya. Vikundi hivyo kimsingi huzingatia **Matendo 2:3-11**. Hata hivyo, vikundi hivyo huchagua tu baadhi ya ishara za Roho “*kunena kwa lugha*” na kupuuza ishara zingine zilizotokea. *Hayawasitizi ishara zingine zilizotokea yaani—mvumo kutoka mbinguni “kama mshindo” wa “upepo uendao kasi” “ndimi za moto” zilizomkalia kila mmoja wao; ukweli kwamba “lugha” zilikuwa lugha za wanadamu zilizo jukulikana—ni lazima leo iwepo pia.* Kwa kuongeza, vikundi hivyo *hupuuza mifano mingine* ya watu ambaa walijazwa Roho pasipo ishara ya kunena kwa lugha kama matokeo ya kujazwa kwao (tazama **Matendo 4:31; 8:17; 9:17-19**).

(2) We must also compare the examples with any didactic teaching on the subject Ni lazima pia tulinganishe mifano yenyenye mafundisho yanayoongoza watu kwenye matendo mema. Kwa kubadili mifano ya “*kunena kwa lugha*” kuwa sharti na amri kama ishara ya ujazo wa Roho wengi *wamepuuza mafundisho ya Paulo* kuhusu karama za Roho na kujazwa na Roho. *Waaminio wote wanayo madhihirisho ya Roho (1 Wakor 12:7—“kila mmoja wetu amepewa madhihirisho ya Roho kwa ajili ya kufaidiana”)*. Kulingana na **1 Wakor 12:7-11, 28-30**, Roho ndiye anayeamua nani awe na karama ipi au madhihirisho gani. Hakuna mtu mmoja aliye na karama zote au madhihirisho yote. Hakuna hata mmoja asiye na karama ye yeyote au madhihirisho ye yeyote. Kwa kweli, **1 Wakor 12:30** Kwa kufafanua si kila mtu atanena kwa lugha. Zaidi ya hayo katika, **Waefeso 5:18-21** Paulo anawaagiza waaminio “*wajazwe na Roho.*” Kisha anaorodhesha madhihirisho yanayotokana na ujazo wa Roho, lakini kunena kwa lugha si mionganoni mwa madhihirisho hayo.

d. *Hushindwa kutofautisha kati ya mambo ya kitamaduni na mambo yaliyo sahihi kwa wote na kwa nyakati zote.* Kusudi letu waaminio ni “*kugeuzwa na kufanana na [Yesu]*” (**Warumi 8:29**). Hata hivyo, mifano ya Yesu haimaanishi kila eneo la maisha yake ni “*maagizo*” ya jinsi ya kuishi sisi, (i.e., kiwango cha usahihi kinachotakiwa sisi kufuata) katika mwenendo wetu wote.

(1) Baadhi ya maeneo katika maisha ya Yesu ni mahitaji ya tamaduni za pale alipoishi. Yesu aliishi Palestina, alipanda punda, alivaa kanzu iliyofumwa toka juu mpaka chini, (haina vipande), aliongea lugha ya kiaramu; hata hivyo, sisi hatulazimishwi na Biblia kufanya hayo yote. Kwa upande mwengine, Yesu hakuwahi kuendesha gari, hakuandika wazo la kufanya utafiti, hakula pizza, au kutumia tarakilishi; hata hivyo, sisi hatukatazwi kufanya hayo. Hayo yote ni mambo ya kitamaduni tu.

(2) Baadhi ya mambo katika maisha ya Yesu hayakuwa hata ya kitamaduni. Yesu hakuoaa, ingawa watu wengi katika utamaduni wake walioa. Kwa hiyo, wapo watu leo

wanaosema kuwa ikiwa mtu anataka kumfuata Yesu kwa ukamilifu inampasa asioe. Hata hivyo maelezo hayo kuhusu maisha ya Yesu kuyageuza na kuyafanya makatazo au amri siyo kibiblia. Hakuna amri ya kibiblia inayokataza kuoa. Yesu alitambua ndoa (**Mat 19:1-9**). **1 Wakor 7** inaruhusu na kuhimiza ndoa. **1 Tim 4:3** anaongezea kusema kuzuia watu kuoa ni “*mafundisho ya mashetani.*”

#### **E. Kanuni zilizopo hapo juu zinaonyesha umuhimu wa kuelewa maandiko kwa usahihi**

Tunaweza kufanya mambo kadhaa ili kukuza ufahamu wetu kuhusu biblia tukihusisha yafuatayo:

1. Kusoma na kutafakari maandiko kila wakati, kuandika kumbukumbu ya mambo tunayopata tunaposoma.
2. Pitia Agano la kale na jipya ili kupata historia ya kibiblia na ufunuo.
3. Wajue wahusika wakuu, mahali pao na nafasi yao katika mpango wa Mungu wa wokovu.
4. Fahamu historia ya matukio makubwa na wakati yalipotokea na utambue uhusiano uliopo.
5. Jua nyakati zilizopo katika vitabu vya Biblia—i.e., nini kiliandikwa, lini, na nani kaandika.
6. Kutengeneza majedwali yetu wenyewe, michoro, dondoo, rejea, na itifikasi.
7. Kuwa na maktaba yetu ya Biblia kwa ajili ya rejea, ikijumuisha vitu vyenye msaada mkubwa kama itifikasi, kamusi ya Biblia, vitabu vyenye ufanuzi mzuri wa matukio ya Biblia, na vitabu vingine vya kujifunza.

#### **IV. Tanzu za fasihi katika Biblia**

Kutafsiri ni lazima kuwe sambamba na kanuni za kifasihi na muundo wa kifungu cha maneno. Tanzu za fasihi ni aina mbalimbali ya kifasihi ya kitabu au maandishi, ikitambuliwa kwa vigezo rasmi(mtindo, tuni, utumiaji wa lugha, yaliyomo, nk.). Biblia ina tanzu nyingi za fasihi (e.g., historia, ushairi, mithali, unabii, uchambuzi, nyaraka [barua], maandiko ya hekima, mbari, mambo yajayo). Vitabu vya Biblia vinaonyesha, kimsingi, Mgawanyo wa kifasihi ufuatao: **Mwanzo-Esta**, na **Matendo ya Mitume** ni vitabu vya kihistoria; **Zaburi na Wimbo ulio Bora** kuwa ni mashairi; **Ayubu**, **Mithali**, na **Muhubiri** ni mashairi ya hekima; **Isaya - Malaki** ni unabii; **Injili** ni maelezo ya wasifu; **Warumi-Yuda** ni nyaraka; **Ufunuo** ni aina za fasihi zilizochanganyika: nyaraka, ufunuo, na maelezo ya hali halisi ya wakati ule.

Hata kama kitabu kinaonekana kuwa na muundo moja wa kifasihi, Vitabu vingi huwa vina muundo wa mchanganyiko kwa sehemu (au “miundo”) ndani yao, kwa mfano, hadithi za miujiza, hotuba, mazungumzo, mifano, vifungu vya sheria, mbari, maadili na orodha ya vifaa, vibadala. Muundo wa kifasihi ni wa muhimu kwa sababu unaamsha matarajio fulani. Kwa kiwango fulani muundo wa kifasihi huonyesha kazi. Hiyo ndiyo sababu muundo wa uandishi unaonekana kutawala au kutoa maana ya aina fulani ya muundo wa kifasihi. Kwa hiyo maongezi au sheria zifanyazo kazi kwa muundo moja wa fasihi wakati mwengine zinawenza zisifae kabisa kwa muundo mwengine wa fasihi.

Zaidi, waandishi wote wasioandika habari za kubuni, maigizo, ushairi, na karibu kila tanzu labda isipokuwa maelezo ya matumizi ya vifaa vya ufundu hutumia kanuni za kitaalamu(nayo ni, njia ambazo mwandishi atajenga maana, msisimko, mtazamo, n.k kuptitia lugha). Njia hizo za kifasihi huhusisha mrejesho, “haki ya mshairi” kurudia maneno, ushawishi, kutoa mwelekeo na aina nyingine nyingi. Tukitambua kuwa kila tanzu ina muundo tofauti. Kutafsiri shairi kana kwamba ni sheria kwaweza kusababisha makosa makubwa zaidiya kimaandiko. Waandishi wa biblia mara kwa mara hutumika lugha za ishara. Kwa uangalifu mkubwa mtu anapaswa afahamu mtindo tofauti tofauti ya uandishi wa Biblia na kutumia ujuzi katika kusoma na kutafsiri. ICBI inaweka msimamo huu katika tamko lilitolewa, “Tamko kuhusu tafsiri ya Biblia la Chicago” (1982: n.p.)

1. “TUNATHIBITISHA kwamba kwa kuwa kuna aina mbalimbali za fasihi, muundo na mtindo, ili kupata tafsiri sahihi ya kina maeneo mengi ya Biblia yanahitaji uchambuzi unaozingatia tanzu za fasihi katika nidhamu ya mafunzo ya Biblia” (Art.XIII). Geisler alitoa maoni yake katika tamko hili kama ifuatavyo: “Kufahamu mtu anatafsiri aina ipi ya fasihi ni muhimu ili kupata uelewa kuhusu tafsiri sahihi. Upimaji wa usahihi wa tanzu ya fasihi utazingatia ufahamu sahihi kuhusu tanzu hiyo ya fasihi.” Mfano haupaswi kutazamwa kama Mambo ya nyakati, wala shairi halipaswi kutafsiriwa kana kwamba ni maelekezo ya moja kwa moja. Kila kifungu cha maneno kina aina yake ya tanzu iliyotumika, hivyo mtafsiri anapaswa kuzingatia hilo pale anapohitaji kutafsiri. Bila ya kutambua aina iliyotumika mtafsiri anaweza kukoseshwa katika kupata maana sahihi ya kifungu. Kwa mfano nabii anaposema ‘miti inapiga makofi’ (Isaya. 55:12) mmoja anaweza kudhani ni maajabu fulani asipotambua kuwa kinachotumika hapa ni shairi na wala si kauli halisi.”
2. “TUNATHIBITISHA kwamba upo umuhimu wa kutafsiri Biblia kwa kuzingatia alisi yake, au ufahamu wa kawaida. Ufahamu halisi ni ule wa kihistoria wa muundo wa maneno katika lugha wenye

maana aliyoeleza mwandishi. Tafsiri inayozingatia uhalisia wa kifasihi inahusisha aina zote za maneno na miundo ya kifasihi inayopatikana kwenye kifungu” (Art. XV). Geisler anatoa maoni katika tamko hili: “Maana ya halisi ya kifasihi ya Maandiko ndiyo inayotambuliwa na na kupewa uzito wa juu zaidi. Ili kuwa na uhakika ikiwa tafsiri ya kiingereza ina makosa ya kifasihi kiuandishi, Maneno ya kawaida na yale yaliyotumika zamani ya lugha ya asili hutumika kuelezea maana. Ufahamu wa kifasihi pia umekusudiwa kutoa ufanuzi zaidi kuhusu ufahamu wa kihistoria katika lugha ya mwandishi. Hii ina maana kwamba tafsiri sahihi ni ile inayovumbua maana ya kifungu cha habari kwa kuzingatia muundo wa lugha na historia muktadha wa utamaduni wa pale ambapo habari imewasilishwa . . . Hili kamwe lisichukuliwe kama kuondolewa kwa mifano au habari zingine zilizotengenezwa au mitindo mingine ya fasihi inayohusisha lugha za ishara.”

Tanzu kuu za fasihi na tanzu ndogo ndogo ni kama zifuatavyo:

#### A. *Simulizi*

Simulizi (wakati mwingine huitwa “hadithi katika tamthiliya”) ni hadithi: ni maelezo ya watu na matukio kwa muda na kipindi. Ni simulizi lenye mwanzo na mwisho. Linahusisha yale mambo ambayo mwandishi anayaona muhimu katika kufikisha ujumbe wake. Simulizi linadhahirisha Mungu anayetenda katika historia. Simulizi linafanya kile kilicho nadharia (i.e., mawazo ya kitheolojia maandiko, na mashauri) liwe halisi na la kibinagsi—inatusaidia sisi “kuona” ukweli ukitumika kwa njia ambayo maelezo ya kawaida ya kweli hayawezi kufikia. Simulizi zipo kwenye Biblia kwa makusudi ya kuwasilisha ujumbe ingawa simulizi pekee haina mamlaka ya mwisho.

1. Katika Biblia simulizi zote zimesimamia msimamo wa kihistoria kwamba uumbaji umefanywa na Mungu. Kwenye Biblia hakuna kitu “kilichojitokeza” tu peke yake. Wakati wote unaposoma simulizi katika Biblia ni lazima ufikiri kitheolojia (kwa sababu simulizi za Biblia zote ni kuhusu Mungu). Kwa kweli, historia iliyoandikwa kwenye Biblia katika AK (na kwenye **Injili na Matendo ya Mitume**) ingefaa iitwe “yaliyosimuliwa au theolojia historia.” Sababu ni kwamba biblia inawasilisha ukweli wa theolojia ukifungamanishwa na kweli ya tukio la kihistoria. Kwa hiyo, Mungu mwenyewe ni kiini cha Simulizi zote katika Biblia. Simulizi hutusaidia kuzipa nyama mafundisho na amri katika Biblia.
2. Biblia inachukua kumbukumbu ya kweli za kihistoria lakini historia katika biblia inachagua kwa makini sana kwa sababu za kitheolojia. Kwa mfano, miaka 335 tangu kifo cha Yakobo na Musa kumbukumbu za uzao hazikuchukuliwa, wakati huo huo miaka 40 ya jangwani imechukua vitabu kuanzia **Kutoka – Kumbukumbu la Torati** (sura 125). Jambo lenye umuhimu kwa waandishi wa historia wa kawaida inaweza isiwe muhimu kwa waandishi wa Biblia na kinyume chake pia ni kweli.
3. Historia ya uzao katika Mashariki ya Kati ya Karibu, ikihusisha lakini si kibiblia tu ilihesabiwa kama haki ya kisheria ya kudai utawala mamlaka na uwezo; pia ilikuwa sehemu ya mambo muhimu ya kujifunza na kuyajua. Kumbukumbu ya uzao nyakati zile zilikuwa na sifa mbili: *kina* (kwa kawaida inachukua vizazi 5 hadi 10); na *yaliyomo* (inaruhusu mabadiliko hasa kwenye majina inaweza—kuacha majina yaliyomo katika historia ya uzao). Kwa hiyo historia ya uzao katika kitabu cha **Ruthi 4:18-22** imeishia vizazi kumi. Inafanya kazi ya kumtambua Boaz na kumweka katika uzao wa saba uliopendelewa na inasaidia kuhalalisha dai la Daudi la kuwa katika kiti cha enzi cha Israeli.

#### 4. Aina kuu za simulizi za biblia ni:

- a. *Taarifa* (habari kwa ufupi);
- b. *Simulizi za Hotuba* (taarifa hasa hasa kuhusu alichosema mtu katika kuweka kumbukumbu na tukio muhimu ni hotuba); na
- c. *Tamthiliya* (simulizi zilizo ndefu na tata). Tamthiliya kiuhalisi yanahusisha: (1) wahusika; (2) ya kitambo, mahusiano, na mazingira ya tukio ya kijamii; (3) migogoro; (4) matatizo na majanga; (5) utatuza wa matatizo; na (6) kufuatilia utendaji au maelezo kwa kina. Uwe mwangalifu kwa yafuatayo katika maigizo ya kibiblia
  - (1) Maelezo ya kina katika simulizi za biblia huwa ni kidogo sana. Kwa hiyo yale yaliyosimuliwa huwa ni ya muhimu sana (ufafanuzi hupatikana kwa njia ya hotuba na matendo).
  - (2) Katika tamthiliya ya biblia wahusika ndiyo msingi. Kuna aina tatu kuu za wahusika: *wahusika wema* (wahusika wa kati wa muhimu sana kwa ajili ya fundisho); *wahusika waovu* (adui wakuu au wanaopingana na muhusika mkuu); na *wapinzani* (wahusika wanaomwogopesha muhusika mkuu kwa kuulezea ugumu au wakati mwingine kwenda tofauti). Kwa mfano katika **1 Samweli 25** Daudi alikuwa ni muhusika mwema, Nabali alikuwa ni mwovu na Abigail alikuwa kizuizi. In **2 Samweli 11-12** Daudi alikuwa kiini cha somo na Uriya alikuwa kizuizi; ingawa Bersheba ni muhimu katika simulizi lakini

jukumu lake ni dogo. Katika **Mwanzo 38** Yuda ni muhusika mkuu na Tamari alikuwa mrekebishaji; wengine walikuwa na kazi ya kusaidia.

(3) Mjadala ni muhimu sana na unaweza kufafanua kusudi la mwandishi. Wazo kuu la mwandishi mara kadhaa huwa linaonekana wakati linapotokea tatizo na wakati wa usuluhishi.

(4) Muundo wa mtiririko. Mtiririko wa masimulizi ya tamthilia muundo wake upo katika misingi mitatu (ingawaje inaweza kuungana pamoja):

(A) *Mpango wa utendaji*—mpango unawekwa na simulizi linatolewa ikielezea jinsi inavyofanyika na inavyopasa kuwa. Kwa mfano katika **Matendo 1:1-8** Yesu analiwaagiza wanafunzi wake kuwa mashahidi hadi miisho ya dunia; sehemu iliyobaki ya kitabu inaelezea jinsi hilo liliwyotendwa.

(B) *Kuelezwu kwa siri*—swali linaulizwa, na kisha kujibiwa. Mfano ni kitendawili cha Samsoni ambayo baadaye ilifafanuliwa (**Waamuzi 14:12-18**).

(C) *Utatuizi wa matatizo*—Tatizo linaelezwa na maelezo yanatolewa kuelezea jinsi linavyotatuliwa. Mfano unahusisha kitisho cha Daudi kwa Nabali na namna ambavyo Abigaili alivyotatua tatizo (**1 Samweli 25**), na uponyaji wa mtu kiwete (**Matendo 3:1-10**).

5. Kama vile ambavyo aya ni jambo la msingi katika kuchambua ujumbe, katika kufafanua tamthiliya tukio ni kitu cha msingi katika uchambuzi. Episodi ni mlolongo wa matukio yanayofanana, yaitokea katika eneo moja, wakati mmoja, na wahusika wakuu wale wale. Kukoma kwa tukio, katika eneo husika, na wahusika kutotajwa au kubadilika kwa muda wakati mwingi huashiria mwanzo wa tukio jipya. Tofauti inaonekana pale tamthiliya inapohusu safari ambapo mahali hubadilika kila mara na hiyo haimaanishi kubadilika kwa tukio. Episodi zaweza kulinganishwa na matukio katika igizo, programu kwenye runinga au mkanda wa video wa maigizo.

6. Simulizi nydingi yaweza kuwa ngumu tunapozitazama katika maana zake na maudhui yanaweza yasiwe na maana wazi. Simulizi zote zimebekwa ndani ya Biblia ili kufunua jambo au kutoa ujumbe. Kutofautisha *kinachoelezwa* (pale ambapo muhusika anasema uongo) dhidi ya kile kile *kinachofafanuliwa* ni muhimu kwa uelewa sahihi wa simulizi. Kurudiarudia ni muhimu ili kuelewa jambo linalowakilishwa au maudhui. Ni lazima kukumbuka kutochanganya ujumbe na muhutasari wa simulizi lenyewe. Ujumbe ni kile ambacho simulizi inalenga kumfundisha msomaji

7. Katika baadhi ya simulizi mwandishi au msimulizi hutoa maelezo ya maoni yake. Pale ambapo msimulizi wa hadithi anaelezea vitu, mara zote huwa anajiamini na anaaminika, na ni mwelekezaji muhimu wa kusudi la simulizi. Kwa mfano msimulizi wa aina hii na maoni yake yanaonekana katika **Mwanzo 39:2; Waamuzi 17:6; 18:1; 19:1; 21:25; Matendo 6:7; 9:31; 12:24; 16:5; 19:20**.

## B. *Mashairi*

Mashairi yanaonekana katika Biblia nzima. Vitabu vikuu vya mashairi ni **Zaburi** na **Wimbo ulio Bora**. Ushairi ni njia kuu ya kifasihi ya kuelezea hisia. Ushairi hauongelei vitu halisi bali vitu vya kufikirika. Kama asemavyo Ryken, “Kanuni ya kwanza ya ushairi ni msingi wa madhanio. . . . Mtunzi wa shairi huongea lugha dhania kwa sababu wanataka msomaji apate *uzoefu* wa matamshi yao kama *taswira na msingi* na siyo tu kama wazo” (Ryken 2002: 247). Ushairi hutusaidia sisi “kuhisi” kweli za Mungu, na kuziona kwa “macho ya fahamu zetu” kwa namna ambayo kusoma maandiko pekee hayawezi kutupatia. Ili kuwasilisha kwa namna hii maelezo ya ushairi siku zote huwa ni mafupi na matamu au yana uzito. Wakati, mahali na hisia zaweza kubadilika ghafla. Ushairi una sifa ya kuwa na lugha za ishara au alama. Ushairi katika biblia hauelezei tu hisia na vitu vya kudhania – bali huelezea maelezo ya maandiko lakini si kwa jumla (siyo kama kwa mfano nyaraka). Ushairi huwasilisha mwilingiano kati hotuba iliyobuniwa na mwanadamu na matokeo ya Sanaa na njia mojawapo ambayo Biblia hutumia kufikia utu wetu yaani—akili zetu (ufahamu), hisia zetu (mihemko), na kule kutaka kwetu (kutenda).

1. Utenzi kama vile aya umejikita katika maana yake. Unazungukia katika dhumuni lake lililokusudiwa. “Ushairi wa kibiblia siyo tu mlolongo wa mistari bali una uzuri na muundo wenye maana kamili” (Wolvaardt 2005: 153).

2. Kama vile ilivyo kwamba msingi wa mwanzo wa uchambuzi wa kifungu ni aya, msingi wa uchambuzi wa ushairi ni stanza (strophe). Stanza (strophe) ni kundi la mistari linalounda seti katika shairi. Kwa mfano, katika **Zaburi 1** mistari wa 1-3 unaunda stanza moja; mistari wa 4-5 nyingine; na mistari wa 6 ya mwisho.

3. Kiashiria cha msingi cha ushairi wa kiebrania ni msambamba. Muundo halisi huwa na sentensi fupi yenye sehemu mbili [A na B, iitwayo “bicolon”], yenye sentensi ya pili inayofanana sana na ya kwanza

( Mara nyingine ushairi ya kiebrania hutumia mstari mmoja [“monocolon”], au mistari mitatu yanaenda sambamba [“tricolon”]. Aina kuu za muambatano au usambamba katika shairi za kiebrania ni:

- a. *Mfanano* (i.e., mstari A na B inafanana sana, mfanano wa mwonekano)—A: *Bwana ni jabali langu, na boma langu, na mwokozi wangu, B: Mungu wangu, mwamba wangu ninayemkimbilia, Ngao yangu, na pembe ya wokovu wangu, na ngome yangu* (**Zab 18:2**).
  - b. *Tofautiana* (i.e., mstari wa pili hutofautiana na wa kwanza)—A: *Kwa kuwa Bwana anaijua njia ya wenyе haki, B: Bali njia ya wasio haki itapotea* (**Zab 1:6**).
  - c. *Endelezi* (mstari wa pili huendeleza mbele zaidi wazo la mstari wa kwanza)—A: *Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, B: Na Mfalme mkuu juu ya miungu yote* (**Zab 95:3**).
  - d. *Fafanushi* (i.e., mstari mmoja hutoa kweli na wa pili hufafanua au huelezea)—A: *Heri atendaye fadhili na kukopesha; B: Atengenezaye mambo yake kwa haki* (**Zab 112:5**).
4. Usambamba ni sifa ya nyingi za zaburi, mithali, maombolezo, baraka, laana, maombi, na hata sheria nyingi na hotuba za kiebrania. Hata hivyo hajiaishia kwenye vitabu vya “kishairi” pekee. Ona, mf., **Isaya 64:8**—A: *Lakini sasa, Ee Bwana, wewe u baba yetu; B: sisi tu udongo, nawe u mfinyanzi wetu; C: sisi sote tu kazi ya mikono yako* (tazama hiyo ni tricolon).
5. Kwa kuwa usambamba ni sifa ya muundo wa fasih za kiebrania pia inapatikana katika AJ, Angalia, mf., Mat 7:17—A: *Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; B: na mti mwovu huzaa matunda mabaya* **Mat 11:30**—A: *kwa maana nira yangu ni laini, B: na mzigo wangu ni mwepesi.*
6. Zaburi si mkusanyiko usio na mpangilio wa nyimbo:
- a. *Zaburi imepangwa katika vitabu “vitano”* Kitabu cha I—**Zaburi 1-41**; Kitabu cha II—**Zaburi 42-72**; Kitabu cha III—**Zaburi 73-89**; **Kitabu cha IV— Zaburi 90-106**; Kitabu cha V—**Zaburi 107-150.** Kila kisehemu kinatambulika kwa kuwa huishia na maneno yasiyobadilika (sifa kwa Mungu) huhitimisha kila kitabu.
  - b. *Zaburi zimegawanyika kutokana na ujumbe unaowakilishwa au aina, ikihusisha zaburi za maombolezo* (mf., **Zaburi 3-7; 9; 12-13; 17; 22; 25-28; 31; 38-40; 42-44; 51; 54-58; 60; 69-71; 79-80; 90; 94; 120; 130; 137; 139; 142**); shukrani (mf., **Zaburi 18; 30; 32-34; 40; 65-67; 75; 92; 103; 107; 116; 118; 124; 129; 135-136; 138**); sifa (mf., **Zaburi 8; 19, 66; 100; 103-104; 113; 117; 146-150**); hekima (mf., **Zaburi 1; 36-37; 49; 73; 119; 127-128; 133**); za kifalme (mf., **Zaburi 72; 89; 93; 95-100**); maombi dhidi ya maadui (mf., **Zaburi 7; 12; 35; 40; 52; 55; 57-59; 69-70; 83; 109; 137; 140**); a kimasih (mf., **Zaburi 2; 22; 69; 110**).

### C. Vitabu vya Hekima

1. “Vitabu vya hekima” vya Biblia (Ayubu Mithali na Muhibiri) huongelea uhalisia wa maisha kivitendo, lakini huangalia maisha kwa namna tofauti na “hekima ya asili ya kitamaduni.” Hekima ya kitamaduni huanza na *mamlaka*—haki, uhuru, cheo, na sifa/upendeleo. Hekima ya kibiblia huanza na *Mungu*—inamtazama na kumtegemea Mungu kama chanzo cha njia ya uzima. Hekima ya kibiblia imetolewa ili kutupa upeo mkamilifu kwa maisha yetu: upo mwelekeo wa kivitendo katika vitabu vya hekima, lakini mwelekeo huo hutuelekeza kuyaona maisha yetu katika uhusiano na Mungu na kumtegemea yeye. Vitabu vya hekima vinatutaka tubadili tamaduni zetu (jambo ambalo ni gumu ikiwa tamaduni zetu zimekuwa na nguvu sana ndani yetu.) Inatakiwa viwe msaada wa kubadilisha maisha yetu. Kulingana na vitabu vya hekima tunatakiwa kwanza kushughulika na nafsi zetu wala siyo ufhamu wetu. Vitabu vya hekima vinaelezea usoefu na hisia za watu, mara nyingi kulingana na mtazamo wa “mtu wa kwanza” Katika AK na AJ, maandiko yameungana katika kusababisha ukuaji katika hekima. Vitabu vya hekima hutusaidia sisi tukue katika kujitoa kwetu, mwenendo wetu na katika jamii.
2. Mithali ni “Kitabu cha hekima” katika mfumo wa ushairi. Mithali ni misemo ya hekima inayoelezea kweli za kijumla katika maisha. Siyo ahadi, unabii, haki, au sharia. Kosa la kawaida katika kutafsiri—*kwa sababu tanzu haijazingatiwa*—ni kuchukulia kuwa kitabu cha mithali ni ahadi za Mungu zinazotakiwa kutarajiwa na waaminio siku za leo. Kwa mfano, **Mithali 22:6** inasema, “*Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.*” Matokeo mazuri hutokea mara kadhaa, na wazazi wanatakiwa kufundisha watoto njia za Bwana. Ingawa mara nyingi watu hutenda tofauti hata kama wamefundishwa “njia iwapasayo kuenenda” Kwa bahati mbaya, **Mithali 22:6** haituhakikishii mwisho mwema (ni msemo wa mithali tu). Nyingi ya mithali hutumia njia moja au nyingine ya usambamba. Zaidi ya hayo siyo mpangilio usio na utaratibu maalumu, bali ni mpangillio unaozingatia maana, au mwingiliano wa matamshi au sauti. Kutambua maudhui, makundi, mpangilio wa mithali badala ya kuzitazama kama semi zilizokatika vipande vipande inaweza kusaidia uelewa wetu na kuthamini.

## D. Unabii na Apokaliptiki

Unabii waweza kuwa eneo lenye changamoto kubwa katika tafsiri ya Biblia. Sababu kubwa za ugumu huo ni kushindwa kutumia kanuni za kutafsiri Biblia zilizojadiliwa katika kitini hiki, na kushindwa kuelewa muundo wa kifasihi wa unabii.

### 1. Muktadha na asili ya manabii wa kibiblia.

- a. *Wana wa Israeli waliishi katika mazingira ya kipagani.* Dini zote za kipagani kimsingi ni za *kilaghai*. Ni mfumo wa watu kuelezea ulimwengu na kutafsiri nafasi yao katika ulimwengu, na kuishi kwa malengo. *Ubashiri* ni hali kujaribu kufahamu kuhusu wakati ujao; uchawi au uganga wa kienyeji ni hali ya kujaribu kupata faida kwa kuwatumia wengine kwa kufuata utaratibu fulani wa kiibada. Tofauti na dini za mataifa, Mungu aliwapa Waisraeli *ufunuo* na akalisimamisha *agano* lake. Katika mazingira haya, Mungu alianzisha taasisi ya manabii kupitia Musa. Kwa njia ufunuo wa kiungu, Israeli walishi utamaduni mchanganyiko.
- b. *Asili ya manabii wa AK.* Nabii alipaswa kuwa: mtu wa Mungu; sauti ya, na shahidi wa Mungu; mtumishi wa Mungu; na aliyejitoa kikamilifu kwa Mungu. Alipaswa kusema akiitoa sauti ya Mungu, kupingana na watu waliokuwa wakisikiliza sauti za watu. Vile vile, alitumika akipingana na tamaduni, kinyume na nguvu ya utawala wa kisiasa.
- c. *Muktadha wa kihistoria/kitamaduni.*

(1) Manabii wa Mungu walitumia neno la Mungu wakati kuna mgogoro wa mahusiano katika agano kati ya Mungu na watu wake. Kazi kubwa ya manabii wa AK siyo tu kubashiri yajayo. Badala yake, manabii wote walikuwa na huduma na ujumbe wa aina mbili: (A) Waliwaonya watu wa Mungu juu ya matokeo mabaya yanayotokana na kuasi njia ya Bwana *kwa maneno ya hukumu*; na (B) Waliwaita watu wa Mungu warejee katika uaminifu *kwa maneno ya matumaini na wokovu*. (VanGemeren 1990: 78-79) Kwa hiyo unabii wa AK unavutia sasa kama ulivyokuwa wakati uliopita.

(2) Manabii wote wa AK, walihusika na kubadili tabia za watu. Ujumbe wao ulikuwa, “Ikiwa utafanya haya, hukumu itakuja; ikiwa utamfuata Bwana, Baraka zitakuja.” Kwa hivyo, unabii wote wa AK, ulikuwa “una masharti” yanayowaelekeza watu kutubu na kubadili tabia zao, hata pale unabii ulipoonekana kama hauna masharti yejote.

(tazama **Yona 3**).

(3) Kihistoria mtu anaweza akaona kubadilika kwa msisitizo wa unabii baada ya kwenda uhamishoni Babeli. Kabla ya huo uhamisho manabii walikuwa wakikazia kuhusu uasi wa wana wa Israeli. Baada ya uhamisho msisitizo ukabadilika na kuwa, wajibu wa watu wa Mungu kijiandaa kwa ajili ya ujenzi wa ufalme wa Mungu.

(Van Gemeren 1990: 213-14)

d. *Mtazamo wa Kifasihi.* Kimsingi manabii wanawasilisha ujumbe wao kwa mdomo; maandishi ya unabii lilikuwa jambo lililofuata baadaye. Vitabu vya kinabii mara kadhaa huwa na mkusanyiko mwangi wa maneno yaliyonenwa ambayo si mara zote yana mpangilio maalumu. Lugha za alama au mifano iliyotumika kwa kiasi fulani zilikuwa zinaendana na maana ya kufikirika kulingana na tamaduni zao.

2. Mkazo upo katika nafsi ya Mungu na siyo kwenye matukio. Ujumbe wa kinabii zaidi ni “*kusema kweli*” ya Neno la Mungu, kuliko *utabiri* wa matukio yajayo. Mkazo wa ujumbe wa unabii ni kuhusu Mungu. Kwa hiyo *kutimia* kwa unabii huwa juu ya *nafsi* (Mungu) na si katika tukio. Kwa vile *kutimia* kwake huwa juu ya *nafsi*, Mungu yupo huru *kutimiza vyovyote* na wakati *wowote* atakaochagua mwenyewe. Mungu hajifungi katika matarajio ya mtu. Kwa mfano, manabii hawakuwa wakisema juu ya Mungu kuja katika mwili, bali kuja kwa Daudi au uzao wake. (mfano, **Isaya 11:1; Yer 30:9; Ezek 37:24**). Hata hivyo, Mungu alikuja mwenyewe na ufalme wa Mungu ukadhihirika katika nafsi ya Yesu kwa namna ambayo manabii wa AK hawakuweza kudhihirisha (tazama **Marko 1:15; Luka 17:21; Mat 16:19** [cp. **Isaya 22:22**]). “Wale wenye msimamo katika tafsiri halisi wa siku za Yesu ndio walioshindwa kutambua *kutimia* kwa matarajio yao kwa njia ya Yesu. Wale waliomtarajia masihi kwa nyanja ya kisiasa na kijeshi, mbadala wa hasili wa Daudi, walishindwa kufahamu kuwa Yesu anayo mengi ya kutoa na wala hajapungua kwa yale wanayotarajia. Wale waliomdhihaki katika majoribu yake hawakuweza kufahamu zaidi ya ufahamu wa asili kuhusu matarajio yake ya kujenga hakalu lililoharinbiwa kwa siku tatu(Mathayo 26:61; cf. Yohana 2:18-22).” (Travis 1982: 139) Hatujui jinsi gani ahadi za Mungu zitatimizwa katika siku zijazo. “Ikiwa tunatambua unabii wa siku zilizopita waweza kutimia kwa namna ambayo hatujui wala hatutegemei, vivyo tutambue kuwa hatuwezi kuuchukulia unabii kama maelekezo ya kina ya wakati ujao. Tunaweza kuona usambamba au mfanano

fulani kwa hali yetu ya sasa tukilinganisha na unabii; ingawaje tunapaswa kuacha nafasi ya tofauti ye yote ambayo yaweza kutokea tusiyoitarajia.” (Green 1984: 105)

3. Mkazo upo kwenye mpangilio na maudhui. “Utabiri wa Agano la Kale kuhusu mwisho wa dunia kwa kawaida umeunganishwa na maudhui na maneno ya msingi kuliko mpangilio usiotetereka (kwa mfano, tazama Danieli 7:8-27; 8:9-26; Ufunuo 16-19)” (Oropeza 1994: 195n.10). Kwa sababu ya jumbe mbili(hukumu na wokovu), hata kama manabii walinena kuhusu matukio mbalimbali lakini maudhui yanayofanana yalionekana kwa wote. Maudhui hayo yalihuisha: Agano la Mungu na watu wake; uwepo wa Mungu; Mungu kama Mfalme; Masihi wa Mungu; Siku ya Bwana; ufalme wa Mungu; roho wa Bwana. Waandishi wa AJ waliona maandishi ya unabii wa AK, kama *mpangilio* kimsingi uliotimizwa katika AJ. Kwa hiyo kama Raheli alivyolia alipokuwa alipokuwa akienda utumwani (mazingira ya **Yer 31:15**), Hivyo Raheli akalia tena wakati Herode aliwapowaua watoto (mazingira ya **Mat 2:18** ambapo Mathayo ananukuu unabii wa Yeremia). Tunahitajika tutazame maudhui na mpangilio huu. Ndani yake tunapata ufahamu wa Ki-ungu.

4. “Uwezekano” katika Unabii. Kama maneno ya hukumu na wokovu, unabii una msingi wa maadili ndani yake. Matokeo ya jambo hili ni: “Mtazamo wa kibiblia kuhusu unabii ni kwamba matarajio siyo lazima utabiri utimie kwa bila ya kukosa. Bali utabiri wa janga au jambo haya lolote ni dokezo ili hatua stahiki zichukuliwe ili kuepusha ubaya uliokusudiwa. Vivyo hivyo utabiri juu ya baraka ni mhimizo au kutiwa moyo ili kuwepo na uvumilivu katika mchakato huo wote kuelekea kwenye mwelekeo sahihi” (Ford 1979: 99n.72) Mungu si nafsi tuli binafsi yenye nguvu. Bali, hutumia lugha ya ishara, Mungu huitikia kulingana na maamuzi wayafanyayo watu kwa kuzingatia amri na maagizo yaliyotolewa na manabii wake. Tunaona hili pale “anapobadili nia yake” kuitikia maombi ya Musa kwa niaba ya Wana wa Israeli baada ya Musa kutoa hukumu yenye kutisha kwa ajili yao (**Kutoka 32:9-14**), na pale alipoacha kuangamiza Ninawi, baada ya Ninawi kutubu (**Yona 3:1-10**). J. Barton Payne analisemea hii hali ya asili ya Mungu ya kutobadilika na mwitikio wa watu kama ifuatavyo: “Syo kwamba ni viwango vya kimungu, Amri zake, au asili yake kubadilika, ukweli ni kwamba, kwa hakika tabia ya Mungu ya kutobadilika ndiyo inayomlazimisha kuwa na matumizi ya tofauti za pande katika kutekeleza kanuni zake zisizobadilika, kwa kuzingatia mabadiliko hayo yanayomzuia mwanadamu anayebadilika badilika. Kipekee unabii umewekwa na Mungu kwa ajili ya kudhibiti tabia za watu ili kuwahamasisha kuyaishi maisha ya kiungu ya utakatifu. Hivyo wanadamu yawapasa watafute na kutumia fursa hiyo ya kuwa na maisha matakatifu . . . badiliko linakuwa sasa si tu kwamba linawezekana bali ni kwamba ni jambo lisiloepukika.” (Payne 1980: 62)

Mungu alitangaza kanuni hii **Yer 18:6-11; 26:12-13; Ezek 18:1-32; 33:10-20**. Wakati mwingine masharti ya unabii huelezwa wazi wazi: mfano, **Yer 38:17-18; 42:7-17; Matendo 27:21-44; Warumi 11:17-24**. Wakati mwingine unabii unayo masharti yake, lakini tabia ya Mungu na mwitikio wa watu kwa masharti yasiyobainishwa: mfano, **Kutoka 32:9-14; Isaya 38:1-5; Yona 3:1-4:2; Mat 19:27-28** (Ahadi ya Yesu kwa wale kumi na wawili kwamba wangehukumu makabila kumi na makabila kumi na mbili ya Israeli ikiwahuisha *Yuda*). Wasomaji wa siku za leo walio na “mtazamo kwamba matukio yaliyotabiriwa au yanayotarajiva kinabii hayawezi kubadilika mara chache huonekana kama ni sahihi sana, Matamko ya siku za kale kwa wana wa Israeli ambayo katika siku zao yalikuwa hayahesabiwi kuwa yataokea kwa ukamilifu wote” (Ford 1979: 75). Hata hivyo, watu wa Biblia hawakuyachukua maandiko ya kinabii kama kweli zisizobadilika kamwe. Jambo linalofanyika kuitikia unabii unaweza kuahirisha unabii au kuharakisha kutimia kwake (**1Wafalme 22:14-20; Hab 2:2-3; 2 Pet 3:8-12**). Katika **1 Sam 23:10-14** Daudi alibadilisha kabisa madhara ambayo yalifunuliwa kwake na Mungu baada ya yeye kufanya tendo la busara. Katika **Matendo 21:10-14** “mkristo rafiki wa Paulo hakuuchukulia unabii [wa Agabo] kama jambo ambalo litatimia bila shaka. Badala yake waliyahesabu kama maonyo ya upendo na kwamba janga hilo laweza kubatilishwa.” (Ford 1979: 99n.72)

5. Manabii hujenga juu ya nabii zilizotangulia. Agano la Mungu lilikua na kuenea kuititia manabii walioendeleza na kukuza kuititia matamko yao ya hukumu na wokovu. Ifuatayo ni mifano miwili ya mwendelezo wa kinabii katika AK pekee:

- Ahadi ya kurithi nchi katika Agano la Ibrahimu (tazama **Mwanzo 12:1-3**)*. Vipengele vyote katika Agano la Mungu kwa Ibrahimu (“Agano la Ibrahimu”) vilifanyiwa maboresho siku baada ya siku. Ukiangalia ahadi ya “nchi” nchi hiyo mwanzoni haikufafanuliwa (**Mwanzo 12:1**). Mwanzoni ilisemekana kuwa ni kile Ibrahimu aneweza kuona kwa macho yake (**Mwanzo 13:14-15**), baadaye ikaelezwa kijografia (**Mwanzo 15:18-21; 17:8**), na hatimaye yakatolewa maelekezo yaliyokamilika kwamba “uzao wako utamiliki malango [kifasihi “zake”] ya adui” (**Mwanzo 22:17**). AK linaonyesha kwamba unabii wa kumiliki nchi uliotimizwa katika uhalisia kwa awamu

mbili (katika siku za Yoshua [**Yoshua 21:43-45**] na wakati wa utawala wa Sulemani [**1 Wafamle 4:20-21**]). Hata hivyo, kwa sababu ya kutotii kwa wana wa Israeli, waliondolewa katika nchi yao, hivyo ahadi ilishindwa kutimia katika AK. Waliendelea kutamani kupata nchi yao na urejesho uliahidiwa wakati wa uhamisho (tazama **Ezek 20:1-44**). Baadaye ahadi ilitimizwa tena kwa sehemu baada ya uhamisho.

b. *Agano la Daudi (2 Sam 7:12-16)*. Yeremia alijikumbusha ahadi ya Nathani kuhusu ufalme wa Daudi na ukuhani wa Walawi, ili kuwahakikishia kuwa watu wa uhamishoni watarejeshwa katika nchi yao (**Yer 33:19-22**). Yeremia pia alijenga juu ya unabii wa Isaya shina la haki litachipuka katika ukoo wa Daudi, na kuongezea kwamba katika makuhani kamwe hatakosekana atakayetoa dhabihu mbele za Bwana (**Yer 33:14-18**; cf. **Isaya 11:1**).

6. Misemo ya kinabii. Manabii wa AK walinenea katika mipaka fulani maalumu, walitumia utaratibu ambaeo waliujua vema na ulio na maana kwa wasikiaji wao. Manabii wa AK walinena kuhusu ufalme wa masiha wa milele wakitumia lugha na kuufaninsha na ufalme wa kawaida wa kiisraeli. E. F. Kevan anatoa angalizo akisema, “katika matamko yao kuhusu ufalme wa Mungu, hata wanaposemea kweli za kiroho zilizo tukufu sana, misamiati ambayo manabii walitumia ni ile ya ufalme wa Mungu waliyoi jua wao katika mazingira yao” (Kevan 1954: 24). Hivyo, walitumia mfano wa hekalu, na Sayuni, na kunena kuhusu ufalme wakimlinganisha na mfalme toka ukoo wa Daudi, akiwa ameketi katika kitie chake cha enzi Yerusalem. Hii wakati mwininge huitwa “misemo ya kinabii”(Irons, “Misemo ya kinabii,” audio mp3)

Hata katika AJ, wakati Mungu alipodihirisha kutimizwa kwa unabii wa AK na wakati waandishi wa AJ wakionyesha utimilifu wa mpango wa Mungu, walitumia lugha ambayo ulimwengu wao unggelawa. Kama Steve Lehrer anavyoolezea, “Mungu anapowatumia manabii kutimia kwa unabii katika nyakati za Agano Jipy, Mungu aliamua kutumia aina za lugha za mifano na kivuli. Ailezea Agano Jipy katika lugha ya Agano la Kale. Akiwaelekeza watu kwenye mpango wake katika namna angavu na ya wazi zaidi ambayo inafahamika na kukubalika na wakati uliopo.” (Lehrer 2006: 85) Mfano ya hili inahusisha; pale Yesu anapotumia mwili wake kama “hekalu” (**Yoh 2:18-22**); kanisa katika ujumla wake huitwa “hekalu” au “sanduku la Agano” katika **1 Wakor 3:9, 16-17; 2 Wakor 6:16-7:1; Waef 2:21; 1 Pet 2:5; Ufunuo 3:12; Ufunuo 13:6**; Paulo anatumia lugha ya sadaka za kutekezwa zilizotolewa katika AK na sadaka zinazotolewa kusaidia huduma yake (**Wafilipi 4:18**; tazama **Kut 29:18**); katika ufunuo watawala katika nyakati za mwisho husemwa kwa cheo cha “wafalme” (mfano, **Ufunuo 16:14; 19:18**); wale wasababishao mapigo wanalinganishwa na farasi ambaeo wanaowaendesa wamejivika silaha za kale (mfano, **Ufunuo 6:2, 4, 5, 8; 9:7, 9, 17**).

7. Kutotimia kwa unabii kihalisia yaani kama ulivyonenwa. Kwa sababu kusudi la Mungu hukua kwa kutegemeana na chaguzi wazifanyazo watu na matukio, unabii mara zote hautimii “sawa na sawa na ulivytamkwa.” Stephen Travis anatoa mfano huu: “Yeremia na Isaya walitabiri kwamba Babeli itaanguka mikononi mwa Wamedi (Yeremia 2:11, 28; Isaya 13:17), na Isaya anaelezea kwa nguvu sana kuharibiwa vibaya kwa Babeli na mauaji yasiyo na rehema ya watu wake (Isaya 13:14-22). Lakini kiuhalisia Babeli ilianguka wakati wa utawala wa Uajemi, ulipata nguvu na kutawala juu ya Wamedi kabla ya kuteka Babeli. Nayo yaani Babeli ikajitia chini ya utawala huo bila kupigana. Mji haukuharibiwa, uliendelea kukaliwa na watu. Hivyo, unabii wa kuanguka kwa Babeli ultimia kiutowala lakini si kama ilivyoolezwa na unabii yaani uharibifu uliotajwa. Vivyo hivyo Isaya 10:28-34 alitabiri uvamizi utakaofanywa na Washami, akielezea kinaganaga jinsi jeshi hilo litakavyoingia toka Kaskazini hadi Kusini, mji kwa mji pembeni mwa milima kupitia Ai, Geba, Gibe, Anathothi na Nobu hadi Milma Sayuni. Kwa uhalisia, Senekarebu alipokuja kuvamia na jeshi lake alifuata mwambao wa pwani akikabili Yerusalem kutokea Magharibi.” (Travis 1982: 28, 137-38).

8. Kubadilika kwa mazingira na namna ya kutimia kwa unabii. Nabii zilizingatia mambo maalumu ya kihistoria; kwa hiyo, mabadiliko ya mazingira yainaathiri namna nabii hizo zinavyotimia. Kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kisiasa na kijiografia ambayo yamebadili hali ya nchi na mpangilio wake tangu nabii hizo zilipotolewa katika AK. Kwa umuhimu zaidi kuja kwa Yesu kumebadili ufahamu wa maarifa ya Kimungu kwa namna ya pekee sana. Hii inamaanisha kwamba, ingawa kanuni zinazofanana hutumika katika unabii kwa nyakati zote na tabia au sifa za Mungu hazibadiliki, hatuwezi kutegemea kwa uhakika nabii za AK ambazo bado hazijatimia kutimia kama watu (au manabii wenywewe) walivyoonyeshwa. Travis anaelezea kuwa: “Kwa kuwa unabii umefungamana na hali fulani maalumu ya kihistoria, umekuwa ukitumia misemo ambayo inaendana na wakati huo. Ibrahimu aliahidiwa nchi. Watu wa uhamishoni toka katika Yerusalem iliyoaribiwa waliahidiwa hekalu jipy (Ezekiel 40-48). . . Na hii ni kwa sababu unabii unalenga jambo moja ambalo, linapokuwa limetimia (kwa mfano,

walipokuwa wanarudi toka uhamishoni), hatuwezi tukaanza kuelezea kwa undani jambo lingine la kihistoria linalofuatia (kwa mfano, Mashariki ya kati ya sasa). Zaidi sana tunaweza kuonyesha kwenda sambamba kwa namna fulani kama AJ linavyofanya, kati ya habari zilizolezwa na manabii na hali ya sasa ya ‘Israeli’ wa leo, yaani Kanisa. . . . Kwa kuwa muundo wa unabii huakisi hali halisi ya wakati ambapo unabii huo hutolewa, tusione ajabu unabii ukitimia kimantiki na wala si kwa namna ile ile iliyoelezwa. Kule kuakisiwa kwa wakati hudhihirisha kwamba ni makosa kukazania kutaka kuona unabii ukitimia kwa kuonyesha hali halisi kama nabii fulani zinavyolezea. Kwa mfano, Isaya alitoa unabii akisema, kuna wakati Washami, Misri na Israeli wataishi kwa amani na kuwa baraka kwa ulimwengu (Isaya 19:19-25). Leo hakuna taifa la Washami na wengi wa makabila yaliyokuwepo Misri wakati wa Isaya ni tofauti na hawa wa siku za leo. Unabii uliotolewa wakati ule hauwezi kutimia kwa uhalisia kama iliyoelezwa wakati ule kwa sasa, ingawa inaweza kuwa picha ya amani kati ya Wayahudi na mataifa inayowezekana ndani ya Yesu Kristo (cf. Waefeso 2:11-22), au uhusiano mzuri kati ya watu wa mataifa yote katika ufalme wa Mungu wa milele ule ujao.” (Travis 1982: 136, 138).

**9. Madhara makubwa ya AJ kwa unabii wa AK.** Maana kamili ya kifungu cha maneno au unabii haiwezi kuwa wazi mpaka pale ambapo Biblia nzima na hatua ya historia ya ukombozi itakapowekewa maanani. Denis Johnson anaweka wazi jambo hili: “Kusoma Biblia kimantiki *kama Neno la Mungu* ni lazima kuhusishe nukuu zote kama muktadha wa maana ya kifungu maalumu cha maandiko” (Johnson 2007: 156). AJ inaathiri kwa kiwango kikubwa unabii wa AK. Kwa kweli, mtu anaweza akasema AJ inabadisha unabii wa AK na ni tafsiri sahihi ya unabii wa AK. Unabii ni eneo la muhimu ambalo Jipy [Agano] ipo katika Kale [Agano] likiwa *imefichwa* na Kale ipo ndani ya Mpya ikiwa *imefunuliwa*. Hivyo, “haifai na wala si haki kutazama Agano la Kale kana kwamba hakuna maandiko ya Agano Jipy yaliyoandikwa” (Walker 1996: 313).

a. *Ufunuo unaoendelea*. Graeme Goldsworthy anatoa maeleo muhimu kuhusu tafsiri ya Bibila, “Haiwezekani kupata maana kamili ya matendo na ahadi za Mungu zilizoandikwa kwa kutazama Agano la kale peke yake” (Goldsworthy 1991: 54). Sababu inayofanya AK peke yake isiweze kutoa maana kamili ni kutokana na fundisho la ufunuo unaoendelea, hii ina maana, kweli za Biblia hazijafunuliwa zote kwa mara moja bali zilifunuliwa kwa mwendelezo kwa kipindi fulani.<sup>1</sup> Kwa hiyo AK ni maandalizi ya Injili; Vitabu vya Injili ni udhihirisho wa Injili; Matendo ya Mitume ni mwendelezo wa Injili; nyaraka ni maeleo ya Injili; na Ufunuo ni matokeo ya Injili. Yesu na waandishi wa AJ walijua hili. Waliona AK kwa ujumla kwa namna fulani kama kitabu kuhusu Yesu. Yeye ni kiini chake na ni maudhui yake<sup>2</sup> naye ni “hitimisho na ufunuo mkamilifu ambao ahadi zote zinamhusu” (Goldsworthy 1991: 64).

Na kwa sababu Biblia hatimaye ni kitabu kuhusu Yesu Kristo ambaye amefunuliwa kwa uhalisi katika AJ, waandishi wa AJ hulitazama AK kama namna ya “viashiria” (Ramm 1970: 260-69; Goldsworthy 1991: 67-69). AJ inafunua Israeli kama taifa la AK, ambalo sheria zake, sherehe zake, na taasisi zake, na nabii za AK kwamba zilikuwa mifano, “alamu”, “ishara,” “vivuli”, “nakala” au “mifano” ya AJ ambazo zilikamilishwa na kuboreshwa katika Kristo na kanisa lake.<sup>3</sup> Willem VanGemeren anaelezea, “Ujio wa Bwana wetu ulibadili kipekee uelewa kuhusu Agano la Kale. Mitume walifahamu maandiko katika nuru ya huduma ya Yesu, ujumbe, na kuinuliwa kwake. Ule ufahamu wa kawaida wa kidesturi kuhusu maneno ya Musa na manabii ni lazima kubadilike kwa kutazama kuja kwa Bwana wetu.” (VanGemeren, 1990: 83)

Edward Young anaelezea umuhimu wa badiliko la kanuni linalotokana na kuja kwa Kristo tunapotafsiri unabii wa AK: “Ufunuo waliopewa manabii kwa namna fulani ulikuwa si wazi kwao”. Zilikuwa zikiitwa ndoto, maono, semi za ajabu. . . . Kwa kuwa ufunuo waliopewa wao ulikuwa pungufu ya ule alioupokea Musa kwa hakika, kwa kuwa una mambo tata, ni lazima tuzingatie kweli hizi tunapotafsiri unabii. Kwa hiyo ni lazima sisi tuepuke kufanya makosa yasiyo ya kimaandiko kwa kufuata kanuni ya kutafsiri kwa kuangalia ‘kweli ya kifasihi ikiwa inawezekana.’ Lugha ya manabii ilihu halii ya kiuchumi mchanganyiko, hivyo ililenga mazingira halisi ya nyakati hizo. Ni katika nuru ya agano jipy inaweza tu kutafsiriwa kikamilifu.” (Young 1952: 54, 215n.21) Kama asemavyo Steve Lehrer, ni lazima “siku zote soma Maandiko ya Agano la Kale kwa lensi ya Maandiko ya Agano Jipy” (Lehrer 2006: 177). Jinsi AJ inavyotimiliza ahadi na “ishara” zake haitoshelezi yenye we katika maeleo. Goldsworthy anatolea ufanuzi, “Hajithibitishi yenye we kwamba Yesu alitimiza ahadi za

<sup>1</sup> “Maono mwendelezo kwamba ufunuo wa Mungu haukuja mara moja mwanzoni, lakini ulifunuliwa hatua kwa hatua mpaka hapo nuru kamilifu ya kweli ilipotuzukia ndani ya Yesu Kristo” (Goldsworthy 1991: 64).

<sup>2</sup> Luka 24:25-27, 44-45; Yoh 5:39-40, 46; Matendo 3:18, 24; 10:43; 26:22-23; 2 Wakor 1:20; 1 Pet 1:10-12; Waeb 1:1-3.

<sup>3</sup> Tazama Mat 5:17; 1 Wakor 10:1-6; 2 Wakor 3:12-16; Wagal 3:23-4:7, 21-31; Kol 2:16-17; Waeb 1:1-2; 8:1-10:22.

Agano la Kale. Wale wayahudi waliotarajia kutimizwa kwa ahadi za Agano la Kale kwa jinsi ya kimwili walishindwa kumtambua Yesu kama utimilifu wenyewe.” (Goldsworthy 1991: 65–66)

b. *Muundo wa kutimia kwa unabii*. Kwa sababu ya asili ya kufanywa upya inayotokana na kuja kwa Yesu na kuanza kwa Agano Jipy, a *mtindo* wa kutimia kwa nabii za AK katika Agano Jipy ni tofauti na mtindo wa Agano la Kale wakati nabii zenyewe zilipotolewa. AJ hujenga katika mawazo ya AK, mara nyingi kwa namna ya ajabu. Hali hii ina matokeo muhimu kwa kuzingati muundo na muktadha wa kutimia kwa unabii wa AK. David Holwerda anafanua, “Kutimilizwa kwa unabii kunapotokea, taasisi ambazo zilikuwa zimetumika na ishara au alama ya hali halisi siyo muhimu. Nafasi zao zimechukuliwa na ukweli ambaio unaziwakilishwa.” (Holwerda 1984: 74–75) Goldsworthy anaongeza, “Hii ina maana kwamba muundo na yaliyomo katika kutimia kwa unabii inazidi kwa mbali muundo na yaliyomo kwenye ahadi zenyewe. . . . Kuzingatia Literalia mazingira *halisi* ya asili ya unabii ina mapungufu makubwa ya kutotaka kusikia yale yanayoelezwa na Agano Jipy kuhusu kutimia kwa unabii. Inakadiria kuwa ni lazima kutimia unabii kufuate muundo ule ule wa asili wa ahadi.” (Goldsworthy 1991: 65, 67).

Ingawa manabii wa AK walielewa unabii kwa njia moja, pale ambapo AJ inapotafsiri unabii wa AK moja kwa moja au kwa namna isiyo ya moja kwa moja, siyo sahihi “kujaribu kutumia kuwianisha mtazamo tofauti toka Agano Jipy [unabii wa AK] unatambuliwa, lakini uelewa wa [unabii] wa Agano la Kale hubakizwa vile vile bila kubadilishwa au kuguswa” (Walker 1996: 313). E. F. Kevan anatoa angalizo, “Mifano ya namna ya kutimia kwa unabii kubadilika inaonekana katika ufalme wa Daudi, Mtumishi, wateule, Mlima Sayuni, taasisi ya kuabudu ya makuhani na kutoa sadaka, na tumaini la Utawala wa Masihi. . . . Bwana wetu mwenyewe alibadili mawazo ya Agano la Kale, kama vile Sabato, kushika sikuu, hekalu, ufalme wa Daudi. Ni kutohana na kubadili kwake huko wayahudi mwishoni walimhukumu hadi kifo chake.” (Kevan 1954: 27).

c. *Tafsiri ya unabii wa AK kwa kutumia AJ*. AJ inafafanua kwamba hatimaye maana na kutimia kwa unabii wa AK huenda zaidi ya hali ya kimwili ya Israeli ya Kale. Kwa hakika, kama vile George Eldon Ladd anavyosema, “Agano la Kale halijaweka wazi jinsi nabii zake zitakavyotimizwa. Zilitimizwa kwa namna ambayo haijawahi kujulikana na Agano la Kale na kwa namna ambayo haikutarajiwa na Wayahudi. Kwa habari ya kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, *Agano la Kale linatafsiriwa na Agano Jipy.*” (Ladd 1977: 27, kwa msisitizo wa asili) Ingawa baadhi wanaweza kusema AJ inaifanya nabii nyingi za AK kuwa “za kiroho”, inafaa zaidi kusema AJ *inatafsiri* au *inahuisha* unabii wa AK. Katika AJ, kutimia kwa unabii unatazamwa katika mwili lakini kwa ufunguo mpya wa kiroho. Ahadi ya “nchi” katika Agano la Ibrahimu na unabii wa mfalme na ukuhani wa Lawi katika Agano la Daudi, iliyojadiliwa hapo juu, inadhihirisha kwa uwazi Zaidi jinsi AJ inavyotafsiri unabii wa AK:

(1) Ahadi ya nchi katika Agano la Ibrahimu (Mwanzo 12:1-3). AJ hutafsiri Kanani ya AK ya kimwili kama alama ya “nchi” ya kweli: dunia katika ujumla wake (**Warumi 4:13**); jiji la mbinguni, Yerusalem mpya (**Waeb 11:8-16; Ufunuo 21-22**). Zaidi sana, moyo wa nchi ya ahadi ulikuwa kuwapatia Israeli “pumzik” dhidi ya maadui zake wote na kuwa na mahitaji yao yote (tazama **Kumb 12:9-11; 25:19; Yoshua 1:23; Zab 95:10-11**). Hilo pia limekuwa na maana tofauti na kuwa wokovu wa wale waaminio au pumzik la kiroho (**Waeb 3:12-4:11**). Hivyo, katika **Warumi 10:1-10** Paulo ananukuu kutoka **Kumb 30:12-14**, ambayo katika AK ujumbe wake unahusika na kutii sheria za Musa na ahadi ya Mungu ya kuwarejesha Israeli waliotubu katika nchi yao. Anatafsiri ahadi hizo za AK kwamba Imani katika Kristo itasababisha wokovu.

(2) Agano la Daudi (2 Sam 7:12-16). Unabii wa Yeremia kuhusu mfalme na ukuhani wa kilawi katika Agano la Daudi (**Yer 33:19-22**) umetimia katika Kristo Yesu. Tofauti na anachosema Yeremia, Kristo anatawala toka mbinguni kama Bwana na si katika kitie cha enzi cha kidunia kama kiongozi wa kisiasa na wa kujeshi (**Matendo 2:22-36; Waeb 1:3**). Zaidi ya hilo, unabii wa Yeremia wa ukuhani wa Lawi wa kudumu hauwezi kupatana na ukweli wa Agano Jipy kutimia “kimwili” kwa unabii wa Agano la Kale. Sababu ni kwamba ukuhani wa Lawi ni “mfano” au “kivuli” tu ya kile ambacho kimewekwa tayari na Kristo katika Agano Jipy (tazama **Waebraenia 7**). AJ inaweka wazi kwamba ni Kristo na kanisa ndiyo walio na ukuhani wa milele (**Waeb 4:14-15; 7:11-8:2; 1 Pet 2:5, 9**). Hivyo, “Wakati Yeremia anaongea kuhusu kurejeshwa kwa mji

wa Yerusalemu na kurejeshwa kwa Taifa la Israeli na kiti cha Daudi kutawala Israeli na kuwaweka salama na kuongezeka kwa ukuhani wa Lawi katika wingi na kutoa dhabihu daima, anatumia lugha hiyo ya pitcha kuelezea kutimia kwa Agano Jipy la Mungu; ambalo ni bora zaidi ya vile inavyoonekana Agano la Kale” (Lehrer 2006: 91).

10. Lugha za kinabii na kutimia kwa unabii. Ni lazima tuwe makini katika matumizi yetu ya lugha—usichanganye “tafsiri halisi” na “tafsiri ya kimwili.” Garlington aneleza kwa usahihi: “‘Halisi’ ni ile inayokubalika. Tukizingatia maelezo ya B. Ramm’s kwamba uhalali maana ya ‘asili’ ya kifungu ni ile ya asili ‘asili,’ ‘inayofaa,’ ‘inayotarajiwa,’ na ‘ya kawaida.’” (Ramm 1970: 119-23) Katika maeneo baadhi, kwa hiyo, maana ya “asili” ni maana inayoashiriwa na kutegemewa” (Garlington n.d.: n.p.n.27; tazama pia Poythress 1993: 48-52). Kwa maneno mengine, njia ya “asili” ya kutafsiri ushairi ni ya “kishairi”; na “ni ya asili” na njia ya kutafsiri “alama”; njia ya “kialama” kutafsiri taswira ni ya kitaswira.

a. “*Wafasiri wa unabii*” wengi wa watu wa siku za leo hawajui namna ambayo AJ hutumia nabii za AK, kwa huziangalia nabii za AK kana kwamba zinasimama peke yake na kwamba ni lazima zitimizwe kama zilivyo, kwa namna ya kimwili kupitia taifa la sasa la Israeli. Mtazamo wao ni kama wa Mafarisayo walioshindwa kumtambua Yesu kwa sababu haendi sawa sawa ufahamu unaotazama mambo “kimwili” na kumtegemea Masihi (km, mtawala wa Israeli wa kisiasa na wa kijeshi). *Pia wanakosa kujua ukweli wa kitheolojia* kwamba mitindo ya AK ilikuwa “ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo” (**Wakol 2:17**). Kwa mfano, ingawa wengi hufikiri kile ambacho ni “halisi” ndicho kinaweza kuwa “dhahiri katika mwili”, na kile kisicho halisi hakiwezi kuwa “dhahiri katika mwili” mwandishi wa **Waeb 8:1-10:1** “anatupa maana tofauti kabisa hekalu halisi ni lile la mbinguni na hekalu la mfano ni lile la kidunia” (Beale 2004: 295).

b. *Tatizo la hao watafsiri ni kwamba wanadhani kimakosa “halisi” maana yake ni “kimwili” na kwamba kinyume cha “halisi” ni “kiroho.”* Ukweli ni kwamba kinyume cha “halisi” ni “kiashiri,” na siyo “kiroho”; “kiroho” kinyume chake ni “kimwili” (tazama Tegart 1999: n.p)

(1) Viashiria vya maneno ni kama ifuatavyo:

(A) *Halisi*—ya kawaida, kiashiria cha moja kwa moja cha kifungu; “halisi” huruhusu lugha ya ishara, lakini katika mazingira hayo hujielekeza katika “ukweli halisi.”

(B) *Kiashiri*—wahusika, matukio, na vitu havitegemewi kuchukuliwa kuwa na maana “halisi” lakini huwakilisha kitu kingine na kuwa na maana nyininge.

(C) *Kimwili*—inayoshikika, imetengenezwa kwa mada; “dhahiri” haipaswi kuchanganywa na “halisi” kwa sababu alama, mifano, na hadithi huwa zinahusisha “dhahiri” vitu, na ukweli wa kiroho “halisi” ipo lakini siyo ya kimwili au Dhahiri.

(D) *Kiroho*—isiyo dhahiri vitu au mawazo, au utawala wa kiroho; “kiroho” haitakiwi kuchanganywa na “viashiria au viwakilishi” ingawa viashiria vinaweza kuwa na mambo ya “kiroho”

(2) Hizo njia nne zinaweza kuunganishwa kaama ifuatavyo:

(A) Halisi na Kimwili—mf., dunia; mwanadamu; ufalme katika **1 Sam 14:47**.

(B) Halisi na Kiroho—mf., mbingu, Mungu; malaika; kweli; haki; upendo; ufalme katika **Marko 1:15 and Luka 17:20-21**.

(C) Kimwili na Kiashiri mf., ziara ya John Banyan, *Mwendelezo wa Ziara*; Hajiri, Sara, Mlima Sinai, na Yerusalemu ya sasa kama inavyotafsiriwa katika **Wagal 4:21-31**; ufunguo, mnyororo, na shimo katika **Ufunuo 20:1**

(D) Kiroho na kiashiri—“utepe” katika barua za C. S. Lewis *The Screwtape Letters*; “joka” wa **Isaya 51:9; Ufunuo 12:9; 20:2**.

11. Maono na lugha za alama. Nyingi kati ya nabii katika Biblia, na sehemu kubwa ya kitabu cha Ufunuo, imetolewa kwa ufunuo na inafundishwa katika lugha ya alama. Maono na lugha za alama *siyo* kama jumbe zenye mafundisho za nyaraka au maelezo ya simulizi za Vitabu vya sheria, vitabu vya historia vya AK, Injili, au Matendo ya Mitume. AK ilitoa unabii katika mfumo wa *maono*, *mifano*, na “semi zilizojificha” (tazama **Zab 78:2; Ezek 17:2; 20:49; 24:3; Hos 12:10; Mat 13:35**). Vile vile, ujumbe wote unaobebwa na **Ufunuo** katika ujumla wake unaanza na mtazamo wa jumla wa Ufunuo, ukianza na **Ufunuo 1:1** neno *sēmainō* (“wasiliana kwa alama”) na *deichnumi* (“onesho”), pamoja na kanuni ya kurudiarudia “Niliona” (au maelezo yanayofanana na hayo) inayotumika kutambulisha alama

au ishara za maono (tazama **Ufunuo 4:1; 12:1-3; 13:1-3; 14:1; 17:1-3**), inaonyesha “asili ya jumla ya mawasiliano kwa njia ya alama,” inavyokinzana na namna ya kawaida ya kuwasilisha habari (Beale 1999: 973; tazama pia ibid.: 50-53).

a. *Maana ya halisi ya maono “inajidhihirisha yenyewe.”* Maono na alama ni kama pitcha au maelezo ya habari. Maono na lugha ya alama zilizotumika katika nabii nyingi zinahitaji tuzizingatia katika hatua nne za mawasiliano: (1) *hatua ya lugha* (nayo ni., kumbukumbu yenyewe ya ujumbe); (2) *hatua ya maono* (nayo ni., alichooona Yohana katika uhalisia; “jambo halisi aliloona”); (3) *hatua ya rejea* (nayo ni., rejea za kihistoria katika maelezo katika maeneo mbalimbali); na (4) *hatua ya alama* (nayo ni., tafsiri ya kile kinachoelezwa na lugha ya alama katika rejea yake katika historia). (Poythress 1993: 41-42)

b. *Umuhimu wa tafsiri na uchambuzi wa maana halisi ya neno.* Wazo kwamba ni lazima mtu atoe tafsiri ya neno “kama liliyvo” isipokuwa pale ambapo mtu amelazimika kutafsiri kwa kutumia lugha ya alama kwa kuonyesha kwa uwazi yale yaliwasilishwa “lazima itiliwe maanani” katika kutafsiri kitabu cha Ufunuo na nabii zingine (hasa mafunuo), ingawa kwa sehemu si lugha za alama, “kitabu kimetumia lugha ya mafumbo” (Beale 1999: 52).

c. *Mfano wa hili unaonekana katika Ufunuo 20:1-6.* Katika kifungu hiki, Yohana: “alitumia maneno ‘miaka elfu moja,’ ‘ufufuo,’ na ‘uzima’ kwa sababu aliona, katika hatua ya maono, watu waliofufuka na kupewa uzima kwa miaka elfu moja. Kwa sababu yote aliyoona na yale aliyosikia katika maono kwanza hakuelewa katika uhalisi katika hali ya kawaida lakini yaliyoonekana katika lugha ya alama na kuwasilishwa. Kwamba maono haya yalitolewa katika lugha ya alama kama ‘mnyororo,’ ‘shimo,’ ‘joka,’ ‘nyoka,’ ‘alifungwa,’ ‘muhuri,’ na ‘mnyama.’ Kwa hiyo, maneno ‘ufufuo’ na ‘uzima,’ kwa mfano, hayatoi maana ya moja kwa moja ya kile kitu halisi alichooona mwonaji ikihusishwa na historia ya wakati huo pamoja na maana ya lugha za alama zisizo na uhusiano wa moja kwa moja. Uchambuzi wa maana ya maneno ya asili ya maneno yaliyotumiwa na mwandishi katika hali hiyo huamua.” (Beale 1999: 973-74) Tunaweza kusema hivyo hivyo kwa habari ya msemo “miaka 1000” katika kifungu kile cha maandiko. Kushikilia tafsiri ya moja kwa moja “halisi” miaka 1000 inahitaji kuendelea kushikilia msimamo huo huo hata kwa habari “ufunguo” na “mnyororo” ulioshikiliwa na malaika katika **Ufunuo 20:1** kwamba ni funguo za kawaida na kwamba “shimo” katika **Ufunuo 20:3** ni shimo la kawaida duniani yenyeye funguo za kimwili na kofuli na muhuri pia ni za kimwili” (Waltke 1988: 273; Jackson 2001: n.p.). Kwa hakika, shimo si la kimwili, lakini “hali ya kiroho iliyopo katikati ya maisha ya kidunia ambayo watu huishi, siyo chini yake au juu ya . . . Shimo ni moja ya vitu vinavyoonyesha eneo la kiroho ambalo shetani na mawakala wake hufanya kazi.” (Beale 1999: 987). Kwa hiyo, watafsiri wengi, pamoja na wale wanaotumia falsafa ya kabla ya milenia Ladd (Ladd 1972: 262) na Osborne (Osborne 2002: 701) wanaafiki kwamba “miaka 1000” ni lugha ya ishara (ya alama). Osborne anatoa angalizo, “Miaka kumi kumi katika Israeli yametumika kama lugha ya alama katika maandishi yao, na inaonekana kwamba hili lina maana ya miaka inayohesabika katika kipindi maalumu kwa ajili ya jambo husika” (Osborne 2002: 701).

12. Mwongozo wa mwisho kuhusu jinsi ya kutafsiri unabii. Kwa kuwa tunajua tofauti iliyopo kati ya Agano la Kale na agano jipya kwa habari ya tafsiri ya unabii, mwelekeo wetu unatakiwa uwe kanuni ya kiroho au wazo lililojificha katika “muundo” wa unabii, badala ya kujikiti katika “tukio linalodhaniwa” kuwa litatokea. Ufuatao ni ushauri wa namna ya kutafsiri alama katika unabii (Green 1984: 74-79; Oropesa 1994: 181-83):

a. *Fanyia kazi lugha za alama kwa unyenyekevu.* Ni lazima tufanyie kazi unabii kwa roho ya unyenyekevu. Hii ni muhimu sana kwa sababu nabii nyingi zina utata na mafumbo. Hata Danieli aliona maono yaliyo juu ya ufahamu wake (tazama **Dan 8:27**). Haishangazi kuona kwamba unabii ni mgumu kuuelewa.

b. *Tambua umuhimu wa msingi wa matumizi ya kutumia maneno ya kudhania juu ya sababu ya unabii.* Unabii si mafundisho ya moja kwa moja kama yalivyo katika nyaraka. Asili ya lugha ya unabii imeruhusu unabii utumike katika vipindi vyote, mazingira yote, na namna za kutimia kwake ambazo hazikufahamika wakati unabii unatolewa. Zaidi ya hayo uchambuzi wa akili za kawaida hauwezi kuvumbua makuu ya lugha ya alama ya unabii, ni lazima “tujifunze kufikiri kwa mtazamo wa taswira.”

c. *Tafuta maana kwa kuzingatia muktadha.* Mafunuo yaliyotolewa kwa mifano katika kitabu cha **Ufunuo** yanaweza kupatikana katika AK. Hilo linatupa muktadha, lakini tunapaswa kujiuliza kwamba *Yohana* alitumiaje hizo alama?

- d. *Tafuta jinsi manabii walivyojihusisha na uchungaji.* Kwa mfano, katika **Ufunuo 2:10; 13:9-10;** na **14:12** Yohana anawaasa wasomaji kuwa na uvumilivu na subira..
- e. *Tafuta wazo kuu.* Maelezo ya kina huonyesha wazo kuu analowasilisha nabii.
- f. *Epuka kuongozwa na vitu vya kinabii vya ajabu vinavyosismua.* Wale wanaodai wamevumbua mambo Fulani “yaliyositirika” kuhusu siku za mwisho, au waliovumbua “kanuni maalumu” ya kupata tafsiri ya biblia huwa wameonekana kuwa waongo.
- g. *Fahamu kuwa nabii nyingi za AK na AJ zimeshatimia.* Pungufu ya asilimia 2 ya nabii za Agano la Kale zinamhusu masihi. Pungufu ya asilimia 5 zinaelezea kipindi cha Agano Jipy. Chini ya asilimia 1 zinaelezea mambo ambayo bado hayajatimia. Manabii kweli walitabiri kwa ajili ya mambo yajayo. Lakini mara nyingi walitangaza kwa habari ya siku za wana wa Israeli, Yuda, na mataifa mengine yaliyowazunguka zilizokuwa zikitarajiwa kutokea punde tu kuliko kutangaza habari ya siku zetu za usoni.” (Fee and Stuart 1982: 150).

13. **Apokaliptiki.** Mara na baada ya Yuda kuwa uhamishoni Babeli, aina ya unabii uitwa “unabii wa siku za mwisho” uliinuka.<sup>4</sup> Aina hii ya unabii iliendelea kushamiri kuanzia 250 BC hadi kufikia AD 200 kwa Wayahudi na katika baadhi ya maandiko ya kikristo. Pia inapatikana katika maandiko zaidi ya yale ya kibiblia. Maandishi ya Unabii wa siku za mwisho kimsingi yanapatikana katika kitabu cha **Danieli** na **Ufunuo (Isaya, Ezekieli na Zekaria)** pia zina viashiria vya unabii wa siku za mwisho). Maudhui yanayofanana yanahuisha historia na miisho, majanga yanayohusika na vitu vya angani, vita katika nguvu za vitu vya angani na kukubalika kwa uongo na kutimia kwa mpango wa Mungu na ufalme wake.<sup>5</sup>

- a. *Apokaliptiki na unabii.* Mambo ya siku za mwisho ni muundo maalumu wa unabii. Beale anafafanua kwamba mambo ya siku za mwisho “ina msisitizo na mkusanyiko wenye uzito sana wa kifasihi na kimaudhui unaopatikana ndani ya unabii” (Beale 1999: 37). Kwa hiyo, yote ya hayo yanayozingatiwa katika kuelewa unabii yanatumika katika unabii wa Mambo ya siku za mwisho Kama Joel Green anavyoeleza kwa ufupi, tofauti muhimu iliyopo kati ya unabii wa kawaida na ule wa apokaliptiki ni kwamba unabii wa mambo ya siku za mwisho unategemea lugha za alama na kwamba unahuishi siku za mwisho: “Katika kutofautisha apokaliptiki na unabii, tofauti iliyo wazi zaidi ni namna ujumbe ulivyowasilishwa. Neno la unabii toka kwa Bwana linakuja kwa njia ya maono au ndoto. Alama, taswira, tarakimu—huonekana katika maandiko ya kinabii—zikitokeza zikiwa zinafafanuliwa zaidi katika apokaliptiki. Maandiko ya apokaliptiki yanatafsiri tena nabii zilizotangulia kutolewa; kwa mfano, Danieli anamrejea Yeremia ‘miaka sabini’ katika Danieli 9:2. Ingawa cha muhimu zaidi ni tofauti ya mwelekeo wa ujumbe. Nabii anatangaza kazi za Mungu katika na ndani ya historia. Waandishi wa apokaliptiki wanatoa taarifa ya wakati ujao usiojulikana bado wakati Mungu mwenyewe atakapoingilia kati wakati wa miisho ya nyakati.” (Green 1984: 62)
- b. *Apokaliptiki na historia.* Ingawa waandishi wa apokaliptiki imejielekeza katika nyakati za wisho, historia ya matukio ya kawaida ni muhimu: “Katika mtazamo wa mambo ya siku za mwisho matukio ya historia ya kawaida ni msingi muhimu wa utendaji wa kazi za Mungu. Kwa mantiki hii kuna mwendelezo kati ya neno “hapa” na “baada ya pale” (Green 1984: 62) waandishi wa apokaliptiki inamtazama Mungu kama mwenyezi na mtawala juu ya historia. Anaipelea historia kuelekea kwenye wakati wake aliokusudia mwenyewe. Nyakati hizo za Mwisho, waaminifu wa Mungu watakombolewa na kupewa taji. Ukweli huu maalumu katika ukristo kwa habari ya mwisho wa mambo yote unaitwa Ufunuo. Ulfgard anasema, “Ukweli muhimu unaotofautisha Ufunuo katika ukristo na waandishi wa apokaliptiki kwa wayahudi katika kutafsiri na kuchambua kwa kina ni kwamba mabadiliko ya muhimu ya kihistoria yamekwisha tokea. Baada ya Mungu kutuokoa katika Kristo, miisho ya dunia ipo katika mikono ya Mungu na Mwanakondoo.” (Ulfgard 1989: 11) Kwa hiyo, maandiko ya apokaliptiki yamejaa migogoro na mambo ya kutisha machoni petu, waandishi wa apokaliptiki hubakia katika tumaini lao.

## E. *Mifano na Mafumbo*

<sup>4</sup> Neno “apokaliptiki” linatumika kama kisifa na kama jina. Baadhi ya watafiti wanashauri kwamba “apokaliptiki” inaelezewa kama aina fulani ya eskatolojia na “apokalipsi” inawakilisha aina mahususi ya tanzu ya fsihi. Tazama Carson na Moo 2005: 714. Ingawaje, Waandishi wengi, wanatumia “apokaliptiki” kuonyesha tanzu mahususi na mtindo wa eskatolojia. Neno hilo litatumika hapa kwa kuzingatia mapana yake.

<sup>5</sup> Mtiririko mzuri wa hotuba wenye sehemu tatu wa D.A Carson kuhusu asili na kazi za apokaliptiki, wenye msisitizo mahususi kwenye kitabu cha Ufunuo wenye kichwa “Kuhubiri Apokaliptiki,” ambayo inaweza kusikilizwa na kupakuliwa kwenye: <http://resources.thegospelcoalition.org/library?utf8=%E2%9C%93&query=carson+preaching+apocalyptic>.

1. Mifano na simulizi kwa pamoja zinaweza kuonekama kama maelezo linganishi yaliyopanuliwa; ina maana, maelezo au simulizi na wahuksika au yale yanayofafanuliwa husimama badala ya kitu au jambo lingine kwa kusudi la kuelezea mwenendo mwema wa kiroho au kweli ya kiroho. Kwa kiasi fulani zinaweza kutofautiana, mfano unawenza kuwa mfupi, ukifua kanuni maalumu, siyo mgumu kuelewa, wenye kufundisha, na wenye mtiririko, unaeleweka au upo wazi na unabainisha hatua za kuchukuliwa.
2. Mfano maarufu katika AK ni ule wa Nathani nabii alipomkabili Daudi katika **2 Sam 12:1-10** (tazama pia **Waamuzi 9:1-21; 2 Wafamle 14:8-10; 2 Nyakati 25:17-19**). Ingawa simulizi hasa ni habari ya kubuniwa iliyotolewa ili kuelezea ukweli wa kimwili au kiroho, Paulo alitumia habari za Sara na Isaka dhidi ya Hajiri na Ishamaeli (tazama **Mwanzo 17:15-21; 18:9-15; 21:1-21**) kama simulizi kwa wakristo na wayahudi (tazama **Wagal 4:21-31**).
3. Maudhui yenyenye kiini kinachomwunganisha Yesu' ni mifano inayohusu ufalme wa Mungu, ambao upo sasa na utakuwepo baadaye pia. Nguvu ya Mungu inayotenda kazi kwa ufunuo binafsi wa Mungu katika kuumba jamii ya watu wanaomtumikia Yesu katika maeneo yote ya maisha yao" (Blomberg 1990: 326). Ufalme unahusu badiliko la mtu binafsi na la kijamii. Katika mifano yake, "Yesu alikuwa na mambo muhimu matatu ya kusisitiza: neema ya Mungu, mahitaji ya uanafunzi na hatari za kutotii" (Ibid).
4. Yesu alitumia mifano "kupata mwitikio hasi au chanya toka kwa wasikilizaji" (Osborne 1991: 241). Njia mojawapo aliyyotumia kufanya hili ni kubadili matarajio ya watu au kubadilika kwa matukio: "Msamaria aliyechukiwa, siyo kuhani wala mlawi, ndiye aliyefunga vidonda vya aliyejeruhiwa na wanyang'anyi (Luka 10:30-37); kwa kawaida wasamaria siyo waokozi bali wanyang'anyi!); Mwana mpotevu ndiye aliyeandaliali sherehe (Luka 15:11-32); maskini na vilema kuketi kwenye sharehe (Luka 14:15-24); wakili aliyebadili madeni ya bwana wake alisifiwa (Luka 16:1-13). Kwa kufanya hivi Yesu anawalazimisha wasikiaji wake kutazama ukweli wa ufalme wa Mungu kwa namna mpya." (Osborne 1991: 243)
5. Yesu alitumia mifano kwa ajili ya kufunua na kuficha jambo akitazama aina wa wasikilizaji wake (tazama Mat 13:10-17; Marko 4:10-13).
  - a. *Yesu alifunua kwa:* (1) kuelezea jambo kwa namna inayoweza kukumbukwa; (2) kwa kuwaalika watu katika kutafakari zaidi kwa wale amba maana hajifahamika kwao kwa upesi; na (3) kujaribu kuwafanya wasikilizaji wakubaliane na Imani au wafuate matendo fulani.
  - b. *Mifano huficha mambo wakati ambapo:* (1) msikilizaji anaposhindwa kupata maana ya lugha za alama zilizotumika; au (2) hata kama ataelewa maana, msikiaji anapokataa kupokea hitaji la ye ye kubadilika katika maisha yake binafsi. Kwa hiyo, katika **Marko 12:12** viongozi wa kiyahudu walitambua ule mfano wa wakulima waovu uliwhusu wao lakini walikataa kubadili na zao badala yake wakazidisha kwa kumwua ye ye mwenyewe.
6. Yesu aliweka wazi mbili kati ya mifano yake, mfano wa udongo (**Mat 13:1-23; Marko 4:1-20**), na ngano na magugu (**Mat 13:24-30, 36-43**). Ingawa, wakati mwingine Yesu humalizia mfano wake kwa mkazo mfupi (**Mat 20:16; Luka 12:21**) au swali (**Luka 7:42; 10:36**). Mikazo hiyo au maswali hayo hutufahamisha kweli kuu ya mfano huo.
7. Ufunguo wa tasfiri ya mifano ipo katika kutambua matendo ya wahuksika, na alama zilizotumika na kile kinawakilishwa na alama zilizotumika:
  - a. *Kanuni ya msingi ya kutafsiri mfano ni,* "wazo moja kuu linamhusu muhusika mkuu." "Kila mfano huwa na wazo kuu moja kwa muhusika mkuu—mara nyingi huwa wawili au watatu—na hawa wahuksika wakuu katika mfano husimamia jambo fulani badala ya wao wenye, na hivyo hutoa sifa ya mfano kuwa simulizi lenye funzo. . . . Wakati huo huo, yaliyomo mbali na wahuksika wakuu huonyesha alama zinazoashiria maana inayokusudiwa kutolewa na wahuksika wakuu, na tafsiri zote za simulizi zenye mafunzo ni lazima zilete matokeo yaliyokuwa na maana kwa wasikilizaji Wapalestina wa karne ya kwanza." (Blomberg 1990: 163)
  - b. *Wahuksika wakuu huwakilisha namna mbalimbali za ufalme wa Mungu—ujumla zinahusika na Mungu, watu wa Mungu na wale amba si watu wa Mungu.* Mathalan, mfano ule wa mwana mpotevu (**Luka 15:11-32**). Blomberg anautafsiri kama ifuatavyo: "(1) Kama ilivyokuwa kwa mawana mpotevu alivyokuwa na fursa ya kutubu na kurudi nyumbani, vivyo hivyo na wenye dhambi wote, haijalishi kiasi cha uovu wao, wanawenza kutubu na kumgeukia Mungu wao na kujutia. (2) Na kama vile Baba alivyojitoa kumfikia mwana mpotevu na kupatana naye, kwa namna hiyo Mungu huwapa wote, wasiostahili na wasiofaa, msamaha wa dhambi ikiwa wapo tayari kupokea. (3) Na kwa kuwa yule mwana mkubwa hakupaswa kuchukia kitendo cha kupochelewa kwa mdogo wake, badala yake kufurahia, sisi nasi tunaodai kuwa ni watu wa Mungu tunatakiwa kufurahi Mungu anapotoa neema yake kwa wale wasiofaa kabisa."

(Blomberg 1990: 174)

c. *Kiini cha mafundisho ya mifano ya Yesu inahusisha:*

(1) Mafundisho kuhusu Mungu. Mungu ni Mwenyezi. Anawaamuru watumishi wake kama atakavyo. Ni mvumilivu. Anavumilia sana kuacha kuwaharibu waovu ikiwa kuwaharibu wao itawafanya wema waharibike pia. Ni mkarimu na mwenye rehema na kamwe hatuwezi kueleza. Hatoi taji kwa kuzingatia kiwango cha faida. Anakwenda mbali sana kwa kuokoa roho za watu. Amewapa watu wote kazi ya uwakili, na anawahukumu kulingana na uamnifu wao.

(2) Mafundisho kuhusu watu wa Mungu. Wale wamfuatao Kristo ni lazima waandaliwe kuacha kila kinachosimama kuwazuia kuishi kama wanafunzi kwa mioyo yao yote. Wanatambua hawastahili kupata upendeleo wa Mungu. Wanajitoa kuishi maisha ya uwakili, kutii amri za Mungu, na kuonyesha kuhusika na walioonewa na kuteswa. Wanaleta mahitaji yao kwa ujasiri mbele za Mungu. Wasifikiri kuwa wengine hawastahili ukarimu wa Mungu, na ni lazima watambue kwamba kutotii kwao na uaminifu wao unaweza kusababisha upotevu wa haki ambazo zinawahusu. Wanatazama kukua kwa ufalme, na wale watakaovumilia mpaka mwisho watakuwa na ushirika na Mungu milele pamoja na kusanyiko la waaminio wote.

(3) Mafundisho kuhusu wale ambaeo si wa Mungu. Kufanya na kukiri yapasayo kwa Mungu na Kristo haitoshi; maisha yanayodhahirisha matunda ya toba ni lazima yafuate. Nafasi na cheo katika taasisi au dhehebu siyo mbadala wa toba ya kweli na matendo ya rehema. Sasa ni siku ya toba; na hakuna dhambi au uovu ulio mkubwa ambaeo Mungu hataweza kuusamehe ikiwa mtu atatubu kwa moyo wake wote. Visingizio vyote vya kubaki nje ya ufalme vinakosa sababu kabisa. Utafika wakati ambaeo haitawezekana tena kutubu; na wale waliomkataa Mungu watakataliwa na kutengwa na Mungu milele na kila kitu kizuri. (Blomberg 1990: 293-96).

d. *Miundo ya mifano ya Yesu.*

(1) Kumi na moja kati ya mifano ya Yesu ipo katika miundo mitatu. Ina wahusika wakuu watatu ambaeo kutoka kwao masomo matatu yaweza hupatikana; wahusika wanahusisha mkuu na washirika wawili wanaopingana au kutofautiana, wanaomwakilisha Mungu, watu wake, na wale wanaomkataa yeye. Haya yanahusisha: *Mwana mpotevu (Luka 15:11-32); Kondoo aliyepotea (Luka 15:4-7); Shilingi iliyopotea (Luka 15:8-10); Wadeni wawili (Luka 7:41-43); Wana wawili (Mat 21:28-32); Mtumishi mwaminifu na asiye mwaminifu (Luka 12:42-48; Mat 24:45-51); Wanawali kumi (Mat 25:1-13); Ngano na magugu (Mat 13:24-30, 36-43); Juya (Mat 13:47-50); Tajiri na Lazaro (Luka 16:19-31); na watoto sokoni (Mat 11:16-19; Luka 7:31-35).*

(2) Kumi kati ya mifano ya Yesu husisitiza mambo makuu matatu. Ingawa zinaonekana kuwa na wahusika zaidi na yenye mfumo tata zaidi kuliko mifano kumi moja hapo juu, lakini hatimaye zinafunua kweli kuu tatu zinazohusika na wahusika watatu au vikundi vya wahusika. Hii inahusisha: *Mfano wa talanta (Mat 25:14-30; cf. Luka 19:12-27); Wafanyakazi katika shamba la mizabu (Mat 20:1-16); Udango (Mat 13:1-23; Marko 4:1-20); Msamaria mwema (Luka 10:25-37); Karamu kuu (Luka 14:15-24; cf. Mat 22:1-14); Mtumishi asiyesamehe (Mat 18:23-35); wakili mbaya (Luka 16:1-13); na Wakulima wabaya (Marko 12:1-12).*

(3) Tisa kati ya mifano ya Yesu ina misisitizo miwili. Ina wahusika wakuu wawili na ina mambo mawili tu inayoelezea na masomo mawili. Inawezekana isiwe na mtu mkuu au bwana mmoja na mshirika mmoja. Hii inahusisha: *Mafarisayo na watoza ushuru (Luka 18:9-14); Wajenzi wawili (Mat 7:24-27; Luka 6:47-49); Mtumishi asiye na faida (Luka 17:7-10); Mbegu inayokua kwa siri (Marko 4:26-29); Tajiri mpumbavu (Luka 12:16-21); Mtini usiozaa (Luka 13:6-9); Kadhi dhalimu (Luka 18:1-8); Rafiki usiku wa manane (Luke 11:5-8); na mwenye nyumba na mtawala (Mat 24:43-44; Luka 12:39-40).*

(4) Sita kati ya mifano ya Yesu ina muhusika mmoja na inafundisha jambo moja. Inahusisha: *Hazina iliyositirika (Mat 13:44); Lulu yenye thamani kubwa (Mat 13: 45-46); Punje ya haradali (Luka 13:18-19); Mbingu (Luka 13:20-21); Mjenzi wa mnara (Luka 14:28-30); na mfalme vitani (Luka 14: 31-32).*

Nyaraka ni barua zilizoandikwa kwa makanisa maalumu au kundi la makanisa au watu binafsi. Kuna barua za “msimu”, hii ina maana ziliandikwa kutokana na, na zinashughulika na, tatizo maalumu au hali iliyotokea kwao wakati huo.

1. Nyaraka za karne ya kwanza kimsingi zilianza na “utangulizi” uliopo kwenye muundo wa salamu za kutoka A, hadi B.” Waandishi wa biblia mara kadhaa walikuza hizi salamu. Nyaraka ziliandikwa kuhusu mambo ambayo ni mahitaji na yanatarajiwa kueleweka kwa wasomaji. **Ufunuo 1:4** ni utangulizi wa kinyaraka, na hiyo inaonyesha kwamba kitabu cha Ufunuo ni waraka na pia ni unabii (**Ufunuo 1:3; 22:18**). Hii ina maana kitabu cha si tu kwa ajili ya unabii wa wakati ujao “nyakati za mwisho,” miaka elfu moja mbele, lakini inahusika na wakati wa sasa pia. Pia mafumbo yake yalitegemewa kufahamika na watu wa karne ya kwanza (tazama pia **Ufunuo 22:7**).
2. Nyaraka ni maandiko ya msingi yanayofundisha. Hayafundishi tu yale yatupasayo kuamini, bali kwanini tuamini, na jinsi ya kufanya kazi yale tunayoamini. Nyaraka kwa njia nyingi zina “mpangilio” au zimeegemea kwenye mijadala ya kiufahamu na yenyen mantiki kuliko maandiko mengine. Ingawa mpangilio siyo mzuri sana, si wa kimantiki sana na kazi za theolojia. Badala yake zinabeba mambo yaliyopo katika maandiko mengine pia.

## V. Kanuni za eksejesia za kutafsiri kifungu cha Biblia

Kanuni hapo juu ya kutafsiri Biblia hutumika wakati mtu anataka kuelewa na kutafsiri maandiko. Hii sehemu inaanza kwa kuelezea jinsi kanuni hii inavyotumika kuchambua na kutafsiri kifungu cha Maandiko.

### A. Mambo ya msingi ya kuzingatia katika mchakato wa eksjesia

1. Anza kwa maombi, na uendelee katika hali ya maombi wakati wote wa kusoma, kujifunza na kutafuta kuelewa kifungu cha maandiko. Kumbuka 1 **Wakor 2:12-14:**<sup>12</sup> *Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.*<sup>13</sup> *Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwana Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*<sup>14</sup> *Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokeimambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.*
2. Ruhusu Biblia iseme na wewe wala wewe usiiongoze. Hii ina maana kwamba jiepushe na wazo linalobuka kabla kuhusu kile ambacho “kinalazimisha maana” ya kifungu. Ni lazima tukatae “kujipanga upya katika kuchunguza” ili tuendane na theolojia inayokubalika. Ni lazima kuheshimu hekima ya walimu wa Biblia na wanazuoni. Sauti ya ndani inaweza kuchangia uelewa. Pamoja na hayo, Neno la Mungu husema nasi, katika mazingira yetu leo. Kwa hiyo, ni lazima tusikie yale Mungu anayosema nasi hata pale ambapo (au hasa hasa) inatupa changamoto au tunapochomwa moyo. “Ikiwa ‘tunajua’ kile ambacho ni *lazima* kisemwe na kifungu, na kuruhusu hicho kitawale uchunguzi wetu, tutawezaje kujifunza kile ambacho *husemwa?* Kama tumejitoa sana kwenye theolojia fulani, inakuwa vigumu kusahihisha chochote katika kile tunachojuwa ambacho si sahihi. Inakuwa ngumu, ngumu kujifunza jambo jipy. Hatimaye, ikiwa tutakataa Biblia iseme nasi, mfumo wetu wa theolojia unakuwa *utamaduni* ambao mamlaka yake huwa juu ya ile ya Biblia yenyewe.” (Doriani 1996: 17)
3. Jihadhari na utamaduni na desturi zako unapokabili kifungu cha maandiko. Pamoja na mtazamo wetu wa kitheolojia, huwa tunachukulia kiraishi tamaduni zetu na desturi—tunazichukulia kama “haki” na “kawaida”. Mara nyingi hatutambui jinsi amabavyo desturi na tamaduni zetu zinavyoathiri namna yetu ya kufikiri na kutazama mambo. Kwa namna nyingi Biblia ipo kwa ajili ya kurekebisha vile tunavyofikiri na kutenda. “Tamaduni ni hatari ikiwa (1) mara moja tunapingana na kitu kama kinaonekeana kuwa kinyume nazo, (2) kwa haraka tunatafsiri kila wazo jipy kwa namna ambayo itakubaliana na tamaduni zetu, au (3) tumejizamisha sana kwenye utamaduni wetu kiasi kwamba hatuwezi kuuona tena” (Doriani 1996: 25). Tunahitaji Mungu atubadilishe kwa Neno lake, kuliko “kurekebisha” Neno lake kuendana na tamaduni zetu, desturi zetu, yale tunayoyapenda na tusiyoyapenda na matarajio yetu.

### B. Eksejesia sahihi na uelewa wakifungu chochote cha Biblia unazingatia vipengele vitatu—uchunguzi; tafsiri; na matumizi

Uchunguzi, kutafsiri, na matumizi, zinatambulika kama sehemu tofauti tatu za tafsiri ya kina ya Biblia. Uchunguzi *kimantiki* huwa kabla ya kutafsiri na matumizi. Ingawaje kiuhalisia haya matatu huingiliana kwa kiwango cha juu sana.

1. Uchunguzi unajibu swalii; “Kifungu hiki kinasemaje?” Uchunguzi ni msingi ambao unakiwa kuuweka ikiwa unataka kutafsiri na kutenda kazi Biblia. Tafsiri sahihi na matumizi sahihi ya Biblia inategemea

uchunguzi sahihi.

2. Tafsiri inajibu swali “Kifungu hiki kina maana gani?” Tafsiri nyingi zitakuwa wazi ikiwa mtu atachunguza kwa makini kifungu kilikuwa kinasema nini kutokana muktadha wake. Huwezi kuelezea maana ya kifungu ikiwa kwanza hujafahamu kinasemaje. Unapoelezea kifungu hakikisha maelezo yake yanaendana na uchunguzi wako.

3. Matumizi yanajibu swali “Ni kwa namna gani maana ya kifungu inatumika kwangu (na wengine) leo?” Matumizi “yanaanza pale ambapo umepambanishwa na kweli na ukaamua kuitikia kwa utii kwenye kweli” (Arthur 1994: 11).

### C. Kuelewa muktadha

*Kama Tulivyosema hapo kabla muktadha ni ktu cha muhimu sana katika kuelewa kifungu chochote cha maandiko.* Muktadha maana yake ‘kile kinachoenda samabamba na kifungu cha maandiko.’ Kumbuka kuna *aina mbili za muktadha unaoathiri kifungu chochote: muktadha wa kifasihi na muktadha wa kihistoria.* *Muktadha wa kifasihi* ni maneno, sentensi, aya, au sura zinazozunguka au kuhusiana na kifungu husika. *Muktadha wa kihistoria* ni tamaduni, desturi, lugha, imani, na historia ya mwandishi na ya hadhira yake ya kwanza. Wakati unasoma, utagundua kwamba muktadha wa kifasihi na wa kimazingira huenda pamoja kama mapacha.

1. Pata mtazamo wa jumla wa kitabu ambacho kinabeba kifungu chako. “Kwa sababu mwandishi anatoa ujumbe wake kwa ukamilifu katika kitabu kimoja, uchambuzi wetu wa maana ya kifungu kimojawapo ni lazima uwe katika muktadha wa kitabu amacho kinabeba kifungu hicho” (Volvaardt 2005: 90). Fuata mtiririko wa mawazo ya mwandishi kadiri yanavyojijenga tangu mwanzo hadi mwisho wa kitabu. Kupata mtazamo wa jumla wa kitabu ni kazi inayohitaji juhudhi hasa. Kuelewa kitabu kwa ujumla wake inafanya kutafsiri kitabu kuwa rahisi zaidi.

2. Mtazamo wa jumla lazima uhusishe muktadha wa kihistoria na wa kifasihi. Mtazamo wa jumla ni lazima uhusishe muktadha wa kihistoria (k.m., mwandishi alikuwa nani; nani waliandikiwa; uhusiano kati ya waandikiwa na mwandikaji; kitabu kiliandikwa lini; kwa nini kitabu kiliandikwa), na muktadha wa kifasihi. Kuhusu muktadha wa kifasihi na “mtiririko” wa kitabu, zingatia zaidi visehemu na aya zinaelekewa kwenye kifungu unachokihitaji, na zile zinazofuata mara baada ya kifungu hicho unachoshughulika nacho.

3. Tambua jinsi kitabu kilivyopangiliwa. Vitabu vingi vya Biblia vimegawanyika katika sehemu kubwa ambazo zinaweza zisiendane na mgawanyo wa sura. Kunakuwepo na visehemu ndani ya sehemu moja kubwa. Kadiri unavyozidi kujifunza kitabu, ndivyo unavyoolewa mantiki ya kitabu na ya mgawanyo wa kitabu kifasihi katika visehemu na sehemu. Kutambua jinsi kitabu kilivyoundwa katika visehemu tofauti tofauti inasaidia kuelewa maudhui makuu ya kitabu na kusudi. Kutambua maudhui hayo na jinsi mwandishi alivyojenga mawazo yake ni kazi ya msingi ya mtafsiri.

a. *Kitabu kinaweza kugawanywa katika sehemu nyingi kwa kuzingatia mambo mengi.* Sehemu zinaweza zikawa kwa sababu ya somo, fundisho, wahuksika wakuu, matukio makuu, wafalme wanaotawala, tarehe, maeneo, nk. Kwa mfano, **Mwanzo 1-11** imejikita katika matukio ya kiulimwengu, lakini katika sura hizo kuna migawanyiko inayohusu uumbaji, kuanguka dhambini kwa mwanadamu na hukumu ya Mungu, gharika, na mnara wa Babeli, **12-50** inaelezea watu fulani maalumu—Ibrahimu na uzao wake—lakini katika sura hizo kuna migawanyo kuhusu Ibrahimu na agano alilofanya Mungu na yeye, Isaka, Yakobo, na Yusufu. Nyingi ya nyaraka za Paulo zinaanza na msisitizo wa kimafundisho, na zinaishia na msisitizo wa kivitendo (k.m., **Warumi 1-11** kimsingi ni mafundisho; **12-16** ni za kivitendo; **Wagalatia 1-4** kimsingi ni za kimafundisho; **5-6** ni za kivitendo).

b. *Muundo wa kitabu kimoja kimoja huwakilisha mtindo maalumu wa maana anayowasilisha mwandishi.* Kwa hiyo, mahali kifungu cha maandiko kilipo pia ina umuhimu. Unaweza ukajiuliza (kama sababu za kuwepo hazipo wazi), “Kwa nini kifungu hiki kipo hapa, na si mahali pengine?” Mifano mitatu inayoonyesha umuhimu wa mahali kifungu kilipo:

(1) Habari za Yuda na Tamari katika Mwanzo 38 yaweza kuwa si mahali pake kwani **Mwanzo 37-50** huongelea habari za Yusufu. Ingawa kuwekwa kwa habari hizo hapo ni kuonyesha tofauti za kimwenendo, za Yuda na uzao wake na Yusufu, aliyekimbia uchafu kwa habari inayomhusu mke wa Potifa (**Mwanzo 39:7-12**).

(2) Habari za ukarimu wa Daudi kwa Mefiboshethi katika **2 Samweli 9** ikitokea katika **2 Samweli 6-10** inayomwelezea Daudi akitawala huku akidumisha wema, uchumi, na uwezo wa kijeshi. Tendo la Daudi kwa Mefiboshethi linaonyesha wema. Kuanguka kwa ufalme unaanza katika **2 Samweli 11**. Kuanguka kunaonekana pale Daudi

anapoamua kwa haraka kubatilisha ukarimu wake kwa Mefiboshethi (**2 Sam 16:1-4; 19:24-30**).

(3) Mfano wa Mwana mpotevu (Luka 15:11-32) unajipatia nguvu kutokana na mahali ulipo. **Luka 15** inatoka katika sehemu kubwa ya kitabu amabapo Yesu anaelekea Yerusalem (**Luka 9:51-19:28**). Mara kadhaa Yesu anaulizwa maswali na mafarisayo Katika **Luka 15:2** mafarisayo wanalamika kuwa Yesu anawapokea na kula na wenye dhambi. Hivyo Yesu akatoa mifano mitatu (kondoo aliyepotea, shilingi iliyopotea, na mwana mpotevu), yote hiyo ikijibu malalamiko ya Mafarisayo. Yote inaongelea mtazamo wa Mungu kuhusu waliopotea. Mfano wa mwana mpotevu ni kilele. Unawahuisha mafarisayo wenywewe. Kaka mkubwa katika mfano wa tatu uliwawakilisha mafarisayo. Yesu anawapa changamaoto “wawakaribishe wenye dhambi ili wajiunge na ufalme” (Doriani 1996: 36), wasiachwe nje wakati wengine wanapokelewa na Baba.

4. Tambua kusudi la mwandishi na dhumuni/madhumuni la/ya jumla la kitabu. Kabla hujajikita katika aya moja au mstari unahitaji kuelewa jinsi aya hiyo inavyoingia katika kusudi na maudhui ya kitabu na sehemu ya kitabu ambacho aya hiyo inapatikana. Kumbuka: mazingira hufunua maana ya maneno na mistari. Jaribu kueleza maudhui ya kitabu, sehemu na kifungu kwa maneno yako mwenywewe. Uwazi wa mtiririko au muunganiko unahusiana na uwazi wa mawazo na uelewa. Kuweza kueleza kwa uwazi dhumuni kwa maneno yako kutasaidia kujua dhumuni. Kushindwa kuelezea dhumuni inadhihirisha kukosa ufahamu sahihi kuhusu dhumuni, maana unayotakiwa kusoma, kujifunza, kutafakari kitabu, sehemu, au kifungu. Katika kufanya hivyo, maombi, itifaki nzuri, kamusi na vyanzo vingine, inaweza kuwa na msaada sana. Vipo vitu kadhaa vinaweza kusaidia kuona kwa wazi kusudi la mwandishi na dhumuni la kitabu, sehemu ya kitabu au aya:

a. *Maelezo yaliyo wazi ya mwandishi kuhusu kusudi, au dhumuni la kitabu, sehemu ya kitabu au aya.*

(1) Mara zote mwandishi ataeleza kwa wazi kwa nini anaandika. Maelezo hayo yanweza kuwa utangulizi mwanzoni mwa kitabu, inaweza kuwa hitimisho la kitabu, au maelezo yenye msisitizo mkubwa katikati ya kitabu. Kwa mfano katika **Luka 1:1-4** Luka anatueleza kwa nini anaandika Injili; **Yuda 3** anatueleza sababu ya Yuda kuandika waraka wake; **Yoh 20:30-31** anaandika kwa ufupi kwa nini Yohana anaadika Injili; na **1 Tim 3:15** inaeleza kwa nini Paulo anamwandikia Timotheo.

(2) Wakati mwingine mwandishi anaweza akatoa maelezo ya kisehemu kidogo kwenye kitabu au anweza kuelezea alichomaanisha mtu mwingine. Kwa mfano, katika **Yoh 2:21** Yohana anatueleza kwa wazi alichomaanisha Yesu aliposema, katika **Yoh 2:19**, “*“Livunjeni hili hekalu nami nitalijenga kwa siku tatu.*” Katika **Marko 7:19** Marko anatueleza lile alilomaanisha Yesu lililofunuliwa katika **Marko 7:14-19** ambalo lingekosekana. Mwishoni mwa **Yoh 4:9** Yohana anaongezea mawazo yake kuwaelewasha wasomaji wake (ambao kimsingi ni mataifa, siyo wayahudi [au wangeelewa bila maelezo]) kwa nini mwanamke msamaria aliuliza maswali ambayo aliyaauliza.

b. *Maelezo yenye dhumuni yaliyotolewa, au yaliyofupisha, kilichochopo kwenye kitabu, sehemu au aya.* Wakati mwingine mwandishi anaweza asiandike dhumuni la kuandika kitabu, au kutafsiri maana ya alichoeleza. Ingawa, kitabu kinaweza kuwa na maelezo ambayo huendelezwa, au yanayofupisha kile kilichosemwa kabla. Wakati mwingine maelezo yanaweza kuishia na wazo moja au kuhamia kwenye wazo lingine. Katika hali hiyo, angalia mstari wa msingi unaolezea vizuri au unaotoa ufupisho wa dhumuni la mwandishi. Kwa mfano, **Mwanzo 1:1** inasema, “*Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.*” Hayo maelezo yanatoa utangulizi na kutoa ufupisho wa simulizi la uumbaji katika kitabu cha **Mwanzo 1-2. Waamuzi 17:6** na **21:25** yote husema, “*Siku hizo hakukuwa na mfalme katika Israeli; kila mtu alifanya kila alichooma vema machoni pake mwenywewe.*” Maelezo hayo hutoa ufupisho wa kuanguka kwa Israeli baada ya kifo cha Yoshua. Katika kipindi cha Waamuzi hakukuwa na mfalme wa wa kimwili lakini kwa umuhimu zaidi hawakuwa na mfalme wa kiroho. Kwa hali hiyo, Ingawa taifa lilipaswa kuwa na Bwana kama mfalme wake. (tazama **Waamuzi 8:23**), hawakumtii Bwana. Matokeo yake, ikadorora katika vita vyake na adui zake (**Waamuzi 1**) hadi vita vya kikabila vya wao kwa wao (**Waamuzi 20-21**). **Yakobo 1** inaeleza mfululizo wa madhumuni makuu ya kitabu. **Yak 1:26-27** inafafanua juu dini ya kweli, na jambo ambalo limefanuliwa kwenye kitabu kizima.

c. *Mawazo muhimu, masomo, maneno na misemo huonyesha dhumuni la kitabu, sehemu na kifungu.* Angalia mtiririko wenyenye mantiki wa mawazo ya mwandishi. Jiulize “hili limeendelezwaje?” Hata pasipo maelezo ya wazi ya kusudi, au maelezo ya wazi ya maudhui, maneno muhimu na semi (ambazo mara nyingi zinarudiwa rudiwa) zinafunua mawazo muhimu au masomo ambayo yanafunua dhumuni la mwandishi.

5. Faida za mtazamo wa jumla wa kitabu chenye kifungu husika.

- a. Unaona ujumbe wote wa kitabu katika ujumla wake.
- b. Unapata ufahamu kuhusu kusudi la mwandishi kuandika.
- c. Unatambua dhumuni kuu la kitabu.
- d. Unatambua muundo wa kitabu.
- e. Unaelewa jinsi kila kifungu kinavyohusiana na kingine na kitabu kwa ujumla.
- f. Unakuwa na msingi unaoeleweka wa tafsiri sahihi na matumizi sahihi (Arthur 1994: 26)

6. Pata mtazamo wa jumla wa kifungu unachojifunza. “Jambo gumu sana kwa mwongofu mpya ni kujifunza kuchambua kwa undani kila aya na kupata muhutasari wa mawazo makuu katika aya. Watu huonekana kuvutia sana na usafanuzi wa kina siyo kupita juu juu. Tunahitaji mtazamo wa jumla hapo, na mwanafunzi anatakiwa kujaribu kuandika muhutasari wa maneno sita hadi nane kwa kila aya. Tunaposoma aya kwa kina sana, maelezo ya muhutasari mara nyingi hurejea sentensi za mwanzo katika aya zaidi kuliko aya nzima. Kosa hilo linaweza likaharibu matokeo ya mafunzo yote.” (Osborne 1991: 23) Osborne anatukumbusha, ijapokuwa, “huu ni mtazamo wa mwanzo unaweza kubadilika ikiwa tafsiri ya kina itafanyika na kukidhi haja” (Ibid.: 24-25).

7. Kufahamu muundo wa sentensi na kifungu ni muhumu sawa na kujua muundo wa kitabu na sehemu. Inasaidia mara nyingi kutengeneza *jedwali au mchoro* au kutumia *rangi* ili kuweka alama kwa ajili kuweka wazi uhusiano uliopo katika sehemu za sentensi, au kifungu, ili kufahamu kitu gani kinafafanua kingine. Kipekee hii inasaidia sana unapoifunza maandiko ya Paulo, kwa kuwa yeche mara nyingi ametumia sentensi ndefu na zilizo ngumu kuelewaka. Mifano mitatu huonyesha hili kama ifuatavyo:

- a. ***Warumi 5:12*** *huweka hitimisho la mtiririko wa wazo* (neno “*Kwa hiyo*” *hudhahirisha hilo*). Mstari pia huanza na nusu ya kwanza ya ulinganisho (maneno “na kwa kuwa kwa mtu mmoja dhambi ililingia” inaonesha kuwa Paulo analingana hilo na kitu kingine zaidi, kwa kutumia maneno kama “*kwa hiyo pia*” au “*kisha baadaye*” [ambayo kimsingi inakamilisha “*kwa hyo*”]). Hata hivyo, Paulo hafanyi ulinganisho kwa haraka, lakini anaanza na kufafanua ubaya wa dhambi. Haelezi wazo lake la msingi na ulinganisho hadi sura ya **5:18** (“*kwa kuwa kupitia kosa moja*”).
- b. ***Waef 2:11-22*** *inaanza na kuelezea wazo ambalo Paulo anajadili alichofanya Yesu ili kuondoa tofauti kati ya Wayadi na mataifa wale walio katika Kristo kwa “kumwumba mtu mpya.”* **2:11-12** inaelezea hali ya awali ya mataifa. Msemo “Lakini sasa,” unaoanzia **2:13**, inalinganisha na hali ya sasa ya mataifa, kwa ajili ya matokeo ya damu ya Yesu. **2:14-22** yote hiyo inaboresha na kuelezea **2:13—2:14-18** inaelezea alichofanya Yesu; na **2:19-22** inaelezea kile anachofanya Kristo (**2:19** huanza, kwa vitendo, alipoishia **2:13**).
- c. ***Waef 3:1-19*** *anaendeleza mawazo yake kuhusu mataifa.* **3:1** inaanza hivi “*Kwa kusudi hili*,” ambayo inarejea yale aliyokuwa akijadili kabla. Ndipo **3:2-13** inaenda mbali sana na mtiririko wa mawazo yake; Paulo hakurejea tena katika mfululizo wa mawazo yake makuu hadi sura ya **3:14**.

**D. Andika dondoo za kitabu, sehemu na kifungu cha maandiko**

1. Njia bora ya kuelewa mtiririko wa kimantiki wa mawazo ya kitabu, sehemu ya kitabu au kifungu cha maandiko ni kuchukua dondoo na kuandika kwenye karatasi. Kuchukua dondoo kutasaidia “tuone” jinsi kitabu, sehemu ya kitabu, au kifungu kilivyopangiliwa. Kuandika dondoo kutasaidia usahihi wa mawazo na uelewa wetu kwa kujilazimisha kukabiliana na kitabu au sehemu ya kitabu au kifungu cha maandiko katika kitabu hicho na kujua anachosema mwandishi na jinsi sehemu hizo zinavyohusiana kwa pamoja. Katika kuandika dondoo za kitabu tutapata uelewa mzuri kwa sababu katika kufanya tutatumia *maneno yetu wenyewe* kuandika orodha ya mawazo yaliyopo katika kifungu cha Biblia.
2. Biblia nyingi zina vichwa vyta masomo ambavyo vimewekwa na wahariri. Itifaki nyingi zinapendekeza dondoo za kitabu, sehemu, na vifungu. Hizo zinaweza kuwa za msaada. Ingawaje, kama ukiangalia matoleo tofauti tofauti ya Biblia na itifaki tofauti tofauti utagundua kuwa zinatofautiana kidogo katika kupangilia sehemu na visehemu katika kitabu. Hutakiwi kufuata tu alichosema mtu mwingine unatakiwa kutafuta wewe mwenyewe.

3. Unawenza kuchukua dondo kwa ufupi au kwa kirefu. Kitu cha muhimu ni kupata mtiririko wa mawazo wa kimantiki wa mwandishi. Kanuni za msingi za kuchukua dondo ni:

- a. *Wazo kuu la kifungu* huwa mada kuu katika dondo.
- b. *Mgawanyo wa dondo* katika visehemu utafanua, utaeleza, utatoa mifano, au utaeleza kwa kina zaidi sehemu zilizotangulia (tazama Arthur 1994: 119-28).

#### E. *Soma kwa njia ya kujiuliza maswali*

Unapojifunza kifungu cha maandiko na mazingira yanayozunguka, zingatia muktadha kifasihi na wa kihistoria/ kitamaduni kwa kina . “Chukua kila dondo kwa kina hasa sababu inayobuka na jambo maalumu” (Doriani 1996: 18). Jiulize maswali (lipi linahusiana na mazingira halisi ya kifasihi au lipi ni la kihistria au la kitamaduni katika kifungu). Yatasaidia kuelekeza fahamu zako kuelewa:

1. Nani?—k.m., Nani aliandika? Wahuksika ni akina nani? Mwandishi anaongea na nani? Anaongea kuhusu nani?
2. Nini?—k.m., Hii ni aina gani ya uandishi? Nini kinaendelea hapa? Matukio makuu ni yapi? Madhumuni na mafundisho makuu ni yapi? Mwandishi anasisitiza nini?
3. Lini?—k.m., Iliandikwa lini? Matukio haya ni ya lini? Yatatokea lini?
4. Wapi?—k.m., Hili lilifanyika wapi? Hili lilisemwa wapi? Litatokea wapi?
5. Kwa nini?—k.m., Kwa nini hili limeandikwa? Kwa nini hili jambo limetajwa? Kwa nini nafasi iliyotolewa kwa ajili ya tukio au fundisho ni kubwa au ndogo? Kwa nini watu hutenda kwa namna fulani inayofanana?
6. Kwa namna gani?—k.m., Ni kwa namna gani jambo hutokea? Ni kwa namna gani ukweli huu huelezwa? Watu wanapaswa kufanya jambo hili kwa namna gani?

#### F. *Zingatia maelezo ya kina ya kihistoria na ya kitamaduni*

1. Maelezo ya historia na ya kitamaduni yatasaidia kuangaza kifungu cha maandiko. Maelezo ya kina ni muhimu ikiwa habari inaweza kusimama bila hiyo. Maelezo ya kina hayana maana kama hayachangii chochote katika kifungu hicho. Inawezekana isifahamike kwa haraka umuhimu wa maelezo ya kina ya kihistoria na ya kitamaduni. Hilo linaweza lisieleweke kwa haraka jinsi ilivyo muhimu kuwa na maelezo ya kina ya kihistoria na ya kitamaduni katika kutafsiri kifungu.

2. Kwa mfano, katika Wagal 2:11-13, Paulo anaeleza jinsi alivyompinga Petro ana kwa ana walipokuwa Antiokia kwa kukataa kula na mataifa walioamini, na kwamba hata Barnaba alichukuliwa na unafiki. Kwa upande mmoja haijalishi tukio limetokea wapi kwa kuwa kinachoelezewa ni fundisho la ukristo na jinsi wanavyopaswa kuenenda ambayo inafanana kila mahali. Kwa upande mwingine historia inapata umuhimu tunapokumbuka kuwa waamini wa kiyahudi walifika Antikio kwa sababu ya kukimbia mateso ya kanisa (**Matendo 11:19**). Juu ya hayo, kanisa la Yerusalemu lilimpeleka Barnaba Antiokia walipojifunza kuwa mataifa wengi wanamjilia Bwana. Barnaba alifurahi na akaja na Paulo hadi Antiokia. Wote wawili waliwatia moyo na kuwafundisha waongofu wapya wa (mataifa) huko. (**Matendo 11:22-26**). Wanafunzi waliitwa kwa mara ya kwanza “wakristo” kule Antiokia (Matendo 11:26). Waaminio wa mataifa walituma michango yao kuwasaidia waaminio wa Kiyahudi, waliopo Uyahudi waliokuwa wakiteseka na njaa. (Matendo 11:27-30). Hapo ndipo maelezo ya kina ya historia yahusuyo unafiki wa Petro na Barnaba yanapopata umuhimu wa ziada. Inaongezea jinsi ilivyo aibu na kuumiza kukataa kula na waamini wanaotoka katika tamaduni na maeneo tofauti.

#### G. *Zingatia mambo halisi yaliyopo kwenye kifungu*

*Mtazamo wa kifasihi ni wa muhimu sana katika kuelewa maana ya kifungu.* Hilo lina umuhimu kwa ajili ya mtazamo wa jumla kuhusu kitabu na unapojifunza kifungu kwa kungalia vifungu vyta karibu vinavyofuata.

1. Wazo la msingi. Maneno ya msingi na misemo ni muhimu katika kuelewa dhumuni kuu na mambo ya muhimu kujuu katika kitabu cha Biblia au kifungu cha maandiko. Hata hivyo, maneno ya msingi ni muhimu kwa sababu yanatuelekeza kwenye wazo la *msingi au somo*. Ni lazima tuwe makini kutofautisha kati ya *neno* la kibiblia na *wazo* au *maneno* yanayotumika kutoa ufanuzi. Hivyo, badala ya kujikita katika kutafuta “maana ya neno” tufikiri kuhusu “kujifunza maana.” “Maana fulani inaweza kuelezwaa kwa kutumia maneno tofauti tofauti. Ikiwa tutajikita katika “maana ya neno” kwa kuchambua neno hilo pekee katika biblia nzima, tunaweza kabisa kuishia kuweka pamoja kondoo na mbuzi tukidhani ni kitu kimoja! Kwa kuongezea, tunaweza kabisa kukosa baadhi ya mafungu ambayo yanaelezea somo kwa maneno mengine.” (Wolvaardt 2005: 62)

- a. *Mifano miwili huelezea umuhimu wa kujua wazo na si maneno pekee:*

(1) Tunapojifunza wazo la “kuzaliwa mara ya pili,” Useni huo unapatikana mara tatu tu

katika Biblia: Yoh 3:3, 7; na 1 Pet 1:23. Ingawa, somo la kufanywa upya kwa mwamini linapatikana katika maeneo mengine mengi, lakini kwa maneno mengine yanayoelezea wazo hilo. Hivyo, mwamini anaitwa “kiumbe kipyä” (**2 Wakor 5:17; Wagal 6:15**), “walioumbwa ndani ya Kristo” (**Waef 2:10**), “waliozaliwa na Mungu” (**1 Yoh 2:29; 3:9; 4:7; 5:1**), “waliouanganishwa na Kristo” (**Warumi 6:5**), nk. (2) Vile vile, Biblia inatumia maneno kadhaa tofauti kuelezea wazo la “fedha”—k.m., “mali,” “utajiri,” “Mammoni,” na “fedha.” **2 Wakorintho 8-9** tunaona mazungumzo ya Paulo marefu kuliko yote kuhusu kutoa “fedha”, lakini hakutumia tena neno fedha.

b. Kutofautisha kati ya wazo na neno linalofanua wazo hilo linatuwezesha kelewa kwa kina zaidi. Hakuna neno moja peke yake linaloweza kutoa maelezo kamili ya wazo, lakini maneno yote kwa pamoja hufanya hivyo. Kwa mfano fikiria wazo la “wokovu.” Biblia inatumia maneno mbalimbali kuelezea kile kilichokamilishwa na msalaba wa Yesu kwetu; yote kwa pamoja yanatoa maana hiyo:

- (1) “Damu; mwankondoo, dhabihu” ni lugha za matoleo ya AK. Inaonyesha kuwa sisi tulikuwa na hatia lakini sasa tumesamehewa.
- (2) “Upanisho; kuletwa karibu” ni lugha za mahusiano binafsi. Huonyesha kwamba sisi tulitengwa na Mungu na kwamba sasa tumerejeshwa katika uhusiano wa karibu na yeze.
- (3) “Dabihu” ni lugha ya kanuni ya utakaso (nayo ni., njia ambayo kwayo ukombozi ulipatikana). Huonyesha kwamba tulikuwa kwenye hasira takatifu ya Mungu, lakini sasa hasira imeridhishwa.
- (4) “Ukombozi; fidia” ni lugha ya sokoni. Inaonyesha kwamba sisi tulikuwa watumwa, lakini sasa tumewekwa huru.
- (5) “Kuhesabiwa haki” ni lugha ya mahakama. Inaonyeha kwamba sisi tulishahukumiwa adhabu lakini sasa tumetolewa na kuhesabiwa kuwa wenye haki.
- (6) “Ushindi; kufunguliwa; kuokolewa” ni lugha za uwanja wa vita. Huonyesha tulikuwa tukikabiliana na adui wenye nguvu, lakini tumekombolewa na tu washindi ndani ya Kristo.

2. Semi na maneno ya msingi. Maneno ya msingi na semi ni zile/yale yaliyo muhimu katika kuelewa maana ya kifungu. Na kama yakiondolewa maana ya kifungu inakuwa imeondolewa. “Ni muhimu kwamba utazame maneno na semi za msingi kwa sababu yanafunua ujumbe aliokusudia mwandishi, msisitizo na jinsi atakavyofikia lengo lake” (Arthur 1994: 37). Wekea maanani kile ambacho sura yezewa husema kuhusu neno la msingi au usemi. Kwa mfano, **2 Timotheo 1** inatoa orodha ya mambo ya kweli kuhusu neno la msingi yaani “Mungu”:

a. Mungu alimfanya Paulo mtume kwa mapenzi yake ( <b>v.1</b> )	f. Mungu hatoi roho ya woga ( <b>v.7</b> )
b. Mungu hutoa neema, rehema na amani ( <b>v.2</b> )	g. Mungu hutoa roho ya uweza, upendo, na utii ( <b>v.7</b> )
c. Mungu ni baba ( <b>v.2</b> )	h. Mungu nguvu ya mateso ( <b>v.8</b> )
d. Mungu anashukuriwa na kutumikiwa ( <b>v.3</b> )	i. Mungu hutuokoa ( <b>v.9</b> )
e. Mungu hutoa vipawa ( <b>v.6</b> )	j. Mungu alituita ( <b>v.10</b> )

3. Kurudiwa kwa maneno, semi na mawazo. Kimsingi ikiwa neno, usemi, au wazo likirudiwa, limerudiwa ili kusisitiza umuhimu wake. Kwa hiyo, udhihirisho kwamba neno, usemi au wazo ni muhimu ni kwamba limerudiwa.

- a. Kuridiwa kwa neno muhimu au usemi inaweza kutokea kwenye kifungu, sura, sehemu, au kitabu kizima. Kwa mfano, katika **1 Yohana** maneno “upendo,” “dhambi,” “kaeni,” na “fahamu” yamerudiwa kwenye kitabu chote, lakini “ushirika” limerudiwa katika sura ya 1 tu.
- b. Kutambua ni maneno gani na semi ambazo zimerudiwa ni muhimu katika kufahamu ujumbe mkuu wa kifungu au kitabu. “Kwa kadiri neno linavyorudiwa, ni kadiri inavyozidi kuwa wazi kwamba neno hilo linawakilisha somo. Kwa kadiri somo linavyojirudia, ndiyo kadiri inavyozidi kuwa wazi kuwa somo hilo linawakilisha dhumuni la kitabu.” (Arthur 1994: 37)
- c. Kurudiwa mwanzoni na mwishoni mwa kifungu kunaongeza msisitizo zaidi. Mwandishi anaposema kitu mwanzoni na mwishoni mwa kifungu (au sehemu au kitabu), ni kama kuweka mwisho wa kitabu kwenye kifungu kuonyesha umuhimu wa wazo. Kwa mfano Paulo anaanza **1 Timotheo** kwa kumwagiza Timotheo “piga vita vizuri” (**1 Tim 1:18**), na anaishia na maneno hayo hayo (**1 Tim 6:12**). Msisitizo huo unazidi kutiliwa mkazo wakati mwandishi anaporudia wazo hilo katika ya kifungu, sehemu, au kitabu. Katika **1 Tim 4:11-16** Paulo anaorodhesha mambo ya msingi kuhusu jinsi kiongozi wa kanisa anavyotakiwa kutenda katika

huduma na maisha. “Kufundisha” kumetajwa mwanzoni (**1 Tim 4:11**), katikati (**1 Tim 4:13**), na mwishoni (**1 Tim 4:16**) mwa orodha hiyo.

d. *Wazo linaweza kurudiwa ili kuonyesha umuhimu wake hata kama si kwa maneno yale yale.*

(1) Kujirudia kunaweza kukatokea ndani ya kifungu, sehemu, au kitabu kizima. Kwa kutazama hili kina cha ufahamu wetu kibiblia utaongezeka sana. Kwa mfano katika **2 Timotheo** wazo la “mateso” limejirudiarudia, inagawa maneno tofauti tofauti yametumika kuelezea—“minyororo” (**1:16**); “magumu” (**2:3, 9**); na “mateso” (**3:11**).

(2) Kujirudia kwa mawazo ya muhimu kunaweza kusiwe wazi katika vipengele vya mwanzo wa kitabu. Kwa mfano katika **Matendo**, matukio mawili tu yamejirudia mara tatu: (1) Maono ya Petro kuhusu wanyama najisi (**Matendo 10:16; 11:10**); na (2) habari ya kuokolewa kwa Paulo (**Matendo 9:1-19; 22:1-13; 26:1-18**). Hii inaonyesha umuhimu wa kipekee unaoonyeshwa na matukio hayo kwa ajili ya asili na ukuaaji wa kanisa.

e. *Matukio maalumu ya kujirudia rudia ni: (1) vifungu sambamba; na (2) nukuu za AK katika AJ.*

(1) Vifungu sambamba ni vifungu tofauti iliyo na habari moja na kwa kutumia maelezo yanayofanana au yanayozungumzia somo linalofanana. Kwa mfano, **Mat 24:1-51, Marko 13**, na **Luka 21:5-36** zote zinaongelea mambo yanayohusiana na tukio moja—Hotuba ya Yesu katika mlima wa mzeituni; **Luka 17:22-37** ni hotuba ya Yesu tena kuhusu jambo hilo hilo. Vile vile, **Waef 6:5-8; Wakol 3:22-25; 1 Tim 6:1-2; Tito 2:9-15**; na **1 Pet 2:18-25** yote yanazungumzia majukumu ya watumwa kwa bwana zao. Vifungu sambamba vyote ni lazima vitazamwe, kwa sababu kila ufanuzi utafunua jambo ambalo halijaelezwatika fafanuzi zingine.

(2) Nukuu za AK katika AJ hutokea mara kwa mara. Chanzo cha AK peke yake ni lazima irejewe kwa ajili ya kuelewa muktadha na kujua historia ya wakati huo. Mara chache maneno katika nukuu za AK kwenye AJ hutofautiana na kifungu kilichonukuliwa. Hii inaweza kutokea kwa sababu waandishi wa AJ mara zote hunukuu kutoka kwenye matokeo ya Septuagint (LXX) ya AK, ambayo ni tafsiri halisi ya kiebrania.

#### 4. M pangilio wa maneno na mtindo wa kifungu au sentensi.

a. *Mara chache kile kinachosemwacho kwanza (kwa mfano, katika orodha) inafanyika kwa ajili ya msisisitizo.* Kwa mfano, katika **Wagal 5:22-23** “tunda ya roho” linaanza na “upendo.” Kwa kweli tunda la roho ni umoja si wingi (nayo ni., “tunda la kwanza la roho ni,” siyo “matunda ya roho ni”). Kwa hiyo, huenda kwa pamoja. Mtu anaweza kuona madhihirisho ya tunda kama madhihirisho ya “upendo” (**1 Wakorintho 13**).

b. *Kupuuza kunaweza kuwa muhimu.* Kwa mfano, Katika kitabu cha **Ruthi 1:14-18** Ruthi anaonyesha unyenyekevu wake kwa Naomi, akaacha nchi yake mwenyewe na watu wake kwa ajili ya Naomi. Katika **Ruthi 1:19-22** Naomi na Ruthi wanarudi kutoka Moabu kuja Bethlehem. Mwanamke mmoja akapiga kelele “*Huyu ndiye Naomi?*” Lakini Naomi akajibu, “*Usiniite Naomi* [nayo ni., “aliyependeza”]; *niite Mara* [nayo ni “uchungu”], *kwa maana Mwenyezi amenitendea mambo machungu. Niliondoka nikiwa nimejaa, lakini Bwana amenirudisha mikono mitupu.*” Katika jibu lake, Naomi hatambui uwepo kabisa uwepo wa Ruthi. Uchungu wake na kushushwa moyo kwa ajili ya kumkosa mume wake na wana wake wawili kulibadili namna yake ya kufikiri na kumfanya awaze habari zake peke yake. Hayo yalimpofusha hata akaona kwamba Bwana amemrudisha “mikono mitupu” wakati Ruthi yupo pamoja naye.

c. *Mipangilio miwili ya kawaida ya kujirudia, kufanana na mwingiliano.*

(1) Kwenda sambamba au mfanano ni pale ambapo mawazo mawili au matatu yanajirudia katika mpangilio wa: A-B-A-B, au A-B-C-A-B-C. Katika **1 Wakor 1:22-23** kujirudia kwa “Wayahudi” na “Mataifa” kupo katika mfumo sambamba:

A—Wayahudi wanataka ishara

B—Wayunani wanatafuta hekima

lakini sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa,

A—kwa Wayahudi ni jiwe la kujikwaza

B—na kwa Wayunani ni upumbavu

(2) Mwingiliano ni pale ambapo angalau mawazo mawili yanajirudia kwa namna ya kuingiliana, nayo ni., katika mpangilio: A-B-B’-A’, au A-B-C-C’-B’-A’. Makundi manne ya kwanza yaliyotajwa katika **Wakol 3:11** Yapo katika utaratibu wa

mwingiliano:

A—Hakuna *myunani*

B—na *myahudi*,

B'—*kutahiriwa*

A'—na *kutotahiriwa*

(3) Mwingiliano unaweza ukahusisha mambo ya msingi yaliyo kiini ambayo yanafanya mengine yajipange juu yake; kiini yawesta kuwa ni jambo linalositisitwa. Muhibiri 11:3-12:2 ni mfano:

A—Mawingu na mvua

B—Nuru na juu

C—Zifikirie siku za giza

D—Yote yanayoletwa na pumzi

E—Furahia ujana wako

F—Lakini sasa Mungu atakuleta hukumu

E'—Furahia ujana wako

D'—Ujana wote ni pumzi

C'—Mkumbuke Mungu kabla ya siku mbaya

B'—Nuru na juu

A—Mawingu na mvua

(4) M pangilio huo si katika kujirudia rudia kwa maneno au semi katika sentensi chache lakini inaweza kuwa kujirudia rudia kwa wazo ambayo yanahusisha kitabu kizima

(tazama Woolvaardt 2005: 222 [matukio ya Samsoni katika maisha yake katika **Waamuzi 14-16** yanaonekana yamepangwa katika mtindo sambamba], 258-62 [kitabu chote cha **Amosi** na sehemu zote na sura zote za kitabu yote yanaonekana kupangwa kwa mtindo wa mwingiliano]).

(5) Kwenda sambamba na kuingiliana inaweza kuwa na kazi zifuatizo:

(A) Yanatengeneza uwiano sawia na uzuri; (B) yanatusaidia sisi kujikita kwenye mada; (C) yanatusaidia sisi kuelewa maana zaidi; (D) yanasisitiza jambo muhimu, na kufuutilia dhumiuni kwa urahisi; (E) yanatusaidia sisi kuona mwunganiko au kutopatana kwa mambo..

## H. Angalia kwa makini matumizi ya lugha

Tafsiri ni juu ya kuvumbua namna maelezo fulani yanavyohusiana na maelezo mengine. Kipekee maelezo ya kina ya muhimu yanayotuonyesha njia ya kupata uelewa wa kifungu inahusisha yafuatayo:

1. Kuunga maneno (viunganishi). “Maneno madogo” yanayounganisha sehemu za sentensi, au yanayounganisha sentensi na aya moja kwa nyingine ni ufunguo kwa ajili ya mawazo ya mwandishi. Kuunganisha maneno kunatengeneza mazingira ambayo neno, usemi au mstari huwa. Kuunganisha kunafanya tuone jinsi semi na sentensi na mawazo zinavyopatana. (mfano 1 Tim 3:1-7 inatoa seti ya sifa za kuwa mwangalizi kanisani; hata kama neno “na” halijatumika mpaka 3:7 kuunganisha sifa hizo tofauti tofauti, mazingira na mpangilio wa maneno pekee unaonyesha kuwa sifa zote hizi ni lazima ziwepo kwa mwangalizi na wala si baadhi yake tu) Anaweza akawa anapinga mambo (katika 1 Tim 3:3 “kuzoelea ulevi au anayekubalika” inapingana na kuwa “mpole, asiwe mbishi”). Anaweza akawa analingalisha vitu (katika 1 Tim 3:4-5 kuwa mwangalizi wa kanisa ni kama kuliangalia familia yako mwenyewe; katika 1 Tim 4:1-2 Paulo analinganisha unafiki unaotokana na kukubaliana na injili ya uongo kama kuchomwa moto dhmiri). Anaweza akawa anatoa sababu ya au kusudi la au matokeo ya kitu fulani (katika 1 Tim 3:6 Paulo anaelezea waongofu wapya hawapaswi kuwa viongozi, na matokeo yatakayopatikana hilo likifanyika). Kwa njia hizi zote mwandishi anaweka wazi maana ya kweli ya kifungu. Viunganishi vya muhimu vya maeneno vinahusisha:

- a. *Maneno yanayoonyesha mwunganiko mwendelezo*—mfano., na; pia; Kwa kuongeza; kisha.
- b. *Maneno yanayoonyesha kinyume*—mfano., lakini; hata hivyo; zaidi sana; pamoja na hayo; bado; ingawa; kisha; vinginevyo.
- c. *Maneno yanayoonyesha ulinganifu*—mfano, zaidi kuliko; pia; kama; ni kama; hivyo pia; vile vile; na;kama.
- d. *Maneno yanayoonyesha kufanana*—mfano., kama . . . hiyo pia; kwa ajili ya . . . kama hivyo . . . kama.
- e. *Maneno yanayoonyesha sababu au kusudi*—mfano, kwa sababu; kwa ajili ya; kwa sababu hii; kwa kusudi hili; tangu; kwamba; ili kwamba; ku; ili.

- f. *Maneno yanayoonyesha matokeo*—mfano., kisha baadaye; kwa hiyo; matokeo yake; Hivyo; kisha.
- g. *Maneno yanayoonyesha hali*—mfano., kama; ikiwa . . . kisha.
- h. *Maneno yahusuyo muda au viunganishi vya muda*—mfano., muda; mpaka; wakati; kabla; baada; wakati; tangu; kisha.
- i. *Maneno yanayoonganisha maeneo ya kijiografia*—mfano., wapi; kule.
- j. *Viunganishi*—mfano., upande (kuelekea; Kutoka; kelekea kwa; mbali na); mahali (juu ya; chini ya; juu ya; pembeni ya; kupitia; ndani ya; kati ya; pamoja; ndani ya; nje ya; zaidi ya; na); uharaka, muda, na mwinge (kabla; kwa sababu ya; kuhusu; kuanzia mwanzo hadi mwisho; kutokana na; baadaye; kwa; kuhusu; kwa niaba ya; kinyume; kutokana na; wakati).
2. Maeleo mengine ya kina kuhusu matumizi ya lugha. Maswali mengi yahusuyo tafsiri yatapata majibu ikiwa tutahusika na anachosema mwandishi, na jinsi anavyosema. Hili linategemea zaidi matumizi ya lugha ya mwandishi katika kile alichoandika. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:
- a. *Aina ya sentensi*. Sentensi inaweza kuwa: (1) maeleo (“sentensi ya kutangaza”—nayo ni., “Hufanya kazi kwa bidii.”); (2) swali (“sentensi swali”—hiyo ni., “Je wao hufanya kazi?”); (3) amri/agizo (“sentensi agizo/amri”—nayo ni., “Fanya kazi kwa bidii.”); au (4) mshangao (“sentensi mshangao”—nayo ni., “Ni namna hufanya kazi kwa bidii!”).
- b. Muundo wa sentensi. Sentensi zina: (1) kima (ni mtu au kitu kinachofanya jambo fulani na kila kitu ambacho kinaboresha kima); na (2) kiarifu ( ni tendo au lolote ambalo linaloongoza au kuboresha tendo [hiyo ni “kikamilishi” cha tendo]). Wakati ikiwa ipo ndapi ya maandishi “Yohana husoma kitabu,” “Yohana” ni kima na “husoma kitabu” ni kiarifu (“husoma ni tendo” ni tendo na “kitabu” [kima cha moja kwa moja] ni kikamilishi cha tendo).
- (1) Sentensi nyingi ni tata zaidi “John husoma kitabu”; zinaweza kuwa na kishari zaidi ya kimoja. *Kishazi kikuu* ni kiini cha sentensi; kinabeba wazo kuu, na kimsingi inahusisha kitenzi, kiima, na kiarifu. *Kishazi kisaidizi* kinahuisha tendo (mara nyingi katika nyakati timilifu), na huboresha kishari kuu. *Kishazi kisaidizi* kinahuisha vitu kama sababu, ulinganifu, mahali, muda, kusudi, matokeo, maeleo, au hitimisho. Mara nyigi vishari visaidizi viinaonyeshwa na maneno kama, kama, kwa sababu, ingawa, nani, yupi, ipi, wapi, kwa nini na kwa vipi.
- (2) Maneno au sehemu zinaweza kuboresha maneno au semi.( msemo ni idadi ya maneno yanayohusiana lakini hazihusishi tendo). Kwa mfano, majina yanaboreshw na vielezi (“kijana mrefu”—“kijana” ni jina; “mrefu” ni kielezi), na vitenzi vinaweza kuboreshw na vitenzi visaidizi (“ombeni bila kukoma”—“ombeni” ni tendo; “bila kukoma” ni semi yenye kitenzi). Sehemu, semi na maneno yanayoboresha yote huongeza maeleo ya kina yanayotokana na matumizi ya lugha yanayotueleza nini hasa kinaendelea na maana halisi ya sentensi.
- c. *Maneno katika sentensi*. Maneno ya msingi yanayotengeneza sentensi ni viunganishi na vihusishaji (tazama hapo juu), majina, viwakilishi, vielezi, vitenzi, na vitenzi visaidizi. Baadhi ya mambo ya kuzingatia kuhusu maneno ni:
- (1) Majina—umoja au wingi (**Wagal 3:16** inafahamisha ukweli kwamba “mbegu” ni umoja, si wingi).
- (2) Viwakilishi—mf., hii; hizi; nani; ya nani; ipi; ile; mimi; wewe; sisi; yeye; sisi; wao; yake; yetu; yako; yao. Viwakilishi peke yake, au kuhama kutoka kiwakilishi kimoja hadi kingine, yawezekana kuwa muhimu. Kwa mfano katika, katika **Luka 15:30** (mfano wa mwana mpotevu) kaka mkubwa hamwiti mwana mpotevu “kaka yangu,” lakini badala yake “huyu mwanaao”; hii inaonyesha hali yake ya nia, na inaongeza msisitizo kwenye tamthiliya na kilele cha mfano. Katika **Waef 2:11** Matumizi ya Paulo ya “wewe” inawakilisha mataifa, lakini matumizi ya “yetu” katika **2:14** na “sisi” katika **2:18** inawakilisha mataifa ambayo wapo sawa na Wayahudi waaminio katika Kristo.
- (3) Vitenzi—nyakati (wakati uliopita, uliopo, na ujao; ); unaoendelea au timilifu. Mara kadhaa wakati mtimilifu huonyesha “utimilifu wa kiungu,” nayo ni., huyu ni Mungu afanyaye mambo kutokea. tazama mfano, **Wakol 3:1**—“*Basi ikiwa mmeifufuliwa pamoja na Kristo*” (ni Mungu ndiye afufuaye; hatujifufui wenywewe).
3. Vipengele vinne vya maana (Wolvaardt 2005: 67-74).
- a. *Tunapotazama lugha katika kiwango cha kutafuta maana (hatua ya maana) maneno yote huonyesha moja ya yafuatayo*:
- (1) Vitu. Kipengele hiki huhusika na vitu vyote au watu (mtu; farasi; ng’ombe), pamoja

na vitu visivyoonekana (malaika; roho), na vitu vya kinadharia (joka).

(2) Matukio. Pamoja na miondoko yote ya hiari na yasiyo ya hiari (kimbia, anguka,) na matendo ya ubongo (fikiri, hisi).

(3) Mahusiano. Kipengele hiki kina kila aina matendo ya kimahusiano. Mahusiano yanaelezwa kwa kutumia vihusishi na viunganishi (ndani, kwenye, baada ya), au matumizi ya vimilikishi (mbwa wa kijana) au matumizi ya muundo wa vinasaba (mbwa wa kijana).

(4) Sifa. Kipengele hiki hutupa ubora, wingi, ubora wa vitu, matukio, mahusiano, na sifa zingine (mfano., kijani, mazuri, nyinyi—kuelezea vitu au mahusiano; upesi, mara chache, mara mbili—kuelezea tukio; zaidi, sana—kuelezea sifa zingine).

b. *Neno hilo hilo au aina ya neno (ny., jina, kitenzi, nk..) linaweza kuhusika na vipengele tofauti tofauti vya kisemantiki kutegemeana na matumizi yake* (n.y., “meza” inaweza tumika kama tukio—“aliweka mjadala mezani”; *kama sifa*—“Kwenye kilele cha mlima ni tambarare kama meza”; au *kitu*—“Kijana alisafisha meza”).

c. *Hakuna ulazima wa uwiano wa 1:1 wa jina na vitu, vitenzi na matukio, sifa na vitenzi visaidizi, na sifa.* Kwa mfano, Katika **Waeb 13:1** “*upendano wa ndugu*” (Kiyunani = philadelphiā) ni *jina* (“*upendano wa ndugu na uendelee*”—RSV; “*Upendo wa ndugu na uendelee*”—NASB), inaelezea sifa ya uhusiano wa waaminio moja kwa mwngine au tukio (“*Endeleeni kupendana kama ndugu*”—NIV).<sup>6</sup>

## VI. Maana ya Maneno na Aina za Semi

### A. Tafsiri maneno kulingana na muda na muktadha

1. Muktadha unaelezea maana ya neno. Neno moja moja likisimama lenyewe linaweza lisiwe na maana zaidi ya maana yake yenye. Hata hivyo, “kama sheria, neno lina maana moja tu katika muktadha huo ambao limetumika” (Wolvaardt 2005: 63). Hata hivyo, *msingi wa mwanzo wa maana siyo neon*, bali ni sentensi na aya ambazo zinabeba muktadha ambao unalipa hilo neno maana. Hivyo, “unapaswa kuijiliza siku zote kwamba hili neno lina maana gani katika muktadha huu?” (Ibid.) Kwa mfano, zote mbili **Warumi 8:39** na **1 Yoh 5:3** zina msemo “*upendo wa Mungu.*” Hata hivyo, muktadha unaonyesha kuwa katika eneo la kwanza unaonyesha upendo wa Mungu kwetu, lakini eneo la pili linaonyesha upendo wetu kwa Mungu.

a. *Kufikri kwamba neno moja lina maana moja kila Mara linapotumika kwenye biblia, bila kujali muktadha inaweza kutufanya tukosee vibaya.* Hii ni kweli kwa sababu maneno mengi yana “upana katika maana zake” (n.y., maana kadhaa). Neno moja linaweza kutumiwa kumaanisha vitu tofauti hata na mwandishi mmoja wa Biblia. Mfano, katika **Matendo 27:20** “kuokolewa” ina maana kuokolewa kutoka mauti ya mwili; katika **Tito 3:5** neno hilo hilo lina maana ya kuokolewa kiroho. Katika **1 Tim 5:17** “heshima” ina maana ya malipo, lakini katika **1 Tim 6:1** ina maana ya heshima.

b. *Vile vile, maneno tofauti yanaweza kuwa na maana inayofanana.* Katika **Mat 20:21** na **Marko 10:37** maneno “ufalme” na “utukufu” yana maana moja. Katika **Mat 12:28** na **Luka 11:20** “Roho wa Mungu” ni sawa na “kidole cha Mungu” (yote humaanisha Roho wa Mungu). Huu pia ni mfano unaoonyesha kuwa vifungu sambamba vinaweza kutupa vitu vya ziada.

c. *Itifaki nzuri, hasa hasa ile iliyozingatia kiyunanai cha asili na kiebrania cha asili vitaonyesha mahali na namna maneno yalivyotumika.* Kamusi nzuri ya Biblia na itifaki pia zitatoa uelewa mbalimbali wa namna maneno yalivyotumika.

2. Neno linaweza kuwa na maana moja tu kulingana na muktadha wa pale lilipo. Hata kama maneno mengi yana maana mbalimbali, na yanaweza kutumika kwa namna tofauti katika maneno mengi ya Biblia, kujaribu kuhamisha maana mbalimbali za neno katika tumizi la neno inaweza kusababisha kosa baya. Kwa hiyo, **Matendo 27:20**, muktadha unadhihirisha ilikuwa ni kupona kimwili kwa kushinda toka kwenye tufani za ziwani katika muktadha huo tunapta maana, ya neno “kuokoka” Hata kama neno hilo mara zote lina maana ya wokovu wa kiroho kusema kwamba “kuokoka” katika **Matendo 27:20** ina

<sup>6</sup> Zingatia kwamba NIV imebadili “upendo” kutoka kwenye jina hadi tendo timilifu, na kuongezea “kila moja,” kwa misingi ya kimaudhui, kuliko kung’ang’ania msingi wa lugha, wa kutafsiri, na inaamua kuona “upendo” kama tukio, na siyo sifa. Hii tafsiri siyo mbaya. Kwa hakika, tukiwa tunatafsiri kifungu, tukibadili muundo wa neno ili kuenda na kipengele cha maudhui kinahusika na kifungu katika maana yake inaweza kutusaidia kuona maana ya kifungu kwa wazi zaidi. Ingawaje, mfano huu haujihusishi na asili ya tafsiri ya “ulanganifu mtambuka”, uliojadiliwa katika sehemu ya II.C. hapo juu.

maana zote mbili yaani wokovu wa mwili na wa roho, kungemaanisha pasipo usahili kwamba wapagani walipokuwa wakisafiri majini walijuhusha na tafakari kuhusu Mungu walipokuwa wakisumbuka na tufani na hata Paulo mwenyewe alitilia shaka uhusiano wake mwenyewe na Yesu.

**3. Uwe makini na mabadiliko ya etimolojia ya neno.** Maana ya neno inabadilika kulingana na wakati. Mafunzo kuhusu historia ya maendeleo ya maana ya neno huitwa “etimolojia”. Maneno ya kibiblia yanatakiwa kutafsiriwa kufuatana na matumizi wakati yanaandikwa. Historia nzima ya neno haikuwepo wakati mwandishi anatumia neno katika kifungu husika. Kwa kutazama kamusi za siku hizi ambazo si za kiyunani wala ya kiebrania, inaweza isiwe na msaada kupata maana ya maneno ya kibiblia. Kujifunza etimolojia ya neno inaweza kusaidia kama vyanzo vipo lakini umakini unahitajika. “Maana ya asili ya neno” inaweza isifae kabisa kupata maana ya neno kama lilivyotumiwa na waandishi wa Biblia. Ni kweli kabisa kwamba waandishi wengi hawakuwa wakijua etimolojia ya neno.

**4. Usikadirie tu kwamba maana ya neno mchanganyiko inategemea muunganiko uliopo.** Neno mchanganyiko ni neno lililoundwa kwa maneno mawili tofauti. Maana ya maneno si lazima ihusiane na maneno hayo yaliyoungana. (mf, “butterfly” haihusiani kabisa na “butter” wala “fly”) (Carson 1984: 28).<sup>7</sup> Maana sahihi inadhihirishwa na muktadha na jinsi mwandishi aliviyotumia hilo neno. Mfano wa kawaida wa tatizo la neno mchanganyiko ni neno la kiyunani lenye maana ya “kanisa”—*ekklesia*: “Neno la kiyunani ekklesia (kanisa) wakati mwingine linaleezwa kama ‘ek’ + ‘klesia’; ‘nje’ + ‘walioitwa’”. Kulingana na maelezo haya kanisa ni watu walioitwa na Mungu. Maana hii ya ekklesia haikubaliani na maana ya neno katika Agano Jipy, wala watumiaji wake wa kale na inaweza kutafsiriwa vema kama ‘kusanyiko la wakristo linaloshirikiana.’” (Wolvaardt 2005: 65)

## B. *Tafsiri maneno kulingana na nahau au aina za semi*

**1. Watu wote huandika na kuongea nahau.** Nahau ni msemo ambaeo unaeleweka na tamaduni fulani ambaeo maana yake si maana ya maneno yaliyotumika—kama nahau ya Waamerika, “piga teke kikapu” “ng’ata vumbi” na “wika” kwa ajili ya “kufa.” Kila utamaduni una nahau zake. Waandishi wa Biblia wanatumia nahau. Kwa mfano, “mbegu” (**Mwanzo 22:17**) ni maana ya nahau inayomaanisha “uzao” “sheria na manabii” (tazama **Mat 5:17; 7:12; 22:40; Matendo 24:14**) inarejea kwenye AK (yote mawili “mbegu” na “Torati na manabii” kuna matukio ya majina kubadilika [tazama hapa chini]).

**2. Watu wote bila kujali utamaduni au lugha huongea na kuandika kwa kutumia lugha za alama katika hotuba.** Lugha ya alama ni matumizi ya neno au semi ambazo hazonyeshi maana ya moja kwa moja kwa kufuata tafsiri ya kawaida. Lugha ya alama mara nyingi inatumia kutia mkazo, kuleta upya wa maelezo au mguso wa kihisia. Vinasababisha mwunganiko kati ya vitu ambavyo vimefichwa kwetu. Maelezo kwa kutumia mifano yanapanda mtazamo fulani ndani yetu kuhusu kile kinachoelezwa na yanatufanya sisi kuwa na macho mapya ya kutazama dunia na katuongoza katika kupokea kweli na kutendea kazi masomo yaliyotolewa kwa njia ambayo hatukutaraja.

**3. Biblia inatumia njia hizi zote za kwaida.** Hiyo mifumo ya kawaida inatakiwa kutazamwa na kukubaliwa. Kosa litatokea pale ambapo nahau zitatafsiriwa kwa kutumia “kanuni ya kawaida” ya “kimwili”. Kwa hakika, njia “halisi” ya kutafsiri lugha ya alama “tafsiri kwa kutumia lugha ya alama”; njia ya “kawaida” ya kutafsiri maelezo yaliyokuzwa ni kutumia njia ya kutafsiri “habari iliyokuzwa”

**4. Kati ya matumizi ya lugha isiyo na maana ya kawaida ambayo maana yake ni tofauti ni ile inayosomeka ni kama ifuatavyo:<sup>8</sup>**

a. *Lugha ya kukadiria.* Wakati mwingine Biblia inatumia tarakimu tofauti na namna ambayo mwanadamu wa kawaida angeitimia, yaani tofauti na namna ambayo wanamahesabu, wataalamu wa tarakimu, wanasayansi wangetumia. Njia mbili ambayo Biblia hufanya hivyo:

(1) Kuelezea vitu kama vinavyoonekeana kwa macho. Hii ni njia ya kuelezea mambo kwa jinsi yanavyoonekana bila kujali maana halisi au ya kisayansi. Kwa mfano, tukirejea kuchomoza kwa jua (**Marko 16:2**) kuchwea (**Mwanzo 15:12**) ni vile vitu vinavyoonekana kwa macho ingawa ule mwonekano wa “kuchomoza” na “kuchwea” ni matokeo ya dunia kuzunguka kwenye muhimili wake. Vile vile, **Zab 104:5**, ambayo

<sup>7</sup> Kitabu cha D. A. Carson, *Upotoshaji wa Eksejesia* (Grand Rapids: Baker, 1984; Toleo la pili, Grand Rapids: BakerAcademic, 1996) inahusisha mafunzo ya maneno ya kawaida, lugha, mantiki, nadharia, na upotoshaji wa kihistoria. Ni kitabu kidogo, na kinafaa kusomwa na wale wanaotamani kuepuka kutafsiri na kutumia maandiko kimakosa.

<sup>8</sup> Uchambuzi mrefu na wa kina wa aina za maneno katika Biblia ni kitabu cha E.W. Bullinger *Aina za maneno yanayotumika katika Biblia* (Grand Rapids: Baker, 1968 [chapa nyininge]). Kitabu kina ukubwa wa kurasa 1000. Pia inayosaidia sana ni ndogo zaidi *Kamus ya alama za Biblia* na Owen, Grist, na Dowling (London: Grace, 1992), ambayo inaorodhesha nyingi alama za Biblia za ulinganifu, uwakilishaji, na mbadala (Tashbiha, tashihisi, taashira, uhuishaji, viiwakilishi, kukuza maana, ishara/alama, na kiashiria).

inasema kuhusu “*dunia kuimarishwa kwenye misingi yake ili isiyumbe*” ni maelezo yanayozingatia kuona kwa macho.

(2) Namba zilizokadiriwa. Waandishi wa Biblia hutumia namba zilizokadiriwa muda baada ya muda. Kwa mfano, idadi ya wana wa Israeli ni **Hesabu 1:20-46** imekadiriwa katika 50 iliyo karibu. **Mat 14:21** inaonyesha kwamba wanaume “5000” waliokula ni makadirio. Inawezekana walikuwa wanaume 4000 waliolishwa katika **Mat 15:32-38**, lakini muono wa juu wa maandiko hauhitaji hilo—hiyo namba inaweza ikawa ni makadirio.

b. *Kuwepo kwa kulinganisha, kuwakilisha mambo, na mbadala.* Mara nyingi waandishi wa Biblia hulinganisha kitu kimoja na kingine; au kitu kimoja kitawakilisha kitu kingine; au kitaelezea kitu kingine ambayo kimewekwa badala ya kingine. Tena, hivi ndivyo watu wanavyoongea katika maisha ya kawaida ya siku kwa siku. Mifano muhimu katika hili ni:

(1) Tashbihi na Mafumbo.

(A) *Tashbihi ni ulinganifu wa vitu viwili tofauti kwa kutumia maneno kama; “kama,” au pea ya maneno “kama . . . hivyo.”* Kwa mfano, **Zab 42:1** (“*Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuoneea shauku, Ee Mungu*”); **Ufunuo 1:14-15** (“*Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto; na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi*”); **Mwanzo 22:17** (“*Katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliiki mlango wa adui zao*”). Angalia mifano ya kuzidisha katika **Mwanzo 22:17** siyo kwamba zote ni tashbihi bali pia kuna mifano ya chuku (kutilia chumvi), na kama vile ilivyo mamia ya mabilioni au trilioni za nyota na mchanga).

(B) *Tashbihi ni kufanya ulinganifu kati ya vitu viwili bila kutumia maneno kama: “kama” au “ni kama.”* Tazama, mfano., **Zab 18:2** amba una tashbihi saba kumwelezea Mungu—“mwamba, ngome, mkombozi, kimbilio, ngao, pembe, na wokovu”; **Yoh 15:5** ina tashbihi mbili—kwanza Yesu anafananishwa na mzabibu; pili anafananisha wasikilizaji wake na matawi.

(C) Tunachambua tashbihi na sitiari inasaidia sana kukumbuka kwamba kila moja ina mambo matatu: (1) mada (nayo ni., mtu halisi, kitu, au tukio linaloongelewa); (2) ufafanuzi (nayo ni., kitu ambacho kinafananishwa na mada); and (3) mawazo yanayoelezea mfanano (sehemu za maana ya mada zinazofanana na ufanuzi). “Uelewa sahihi wa sitiari ye yeyote au tashbihi hutegemea kutambua mfanano kati ya mada na ufanuzi. Mada na ufanuzi hazifanani kwa namna ye yeyote isipokuwa katika *kipengele kimoja mahususi cha maana zao*.” (Volvaardt 2005: 138). Kwa hiyo, katika msemo “Benjamin ni mbwa mwitu mwenye kurarua” (**Mwanzo 49:27**): Benjamin ni mada; mbwa mwitu mwenye kurarua ni ufanuzi; na kuwa mkali na mharibifu ni maelezo ya mfanano.

(2) Tashihisi.

(A) *Tashihisi (pia inajulikana kama kufananisha) ni aina ya tashbihi ambayo vitu amavyo si mtu (Mungu, mnyama, kitu, dhana, au msemo unaelezea kiini cha habari) unapoelezewa kana kwamba ni mtu au kina utu wake.* Kwa mfano, Mungu anaelezewa kwamba ana mikono (**Isaya 49:16**) na macho (**Hab 1:13**); mito inaambiwa “ipige makofi” (**Zab 98:8**); vilima “visikie” na milima “isikilize” (**Mika 6:1-2**); “*Hekima anapiga kelele mtaani, anapaza sauti yake katika pembe*” (**Zab 1:20**); “Mammon” (i.e., mali) amehuishwa kama Mungu katika **Mat 6:24** na **Luka 16:13**.

(B) *Kinachohusiana na unafsishaji ni kuwapa wanyama sifa ya Mungu, ambayo ni aina ya tashbihi ambayo humtaja Mungu kuwa na sifa za mnyama.* Tazama, mf., **Zab 17:8** (“*Nifiche katika kivuli cha mbawa zako*”).

(3) Taashira. Taashira ni semi inayowakilisha wakati neno moja au au semi inapowakilishwa na nyingine ambayo ina uhusiano wa karibu kama katika matumizi ya Washingtone badala ya Serikali ya America, au silaha badala ya nguvu ya kijeshi.

Mfano, **Isaya 22:22**—“*ufunguo wa nyumba ya Daudi*” inawakilisha dhana ya utawala au mamlaka ya ukoo wa kifalme **Amosi 7:9**—Isaka anawakilisha watu wa Israeli; **Marko 1:5**—“*Nchi yote ya Uyahudi ilikuwa ikimwendea*” inawakilisha “nchi” badala ya watu katika nchi (zingatia usemi “*Nchi yote*” pia ni mfano wa chuku [tazama hapo chini].

(4) **Kiwakilishi.** Kiwakilishi ni semi inayofanana katika uwakilishi ambayo sehemu kidogo huwakilisha kitu kizima (kama mkono badala ya baharia), kitu kizima badala ya kisehemu (kama *sheria* badala *askari polisi*), maalumu badala ya yote (kama *kata shingo* badala ya *mauaji*), ya jumla badala ya maalumu (kama *mwizi* badala ya *mdokozzi*), au malighafi badala ya kile kinachotengenezewa nacho (kama *chuma* badala ya *silaha*). Mfano, **Matendo 5:9**—“*miguu ya wale waliomzika mume wako* [maana yake ni “*watu (wanaume)*” (sehemu badala ya yote)] *wapo mlangoni*”; **2 Sam 17:24**—“*Na Absalomu akavuka mto Yordani, ye ye pamoja na wanaume wote wa Israel*” [hiyo ni, “*wanaume wengi*,” kwa sababu Daudi alikuwa na wafuasi wake pia, (yote badala ya kisehemu)] *pamoja naye*” (huo pia ni mfano wa Chuku); **Waamuzi 12:7**—Yepta akazikwa “*katika miji* [wingi badala ya umoja] *ya Giadi*. ”

(5) **Kukuza maana.** Kugawanya maana, ni wakati ambapo kitu kizima kinawakilishwa na sehemeu mbili zinazokinzana. Mf., **Zab 139:2**—“*Unanjua wakati niketipo na wakati niinukapo*” (ina maana, “Unajua kila hatua niichukuayo”); **Isaya 45:6**—“*Ili watu wapate kujua toka mawio hata machweo ya jua*” (maana yake, “ili watu wajue siku nzima” au “wakati wote”).

(6) **Taashira.** Taashira ni wakati kitu au tendo linapowakilisha tabia njema au kweli fulani ya kiroho, kweli hiyo inaweza ikawa ya wakati uliopita, uliopo au ujao. mf., **Isaya 42:6**—Mungu huchagua mtumishi wake “*kama nuru kwa mataifa*” (huu ni, kama mfano, wa mwakilishi wa Mungu; pia tazama “*kama nuru*” ni tashbiha); **Ufunuo 20:1-3**—Na malaika alikuwa na “*ufunguo wa kuzimu na mnyororo mkubwa kwenye mkono wake*,” ambao kwa huo alimfunga shetani na kumtupa kuzimu akamfunga na kuweka muhuri (hizo zote ni ishara zinazoonyesha kuzuiwa kwa kazi za shetani, haiwezi kuwa vitu dhahiri vya kimwili kwa kuwa shetani ni roho, si nafsi yenye mwili; kumbuka hata hizo ishara halisi za vitu vya kimwili vina umuhimu wake kiishara—mfano kiti cha enzi huwakilisha mamlaka).

(A) Mara mara nyingi hutumuia vitu halisi au matendo kuwakilisha kuashiria ukweli fulani. Kwa mfano, **Hos 1:2; 3:1** (Hosea anamchukua mwanamke kahaba kuwakilisha kukosekana kwa uaminifu kwa wana wa Israeli, na upendo wa Mungu usioshindwa kwa ajili yao pamoja na kutotii kwao); **Matendo 21:11** (Agabo anajifunga mikono na miguu kwa mshipi wa Paulo kuashiria jinsi atakavyochukuliwa kama mfungwa.).

(B) *Kitu kimoja kinaweza kuwalisha jambo zaidi ya moja.* Kwa mfano, joka anawakilisha kifo cha Kristo msalabani ambako alibeba dhambi za ulimwengu za watu (**Yoh 3:14**), na pia shetani (**Ufunuo 20:2**).

(C) *Tarakimu inaweza kutumika kama ishara.* Kwa mfano, Yesu’ kuwachagua wanafunzi/mitume kumi na wawili (tazama **Mat 10:1; Matendo 1:12-26**) inaonyesha makabila kumi na mbili ya Israeli (tazama **Mwanzo 49:28; Mwanzo 21:12, 14**). Kwa hiyo, Yesu ni utimilifu wa kile kilichopo katika AK, na huleta maagano yaliyopo katika AK katika kutimia. Matokeo ya ishara ya tarakimu ni lazima ishughulikiwe kwa uangalifu. Mara kadhaa ishara ya namba haiendani moja kwa moja na “namba halisi”. Kwa habari ya wanafunzi kweli walikuwa kumi na wawili, lakini matumizi ya namba hiyo *ni ya kiishara*.

(D) Mwongozo sahihi kabisa wa kutafsiri ishara ni: i. Jinsi Biblia yenye we inavyotafsiri ishara, inafanya hivyo kwa wazi; na ii. Muktadha. Ikiwa kati ya haya hakuna kinachoelezea maana ya ishara, haitakiwa kubuni tafsiri yake bali ni kukiri kwamba ishara hiyo haijaeleweka.

(7) **Kiashiria.** Kiashiria ni ufanuzi wa AK uliobuniwa na Mungu unaohusiana na asili ya kiwango cha juu halisi cha AJ na matumizi ya asili ya AK (uhalisi wa AJ unaitwa “kiashiria hasi”). Kwa hiyo, asili kwa namna moja inaenda sambamba au inawakilisha kiashiria hasi Ili kitu kiwe kweli “asili” Biblia inahitaji kuonyesha kwa wazi hilo, na pia ionyeshe wazi “kiashiria hasi” ni kipi. Baadhi ya mambo yapo wazi: **Warumi 5:14**

inamwelezea kwa wazi Adamu kuwa ni aina ya Kristo. Baadhi ya mambo hayahitaji nukuu ya moja kwa moja, lakini nukuu za AJ kutoka AK inaweza kudhihirisha kiashiria Katika **Yoh 3:14** ulinganifu wa wazi wa kifo cha Yesu na nyoka wa shaba ambaye Musa alimwinua jangwani (**Hes 21:9**) inafanya nyoka wa shaba kuwa ni “Kiashiria”. Visa vingine vinaweza vikawa na utata zaidi. Matumizi ya maneno yanayofanana, maudhui, na mwenendo unaweza ukafanya kiashiria “Yusufu, kwa mfano, ni muhimu katika kutunza uzao wa agano kutoka kwenye njaa wakati wa njaa na ukame, na taabu yake hakustahili ni muhimu kwa jukumu lake la kuwa mwokozi. Bado katika Agano la Kale, nukuu zinazomhusu Yusufu katika Agano Jipyä kuhusu Baraka za Yakobo kwa wana wawili wa Yusufu (Waeb. 11:21). [Hata hivyo] tunatambua kuwa mateso ya Yusufu na matokeo yake mazuri, kwa ufupi na kwa uwazi, yalikuwa kivuli cha mateso Yesu na wokovu unaotokana na hayo. Yusufu ni kiungo cha muhimu sana katika historia ya agano aliyoileza Stefano katika Matendo 7. Kwanza kwa Yusufu, kisha kwa Musa, kisha kwa manabii kwa ujumla, na mwishoni, kwa sababu za hali ya hewa, kwa Mwenye haki Mmoja, kurudia kwa mlolongo huo kulitokea.” (Johnson 2007: 214-15) Katika kujaribu kujua mahusiano ya kimahusiano, mmoja anatakiwa kuwa mwangalifu ili kuepuka kwenda zaidi ya kinachoelezwa na maandiko pale panapokuwa na msingi mdogo, kama ilivyo kawaida katika ukristo usioenda katika ufahamu, kama inavyoilezwa katika mtazamo wa Origen kuhusu mfano wa Msamaria Mwema: Mtu aliyekuwa anashuka ni Adamu na Yerusalem ni paradiso, Yeriko ni dunia, wezi ni nguvu mbaya, kuhani ni sharia, walawi wanawakilisha manabii, msamaria ni Kristo, madonda huwakilisha kutotii, punda ni mwili wa Bwana Yesu, mwuguzi ni kanisa, dinari mbili ni Baba na Mwana, mtunzaji ni mwenyekiti wa kanisa, Msamaria ahadi ya kurudi ni mfano wa ahadi ya Yesu ya kurudi mara ya pili. (Roukema 2004: 62) Kwa upande mwingine, Kristo na mitume walilionia Agano la Kale lote kwa namna fulani kama kitabu kuhusu Yesu (**Luka 24:25-27, 44-45; Yoh 5:39-40, 46; Matendo 3:18, 24; 10:43; 26:22-23; 2 Wakor 1:20; 1 Pet 1:10-12; Waeb 1:1-3**). Kwa sababu hii, “Utendaji wa kila mpatanishi wa agano na muhusika –kiongozi mkuu, nabii, kuhani, mwamuzi, mfalme, mume, baba, mwana, wazazi, watoto, mtumishi-hatimaye ni kutoa tafsiri katika nuru ya yale yanayoakisiwa (au yasiyoakisiwa sawa sawa) na utii mkamilifu utakaoonyeshwa na Yesu kama Bwana wa watu wake-kwa ujumla upatanisho kwa njia ya mateso uliotimizwa na Yesu Mwana wa Mungu na ndugu wa watu wake. . . . Kwa hiyo tabia mchanganyiko ya viongozi wa maagano inawafanya kila mmoja wao , kulingana na ofisi yake kwa njia moja au nyingine kuashiria ujio wa Mkombozi Ajaye ambayo katika yeze kazi ya nabii, kuhani, na mfalme zitatimizwa kwa ukamilifu wote.” (Johnson 2007: 216) Johnson anahitimisha hivi: “Usomaji makini wa Agano la Kale unaomlenga Kristo unahitaji kuzingatia kikamilifu muktadha halisi na muktadha wa kihistoria wa kila kifungu. . . . Ugunduzi wetu wa kufanana kwa mifano (vile vile kama kiashiria halisi na kiashiria hasi) ni lazima utokane na uthibitisho wa muktadha wa maandiko siyo tu matokeo ya fikra zetu wenywewe. Mitazamo ya kihalisia au inayozingatia lugha pamoja na maudhui na muktadha mzima wa mambo muhimu, ni uthibitisho muhimu unaotambulisha muunganiko wa kiungu kati ya watu wa Agano la Kale, matukio, au taasisi na mtazamo wa kutimizwa kwa Agano la Jipyä, ambao kiini chake ni Kristo na Kanisa lake.” (Ibid.: 329, 214)

c. *Vielelezo* vya *kiufahamu, kihisia, na matokeo ya mahojiano*. Mazungumzo kwa vitendo mara zote yapo kwa ajili ya kusisitiza jambo fulani. Vitendo vilivyoilezwa hivi punde vinaweza kuitwa vitendo “viwakilishi”, kwa sababu vimetumika kuwakilisha jambo au wazo kwa kutumia msemo ulioazimwa kutoka mahali fulani. Vielelezo hivyo vinaweza kuitwa vitendo visivyo-“wakilishi” vinahusika na kuhimiza tokeo au mtazamo wa msikiaji au msomaji. Ni kawaida sana kutokea katika mazungumzo zaidi kuliko katika maandishi.

(1) *Chuku (kutilia chumvi)*. Chuku ni kutilia chumvi mazungumzo kwa nia ya kusisitiza jambo. Mfano, **Zab 119:136** (“*Macho yangu yachuruzika mito ya maji*”); **Mat 5:29** (“*Jicho lako la kuume likikukosesha, ling’oe ultupe mbali nawe*”).

(2) *Meiosis (Leitotes)*. Ni kufanya jambo moja liwe dogo ili kukuza lingine. Kwa mfano, **Hes 13:33**—“*tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi*” (namna hii ya kuongea, na wale kumi wa Musa’ kati ya wapelelezi kumi na mbili, inakuza kiasi cha uwezo wa wakanaani; pia tazama neno “kama

mapanzi” semi inayotumika kuelezea maana nyingine); **1 Sam 24:14**—“*Unamwinda nani? Ni kuwinda mbwa mfu, au kiroboto?*” Ikilinganishwa na meiosis tunapata *tapeinosisi*, ni kufanya jambo lionekane dogo ili kukuza lingine. Mf., **Zab 51:17**—“*Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau*” (yaani., Kwa furaha Mungu ataukubali moyo “uliovunjika na kupondeka”); **Warumi 1:16**—“*Siionei haya Injili*” (yaani, “Nina uhakika sana na ninahesabu kuwa ni heshima kubwa na utukufu kuhubiri Injili”).

(3) Kinaya. Kinaya inaelezea maelezo yaliyo kinyume na kile kinachotarajiwa kwamba kimeelezewa. Inaweza kuonekana kwa namna mbili:

(A) *Kinaya ni usafanuzi wa wazo libluniwa kutoa maelezo yaliyo kinyume cha kile kinachoelezwa kwa hali ya kawaida.* Mf., **Ayubu 12:2**—“*Hapana shaka ninyi ndinyi watu halisi, Nanyi mtakapokufa, ndipo na hekima itakoma!.*”;

**26:2-3**—“*Jinsi ulivyomsaidia huyo asiye na uwezo! . . . Na kutangaza ujuzi wa kweli kwa wingi!*” (Rafiki zake Ayubu hawakumpa msaada wala ujuzi); **1 Wakor 4:8**—‘*Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi. Naam, laiti mngemiliki, ili sisi nasi tumiliki pamoja nanyi!*’ (kanisa la Korintho kiuhalisia lilikuwa limejaa mabaya, migogoro na dhambi).

(B) *Kinaya pia inaweza kutumika katika muktadha mpana na siyo katika maneno yanayotumiwa tu, kwa namna hiyo inatoa ujumbe unaopingana na kile kinachotarajiwa kuwakilisha.* Kwa mfano, katika **Yona 1:1-14** tunaona Kinaya pale ambapo nabii wa Mungu anaonekana kukosa utii na kuwa na hali ya kutojali maisha au usalama wa watu wengine lakini wapagani wanaonyesha kujali maisha na usalama wa watu wengine na wanaomba kwa bidii katika maombi yao kwa Mungu.

(4) Tafsida. Tafsida inasimama badala ya neno ambalo linaudhi ili kutoa ujumbe bila kuudhi. Mf. **1 Sam 24:3**—“*Kkufunika miguu*” maana yake “kujisaidia haja kubwa”; **1 Wakor 7:3, 5**—“*Ampe mkewe haki yake*” na “*mkajiane tena*” ni tafsida ya maneno “mkutane kimwili.”

(5) Maswali Balaghaa. Katika AK na AJ mara kwa mara maswali huulizwa. Katika AJ yapo maswali 1000 yaliyoulizwa. Maswali yapatayo 300 ni “halisi” maswali yanayoulizwa kwa ajili ya kupata taarifa. Maswali 700 yaliyobaki yanajulikana kama “maswali ya baghala” kwa sababu yameulizwa si kwa ajili ya kutaka taarifa ila kutoa taarifa yakihusisha mtazamo na maoni ya msemaji. Maswali balagha yanaeleza ukweli na kuweka mkazo wa jambo analoelezea msemaji. Majibu ya Mungu kwa Ayubu katika **Ayubu 38-41** yamebeba maswali balagha. Yesu aliuliza maswali balagha mfululizo katika **Mat 5:46-47; 7:3-4, 9-11; Luka 12:25-26, 28.** Paulo alifanya jambo hilo hilo katika **1 Wakor 1:13 6:15-19.**

## VII. Matumizi ya Kifungu

### A. *Matumizi ya Biblia kimsingi yanahusiana na uelewa wake*

Uelewa wa Biblia haujakamilika kama hatutumii. “Mchakato wa kutafsiri haujakamilika ikiwa utakoma katika hatua ya maana” (Klein, Blomberg, na Hubbard 1993: 401). Biblia kamwe haipo ili watu wajifunze kwa ajili ya kupata maarifa tu “ujuzi wa akilini”. Bali, Biblia imekusudiwa kuwa ufunuo wa Mungu kwetu kwa ajili sisi kutumia katika maisha yetu (mfano, **Kumb 6:1-3; Zab 119; Yoh 13:13-17; 14:21-24; 2 Tim 3:16-17; Waeb 5:11-14; Yak 1:22; 2:19-20**). “Kushinndwa kutumia kwa kawaida inahusisha kushindwa kuelewa *kikamilifu*. Hiyo inahusisha kumwitikia Mungu, anayejiwakilisha mwenyewe katika Maandiko. Ikiwa hatutaelewa au *kulitambua*, hatumwelewi wala kumtambua *Yeye*. . . . Ikiwa kusanyiko linaishi maisha ya ukamilifu lakini linapuuza wageni wanaotoka katika jamii zingine na makabilo, hawana uelewa sahihi kuhusu kanisa. Ikiwa wanandoa wanameshika kwa moyo Waefeso 5 lakini mume anajaribu kuishi kwa kumtawala mke wake ambaye anampinga kwa kila kitu, watakuwa bado hajafahamu kifungu hicho.” (Doriani 2001: 22, 76) Kwa hakika, kujuu maandiko bila kuyatumia ni dhambi (**Yak 4:17**; tazama pia **Yak 2:19**). Kwa upande mwininge wakati tunayatumia maandiko, ufahamu wetu wa theologia unaongezeka kina na kukua, kwa kuthibitishwa au kubadilishwa (tazama **Zab 111:10**).

### B. *Matumizi hatimaye yameweka mizizi katika lengo lake la kufanana na Kristo*

1. Matumizi ya Neno la Mungu siyo tu kubadilika kwa nje kwa kufuata sheria zilizowekwa. Kutumia

Biblia au kufanya kazi Biblia ina maana *kubadilishwa maisha yetu*. Paulo alisema, “*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni mili yenu iwe dhabihu iliyohai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanya upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyomema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*” (**Warumi 12:1-2**)

2. Kubadilishwa kwa maisha kunatokana na neema ya Mungu inayotukomboa sisi, inayofungua fahamu zetu kuyajua maandiko, na kutupa uhusiano mpya na Yeye kwa njia ya Kristo. Lengo la kubadilishwa huko ni ili kwamba tumjue Mungu na kuwa kama Yeye—“*tukibadilisha na kufanana na Mwanaye*” (**Warumi 8:29**; tazama pia **Mat 5:48; Yoh 17:3; 2 Wakor 3:18; Wafilip 1:3-6**). Kubadilishwa ni kudhihirishwa “utu wetu mpya” ndani ya Kristo (tazama **Waef 4:17-24; Wakol 3:9-10**). Kwa hiyo, ni lazima iwe kutoka “ndani kwenda nje” na lazima ibadilishe mwenendo wetu wote katika maeneo yote ya maisha (mawazo, maneno, na matendo). Ni lazima yawe maisha yanayoakisi thamani, kanuni, na kweli za Biblia” (Stanley na Jones 2006: 95). Ni maisha matakatifu, yakitegemea utu wa ndani uliobadilishwa, ambao unajionyesha wenyewe kwa kumpenda Mungu na watu wengine (tazama **Mat 15:15-20; Marko 7:14-23; Mat 7:17-18; 12:33-37; 2 Wakor 7:1; 1 Pet 1:13-17; Mat 22:35-40; Yoh 13:34-35**).

#### C. *Matumizi sahihi yanatokana na hemenutiki sahihi na eksejesia*

Hemenutiki nzuri inatuelekeza kwenye uelewa sahihi wa kifungu ambacho hatimaye kitawezesha tuweze kufanya matumizi sahihi ya kifungu. Tumeona mifano kadhaa kufikia hapa, ikihusisha:

1. Kuangalia vifungu vingine ili kuielewa mada kwa ukamilifu zaidi. Kufanya hivi kunatusaidia kutoingia kwenye upotofu wa mafundisho yanayosema “ipatie jina-na idai”, na kutusaidia kuomba kwa namna inayomhesimu Mungu (tazama sehemu ya III.B.4.b., hapo juu).
2. Kutofautisha kati ya maelezo na maagizo. Kwa kufanya hivyo tunajifunza kutomwekea Mungu masharti yasiyo na mantiki (tazama sehemu ya III.D.3.b., hapo juu).
3. Kuchukulia maanani aina ya fasihi iliyotumika. Kwa kufanya hivi hatutamkosoa Mungu kwa kushindwa kutimiza ahadi zake, watoto wetu wanapokuwa wamekengeuka wakati tumewalea vema (tazama sehemu ya IV.C.2., hapo juu).

#### D. *Matumizi yasiyo sahihi yanatokana na hemenutiki isiyo sahihi na eksejesia*

1. Kuchukulia Biblia kana kwamba ni kitabu cha “kichawi.” Wakati mwengine watu wanapotafuta uongozi wa Mungu wakati wa kufanya maamuzi hufungua Biblia ili kwamba mstari ambao macho yatabahatisha kuuona wanahesabu kuwa ndiyo Neno la Mungu kwao kwa ajili ya maamuzi ambayo wanataka kuchukua. Huko ni kutumia Biblia kana kwamba ni “kitabu cha kichawi.” Klein, Blomberg, na Hubbard (1993: 404) walitoa taarifa ya tukio la kijana mmoja aliyekuwa anajiuliza aende chuo au asiende. Alifungua Biblia bila utaratibu na macho yake yakaangukia kwenye **Ezek 27:25** ambao unaongelea juu ya watu kutoka Tarshishi kwenda Tiro kwa meli. Ingawa kifungu hicho hakikuwa na amri yejote kuhusu mtu kwenda popote kwa meli, na haihusiki na askari wenyewe silaha, Yule kijana akatafsiri kifungu kwamba kinamtaka ajiunge na mafunzo ya askari wa majini. Mungu hajawahi kusema atatupa mwongozo kwa njia hiyo. Hata wazo kwamba, “mstari nitakaoona kwanza nitauchukua kama uongozi wa Mungu kwangu” ni kumwekea Mungu masharti yasiyo na mantiki.
2. Kiroho cha uongo—“kutafsiri” Biblia “kwa Roho” badala ya eksejesis ya Neno. Baadhi ya watu hunukuu **1 Wakor 2:14** (“*mambo ya Roho . . . yanatambulika kwa roho*”) na **2 Wakor 3:6** (“*andiko huua bali Roho anahuisha*”) nje ya muktadha, kusema kwamba watu walio hai kiroho hawahitaji kuchambua maandiko kwa makini kwa kutumia ufahamu wao bali wanahitaji “roho” kupokea “ufunu” kuhusu kile ambacho Biblia inamaanisha. **1 Wakor 2:14** inasema kwamba ni Wakristo tu wataelewa kile “*mambo tuliyopewa sisi bure na Mungu*” (**1 Wakor 2:12**). Watu ambao hawajabadilishwa hawatafahamu mambo haya, kwa sababu wangefahamu wasimgemsulubisha Yesu (**1 Wakor 2:8**). **2 Wakor 3:6** inagonganisha Agano Jipyä na lile la Kale ambayo baadhi ya waalimu wa uongo wanashilikilia ingawa Yesu ameshakuja. Pili, hiki “*kiroho cha uongo*” njia ya “*kutafsiri Biblia*” hufanya Biblia iseme mambo tofauti kwa watu tofauti. Msingi wowote wa maana iliyokusudiwa ya kifungu huondolewa. Kwa hiyo Biblia inaweza kutumika kuhalalisha kila aina ya uovu na matendo yasiyo ya kikristo.
3. Kushindwa kuchukulia maanani muktadha wa kihistoria au muktadha wa kifasihi. Watu wengi wametumia Biblia vibaya kwa kushindwa kuzingatia muktadha wa kihistoria na ule kifasihi wa mistari ambayo wanaitegemea. Kwa mfano. Watu wengi hutegemea **Wafil 4:13** (“*Ninayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu*”) wakiwahakikishia watu kwamba au wao wenyewe watafanikiwa katika

kila kitu ambacho “wanahisi” wanaongozwa kufanya. Hata hivyo, muktadha wa kifasihi (hasa **Wafil 4:11-12**) unaonyesha kwamba matumizi ya ule mstari unahusiana na *kuridhika bila kujali hali ya uchumi*. Paulo alikuwa anakumbana na ugumu wa uchumi na mateso, hata hivyo alikuwa anafurahia vile alivyopewa, na akaendelea kuhubiri Injili pamoja na upinzani huo wote.

4. Tunatakiwa kuwa makini tunapopokea “mwongozo binafsi” au “hisia” kwamba ni Mungu anasema kibinafsi na sisi moja kwa moja, kwa kutumia kifungu cha maandiko ambacho hakitumiki au hakiwezi kutumika. Hag 2:19 inasema “*Kuanzia leo na kuendelea nitakubariki wewe.*” Mtu anayeomba juu ya mahitaji yake binafsi anweza akahisi kwamba Mungu anatumia mstari huo kumhakikishia kwamba atashughulika na mahitaji yake siku hiyo. Mtu aliyekomaa kiroho atajua muktadha wa kifungu, kwani kinaongelea kwa hakika kuhusu Baraka ambazo Mungu ameanza kuziachilia kwa wale watu wa uhamisho waliorudi Yerusalem kama matokeo ya utii wao wa kujenga hekalu, na kwamba hakuna uhusiano wa kitamaduni katika “kweli kamilifu” katika kifungu ambacho kinasema Mungu atakutana na haja zake siku hiyo. Mungu anaweza kwa hakika kusema na sisi kupitia Neno lake. Hata hivyo, watu wengi inawezekana wamefikiri kimakosa kwamba Mungu alikuwa anaongea na wao kibinafsi kwa njia hii hata kama hakuwa akiongea nao, na matokeo yake yakawa ni huzuni kwa ajili yao na wengine. Wolvaardt anatuonya kwa hekima: “Hesabu hamasa ye yeyote inayotoka kwenye kifungu cha Biblia ambacho hakitumiki kama hamasa ambayo haitoki kwenye Biblia. Ni lazima kutofautisha mwongozo binafsi unaotoka kwenye kifungu cha Biblia ambacho hakina kweli kamilifu zinazofaa kutumiwa na ule mwongozo ambao una kweli kamilifu zinazotumika. Tunaposhughulika na kweli kamilifu, ni lazima tuwakilishe kwa namna hiyo kwa sababu Mungu anataka aseme kwa mamlaka kupitia Neno lake. Kama ni mwongozo binafsi, hauhusiki na kweli kamilifu, basi ijulikane hivyo na kwa unyenyekevu kwa sababu inawezekana labda mimi sijaelewa uongozi wa Mungu! Kutofanya hivyo kutasababisha hisia kwamba Biblia siyo ya kutegemewa au kwamba mwongozo binafsi ni kamilifu.” (Wolvaardt 2005: 37)

#### **E. Maadili, mafundisho, na mifano ya kibiblia**

Matumizi yanafanana na kutafsiri kwa njia hii, kama vile ambayo maana inashuka “*kutoka juu kwenda chini*” (i.e., maudhui ya kifungu na aya huamua maana ya mstari na maneno), kwa hiyo pia kuna mtiririko katika mlolongo wa matumizi kutoka kwenye ujumla kwenda kwenye mahususi. Matumizi yote huanza kutoka kwenye lengo letu la kubadilishwa na kufanana na Kristo. Ili kufikia hapo, Biblia inatupa mlolongo wa vyanzo vya matumizi:

1. Maadili. Maadili ni kanuni ya msingi ya maisha kikristo. Kama chanzo cha matumizi maadili yapo karibu kabisa na lengo. Kwa hiyo, maadili ni chanzo cha jumla kabisa cha matumizi. “Zinatoa mwongozo kwa mwenendo mpana wa tabia bila ya kulenga tendo mahususi” (Doriani 2001: 84). Maadili yanahuisha mawazo kama: “*Utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili zako zote*” (**Mat 22:37; Marko 12:28-30**); “*mpende jirani yako kama nafsi yako*” (**Mambo ya walawi 19:18; Mat 19:19; 22:39; Marko 12:31, 33; Luka 10:27; Warumi 13:9-10; Wagal 5:14; Yak 2:8**); “*watendee wengine kama wewe unavyotaka wakutendee*” (**Math 7:12; Luka 6:31**); “*tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake*” (**Mat 6:33**); “*aliyepewa vingi kwake vitatakwa vingi*” (**Luka 12:48b**); “*vua utu wa kale na kucaa utu mpya*” (**Waef 4:22-24**); “*nia yetu ni ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, tujitahidi kumpendeza yeye*” (**2 Wakor 5:9**); “*lengo la mafundisho yetu ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki*” (**1 Tim 1:5**); “*msijiwekee hazina duniani bali jiwekeeni hazina mbinguni*” (**Mat 6:19-20; Luka 12:21**). Tambua kwamba maadili haya siyo yote ni amri. Maadili yanatupa sisi mipaka ya msingi au mtazamo wa namna tunavyoendesha maisha yetu. Yanatumika pale tunapofanya yale mambo na kufanya yale matendo ambayo yanayoendana na maadili, na kukataa yale mambo na matendo ambayo hayaendani na maadili.

2. Mafundisho. Mafundisho ni kweli za msingi za imani ya Kikristo. Mafundisho siyo mfumo mwingine tofauti ya Maandiko bali yameibuliwa kutoka kwenye Maandiko yote. Mifumo yote ya Maandiko inafundisha na ina matokeo ya kitheologia na ya kifundisho. Mafundisho ya kikristo huelezea ukweli halisi-asili ya Mungu, ya mwanadamu, kweli za kiroho na matokeo yake. Mafundisho yanahuisha mambo kama: Mungu wa Biblia ni Mungu wa pekee wa Kweli, Mungu ni utatu, Mungu aliumba ulimwengu, Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake, wanadamu wametenda dhambi, na nguvu ya dhambi ikayo ndani ipo katika vilindi vya utu wetu; Mungu alikuja duniani katika nafsi ya Yesu Kristo; hatuwezi kuijio koa wenywewe kutoka kwenye nguvu na hisia za dhambi, lakini tunaweza tu kupokea wokovu kwa neema kwa imani kwa njia ya Kristo; Roho Mtakatifu anakaa ndani ya waaminio; Kristo anatuita sisi kuishi maisha ya uaminifu na utii kwake kwa kuishi maisha ya upendo na kuwashudumia wengine; Yesu anakuja tena, naye atawahukumu walio hai na wafu, watu wote wana hatima ya milele,

au mauti ya milele jehanamu kwa wasioamini au uzima wa milele katika nchi mpya kwa waaminio.

a. *Mafundisho yanatumika tunapojiuliza maswali kama, “Kama fundisho X ni kweli, nini kinafuata?” na “Tabia yangu inatakiwa iweje ili iwe sawasawa na imani ninayokiri?”* (Doriani 2001: 85-86). Tunatumia mafundisho pale tunapoishi kwa kuyafuata.

b. *Kwa kuwa mafundisho yanatupa pitcha halisi ya ulimwengu, yanaongoza fahamu zetu.*

Kadiri imani yetu inavyobadilika, yapasa mitazamo na matendo kubadilika. Kwa mfano:

(1) Moja ya matokeo ya Mafundisho ya kwamba Mungu ni Utatu. Mungu yupo katika Utatu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu). Hii ina maana Mungu ni wa mahusiano. Kila nafsi katika utatu ina uhusiano wa upendo mkamilifi na nyingine katika Utatu. Mungu alituumba sisi kwa mfano wake. Kwa hiyo inatupasa kuhusiano na kupendana. Hatupaswi kujitenga na watu, bali tunapaswa kujitahidi kuwa na upendo na mahusiano mazuri na wengine.

(2) Moja ya Matokeo ya fundisho la hali ya dhambi ya asili ya mwanadamu. Kwa sababu ya fundisho la kikristo kuhusu mwanadamu kwamba ni mwenye dhambi, nguvu ya dhambi ikaayo ndani ya kila mtu, na watu kutengwa na Mungu, hatushangai wakati watu wanadanganya, wanaiba, wanatenda ujisadi, na kutusaliti sisi. Hatupaswi kushangaa watu wanapojiinua wenyewe na mafanikio yao wenyewe. Tunajua kwamba wamekosa amani ya ndani, usalama, na kujiona muhimu kwa namna zingine. Kwa hiyo wanajaribu kupata amani, usalama, na umhimu kwa njia zingine. Tunapoelewa mambo haya –yalijoka kwenye mafundisho ya kikristo—mtazamo wetu kuhusu wengine unabadijika na hatutaitikia maumivu au kuumizwa kama wengine wanavyofanya.

3. Mifano. Katika Agano la Kale na Agano Jipya masimulizi yake yanatupa mifano kwa ajili ya sisi kujifunza (tazama **Warumi 15:4; 1 Wakor 10:1-6**). Yesu alitoa mifano ya Biblia katika kukabiliana na shetani na mafarisayo (tazama **Mat 4:4, 7; 12:1-7**). Paulo aliwaambia watu “*wamfuate yeye*” (**1 Wakor 4:16; 11:1; Wafil 3:17**). Biblia haifichi dhambi hata za waamini (mfano., ulevi wa Nuhu, **Mwanzo 9:21**; Uongo wa Ibrahimu na ushauri kwa Sara wa kudanganya, **Mwanzo 12:10-20**; uzini wa Daudi na kuua, **2 Samweli 11**). Kwa hiyo, mifano inaweza kuwa hasi au chanya, mizuri au mibaya.

a. *Masimulizi ya kibiblia yanaturalika sisi kutathmini wahusika na matendo yao, na kujilinganisha na wahusika ili kupata mwelekeo wa kiroho au maonyo.* Wakati mtiririko wa matendo ya uaminifu unapotengeneza mkondo, hasa pale Mungu anapobariki matendo, tunapata mwongozo wa kufuata leo. Matendo ya kipekee siyo ya kawaida, hasa pale ambapo Mungu hakuyabariki na hayaendani na baadhi ya maagizo ya kiwango cha tabia. Pale ambapo simulizi halishauri au kumhukumu muhusika au matendo yake na hakuna mkondo au mtiririko, hatupaswi kuandaa somo la maadili kutoekana na mfano huo wa simulizi.

b. *Hata nyimbo za kibiblia na maombi zinatujenga sisi pale tunapozitafakari na kuzifanya kuwa zetu.* “Watu huthamini kile wanachosifu. Tukimsifu Mungu kwa haki yake, tunathamini haki. Tukisifu ukarimu wake wa upendo, tunafurahia ukarimu wa upendo. Kwa kumsifu Mungu kwa mazuri hayo, tunayathamini hayo na kuyaingiza katika maisha yetu wenyewe” (Doriani 2001: 92).

c. *Ni lazima tuwe makini sana tusifanye mfano kuwa amri.* Ni muhimu sana tukumbuke tofauti muhimu iliyopo kati ya maelezo na maagizo (tazama sehemu ya III.D., hapo juu). Yale yaliyomo ndani ya mifano ya kibiblia yanakadiria kwamba tayari tunajua lengo, maadili ya kibiblia, na mafundisho ya kikristo. Mifano inatakiwa iangaliwe kwa usahihi zaidi kama uthibitisho wa matumizi au kinyume cha matumizi tunayoshauriwa kutoka katika vifungu vingine.

#### F. Sheria, amri, na masharti ya kibiblia

Sheria, amri, na masharti yanalenga jambo maalumu kuliko kweli, mafundisho, na mifano. Katika kila nyakati sheria imekuwa na kazi mbili za muhimu: (1) kuhukumu wasioamini; na (2) inafanya kazi kama mwongozo kwa waumini wa namna ya kuonyesha upendo wao kwa Mungu (Lehrer 2006: 122). Kama yalivyo mafunuo mengine katika Biblia, sheria ya kiungu inajifunua hatua kwa hatua katika Biblia nzima.

##### 1. Mtazamo wa jumla wa sheria ya kibiblia.

a. *Wanadamu wameumbwa kwa sura ya Mungu, na maarifa ya Mungu ya kujua mema na mabaya imeandikwa katika hali ya asili ya watu wote.* Hilo ni kweli hata kabla Mungu hajatoa Amri Kumi na sheria zingine zote za AK kwa Musa (tazama **Warumi 1:18-23; 2:14-16**). Sheria ya Musa ilitolewa ili kutamka rasmi sheria ya kiungu, lakini pia kuidhinisha sheria maalumu na matumizi kwa Taifa la Israeli lililosimama katika mahusiano ya agano ya kipekee

na Mungu. Kwa hiyo, “sheria ya Mungu inasimama ikijitegemea pasipo sheria za Musa. Kwa hakika kuna mwingiliano, lakini siyo mambo mawili yanayofanana kabisa.” (Wells na Zaspel 2002: 143) Sheria za Musa zinadhahirisha tabia na utakatifu wa Mungu (msemo “*Mimi ni Bwana Mungu wako*” umerudiwa rudiwa katika sheria za Musa na maagizo). Sheria iliwekwa ili kufunua dhambi (**Warumi 3:19-20; 7:7-12**); “kuongeza” dhambi (**Warumi 4:15; 5:13-14, 20**); na kuwafunga chini ya dhambi (**Warumi 7:23; 8:2-3; Wagal 3:10-13; 5:1; Wakol 2:14**). Na kuwaongoza watu kwa Kristo (**Wagal 3:15-4:31**; tazama pia **Warumi 7:24-25**).

b. *Yesu alitimiza sheria kwa niaba yetu juu msabani (Mat 5:17-20; Yoh 19:30; Warumi 10:4; Waef b2:14-15; Wakol 2:13-15)*. Yesu alisema aliquja “kukamilisha” sheria (**Mat 5:17**). Kwa kawaida neno lina maana ya “kuifikisha kwenye maana iliyokusudiwa” (Hays 2001: 29). “Yesu hakuwa anasema sheria ni makatazo ya milele kwa waamini wa Agano Jipy. Kama hivyo ndivyo, Wakristo wa leo wangetakiwa kuendelea kufuata sheria za dhabihu na maadhishimo pamoja na zile za kimaadili na hilo lingekiuka kwa wazi maeneo mengine ya Agano Jipy” (Ibid.). Badala yake, kazi ya Yesu msalabani ilihitimisha *kusudi na asili ya makatazo* ya sheria ya AK (Sheria ya Musa). Kwa hiyo, wakristo hawapo chini ya au hawafungwi na Sheria za AK, amri, na masharti (**Warumi 6:14; 7:6; Wagal 3:1-4:7; 5:18**; pia tazama **Wakol 2:8-17**). “Kwa hali hiyo, hatutegemei Agano la Kale kuwa maelezo ya mwisho kama sheria ya maisha ya mwumini wa Agano Jipy” (Wells na Zaspel 2002: 149).

c. *Kuja kwa Kristo kulianzisha Agano Jipy na, sambamba na hilo, nyakati mpya za “sheria ya Kristo” (Wagal 6:2; 1 Wakor 9:19-21; tazama pia Warumi 7:4; 8:2)*. Kwa kuja kwa Kristo kumetokea “badiliko la sheria” (**Waeb 7:11-12**). Agano la Kale ni “*kuukuu*” (**Waeb 8:13**). “*Aondoaa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili*” (**Waeb 10:9**). Badala ya kuwa tunawajibika kwa Agano la Kale, sasa tunawajibika kwa Agano Jipy—“*Sheria ya Kristo*” (**Luka 22:20; 1 Wakor 11:25; 2 Wakor 3:6; Waeb 8:8-13; 9:15**). “*Sheria ya Kristo*” siyo tu mafundisho ya Yesu lakini pia yale ya waandishi wa AJ (tazama, mf., **Yoh 14:24-26; 16:12-15; 17:8, 18-20; 1 Wakor 14:37; Wagal 1:11-12; Waefeso 2:20; 1 Wath 2:13; 2 Wath 2:15; 3:6, 14; Waeb 2:3; Ufunuo 1:11**). Kwa msimamo huo, tunaweza tukazingatia matumizi ya sheria, amri, na masharti ya AK na AJ.

2. Sheria, amri, na masharti ya AK. Leo, hakuna aliyepo *moja kwa moja* chini ya amri *yoyote*, sheria na masharti ya AK kwa sababu tupo kwenye kipindi cha Agano Jipy na sheria ya Kristo. Hata hivyo, bado tunaweza kupata ufahamu kutoka katika hizo kwa ajili ya maisha yetu. “Yesu kwa Musa ni kama alivyo kipepeo kwa kiwavi. . . Ndani ya Kristo Musa anafikia ukomavu na kutokeza akichanua kikamilifu. Sheria ya Musa bado zina umuhimu, lakini ni pale tu zinapokuja kwetu kutoka kwenye mikono ya Bwana Yesu. Wakristo leo ni lazima waendelee kusoma habari za Musa na ni kwa faida kubwa, lakini wanaposoma ni lazima wavae miwani ya Kikristo” (Wells na Zaspel 2002: 157). Namna ya kutazama sheria, amri na masharti ya AK kimsingi ina pande mbili.

a. *Chunguza sheria, amri, na masharti ya AK kama matumizi maalumu au mifano ya mahali pote au kanuni za jumla na zitumie kwa kuzilinganisha*.

(1) Sheria, amri, na masharti ya AK: “toa mifano iliyovuviwa ya namna ya kuhusisha kanuni kwa mapana. *Sheria zinahuisha, zinazeleza, na kusafanua kanuni*. Sehemu za kisheria za sheria ya Musa zinaonekana kama zinatosheleza mwanzoni, lakini ukizitazama kwa karibu zitafunuliwa kwako kwamba ni sheria kwa ajili ya jambo maalumu zinazolezea kanuni ya jumla. Hizi sheria ni maalumu kwa ajili ya utamaduni wa wakati ule, na hivyo kuzifanya kuwa ngumu kuzitafsiri kutoka utamaduni mmoja kwenda mwingine. Bado yanatoa upekee, shehena ya kina ya sheria za kibiblia tunazohitaji.” (Doriani 2001: 246)

(2) Sheria, amri, na masharti ya AK leo zinatumika pale tu ambapo zinafanana kwa hakika na zile zilizopo kwenye Agano Jipy na kwenye mazingira yetu ya sasa. Ikiwa badiliko kati ya AK na AJ inasababisha “*badiliko la sheria*” (**Waeb 7:12**) kwa kiwango ambacho sheria ya AK, au mazingira ambayo yanahusiana nayo, hayafanani na sheria ya AJ ya Kristo au mazingira halisi tunayokutana nayo sasa, kufanana kokote kati ya sheria ya AK au hali na hali yetu ya sasa inafanywa dhaifu na kukosa umuhimu (au hata kutofaa kabisa).

b. *Chunguza jinsi AJ inavyochukulia sheria, amri na masharti ya AK*.

(1) Jukumu letu kama watafsiri ni kufahamu namna AJ inavyoshughulika na sheria za AK. “Kutafuta jinsi ambavyo sheria ya Musa imepata kushughulikiwa na Yesu na/ au waandishi wa AJ wamehitaji wajiusishe kwa kina. Lakini katika hii kazi ya mtafsiri-ni

lazima atumie Biblia yake nzima. Ni lazima asome Biblia yake nzima kama mkristo, kutoka kwenye mtazamo wake wa Agano Jipy, ili awe na uhakika, lakini ni lazima ametumie Biblia yake yote. Sheria ya Musa imetimizwa katika sheria ya Kristo, na ni lazima tuangalie na kuona uhalisia wa hili katika kila kipengele.” (Wells na Zaspel 2002: 160)

(2) Mara nyingi Yesu na waandishi wa AJ wamebadili sheria za AK kwa:

- (A) *Kubadili misingi yake*—ku waheshimu wazazi inahusiana na waamini duniani, siyo Waisraeli katika nchi ya Kanani, na udhihirisho kwamba ukiri wa imani ya mwana ni sahihi . . . [na kama] wakivumilia katika hili wanaweza wakajihakikishia kwamba wao kwa hakika ni waaminio na watakuwa na Mungu wanayempenda milele.” (Lehrer 2006: 137-46, **Waef 6:3**).  
(B) *Kuwakataza wao*—talaka (**Mat 5:31-32**).  
(C) *Kuwaruhusu wao*—sheria za vyakula (**Marko 7:19**); tohara (**Wagal 5:1-2**).  
(D) *Kuzikuza*—kuua kunahusisha chuki (**Mat 5:21-22**); uzinzi huhusisha tamaa (**Mat 5:27-28**).  
(E) *Kuziruhusu au kuzikuza kwa wakati huo huo au vinginevyo kuzibadilisha*—hatupaswi kuapa kabisa, bali kuwa wakweli katika mazingira yote (**Mat 5:33-37**); badala ya “jicho kwa jicho” tunatakiwa kutenda kutenda mema kwa wengine bila kujali ni wabaya kwetu (**Mat 5:38-42**); kuwapenda jirani zetu kunahusisha kuwapenda adui zetu (**Mat 5:43-47**).

c. *Mifano mitatu inayoonyesha jinsi Sheria, amri na masharti ya AK zilivyotazamwa kama matumizi maalumu ya kanuni kwa watu wote katika AJ, na kutumika kwa ulinganifu*

- (1) Sheria za AK kwa ujumla. Yesu na Paulo wote walinukuu amri za AK kama mfano wa kanuni kuu-sheria ya upendo (**Mat 22:36-40; Warumi 13:9**).  
(2) Sheria za Sabato za AK. Yesu anazitaja sheria za Sabato akizielekeza kwake na kwenye kanuni ya huruma (**Mat 12:1-8; Marko 2:23-28; Luka 6:1-11**). Alionyesha kwamba hata zile sheria za msingi za AK zinapaswa kukiukwa ikiwa kwa kuzitii tutaenda kinyume na kanuni ya msingi.  
(3) Kumb 25:4—“Usimfunge ng’ombe kinywa apurapo nafaka.” Kwa nyakati mbili (**1 Wakor 9:9; 1 Tim 5:18**) Paulo alinukuu sheria inayomhusu ng’ombe. Mara zote mbili aliitazama hiyo sheria kama mfano wa matumizi ya *kanuni kwa mapana yake*. Paulo alinukuu sheria kuunga mkono kanuni kwamba *wale wanaongoza kanisani na kufundisha Neno la Mungu wanapaswa kulipwa*. Kumbuka kwamba katika muktadha halisi au wa kihistoria wa AK hakuna mstari unaoonyesha chochote kuhusu kuwalipa viongozi wa kiroho. Kwa habari ya unabii, AJ wakati mwingine hutumia vifungu vya AK kwa namna nyingine. Ndiyo maana ni lazima tutazame AK kwa macho ya AJ (siyo kinyume chake).

d. *Mfano wa Yesu wa Sheria ya Sabato na mfano wa Paulo wa ng’ombe ni lazima ututie moyo na kutusukuma kutenda.* Wote wawili walitazama kwenye kanuni ya msingi ya sheria, na siyo maandishi ya sheria pekee. Hata hivyo, sisi siyo Yesu wala Mitume. Paulo aliitazama sheria kwa muktadha halsia au wa kihistoria katika **Kumb 25:4**. Hiyo kanuni inaonekana kuwa inahusiana na wajibu wa kumtendea kila mtu kwa usawa na haki kwa sababu watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, na kwa wakristo utakuwa ni wajibu mkuu kiasi gani: hii ina maana kuwa “ikiwa Bwana alilinda haki ya ng’ombe kama fidia ya halali wapurapo nafaka za Wana wa Israeli, ni kwa kiasi gani anategemea kwa wale aliomwakomboa kutoa mahitaji ya vitu kwa wale wanaopanda katika mioyo yao mbegu ya Injili iletayo uzima!” (Johnson 2007: 282) Tunaweza kutazama kimantiki kanuni za msingi za AK, lakini tunapaswa kufanya hivyo kwa kutumia kanuni za hemenutiki na eksejesis sahihi.

3. Sheria, amri, na masharti ya AJ.

- a. *Sheria, amri na masharti ya AJ (i.e sheria ya Kristo) yanaweza kutumiwa moja kwa moja leo kwa namna ambayo AK haiwezi.* Mifano ya sheria za AJ zinazotumika moja kwa moja ni pamoja na: **Warumi 12:9-21; 1 Wakor 6:18; Waef 4:25-32; 1 Wath 5:16-18;** na **Waeb 10:23-25**.  
b. *Sheria, amri, na masharti ya AJ, hayashughuliki na mambo yote yanayohitaji kwa jamii zetu za leo.* Vitabu vya AJ viliandikwa kwa makanisa maalumu na watu binafsi, na vilishughulika na mambo binafsi ambayo haya makanisa yalikabiliana nayo kwa muktadha wa tamaduni zilizokuwepo wakati ule. Matokeo yake, hata sheria za AJ, amri na msharti tunaweza kuhitajika

kuangalia kanuni zilizojificha ndani ya sheria hizo na kuzitumia kwa kutumia *ulinganifu* kulingana na mazingira halisi tuliyonayo. Kwa baadhi ya mambo, hasa mahali utamaduni umebadilika, tunaweza hata kwenda zaidi ya maneno ya sheria, amri na masharti ya AJ na kutumia “nia” ya ukombozi ya maneno hayo.

**G. Kuna “umahususi na pengo la jambo” kati ya jambo ambalo linaelezwa na Biblia na tunalokutana nalo, kwani Biblia haiongelei moja kwa moja au kimahususi kila jambo ambalo tunaweza kukutana nalo**

1. Biblia haikuhusika kimaalumu na kila kitu ambacho kinahuhsika kwa jamii ya siku zetu leo. Biblia ni mwongozo unaotosha wa jinsi tunavyotakiwa kuamini na kuishi. Inashughulika moja kwa moja au kimaalumu na jambo fulani maalumu ambalo watu walikumbana nalo wakati inaadidikwa. Maendeleo ya kiteknolojia yameibua maswali ambayo hayakuwa rahisi kuulizwa wakati Biblia inaadidikwa (mf). Kukuza kiumbe kwa kutumia vinasaba “kukuza viumbe kimaabara”). Tamaduni tulizonazo leo zinaweza kuwa tofauti sana na zile zilikuwepo nyakati za Biblia. Kwa hiyo, jambo ambalo Biblia inashughulikia linaweza lisifanane na jambo au hali ambazo sisi tunajikuta nazo. Zaidi ya hayo, Biblia haijalazimika kuongelea kila kitu kwa ukamilifu au kwa kina katika kila jambo ambalo limejadiliwa ndani yake.
2. Wakati tunapokutana na jambo ambalo halijaongelewa na biblia moja kwa moja au kimaalumu, tunatakiwa kutafuta jambo linalofanana na hilo kwenye Biblia, mafundisho, mifano, sheria, amri, na sheria ambazo zinakubalika katika hali yetu, jaribu kutavumbua kanuni na “nia” ya ukombozi ambayo ipo nyuma hizo kweli, mafundisho, mifano, sheria, amri, na sheria na zitumie kwa namna inayoendana na mazingira yetu. “Ulinganifu” ni mfanano kati ya vitu viwili amba o unategemea (mfano kuna ulinganifu kati ya moyo na pampu). Tunakabiliana na jambo ambalo Biblia haijalielezea moja kwa moja tunaitumia Biblia kwa kufananisha kwa: a. kutambua hali za kibiblia na vifungu (ikihuhsisha ukweli, mafundisho, mifano, sheria, amri, na sheria) ambavyo vinaonekana kufanana na kufaa (i.e., mfanano) katika hali yetu; b. kutafuta kanuni za kibiblia na nia ya ukombozi nyuma ya hizo hali za kibiblia na vifungu vyake; na c. kutumia kanuni na nia ile kwa ajili ya mazingira yetu.
3. Ulinganifu ni mzuri ikwa tu unafanana na hali tunazokutana nazo leo. Kutumia kweli za kibiblia, mafundisho, mifano, na sheria kwa kufananisha ni sambamba na kutumia maamuzi yanayokubalika kisheria katika mazingira mapya kwenye mahakama ya kisheria. Ikiwa mazingira au hali iliyo iliyojificha nyuma ya kweli, mafundisho, mifano, sheria, amri, au masharti ya kibiblia ambayo tunafikiria yanafaa kwa mazingira yetu hayafanani na mazingira tunayokutana nayo, hiyo hali ya kufanana ni dhaifu na inapungua thamani (au bila thamani kabisa). Biblia ni mwongozo unaotosha kwa yale tunavyotakiwa kuyaamini na jinsi tunavyotakiwa kuishi. Hivyo, tutaona kwamba kila jambo la kimaadili tunalokutana nalo, kwa hakika litakuwa linahusiana na kanuni ya kibiblia inayofaa kwa tamaduni zote, nia ya ukombozi ya kibilia, na kweli kamilifu za kibiblia. Hata hivyo, kwa kuwa Biblia haishughuliki kimaalumu na kila jambo ambalo tunaweza kukutana nalo, tunaweza kuzipambanua hizo kanuni, nia, na kweli kamilifu ikiwa tu tuna ujuzi wa kutosha wa Biblia na ufahamu wa kuweza kufanya eksejesi ambayo ni sawa na sahihi.

**H. Kuna “pengo la kitamaduni” kati ya utamaduni wa Biblia ikihuhsisha—sheria, amri, na masharti kulingana na tamaduni hizo—na tamaduni tofauti za siku tunazoishi leo**

1. Mawasilano ya Mungu (Biblia) yalitolewa katika wakati fulani maalumu, katika utamaduni maalumu, kwa watu maalumu, amba o walikuwa wanakabiliana na mazingira mahususi. Hata hivyo, Mawasiliano ya Mungu, yalirekodiwa ili kutumika kama ujumbe kwa watu watakaofuata baadaye. Matokeo yake, “Changamoto kubwa ya kielimu ya kutumia maandiko *ni kuziba pengo kati ya tamaduni za Biblia na tamaduni za sasa*” (Doriani 1996: 143). “Ingekuwa ni kujidanganya kutangaza katika ulimwengu wetu msimamo wa kitheolojia bila kupeleleza hadhi yake ya kitamaduni au uwezekano wa kuweza kutumika kwa tamaduni mbalimbali” (Webb 2001: 24). Pengo la kitamaduni linasababisha umuhimu wa matumizi ya kanuni za hemenutiki na eksejesi sahihi—hata kwa sheria za AJ, amri, na masharti. Zaidi ya hilo, katika mambo mbalimbali maagizo ya kibiblia yanakusudia *kushughulikia tamaduni* ili kuwafungua watu kutoka kwenye vifungo vya tamaduni zao. Matokeo yake, hata sheria za AJ, amri, na masharti hayatakiwi kutumika “bila kuchambuliwa” bali kwa kuyafanya maboresho, yakisimamia kanuni za msingi, ili kuendana na hali zilizopo. Hii ina umuhimu mkubwa kwa wakristo tunapoitikia utamaduni unaobadilika: tunatakiwa kuzipa changamoto tamaduni zetu pale zinapokinanza na vithaminisho vya kifalme, lakini tukijifananisha na mambo yanayohusiana na tamaduni zetu wala “siyo kweli kamilifu”
2. Siyo sheria zote, amri, na masharti, yanaweza kutumika kwa namna inayofanana katika muundo amba o zimetolewa kwa sababu siyo sheria zote, amri, na masharti zimetolewa kama maagizo

makamilifu ya Mungu kwa watu wote na tamaduni zote.

- a. *Watu wengi, wakiwemo wachungaji wengi na walimu wa Biblia hawaelewi kwamba “sehemu nyingi za Biblia hazikuandikwa kuunda jamii kamilifu yenye haki na usawa mkamilifu”* (Webb 2001: 41). Kwa hiyo, ugumu mwagine katika kutumia sheria zote za AJ, amri, na masharti moja kwa moja katika njia iliyonyooka ni kwamba, “Maandiko yenyewe yana kitu tunachokiita ‘vithaminisho vya kifalme’ (vile ambavyo vinaingia kwenye tamaduni zote na wakati wote) pamoja na vithaminisho vya kitamaduni(vile ambavyo vimefungwa ndani ya utamaduni mmoja na muda)” (Webb 2001: 23). Ni sehemu ya matumizi ya kazi ya kutafsiri kutofautisha kati ya hayo mambo mawili.
- b. *Ni kwa sababu tu ya uwepo wa mabadiliko ya kitamaduni kulingana na wakati, na ukweli kwamba tamaduni zetu zinatofautiana na zile za nyakati za Biblia, ndiyo inayotusaidia kuona kwamba siyo sheria zote za Biblia, amri, na masharti ni matamko ya vithaminisho vya kifalme kwa kila tamaduni na kila wakati.* “Ndani ya kifungu cha Maandiko tunaona sehemu ambazo ni za kila tamaduni(kwa mfano upendo kwa ajili ya jirani) na sehemu ambazo ni za kitamaduni, au kwa uwazi zaidi sehemu ambazo zina vipengele vya kitamaduni (mf., vifungu vya kitumwa). Kwa msomaji wa awali haya mambo mawili—ya kitamaduni na yale ya kila tamaduni—havikuwa vinapingana. Kwa namna zote, tofauti kati ya hayo mawili isingeonekana kwa msomaji wa kwanza. Ni katika muktadha wa utamaduni mwagine tofauti hizo zinaonekana kwa urahisi kutoekana na kanuni ya kupingana.” (Webb 2001: 24)
- c. *Mifano ya sheria iliyo na mipaka ya kitamaduni imetolewa kwenye Biblia.* Vifungu vya kitumwa, haki ya mzaliwa wa kwanza wa kiume vifungu vinavyoongelea kuhusu serikali ya kifalme au ilioegemea kwenye utawala wa mwanaume badala ya utawala wa sheria, vifungu ambavyo vinaonyesha umiliki wa mwanaume na utawala dhidi ya wanawake, na mambo mengine kama hayo vina kiwango cha kufungwa ndani ya mipaka ya utamaduni.

3. Sababu za Biblia kutamka vithaminisho na sheria ambazo zimefungwa katika utamaduni mmoja.

Kuna sababu kadhaa kwa nini Biblia—ikihusisha amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu Mwenyewe—zinatangaza mambo ambayo ni kitamaduni tu pamoja na vithaminisho vya kifalme ambavyo ni kwa tamaduni zote. Hizi zinahusisha yafuatayo:

- a. *Vithaminisho vinavyotolewa na Biblia vinahusiana na utamaduni ili vifae na kueleweka.* “Ulimwengu wa kale katika kilimo chake, ulijikita katika utawala wa kifalme, familia kubwa, mambo yahusuyo mapambano dhidi ya maisha, na kadhalika, inachangia kwa umuhimu mkubwa katika uundwaji wa Maandiko katika mipaka ya kikombozi. Mambo mengi yaliyokuwa kweli katika ulimwengu wa kale si sehemu ya ulimwengu wetu wa leo. . . . Kama baba mwenye busara, Mungu anaongea na watoto wake kwa lugha, mtazamo na uhalisia unaoenda sambamba na ulimwengu wanaouona na kuuishi. Matamko mengi katika Maandiko huakisi aina hii ya kipengele cha mtazamo wa kijamini.”(Webb 2001: 64, 65)
- b. *Watu hawawezi kubadilisha misimamo isiyobadilika kirahisi, kwa hiyo mara nyingi ni lazima wasukumwe “hatua kwa hatua” kuelekea kiwango cha thamani za maisha.* “Wachungaji wanatakiwa kutambua kimaalumu kipengele hiki cha kichungaji katika maandiko. Katika kuwapeleka watu kuelekea kwenye lengo fulani, wachungaji wenyewe busara huwachunga watu wao kwa kiungana na kwa upendo kwa mwendo amba wanaumudu. Mchungaji anaenda vema na wakati anaelewa mtu hawezikubadilisha mtazamo kuhusu mambo ya kawaida ya maisha ya mtu mwagine kwa siku mmoja. . . . Waandishi wote wawili wa kiungu na kibinadamu hufanya kazi pamoja kiungwana katika uhusiano wa kichungaji kwenye jamii ya agano. Vifungu vya kibiblia mara zote huwakilisha barua za kichungaji, yaliyoandikwa ukiakisi moyo wa huruma wa kichungaji. Maneno yao yanaundwa “kuvuta” watu waliopo kwenye agano kwenda mbele kwa kadiri iwezekanavyo kama vile mpira lakini bila kuruhusu “kukatika.” Mabadiliko siku zote ni magumu. Watu hawawezi kubadilisha taratibu zao za kijamii kirahisi. Mungu anawapitisha watu wake kwenye njia ya mabadiliko yanayowezekana kufanyika kwa namna inayotambua asili ya mwanadamu.” (Wells 2001: 59, 58) Njia hii ina kipengele kinachofundisha na kipengele cha kichungaji. “Maandiko, kama njia nzuri ya mafundisho, yameandalowiwa kuwatoa watu mahali walipo (panapojuilikana) na kuwasaidia kufiki kwenye hatima inayotarajiwa (pasipojuilikana) amabayo ina mwendelezo sambamba na yaliyopo ili kwamba njia itokee ya kufikia hatima inayotarajiwa” (Ibid. 60). Kwa kiwango kikubwa kuna kuchanganyikiwa kunakojitokeza katika maisha yetu kati ya natharia na halisi.
- c. *Katika tamaduni za kibiblia zilizopo, hata zile za kikombozi kwa kiwango cha chini, thamani zilizojifunga katika utamaduni na mifumo ya kijamii, ndani yake zina vithaminisho vizuri vyenye*

*mwengamo wa kifalme.* “Kwa mfano, utumwa ulikuwa kama jambo la mtandao wa huduma ya kijamii katika utamaduni wa kale. Hasa muundo wa utumwa kwa sababu ya deni katika Israeli ulisaidia wale walio na mahitaji makubwa ya kifedha. Ilifanya kazi nzuri na ya heshima.” (Webb 2001: 64) Kwa hiyo, hata pale ambapo Biblia imetoo “maadili ya kitamaduni” yanayohusiana na mahali na wakati ambapo Maandiko yalisomwa kwa mara ya kwanza, bado yalikuwa yakisema *kwa nia ya kuwakomboa watu waliokuwa katika tamaduni hizo.*

d. *Ili kutunza yale ambayo mwishoni yana umuhimu mkubwa ina maana kuwa utaweka mambo mengine ya thamani katika nafasi ya pili.* Mungu ana vipaumbele, hata kati ya vitu ambavyo aliwaamuru watu wayafanye ambayo ni mazuri. Kwa hiyo, uaminifu na moyo uliopondeka ni bora kuliko sadaka (**1 Sam 15:22; Zab 51:17; Hos 6:6**). Haki, rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu ni mahitaji ya muhimu sana (**Mika 6:8**). Amri kuu kuliko zote ni kumpenda Mungu kwa miyo yetu yote na kuwapenda jirani zetu kama sisi wenyewe (**Mat 22:36-40; Marko 12:28-34**). Haki, rehema, na uaminifu ni “*ni kati ya mambo mazito ya sheria*” (**Mat 23:23**). Kwa kuongezea katika mlolongo wa mpangilio katika amri alizotoa Mungu, thamani ya kuhubiri Injili ni kubwa zaidi ya miradi mingine ambayo ina kipaumbele cha chini. “Mara nyingi mafundisho ya Maandiko hayaakisi maadili makamilifu kwa sababu yamemezwa na uzuri wa kiwango cha juu wa uwezeshaji wa misheni. Kutimizwa kwa misheni ya kikristo Mara nyingi kunawavuta waamini kutoa kilicho bora kwa maisha kwa ajili ya kuwavua wengine. Au, inakadiriwa kuachana na kutafuta heshima katika maeneo yote ya maisha, na kuridhika na maisha yenye ubora wa wastani kunahitajika, ili kuweza kuweka mkazo katika kusudi kuu la umisheni.” (Webb 2001: 63)

4. Kushindwa kutofautisha kati ya mambo yanayohusiana na utamaduni peke yake na yale ambayo yanavuka tamaduni—“*kweli kamilifu*” ni sababu kubwa inayotokana na makosa katika matumizi ya uhuru na kuwa chini sharia. “Hatutakiwi kufanya vitu ambavyo vinafaa kwa tamaduni zote na kuvifanya kuwa vya utamaduni mmoja tu. Kwa upande mwengine, hatutaki kuvifanya vitu vya kitamaduni na wala si kweli kamili na kuvifanya kuwa kweli kamilifu kwa kila utamaduni.”

(Webb 2001: 24)

a. *Uliberali* kwa sehemu kubwa unachukulia “*kweli kamilifu*” za Biblia ambazo zilitumika kwa wapokeaji wa awali na watu wengine wote, na kuvitazama kama vya kitamaduni tu na “*vinahusika*” na wapokeaji wa awali tu na kwamba wengine wote wanatakiwa kupuuza. Maliberali wana tabia ya kuchukulia kila kitu kuwa ni cha kitamaduni.

b. *Kujiweka chini ya sheria* kinyume chake. Waishio chini ya sheria huchukua zile sehemu za Biblia “*zinazohusika*” na utamaduni ambazo zilikuwa na maana tu kwa wapokeaji wa awali tu, na kuvichukulia kama “*kweli kamilifu*” zinazotakiwa kutumiwa na watu wote. Kwa uhalisia, waishio chini ya sheria wanatazama kwenye muundo wa amri ya kibiblia, lakini kamwe hawatazami muktadha au kanuni ilijoificha nyuma ya amri na mfumo.

5. Kufanya uchambuzi wa tamaduni katika Biblia ni muhimu ili kuthibitisha matendo yetu wenyewe na kuweza kutoa sababu pale tunapokuwa hatufanyi kama yalivyo maadili ya baadhi ya sehemu za maandiko.

a. *Uchambuzi wa tamaduni za Biblia ni wa muhimu ili tuthibitishe matendo yetu wenyewe.*

“Makanisa mengi ya Magharibi leo kamwe hawafanyi kama Biblia inavyosema (kwa namna ya inayoelezwa) kuhusu kufunika kichwa, busu takatifu, kuosha miguu, mtindo wa nywele, utumwa, na kadhalika. Lakini hatukuweka wazi kwa nini tumeacha baadhi ya matendo na huku tukiendeleza mengine. Kukosekana kwa maelezo na msimo kumeacha matatizo yanayochoma kama miiba kwa kizazi kinachokuja cha Wakristo.” (Webb 2001: 246)

b. *Uchambuzi wa tamaduni za Biblia ni wa muhimu ili kuweza kutoa sababu kwa nini tunatenda chini ya kiwango cha maadili yanayopatikana katika maandiko.* Mpaka pale tutakapojobu kutockana na utamaduni uliokuwepo wakati maandiko yanatolewa, tutaendelea kushindwa kujitetee dhidi ya hoja zinazotokana na kuachwa kwa wazi kwa baadhi ya matendo, amri, sheria na masharti yanayopatikana kwenye Biblia. Baadhi ya hoja za kupinga zinaita Biblia kuwa ni ya kinyonyaji au ya kinyanyasaji ikizingatia watumwa au wanawake. Ingawa, hivyo ni kusema kuhusu maandiko kutoka kwenye utupu, bila kutambua kwamba kulikuwa na muktadha wa kijamii na mambo ya kitamaduni yaliyosalia kwenye maandiko. Hiyo ni namna ya kizamani [i.e., kumwakilisha mtu fulani kama tokeo au kitu fulani kama tukio nje ya mlolongo uliokuwepo au mtiririko wa kitamaduni] ya kusoma kifungu! Kwa kuhusisha na wapi au lini maandiko yamesomwa kwa mara ya kwanza, walinena kwa nia ya ukombozi na jamii zilizokuwepo.” (Webb 2001: 254) Kwa hiyo, kushindwa kwetu kuchambua matokeo ya

utamaduni katika Biblia inaumiza juhudini zetu za kiinjili na kuweka vikwazo kwenye imani za watu.

### **I. Sababu zinazosaidia kuelewa vifungu vya Biblia vilivyofungwa kwenye utamaduni fulani na vile vya tamaduni zote**

Kufanya uchambuzi wa kitamaduni wa Biblia—yaani., kujaribu kutofautisha kati ya kifungu cha biblia ambacho kinaelezea jinsi kinavyovuka mipaka ya kitamaduni “halisi” au “kweli zisipitwa na wakati” (yaani., zile zinazotumika kwa watu wote na wakati wote), na zile ambazo “za wakati maalumu” au “maalumu kwa ajili ya utamaduni husika” (yaani., zinazofungwa na utamaduni fulani maalumu wa kibiblia ambaa mwandishi alikuwa akishughulika nao), au una matumizi yenye mipaka kwa sababu nyingine—zinaweza kuwa ngumu sana. Hii ndiyo maana matumizi sahihi, kama uchunguzi sahihi wa maana halisi ya neno ni sanaa na sayansi pia. Inahitaji ujuzi. Maswali yafuatayo na vigezo, kutoka kwa Klein, Blomberg, na Hubbard (1993: 411-21), Doriani (2001: 249-50), Webb (2001: 69-235), na Tiessen (1993: 189-207), zinaweza kusaidia sisi kutambua ikiwa kanuni za kibiblia au ulingalinifu unafaa kutumika kila wakati na mahali pote au kuna mipaka kwa tamaduni fulani maalumu au hali iliyokuwa inashughulikiwa katika Biblia wakati huo. Pamoja na hayo tunapaswa kukumbuka kwamba hakuna sababu kati ya hizi ni sawa kila wakati. Siyo zote zinatumika kwa jambo mahususi. Baadhi zinaweza kuelekeza katika mwelekeo fulani na baadhi mwelekeo mwingine.. Hata hivyo kwa kujiuliza maswali yafuatayo; tunaweza kutambua, kwa hali yeoyote ile, ni kigezo au ukweli upi una umuhimu mkubwa na msukumo wa jumla wa kutaka kufahamu ikiwa kifungu chenyewe kina mipaka ya kitamaduni au la.

1. Je kifungu peke yake, au muktadha mzima wa kitabu chenyeye kifungu kinalazimisha matumizi kwa hali zote au kinasilitiza matumizi ya kiujuu? Ahadi zenyenye masharti zina maana pale tu ambapo masharti yamezingatiwa. Hivyo, maelezo ya Yesu' **Mat 7:7** ("Ombeni nanyi mtapewa") ni sharti kwa mujibu wa muktadha mzima wa **Mat 6:1-15** kwamba maombi yetu siyo ya kibinagsi na ya kujitokuza, bali yanatukuza Jina la Mungu na kutamani ufalme wa Mungu na ni kujiweka katika mikono yake na mapenzi yake mema. Yesu anamtahadharisha Petro kwamba angekufa kwa ajili ya imani yake (**Yoh 21:18-19**) kwa kuzingatia maelezo yake kwa Yohana kwa habari siku zake zijazo (**Yoh 21:20-23**). Hayo ni mahususi kwa hao wahusika. Pamoja na hayo, aya zingine zinatusaidia kufahamu kwamba mfano wa Petro si wa kipekee lakini ni mfano wa kanuni ya jumla kwamba "mtumwa si mkuu kuliko bwana wake" (**Yoh 13:16**), na "wote wanaotamani kuishi kwa ajili ya Mungu ndani ya Kristo watateswa" (**2 Tim 3:12**). Hata maagizo ya jumla ya Yesu yatahitaji kustahilishwa na vifungu vingine na kanuni. Hivyo, katika **Mat 5:39** alisema tusishindane na mtu mwovu; hata hivyo, katika **Mat 10:23** akasema kimbieni mnapotewa.  
2. Je ufunuo kuhusu aya unaweza kuwa na matumizi ambayo ni kinyume na kitabu chenyeye aya hiyo? Hili swali linapaswa kuulizwa kwa ajili ya kila kifungu cha AK. Lakini pia katika AJ. Katika **Mat 10:9-10** Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wasichukue fedha wala chochote pamoja nao, bali wategemee ukarimu wa wale wanaowahudumia. Katika **Luka 22:35** Yesu akabadili ile amri, akawaagiza wachukue panga na mikoba pamoja nao. Katika **Luka 10:1** Yesu aliwaambia wanafunzi wake waende wawili wawili," lakini katika **Matendo 20:4** Paulo aliongozana na wengine saba. Kwa ujumla zaidi, katika **Mat 5:41-42** Yesu anasema tunapaswa kwenda maili mbili zaidi na kila anayetusihii kwenda naye maili moja. Ingawaje, kutumia misemo hiyo bila kuzingatia hali zingine na maandiko (mf., **Zab 37:21** kuhusu fedha) itakuwa siyo sahihi. "Ikiwa kwa mfano, Mimi ni mtaalamu wa upasuaji wa moyo na ninaelekeea kufanya upasuaji, Sipaswi kwenda na mtu hata maili mbili. Ni lazima niseme hapana na niishie mwisho wa maili ya kwanza na niage kwa haraka huku nikimtakia safari njema. Nina mambo mengine ninayojua ninatakiwa kufanya, na ni lazima nifanye maamuzi. . . Ikiwa ninadaiwa na mwenye duka ambaye tayari nimeshatumia bidhaa zake, siko huru kumpa fedha hizo yeye anayeniomba-labda kuwe na mazingira mengine maalumu sana yanayolazimu. . . Katika mazingira nyeti tunatakiwa kujihoji wenywewe, na kusema hapana 'Nifanye sawasawa na Yesu anavyooleza katika maelezo yake?' lakini 'Je mimi ni aina ya mtu ambaye Yesu anamweleza haya?'" (Willard 1997: 179-80)  
3. Je yapo mafundisho maalumu 'yanayopingana' mahali popote yanayoonyesha kuwa yanahuu hali fulani maalumu na ya pekee? Agizo la Mungu kwa Ibrahimu kumtoa mwanaye Isaka (**Mwanzo 22**) Na Hosea kumwoa kahaba (**Hos 1:2**) ni mifano miwili ya mafundisho hayo. Usiue (tazama, mf., **Kutoka 20:13; Ufunuo 21:8**) na usafi katika mahusiano ya ndoa (tazama, mf, **1 Wakor 6:16-20**) ni maadili ya msingi ya kibiblia na ya kikristo. Hata hivyo, mifano hiyo pia ni maelezo ya uaminifu wa Mungu katika mazingira magumu sana na uaminifu wa Mungu kwao.  
4. Je matumizi ya awali ni kwa ajili ya wale tu walioandikiwa? Kipengele cha kifungu kinakuwa kwa ajili ya mlengwa peke yake zaidi pale kinapokuwa kimemlega yeye kibinagsi katika maelezo yake. Aidha muktadha unaofuata mara au aya inayofuata inaweza kutoa mwanga ikiwa matumizi ya kifungu

ni kwa ajili ya mtu binafsi aliyeandikiwa au kwamba kinaweza kutumiwa kwa ajili ya wengine pia kwa nyakati na mahali pote. Kwa mfano Yesu alimwambia, Yesu alimwambia “yule tajiri kijana,” mtu binafsi, “*aende akauze vyote na kuwapa masikini*” (**Marko 10:21**; pia tazama **Mathayo 19:21; Luka 18:22**). Ingawa, katika **Luka 19:1-10** Zakayo hakuagizwa kuuza vyote alivyonavyo na kuwapa masikini pamoja na kwamba Zakayo kama yule mtawala kijana ni mtu tajiri. Badala yake Zakayo kwa hiari yake akachagua kutoa nusu ya mali yake kwa masikini na alipongezwa na Yesu kwa kufanya hivyo. Hii inaonyesha kwamba hitaji la kuuza vyote ili kumfuata Yesu si kwa wote. Vile vile, katika **1 Tim 5:23** Paulo alimwambia Timotheo “*Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara.*” Hayo ni maagizo ya wazi na siyo maelezo tu.. Je hii ni “theolojia kuhusu pombe”? Kwa maana hiyo sasa wakristo wote wanatakiwa kunywa pombe? Jibu ni “hapana.” “lako” inaelezea umoja, ikionyesha kwamba Paulo anaongea na Timotheo kama mtu binafsi na siyo kanisa kwa ujumla. Pia, **5:23** ni “iko pembeni” (ni mapendeleko mafupi yasiyohusiana na masomo yanayowasilishwa na vifungu vinavyozunguka mstari huo). Maelezo mengine ya mstari yaliyosalia yanatoa sababu ya ushauri wa Paulo ikiwa ni kanuni ya uwakili na mtu kuujali mwili wake mwenyewe. Kwa hakika kulikuwa na tatizo kwenye maji mahali ambapo Timotheo alikuwa, na hilo lisababisha tatizo la tumbo kwa Timotheo. Mvinyo ulikuwa na uwezo ya kutatua tatizo hilo. “*Kwa ajili ya*” inadhihirisha kuwa Paulo alikuwa anatoa maelekezo ya kitabibu. Maelezo ya ziada ya Paulo yalilenga kuhusika kwake kwa ujumla kwa ajili ya afya ya Timotheo na uwakili wa mwili. Hakuna lolote linaloashiria kutoa msimamo wa kitheolojia kuhusiana na pombe katika hili. AJ linafafanua katika maeneo mengi somo hilo, kwa njia ya maelekezo na maagizo (mf., **Yoh 2:1-11; Warumi 13:13; 14:1-23; 1 Wakor 5:11; Waef 5:18; Wakol 2:16; 1 Tim 3:3; 8; Tito 1:7**). Aya hizo zote (na zaidi), pamoja na AK hulisemea somo hilo, zinapaswa kujifunzwa ili kupata msimamo wa kitheolojia kuhusu pombe. 5. Je kifungu kinasimama chenyewe kuelezea kanuni nzima ya kimaadili au ya kitheolojia au ni udhihirisho wa uwepo wa au maelezo ya kanuni katika mapana yake? Kipengele cha kifungu kinaweza kuhusika na utamaduni na mafundisho yake maalumu yanaweza kuwa hayaendani na kanuni ya jumla ya kimaandiko au kama ikiwa ni matokeao ya matumizi ya kipekee zaidi ya kanuni ya jumla. Misemo fulani mahususi inaonekena kuwa ya kitamaduni zaidi kuliko ya kijumla. Kwa mfano, sheria ya kuwajali maskini katika (**Mambo ya Walawi 19:9-10; 23:22**) inaonekana kuwa ni matumizi ya kipekee ya kannuni ya jumla ya kuwajali masikini. Kwa hiyo, sheria ya kukusanya mavuno inaonekana kuwa ya kitamaduni lakini kanuni inayosimamiwa inatumika kwa tamaduni zote. Katika **Luka 7:46** Yesu alimkemea mwenyeji wake kwa kutompaka kichwa chake mafuta lakini akampongeza mwanamke kwa kumpaka marahamu. Kupaka mafuta kunaonekana kuwa ni tendo la kitamaduni la kudhihirisha kanuni ya jumla isiyo ya kitamaduni ya kuonyesha heshima kwa watu wengine.

6. Je sababu ya kufanya jambo fulani linaweza kuwa “utamaduni na kwa ajili ya utamaduni huo tu,” au linazingatia sababu za wakati husika tu kwamba haliwezi kuhamishika na kutumika kwa tamaduni zingine au kuna masharti ya kitamaduni yaliyoelezwa kwenye maandiko au yamedhaniwa kuwepo na mwandishi ambayo yanafanya kifungu kisiweze kutumika kwa namna inayolingana? Namna moja ya kutazama mazoea fulani ikiwa ni ya kitamaduni au ya kijumla ni kuchunguza kama linahusu matendo ya maadili au linalofaa zaidi. Hii inafanana, lakini siyo sawa sawa, kwa swali lifuatato. Jambo la kimaadili mara zote linakuwa si la utamaduni mmoja tu. Jambo linalofaa au linalokubalika kwa jamii linalekeea kuwa la kitamaduni zaidi. Ikiwa kifungu cha maandiko ni ya kitamaduni au la mazingira hayo kwa wakati huo, matumizi yake yanakuwa yamefungwa katika utamaduni huo na wakati huo. Vile vile ikiwa ukweli wa msingi wa maelezo ya kibiblia hauwezi kudumishwa unapohama kutoka utamaduni mmoja kwenda mwингine basi ukweli unaoweza kudumishwa hudhihirisha kuwa yapo mambo yaliyofungwa katika utamaduni husika pekee. Kwa mfano, rejea katika **1 Wakor 11:2-16** kuhusu nywele ndefu kwa wanawake, kama iliyotajwa katika **11:5-6** kwamba nywele fupi ni “aibu,” inaonekana kuwa maalumu kwa utamaduni husika. Muktadha wa kihistoria unaonyesha kuwa mwanamke amejaribiwa na kupatikana na hatia ya uzinzi, au anaonekana kujihuisha na usagaji. Hizo sababu zinazohusu tamaduni hazitumiki leo katika tamaduni nyingi. Kufunika kichwa na urefu wa nywele unatofautiana kutoka tamaduni moja na nyingine. Kwa hiyo, matakwa ya aya hayatumiki kwa namna ile ile leo. Pamoja na hayo, Mazungumzo ya Paulo yana mengi ya kuleleza zaidi ya hilo. Katika **11:3, 7-12** anapitiliza kwenye uumbaji wenye na maumbile (ambayo kipekee inaweza kuwa ya kitamaduni), inatoa siri ya kufananisha na malaika, na tena anelezea usawa na kutegemeana kijinsia. Kwa uchache sana hatupaswi kutofautisha kubagua jinsia na kudharau, lakini tufanye kwa kuangalia tamaduni kwa namna nzuri na kwa umakini mkubwa. Vile vile kwa sheria ya kukusanya mavuno (**Mambo ya Walawi 19:9-10; 23:22**) Inajitokeza ikiwa na maudhui ya jambo lifaalo kwa kuwa na idadi kubwa ya wakulima na ikilingalinganishwa na mashamba. Katika mifumo mingi ya leo, majirani pekee

ya wakulima ni wakulima wengine, na masikini huishi kwenye maeneo ya vijijini. Kwa hiyo sababu ya sheria hiyo haiwezi kuwa sawa kwa tamaduni zote. Msemo wa Yesu kwamba wanafunzi “*wanapaswa kuoshana miguu wao kwa wao*” (**Yoh 13:14**) inakuwa na maana inakubalika katika mazingira ya wakati ule kuliko wakati huu wa leo mahali pengi, kwa sababu inakadiria mazingira ni ya, usafiri wa miguu; bila viatu au kwa kuva kanda mbili; kukosekana kwa maji yanayotiririka; majira ya joto; na njia za vumbi.

**7. Je kufanya kazi kifungu kama kiliyyo katika mfumo wa kitamaduni inatimiza kusudi au lengo la awali au alilokusudia mwandishi?** Kifungu kinaweza kufaa kwa tamaduni zote, au angalau kinaweza kuhamishika kwenda kwenye tamaduni nyingine katika mfumo ule ule wa kibiblia, ikiwa kuendelea kulitendea kazi katika utamaduni wetu litaendelea kutimiza kusudi la awali. Kwa upande mwingine kifungu kinaweza kuachwa kutumika ikiwa kulitumia hakutimizi kusudi la awali lililolengwa. Katika mazingira fulani tamaduni zile zile bado zipo lakini kinachomaanishwa au kuonyeshwa ni tofauti. Katika hali hizo kifungu cha awali kinaweza kurekeblishwa au kuachwa kabisa. Kwa mfano, **Warumi 16:16** inatuambia “*salimianeni kwa busu takatifu*.” Katika tamaduni nyingi wanaume husalimiana kwa busu. Katika tamaduni zingine hiyo humaanisha ushoga. Katika tamaduni zingine husalimiana kwa busu lakini hawabusu wanaume. Na katika tamaduni zingine inakubalika kwa wanawake na wanaume kusalimiana kwa busu. Kwa hiyo, kusalimiana kwa busu bado kunaendelea, lakini katika tamaduni zingine tafsiri ni tofauti na ile iliyokusudiwa na Biblia. Kwenye tamaduni ambazo kufanya hivyo kuna maanisha ushoga kufanya hivyo hakutimiza kusudi la kibiblia. Katika tamaduni hizo kusalimiana kwa kukumbatia na kupeana mikono ni kutimiza kanuni ya mstari huo, ni kutambuana kama ndugu katika Kristo kwa upendo wa kweli. Katika “sheria ya kutovuna mazao ya pembezoni” mfano (**Mambo ya Walawi 19:9-10; 23:22**), wakati ambao muundo ni kwamba jirani wa mkulima ni mkulima na kwamba masikini huishi kijijini. Wakulima kuacha kuvuna pembe za mashama yao kusingesaidia masikini bali kutasababisha mazao yasiyovunwa kuoza. Kwa kung’ang’ania kutimiza maandishi ya sheria kungefanya sheria isitimie. Vifungu vingi vinadai “utii” (wa watumwa kwa bwana zao), **1 Tim 6:1; Tito 2:9-10**), (wa raia kwa serikali zinazotawala, **1 Pet 2:13-15**), (wa wake kwa waume zao), **Tito 2:4-5; 1 Pet 3:1**), *kwa kusudi la kufanya injili iwavutie wengine*. Kwa muktadha wa siku hizi za karibuni sana, kuzungumzia kuwatii wengine, kutumikia wengine au namna ya utumwa “utii” katika ajira, kwa wafanyakazi wa serikali, au kwenye ndoa si tena kivutio kwa injili kukubaliwa na wale ambao wananyenyekewa. Ajira, serikali, na ndoa katika tamaduni nyingi leo ina sifa nyingi za kufaidiana kuliko ilivyokuwa katika tamaduni zile za zamani za Biblia. Utumwa ni kinyume cha sheria. Waajiriwa wana haki ambazo watumwa hawana. Nchi, wakiwemo viongozi wamebanwa na utawala wa sheria. Watu wanaoishi kwa demokrasia wana haki ya kupingana na viongozi wao. Wanawake wana haki za kisheria kupata elimu na fursa ambazo hawakuwa nazo katika tamaduni za zamani. Kwa hiyo wakati tukionyesha heshima, tofauti, na heshima kwa hizi tamaduni zote (tazama **Mat 20:25-28; Waef 5:21**), “utii” *katika namna inayoelezwa kwenye Biblia kwa wakati ule siyo sawa na leo*. Ni lazima tuzingatie mazingira yetu yaliyobadilika leo, ili kwamba tusiingie katika makosa ya kufanya jambo kwa namna ile ile inayosemwa na kifungu na kushindwa kutimiza kusudi la kibiblia lililokusudiwa na kifungu hicho hapo mwanzoni.

**8. Je amri za kibiblia au matumizi yake yalipingana na maadili ya tamaduni za wakati wake?** “Andiko linaponena kinyume na mazoea fulani ya mfumo wa maisha ya watu wa kale, kutofautiana huko na muktadha wa wakati ule unatoa uhalali wa kutumika kwa tamaduni zote. . . Wazo la kutofautisha linasema hivi: uwezekano wa kipengele cha kifungu kuwa cha kitamaduni unaongezeka kwa kadiri ambavyo kipenge cha kifungu kinavyokubaliana nadesturi za uatmaduni wa ulimwengu wa kale.” (Webb 2001: 158) Pande zote mbili za kanuni hii zinafanuliwa kwa kuzingatia taasisi ya utumwa. “Kwa kadiri ambavyo andiko halipindi utumwa kama taasisi ya kijamii, linaongeza uhalali wake wa kuwa la kitamaduni katika kifungu hicho. Kwa upande mwingine, taifa wakati walipotoka kabisa kwenye utamaduni unaowazunguka linakuwa katika wakati wa raha au machungu katika utumwa. . . . Hii inabeba akiba ya ajabu ya kutoa matokeo ya mwingilano wa kitamaduni, siyo kwa mtido wa maneno fulani maalumu yaliyojitenga na yasiyobadilika (nayo ni., kuunda miji ya makimbilio ya wafungwa leo) lakini katika muundo wa nia ya kukomboa (nayo ni., kutumia tena nia ya andiko kulekea kwenye namna bora zaidi ya kuwatendea binadamu kwa heshima na kutokomeza utumwa). Vipengele vinavyohusu utumwa leo vinatoa sauti kubwa zaidi kuliko vilivyofanya wakati ule katika desturi zao.” (Webb 2001: 158) Vivyo hivyo, hukumu ya Biblia dhidi ya ushoga na dhambi za uzinzi ilikuwa ni kinyume na tamaduni zao. Hivyo, hii inamaanisha kuwa mtazamo wa Biblia kuhusu mahusiano ya mume na mke haukuwa wa kitamaduni yaani si kwa ajili ya tamaduni ya Wapalestina na Roma ya zamani. Kama vile mfano mwingine wa maelezo ya Yesu kwamba viongozi wawe watumwa (**Mat**

**20:20-28)** ulikuwa tofauti na utamaduni wake mwenyewwe. Hii inaonyesha kuwa uongozi wa kikristo wa kutumika ni kwa tamaduni zote. Kwa namna nyingi Biblia inawaita wakristo kama manabii wa AK. kuishi si kwa kufuata tamaduni. Ukristo unawenza kudhihirishwa katika utamaduni wowote lakini haufungwi na utamaduni wowote. Sisi ni watumwa wa Kristo na wala siyo wa utamaduni wetu. Tunapaswa kumweka Yeye kwanza katika maisha yetu na wala si tamaduni zetu.

9. Je mambo yenye maulizo yanayofanana kwa karibu katika kifungu cha Biblia ni ya kitamaduni au yale yanayofanana yanavuka tamaduni? Kipengele cha kifungu kinaweza kuwa cha kitamaduni ikiwa mambo yanayohusiana kwa karibu na kifungu au jambo hilo limefungamanishwa na utamaduni.

“Jambo linalohusiana ni lazima liwe limeunganika kimsingi au liwe lina uhusiano wa kimantiki na jambo lenyewe . . . na (kwa umuhimu zaidi) lina mfanano unaoshikika na jambo lililopo.” (Webb 2001: 163, 171). Kwa mfanano, kwa kuzingatia desturi za kijamii za uongozi wa kiroho katika Biblia nzima, yafuatayo ni baadhi, lakini kwa namna ye yote yanayohusiana na yenye thamani ya juu kitamaduni.: (1) mtazamo kuwa mwanamke ni mali (**Kutoka 20:17; Kumb 5:21; Waamuzi 5:30;**) (2) mwanamke anatolewa kwa mamlaka ya baba yake kwenda kwa mume wake (**Hesabu 30:1-16; Kumb 22:19, 28-29;**) (3) umiliki na urithi ni kwa ajili ya wanaume tu isipokuwa kwa mazingira maaalumu (**Heasbu 27:5-8; 31:1-9; Kumb 21:16-17;**) (4) kuna msisitizo mkubwa kwa ubikira wa mwanamke lakini siyo kwa mwanaume (**Mambo ya Walawi 21:13; Kumb 22:13-21;**) matukio ya uzinzi kwa mwanamke na mwanaume yameshughulikiwa tofauti (**Mambo ya Walawi 20:10; Hesabu 5:11-31; Kumb 22:22-24.**) Ukweli kwamba mambo yanayohusiana kwa karibu ni ya kitamaduni inaeleza kwamba uongozi wa kiroho uliopo kwenye Biblia kwa mambo hayo siyo uongozi wenyewe wa kiroho ni wa kitamaduni. Moja ya sifa za “mambo yanayohusiana kwa karibu” kigezo ni kutumia orodha ya vikundi vinavyopatikana kwenye Biblia nzima. Sehemu moja ya kikundi cha orodha au kikundi si la kitamaduni ikiwa sehemu zingine si za kitamaduni, na inaonekana kuwa ya kitamaduni ikiwa sehemu zingine ni za kitamaduni. Kwa hiyo vifungu “mchanganyiko” (**Kumb 22:9-11**) inaonekana kuwa ya kitamaduni zaidi, lakini heshima na orodha iliyoambatana nayo inaonekana kuwa si ya kitamaduni (mf, **Yer 7:9; Hos 4:2; Marko 7:21; Wagal 5:22-23**).

10. Je msingi wa kifungu cha Biblia imeweka mizizi yake katika uumabji wa Mungu? Kwa sababu Mungu ameuita uumabji wake “*vema sana*” wakati alipokamilisha (**Mwanzo 1:31**), na dhambi ilikuwa bado haijaingia duniani, kifungu kinaweza kuwa si cha kitamaduni ikiwa misingi yake ipo katika maelezo ya uumbaji wa Mungu. Mume mmoja na mke moja, ambayo ipo kwenye **Mwanzo 2:24**, na kuthibitishwa na Yesu (**Mat 19:4-6**) na Paulo (**Waef 5:22-33**), ni mfanano mmojawapo (hata kama kuo wake wengi na talaka kumevumiliwa katika maeneo machache). Vile vile, wanawake vivyo hivyo huwa na “sura ya Mungu” na ni washirika wa Mamlaka ya Mungu ya kutawala uumbaji pamoja na wanaume (**Mwanzo 1:26-28**). Hata hivyo, ukweli ni kwamba si lazima kitu kikiwa na mizizi yake katika uumbaji kifae kwa tamaduni zote. Ukweli wa uumbaji na wa mpangilio wa uumbaji kabla ya anguko hazifanyiki amri zikiwa zenyewe, lakini ni maelezo tu. Si kila kipengele cha mpangilio wa uumabji kimekuwepo namna kilivyo ili kuweka msingi wa maadili kwa vizazi vyote vinavyokuja. Kwa mfanano Adamu na Eva walioana si amri kwa kila mwanaume kuo na mwanamke kuolewa (tazama **Mat 19:10-12; 1 Wakor 7:7-8**), na kuoana hakutakuwepo katika mbingu mpya na chi mpya (**Mat 22:30**). Hata uumbaji wa Mungu, misemo waliyopewa Adamu na Eva kabla ya anguko ilikuwa katika muktadha wa ‘utamaduni’ wa Edeni. Kwa hiyo, vitu vinavyohusiana na uumbaji kama chakula cha asili ambacho ni mbogamboga, kilimo kama kazi, na kushika sabato zote ni tamaduni na zina mwisho. Usemi kwamba “*Zaeni na kuongezeka, na mkaijaze nchi*” (**Mwanzo 1:28**), ultolewa katika mazingira ya dunia kuwa tupu pasipo watu wengine duniani kote. Leo wanadamu *tayari* “wamejaza nchi.” Kuna mabilioni ya watu. Katika maeneo mengine kuna msongamano, wazazi wana watoto wengi wasioweza kuwatunza kamwe. Pamoja na hayo, “Ulimwengu wetu unatofautiana sana na bustani. Katika hali hii, taratibu zilizokuwepo wakati wa uumbaji ni lazima zifanyiwe uboreshaji wa nguvu.” (Webb 2001: 125)

11. Je kifungu cha Biblia kimeweka mizizi katika anguko au laana? “Kuna mantiki moja tu kwamba kifungu ambacho ni laana kinaweza kuwa sawa katika tamaduni zote (kama kiashiria, ‘ni nini’) na mantiki nyingine ambayo ni ya utamaduni husika tu (kama jambo la kufaa kufanyika, ‘nini kinapaswa kfanyika’)” (Webb 2001: 121). Siyo sehemu ya utume wa Kikristo kuendeleza laana, lakini kupambana nayo. Uchungu wakati wa kuzaa mtoto, magugu, kifo hayo ni ya kawaida kutokea (**Mwanzo 3:16-19**). Hata hivyo, tunatumia kwa usahihi dawa za kileo kupingana na magonjwa na mauti, na teknolojia ya kileo ili kupambana na magugu.

12. Je kifungu cha Biblia kimekita mizizi yake yake katika ukombozi na kuumbwa upya? Kipengele cha kifungu cha Biblia kinavuka tamaduni ikiwa kinaelezea uumbaji mpya. Kwa hiyo yatupasa kuzingatia ni wapi mpango wa Mungu wa ukombozi umeelezwa au matumizi yake yanapojitokeza. “Kama vile

ambavyo desturi na maadili za wanadamu zilivyo na uhusiano na maadili makamilifu ya Mungu ya asili, kwa jinsi hiyo pia yanahusiana na mpango wake wa wokovu. . . . Matakwa ya maadili ya kawaida ya wanadamu yanapatana na maelekezo ya jumla katika mpango wa Mungu.” (Tiessen 1993: 203) Kwa msisitizo zaidi, “Ikiwa utaratibu wowote utapewa hadhi ya umuhimu unaodumu, unapaswa kuwa unapatikana kwenye maelezo ya uumbaji mpya. Utaratibu wa awali wa uumbaji, kama msingi kwa vile ulivyo, hauonyeshi kuwa katika tamaduni zote kama ilivyo katika maelezo ya uumbaji mpya. Kinyume chake, uumbaji wa awali unaonekana zaidi kufungwa katika utamaduni zaidi katika vipengele vyake.... Mtu habadiliki katika umbile lake la asili kama ilivyo katika mahusiano ya mtu kubadilika. Mahusiano yanatakiwa yakamilishwe na kupangiliwa upya kutokana na upendo mkamilifu wake Kristo. Vipengele vya muhimu vya uumbaji wa asili kama vile kabila na jinsia haviondolewi katika uumbaji mpya wa mwanadamu. Vinabaki na kutambuliwa, kutakaswa na kushangiliwa. Ubinadamu mpya ni lazima utumie hizo tofauti kubariki na kuinuka juu badala kuharibu na kupata hasara.” (Webb 2001: 147-49) Hivyo, “*mtu mpya mmoja*” aliyembwa “*ndani ya Kristo*” (**1 Wakor 12:13; Wagal 3:28; Waef 2:15; Wakol 3:11**), wakati ukabila wa zamani, utaifa, jinsia, na mgawanyo wa madaraja ya uchumi yote yanakosa hadhi ndani ya Kristo, na kuunda msingi mpya wa mahusiano ya kibinadamu.

13. Je kuna mawazo yenye ushindani wa maana katika Biblia kuhusu msimamo wake katika tamaduni husika? Kipengele au maudhui inakuwa na haki zaidi kwa tamaduni zote ikiwa kulikuwa na mawazo mengine ya kitamaduni yenye ushindani wa wazi katika utamaduni huo kwa ujumla. Kinyume chake, kifungu au maudhui yake yanakuwa ya kitamaduni zaidi ikiwa mwandishi hakuonyesha kuwepo kwa mawazo mbadala ya kitamaduni kwa wakati huo. Kwa mfano, katika utamaduni wa nyakati za Biblia mfumo wa uongozi ulikuwa wa kifalme tu, demokrasia haikuwepo kabisa. Vile vile utumwa ulikuwa ni mfumo wa maisha uliokubalika katika jamii na hakuna utamaduni uliokuwa una mawazo ya kutokomeza utumwa. Hizo taasisi za kijamii yaani utawala wa kifalme na utumwa yote mawili yalikuwa ya kitamaduni na si kwa tamaduni zote. Zote mbili zilikuwa sehemu ya muktadha wa tamaduni ambazo waandishi waliishi na kuandika.

14. Je maelezo yaliyopo katika kifungu cha Biblia yanakinzana na ukweli wa kisayansi au wa kijamii? Kifungu au maudhui yaweza kuwa ya kitamaduni, au yaweza katika lugha ya kawaida, kama inapingana na ukweli wa kisayansi wa siku za leo. Kwa mfano, **Isaya 3:12** inatoa maelezo ya kudharau uongozi wa mwanamke, ikionyesha kuwa wanawake huwa viongozi wasio na uwezo, ikiwalinganisha na watoto. Kwa kuwa Israeli walikuwa hawatawaliwi na wanamke au watoto, Isaya akitumia lugha ya utamaduni wao ya kuwaonyesha namna inavyowapasa kuona aibu kama taifa. Wakiwa wameweka kiwango kidogo cha elimu ambayo wanawake wanaweza kupokea na pia majukumu machache ambayo mwanamke amepewa kulingana na utamaduni inawezekana kulikuwa na mambo ambayo Isaya ameyaona kwa kuchunguza katika jamii na kuyabainisha kisayansi. Hata hivyo leo wanawake wanapata elimu inayolingana na ile wanayopata wanawake na wanaweza kutimiza majukumu ya kijamii na kuongoza ofisi. Utafiti umeonyesha hakuna uduni au kutoweza kwa upande wa wanawake ikilinganishwa na wanaume kwa habari ya uwezo wa kujifunza au kuongoza. Wanawake wanatoa mchango wa maana sana kwa ngazi zote za kijamii, na wanawake wengi wameshaonekana wakiwa viongozi wazuri sana. Kinyume chake, “wakati suala la jinsia ni la kitamaduni katika nyakati za Isaya, kanuni pana inayovuka mipaka ya kitamaduni ipo hata leo kwamba watu walio na tabia za kitoto au wasiokomaa huwa viongozi dhaifu” (Webb 2001: 224).

#### **J. Hatua tano za kuweka daraja kuziba pengo la kitamaduni ili KUWEZA kutumia sheria, amri, na masharti ya kibiblia katika mazingira ya sasa**

Njia zifuatazo ni kwa mujibu wa Doriani (1996: 146-47) na Hays (2001: 30-35) (tazama pia **NYONGEZA C: J. Daniel Hays, “Kutumia sheria za Agano la Kale Leo”** na **NYONGEZA D: T. Wayne, Dye, “Utamaduni na Dhamiri: Kweli za Biblia na Tofauti za Tamaduni”**).

1. Tambua maana ya asili na matumizi. Hii inatuhitaji sisi kutumia ujuzi wetu wa hemenutiki na eksejesi.
2. Gundua kanuni ya mwingiliano wa kitamaduni nyuma ya amri husika. Nini kilikuwa “kinahusiana” tu na watu ambao walipewa amri ya kibiblia dhidi ya kile kilicho “kamilifu” (i.e., inayotumika siyo tu kwa wapokeaji wa asili lakini kwa watu wote au waamini wote, mahali popote na nyakati zote) ni moyo wa jambo. Hii inaweza kututaka sisi tutofautishe *muundo* wa amri na *kusudi* (nayo ni., maana, lengo, “kamilifu,” au kanuni nyuma ya amri). “Tunapokuwa na mashaka iwapo kitu fulani ni cha kitamaduni au ni ukweli mkamilifu ni muhimu kukiweka kwenye muktadha mpana wa ujumbe wa Biblia” (Wolvaardt 2005: 300). Kufanya hivyo kunahitaji ufahamu mzuri wa maarifa ya simulizi la Biblia kwa ujumla, na maadili, fundisho, na mifano inayoiunda. “Mtu anavyoelewa vema zaidi ujumbe mpana wa

Biblia, ndivyo inavyokuwa rahisi kwake kuelewa na kutofautisha kati ya kweli kamilii na hali ya kuhusiana” (Ibid.: 28). Kwa mambo mengi (lakini kwa namna yeyote siyo yote) yaani muundo wa amri na kanuni iliyo nyuma yake inaweza kuwa wazi, na yawea kutumika vile vile na inaweza kutumika sawa na ilivyoelizwa, hasa kwa mambo yahusuyo AJ. Hata hivyo tunatakiwa kuwa makini ili “tusipitilize katika kuelezea” amri, kanuni au matumizi. Ni lazima tutambue kiwango cha uhakika tulionao kuhusu kanuni tuliyogundua na matumizi tuliyopendekeza.

3. Gundua hali inayofanana na hiyo leo. Hii inatuhitaji sisi siyo tu kujua mambo mawili hapo juu, bali mchambuzi mzuri wa utamaduni wetu wenye. Kwa kujua hili tunahitaji kutambua tofauti ya maana inayoweza kuwepo kati ya hadhira ya awali na waamini wa leo. Tunahitaji kufikiria kwa kina juu ya kwanini hali fulani mahususi leo inafanana na hali iliyokuwepo nyakati za Biblia. Sheria zote za AK, amri, na masharti na mengi ya maagizo ya AJ, yanayotumika kwa kuwa yana ulinganifu, *ikiwa yana na matumizi yeyote*. Matumizi ni sahihi pale tu ambapo hali ya Biblia na ya kawaida ya kimaisha zinaendana kwa hakika.

4. Shauri matumizi sahihi ambayo yanahuisha kanuni kwa ujumla wake. Katika kufanya matumizi, tunaweza katika mazingira baadhi kwa haki:

- a. *Kuendeleza amri ya kibiblia.* Kwa mfano, kutokutamani punda wa jirani yako (**Kutoka 20:17**) matumizi yanaendelezwa hivi (nayo ni., usitamani gari la jirani yako).
- b. *Badili amri za kibiblia ambazo zimeegemea mazingira tofauti ya kitamaduni.* Kwa mfano, badala ya kumsalimiana kila mmoja kwa “busu takatifu” (**Warumi 16:16**) kushikana mikono au kukumbatia inaweza kutumika.
- c. *Wekea mipaka amri ya kibiblia.* Kwa mfano badala ya kutumia mvinyo kodogo kwa ajili ya matatizo ya tumbo (**1 Tim 5:23**) tunaweza kutumia dawa ya kuonda asidi au maji ya chupa au aina nyingine vinavyopatikana.
- d. *Hata kubadili amri ya kibiblia ikiwa matumizi yake halisi yapo kinyume kabisa na sababu au kanuni iliyopo nyuma yake.* Kwa mfano, katika **1 Tim 5:3-16** mjane wa zaidi ya miaka sitini asiyi na au wajukuu, ingawa kimsingi inafaa katika mazingira ya Paulo ya wakati ule, asingeweza kusaidiwa ikiwa ana urithi, mafao ya uezee ni anapokea msaada wa serikali. Kwa upande mwingine, mjane kijana mwenye watoto angehitaji msaada zaidi kama watoto wake hawawezi kumsaidia (wanaweza kuwa wadogo, au familia yake inaweza kumkataa, kwa mfano, ikiwa ameokoka kutoka kwenye Ukristo kwenda Uislamu), ikiwa hana matarajio ya kuolewa (kwa mfano, kama ana VVU/UKIMWI), au sababu zingine.

5. Linganisha matumizi yaliyopendekezwa na maandiko mengine, maalumu kwa mafundisho ya AJ. Ikiwa matumizi yanashikamana na baadhi vifungu vya kibiblia, tunapata ujasiri katika hayo. Lazima tuwe makini na amri ya kibiblia ambayo ipo mbali kabisa na mazingira ya sasa. Mifano ya biblia inaweza kuthibitisha au kushindwa kuthibitisha, matumizi yetu tuliyopendekeza.

6. Mifano ya AK na AJ inafafanua maelezo hapo juu:

- a. *Mwanzo 22:1-2—Amri ya Mungu kwa Ibrahimu kumtoa Isaka.* Katika muundo wake, hii ilikuwa “amri maalumu” aliopewa Ibrahimu, siyo “amri ya jumla” waliyopewa watu wote waaminio au Wana wa Israeli. Hilo ni dokezo moja kwamba amri hiyo “maalumu” ilikuwa “inamhusu” Ibrahimu, na siyo “kweli kamilifu” kwa tamaduni zingine. Kulinganisha maandiko mengine kunafunua kwamba hakuna amri zingine zinazofanana na hiyo, na pia inaonyesha kwamba Mungu anapinga na kuzuia kumwaga damu isiyo na hatia (tazama **Kutoka 20:13; Mithali 6:16-17**). Hata hivyo, hata aya hii inaelezea kanuni ya jumla inayovuka tamaduni zote, “uwe tayari kumtumikia Mungu kwa kile ukipendacho sana,” siyo “nenda uchinje watoto wako.”
- b. *Kutoka 22:19; Mambo ya Walawi 18:23; 20:16; Kumb 27:21—Sheria za Musa ambayo inapinga kulala na mnyama.* Amri hizo hazikurudiwa katika AJ. Hiyo haina maana kwamba bestiality sasa inaruhusiwa katika Agano Jipy. Tunajuaje hilo? Jibu ni kwamba tunaweza kuangalia nini AJ inasema kuhusu mahusiano ya kimpenzi. Katika **1 Wakor 7:2** na **Waeb 13:4** Waandishi wa AJ wanakataza mapenzi nje ya ndoa. Zaidi ya hayo, **1 Wakor 6:18** na **1 Wath 4:3-5** inazulia “uasherati.” Kanuni ya AJ ni wazi. Sheria za AK zinazuia kulala na mnyama ni matumizi ya kanuni hizo.
- c. *Kumb 22:8—“Utakapojenga nyumba mpya, fanya ukuta kandokando ya dari lako, usije ukaleta damu juu yanyumba yako, mtu akianguka huko.”* “Kwanza, tunapata hisia ya mwanzo. Kwa sababu zilifanya kazi, zilisherehekewa, pia walilala kwenye paa zao, wana wa Israeli walielewa kwa hakika kwa nini walitakiwa kujenga kuta kuwazunguka [muktadha wa kihistoria unaonyesha sababu na umuhimu wa sheria hiyo]. . . . Pili, tunatafuta kanuni. Kwa kuwa watu

wa Magharibi mara chache hupanda juu ya dari zao, hatuhitaji kuta leo. Lakini ni lazima tutafute kanuni ya awali na namna ya uwezekano wa kuhamisha katika siku zetu. Upendo unabeba upendo kwa majirani [*ukweli* wa kibiblia] na inahifadhi maisha kwa kuweka tahadhari inayozua majeraha ya ajali. Kwa hiyo, Musa anaweka sheria kwa ajili ya usalama. Tunatumia kanuni zinazofaa leo pale tunapoweka vitu imara kwenye paa na kuweka vizuizi pembeni mwa ngazi za kupandia. Tunapanua wigo wa kanuni hizo hadi kwenye barabara kwa kuweka bamsi zinazopunguza mwendokasi.” (Doriani 2001: 242-43)

d. ***Warumi 16:16***—“*Salimianeni kwa busu takatifu.*” Katika kulinganisha hili na maandiko mengine tunaona maelekezo yanayofanana yametolewa katika **1 Wakor 16:20; 2 Wakor 13:12; 1 Wath 5:26;** na **1 Pet 5:14.** Hata hivyo, mistari hiyo haielezei umhimu wa aina fulani ya salamu au kwani aina au tendo lifanyike kama kupinga mtindo fulani wa kusalimiana. Hilo kimsingi inazaa swalii kwamba ikiwa uzoefu huu umefungwa katika utamaduni fulani au unahitajika kutumika kwa tamaduni zote kama kweli kamili au “unahusika” na utamaduni tu. Tunapozingatia ujumbe mpana wa Biblia nzima, “Kuhusu mtindo wa kusalimiana, ifahamike wazi kwamba maelekezo kwamba kubusu ni kweli kamilifu kwa Wakristo wa nyakati zote, haukuliani na ujumbe wa jumla wa Biblia—ujumbe wa wokovu uliopatikana pasipo sisi kustahili na usafi wa tabia kama mwitikio kwa wokovu huo.” (Wolvaardt 2005: 28). Ingawa kubusu kulikuwa kunakubalika katika utamaduni wa kirumi, na katika tamaduni zingine leo, katika tamaduni zingine kufanya hivyo inamaanisha ushoga au tabia ya uzinzi mambo ambayo yote mawili yanakatazwa na Biblia. Matokeo yake, ingekuwa ni ni vibaya kwa uzoefu huu kuonekana kama “kweli kamilifu.” Hapo inaonekana kwamba kuna kanuni ya wazi nyuma ya amri hii, inayosema, salimia waamini wenzako kwa namna ambayo inadhihirisha upendo wako na heshima kwa kila mmoja katika Bwana. Hilo linaweza kufanya kwa kubusu, kukumbatia, au kushikana mikono, au kwa njia nyingine inayokubalika ya kusalimiana. “Sababu ni kwamba kweli kamili [kumsalimia kila mtu kwa upendo wa kweli] inafaa kwa tamaduni zote, lakini kwa vitendo itatofautiana kulingana na uzoefu wa kila utamaduni” (Ibid.: 29).

e. ***1 Tim. 5:9***—“*Mjane asiandikwe[kupokea msaada wa kifedha kutoka kanisani] isipokuwa umri wake amepata miaka sitini.*” Kwa kutazama juu juu, “umri wa miaka 60” mahitaji ya umri siyo hitaji la jumla. Kwa hiyo, Makanisa mengi, yanatumia hiki kigezo cha umri “hivyo hivyo ilivyo,” kama amri iliyo wazi kwa makanisa yote. Hata hivyo, kuelewa *muktadha wa kihistoria na wa kitamaduni* hutupa taswira nzuri zaidi. Miaka sitini ni miaka ambayo mtu alitambulika kama “mzee” (Knight 1992: 223). Sitini “yawezekana ulikuwa umri wa mwisho kwa mtu kutegemewa kufanya kazi na kujipatia mahitaji yake mwenyewe” (Blomberg 1999: 209). Katika karne ya kwanza wanawake wachache sana chini 4% waliishi hadi kufikia umri wa miaka 50. (Lysaught 2005: 67n.18). Walikuwa kundi hatarishi zaidi na walikuwa kwa nadra na rasilimali za kutegemea. Kinyume chake, leo, kwa uchache katika nchi nyingi za Magharibi, miaka 60 siyo umri wa “uzee,” na kuna rasilimali nyingi za serikali na kuna vyanzo vingine kwa ajili ya matunzo ya wazee. Matokeo yake, mahitaji ya walio na “umri wa miaka 60” yanaonyesha jambo ambalo ni tofauti kati ya utamaduni wa Paulo na utamaduni zetu nyingi za leo. Zaidi ya hayo, muktadha mpana wa uhalisia ni kwamba Biblia nzima haishauri kuwa umri wa miaka sitini una umuhimu fulani (lakini cf., **Mambo ya Walawi 27:1-7** mahali ambapo kuna idadi kubwa ya kukomboa watu waliota nadhiri ngumu; gharama ilienda hadi kufikia miaka sitini). Hilo linatueleza kuwa umri wa miaka 60 hauhitajiki kutumika kwa ulimwengu mzima kama “sheria” lakini unaweza kubadilishwa kama muktadha wa mahali husika unavyohitaji.

#### **K. Kutumia hemenutiki ya “mchakato wa ukombozi/nia ya ukombozi” kuziba pengo la jambo na la kitamaduni pale amri za kiblia, sheria na masharti yanapokuwa HAYAWEZI kutumika kama yaliyvo kwa kuwa hayakuwa maagizo makamilifu ya Mungu kwa watu wote na tamaduni zote**

1. “Hemenutiki tuli” mara kwa mara haishughuliki na “vithamisho vya kitamaduni” vile vilivyotajwa kwenye Biblia hasa vile vilivyopo katika AJ. “Wale wanaotumia mtazamo usiokubali kubadilika hawajishughulishi na hali ya sasa ya ulimwengu na kuijuliza maswali magumu. Kwa mfano wanaogopa kuijuliza, Kwa mfano, ni wapi maadili yetu siku za leo *yanapita* maadili ya Maandiko yasiyogundulika kama inavyoonekana katika maneno yaliyositenga katika kurasa zake (hii ina maana, ni wapi maadili yetu ya siku za leo *yanazidi* maadili ya kimaandiko yasiyogundulika)?” (Webb 2001: 254-5)

a. *Hemenutiki “tuli” “inatambua kuwa maneno ya mafungu yanatoka kwenye makondokando au pamoa na himizo la kiwango cha chini juu ya nia ambayo ni kiini cha kifungu na hivyo*

*kudhibiti matumizi ya kileo ya maandiko pale mahali ambapo maneno yamejitenga kutoka katika muundo ule wa kale*” (Webb 2001: 30-31). Ikiwa tunatumia “hemenutiki tuli” ambayo inazingatia tu kutumia maneno ya Maandiko, kama yalivoandikwa, kwa mazingira haya ya kileo, bila kufikiria nia iliyokuwa nyuma ya yale maandiko, au mabadiliko ya kitamaduni, au mabadiliko ya maandiko kulingana na wakati, tutalazimika na kuchagua na kuchukua fungu lipi la maandiko tulisimamie, au kutojali kabisa kifungu cha maandiko ambacho kina “tatizo kubwa” (mf., nyingi ya maandiko yanahusu utumwa). Hilo linaweza kusababisha hata kutotumia sheria za AJ, amri na masharti katika muktadha wa tamaduni zetu za leo.

b. *Kutumia vifungu vinavyohusu utamaduni mmoja tu kulingana hemenutiki “tuli”* “Embu fikiri kukubaliana na adhabu ya viboko ya waajiri kwa waajiriwa ambayo Petro anaelezea kwa ajili ya Injili. (1 Pet 2:18-25). Au, fikiri kuhusu kuwaelimisha waajiri wa leo kwa kutumia mtazamo wa vitabu vya sheria vya Musa kwamba, kuwaadhibu waajiriwa wao hata kuwaumiza hata karibu ya kifo hawataadhibiwa kisheria (Kutoka 21:20-21). Au, inawezekana katika ulimwengu wetu wa leo kutoa adhabu tofauti kwa waajiri wanapowanyanya kijinsia waajiriwa wao (= mtumwa) na pale inapokuwa kati ya mwajiri au aliyejjajiri binafsi (= huru) (Kumb 22:25-27; cf. Mambo ya Walawi 19:20-22). Mifano hii, kwa hakika, inaonyesha asili ilio hatari ya hemenutiki tuli.” (Webb 2001: 36-37)

2. “Mchakato wa kikombozi” au “nia ya ukombozi” ya hemenutiki inaweza kushughulika na zote mbili yaani “vithaminisho vya kitamaduni” na “vithaminisho vya kifalme” vilivyopo ndani ya Biblia.

Hususan katika eneo la mahusiano ya kijamii, kiserikali ya kibinadamu, inaweza kulazimu kutumia nia ya kiukombozi au mchakato wenye kukomboa amba ni kiini kilichopo kwenye sheria ya kibibia, amri, au sharti, na kuitumia ile nia ya ukombozi kwa utamaduni wetu wa siku ya leo. Katika **Mathayo 5** na **9** “Yesu’ mtazamo wake unaenda mbali sana katika maneno yake yaliyojitenga ili kuleta upatanisho kwa kwa nia yake mbacho ni kiini cha msingi. Bila kutatizika Yesu anashughulika na nia ya kifungu cha Agano la Kale na kuhusisha jamii yake namna ya kuboresha kwa ajili ya utamaduni wao. Pamoja na mhimizo wake wa matumizi ya rohoni ya maandiko, anawafundisha kwa namna ya kiukombozi wakati wanaposoma maandiko ya Biblia.” (Webb 2001: 62) Kwa upande mwingine tukijifunga katika maneno yaliyojitenga ya maandiko tunaweza kushindwa kutumia katika utamaduni wetu, “roho ya ukombozi iliyozalisha andiko hilo pale mwanzoni. . . . Kupuuza kutumia nia ya ukombozi ya kifungu cha maaandiko inasababisha kutokomeza nguvu ya injili ambayo ingeweza kuachiliwa katika ulimwengu wetu wa sasa”. (Webb 2001: 33, 50). Kwa hiyo mwelekeo wa kutumia “mchakato wa ukombozi/nia ya ukombozi” katika maandiko inaruhusu kwenda zaidi ya matumizi ya awali ya maandiko katika ulimwengu wa kale, ili kwamba matokeo ya mchakato ambayo yaliletwa na maandiko lakini hayakutokea kikamilifu na kuhitimishwa yawefe kukamilika katika ulimwengu wetu leo.

3. Kutathmini “mchakato” wa ukombozi katika Biblia. Katika kutathmini mchakato au mwondoko wa kiukombozi na nia ya ukombozi kwenye Biblia, tunahitaji kutathmini uhusiano kati ya sheria za kibibia, amri, na masharti yaliyo katika muktadha wa kitamaduni. Wakati mwingine maandiko yanachukua “mchakato wa awali” ili kuboresha desturi ya tamaduni za kale kiasi kwamba inaruhusu mchakato zaidi kuwezekana kufanyika kwa namna inayofaa kwa ajili ya utamaduni husika. Mchakato wa mabadiliko kwa maandiko ni muhimu sana ili kuonyesha mwelekeo wa mchakato mwingine ikiwa unaofaa. Kwa hiyo, mwelekeo wa mwondoko au mchakato ni lazima utathminiwe kwa kuzingatia mwelekeo mpana wa kitamaduni. Vigezo vitatu vya mchakato vinatupa uelewa wa nia ya msingi ya kifungu. Kama hivi vigezo vitatu vitaelekeza kwenye mwelekeo mmoja, hapo tunapata mawazo kwamba msimamo wa somo uliopo na kuendelezwa katika AJ unaweza usiwe msimamo wa mwisho wa Mungu kwa nyakati zote, mahali pote na tamaduni zote. Kwa maneno mengine nia ya andiko inaweza kushauri uwezekano mpya unaweza kutazamwa kwa ajili ya utamaduni wetu leo kwa kuzingatia mabadiliko yaliyowahi kutokea huko nyuma katika Biblia. Hizo hatua tatu au vigezo vya mchakato ni (Webb 2001: 73-83):

a. *Mchakato/Mwondoko wa kigeni*—nayo ni, badiliko linaloendana na mazingira ya kale ya Mashariki na utamaduni wa Warumi wa Greco. Toafauti na tamaduni zinazozunguka watumwa wa kisraeli walikuwa wanawekwa huru katika mwaka wa yubilee (**Mambo ya Walawi 25:39-42**).

b. *Mchakato/mwondoko wa ndani*—nayo ni., badiliko linalolinganishwa na kile kilichokuwa kinaendelea kwenye jamii yenye agano. Bwana wa kikristo waliaswa kuwatendea watumwa wao kama Kristo anawatendea wao kutoka miyoni mwao, vivyo hivyo watumwa wa kikristo walitakiwa kuwatendea bwana zao (**Waef 6:5-9**).

c. *Mchakato/mwondoka wa kiibada*—nayo ni., badiliko lililotokana na mtazamao mzima wa

kiukombozi, kama vile AK kwenda AJ. Kukosekana kwa mwendelezo kati ya AK na AJ inaonyesha kuwa kifungu hicho cha AK ni la kitamaduni. Kwa mfano mitindo yote ya ibada ya agano la kale (hekalu, ukuhani, sadaka za wanyama, nk.) iliachwa katika AJ, hata mambo muhimu ya AK kama vile tohara na sheria za vyakula. Zaidi ya hayo, wanaume katika AJ wanatakiwa kuwapenda wake zao na kujidhabihu kwa ajili yao, kama Kristo alivyolipenda kanisa na kujitoa kwa ajili yake (**Waef 5:25**). Haya mabadiliko makubwa kati ya AK na AJ yanadhihirisha kuwa desturi hizo za AK zilikuwa za kitamaduni.

d. *Sababu zingine mbili za kibiblia na za kitamaduni zinashauri kwamba mwondoko/mchakato zaidi unaweza kufanywa tunapotumia nia ya Biblia ya kiroho katika mifumo ya kisasa.* Sababu zifuatazo, zinatakiwa zisiwe za kubadilika badilika na ziwe na mwelekeo mmoja ikihusishwa na utamaduni kama vile mwondoko/mchakato wa kigeni, mwondoko/mchakato wa ndani yaani wa jamii husika, na mchakato/mwondoko wa kiibada kama tulivyojadili hapo juu:

(1) **Mawazo mbegu**, “Mawazo mbegu au wazo mbegu” katika maandiko, yanayoathiri mahusiano katika jamii, yanaweza kushauri au kuchochea mwondoko/mchakato zaidi wa mabadiliko kuhusu somo fulani wakati ambapo wasomaji wa siku zijazo watakapoona matokeo yake. Wazo la usawa “ndani ya Kristo” ni mfano mmoja. (mf, **Gal 3:28**). Wazo hilo lina matokeo ya kitheolojia, lakini pia matokeo ya kijamii ambayo yanaweza kufanyiwa kazi kutokana na muda.

(2) **Mpishano**. Kipengele cha kifungu kinaweza kikajifunga katika desturi za kitamaduni ikiwa desturi hizo za kijamii “zimepishana” na na vifungu vingine vyta Biblia. “Kama msingi wa wazo mbegu ni hafifu na kimya katika muundo wake usio wazi hivyo mpishano huo unatamkwa kwa wazi kama mpishano wa kibiblia ambaio unatokana na desturi za kitamaduni.” (Webb 2001: 91). Kwa mfano AK na AJ zinazungumzia kwa kuzingatia ukuu wa mkono wa kuume (tazama **Mwanzo 48:18; Kutoka 15:6; 1 Nyakati 6:39; Zab. 110:1; Mat 22:44**). Hata hivyo, katika mpishano huo na desturi za kitamaduni, Mungu alimtumia mtu wa mkono wa kushoto kumshinda Elgon (**Waamuzi 3:12-30; 20:16**). “Hiki kifungu kinachoonyesha mpishano kinatupa sisi dondoo kwamba ukuu wa mkono wa kuume na ule uduni wa mkono wa kushoto unaohusika na utamaduni” (Ibid.: 93). Vile vile, ingawa **1 Wakor 11:4** inanena ya kuwa nywele ndefu kwa wanaume ya kuwa ni aibu, maandiko mengine katika Biblia (kwa mfano, kuhusu wanazareti) wanaume walimheshimu Mungu kwa kutokata nywele zao. (**Hesabu 6:1-21; 1 Sam 1:11**). Kuna kupishana kwingi kuhusiana na wajibu wa mwanamke katika Biblia nzima, ikihusisha Hulda aliyetafutwa na mfamle na kuhani, ambaye alitoa neno la Mungu kwao kwa mamlaka. (**2 Wafalme 22:14-20; 2 Nyakati 34:22-28**); Prisila, aliyemfundisha Paulo na pia anatajwa kabla ya mume wake Akwila (**Matendo 18:24-26**); na usawa katika haki katika tendo la ndoa na mamlaka katika ndoa (**1 Wakor 7:3-5**).

e. *Mwendelezo kati ya AK na AJ haimaanishi kuwa kuendelezwa huko ni uthibitisho kuwa jambo hilo si la kitamaduni pekee.* Sababu ni kwamba AJ inaweza kushindwa kutofautisha baadhi ya kweli za AK kwa sababu za kitamaduni zinazofanana kwa maagano yote mawili. Kwa hiyo uchambuzi wa kitamaduni ni lazima ufanyike tunapojiliza ikiwa desturi fulani yapasa kuendelezwa leo katika muundo ambaio uliotumika nyakati za Biblia. Kwa mfano, AJ inasisitiza maadili ya amri 10, ambazo ni kwa tamaduni zote (isipokuwa amri ya 4 kuhusu kushika sabato, ambayo imeundwa upya au kubadilishwa). Kwa upande mwingine AJ haikufanya marekebisho yoyote utumwa wala uongozi wa kifalme. Zaidi, “busu takatifu” inaungwa mkono na maagano yote mawili AK (**Mwanzo 27:27; 29:13; Kutoka 4:27; 18:7; 1 Sam 20:41**) na AJ (**Warumi 16:16; 1 Wakor 16:20; 2 Wakor 13:12; 1 Wath 5:26; 1 Pet 5:14**). Hata hivyo, desturi hizo zote ni za kitamaduni na haziwezi kufaa kwa kila tamaduni.

4. “**Mchakato wa kikombozi**”/“**Nia ya ukombozi**” inavyoiezwa katika kutafsiri maandiko.

a. *Webb aliyeanzisha muundo huu anaelezea hivi “Kanuni ya X=>Y=>Z ”* (Webb 2001: 31): “Mahali pa katikati (Y) inasimama ikiwa maneno yaliyojtenga katika Biblia yametumika kama msingi wa somo. Kisha, kwa upande wa kifungu cha Biblia, mmoja ni muhimu ajiulize swali la kimtazamo: Nini uelewa wangu wa kifungu cha Biblia, ikiwa ninatazama katika mtazamo wa *utamaduni wa asili* (X)? Pia, kifungu cha Biblia kinaonekanaje katika mtazamo wa utamaduni wa siku zetu za leo, pale inapoonyesha maadili mazuri zaidi ya kijamii—ina okaribiana na *maadili makamilifu* (Z) na nia ambayo inafunuliwa katika maneno yaliyojtenga ya kifungu cha Biblia?

b. *Kutafuta “nia ya ukombozi” ya msingi wa kifungu cha Biblia.* “Kutafuta nia ya ukombozi ya kifungu cha Biblia ni jambo linalohitaji umakini mkubwa. Siyo wazi na kuelezeza kama kusoma kifungu kwenye ukurasa. Ili kupata nia ya kifungu, mtafsiri ni lazima apambanue kifungu kinatoa sauti gani katika muktadha mbalimbali wa kijamii uliokuwepo kwa wakati ule. Kutengeneza mitindo miwili ya maisha ni muhimu: ya kijumla (pana), ya kigeni ya kale Mashariki ya karibu na Wagiriki-Warumi (ANE/GR) muktadha wa kijamii na ule uliofuata mara, na mtindo wa kanisa/Israeli. Mmoja ajiulize, ni mabadiliko au maboresho gani maandiko yanafanya katika jamii yenye agano? Na ni kwa namna gani kifungu kiliathiri kwa mapana ulimwengu wa ANE/GR? Kwa kuititia kufikiria hili na mitindo ya maisha ya kijamii msomaji ataanza kuona nia ya ukombozi ya kifungu. Pia, mtindo wa tatu unaruhusu njia moja nyingine ya kutambua nia ya ukombozi, iitwayo, mchakato wa kiibada katika nyakati za Biblia. Mchakato/mwondoko kati ya AK na AJ yamkini ni jambo linalofahamika sana kuhusu kuhamza kwa utaratibu wa kiibada.” (Webb 2001: 53)

5. Tofauti kati ya nia ya ukombozi na “kanuni” ya msingi ya kifungu. “Mmoja aweza kufananisha kanuni kama matanga ndani ya mashua. . . Nia ya ukombozi, pamoja na hayo, ni jambo lingine-inafanana kabisa na upopo unaosukuma matanga ili mashua iende mbele. Tukitumia vifungu vinavyoelezea utumwa katika ajira za leo, kutafsiri biblia kusikoruhusu mabadiliko itadai kwa ujumla kuelekea katika . . . kanuni ‘nyenyekeea ili kutii wale wenye mamlaka mahali pa kazi,’ kwa kudhani kuwa hii inahusika na nyakati hizi mbili. Kwa kutazama kanuni hiyo, tafsiri ya biblia isiyokubali mabadiliko inashindwa kusukuma vya kutosha . . . kuwajibika kwa ajili ya tofauti za umiliki (dunia yao) na mahusiano ya kimkataba (dunia yetu). Lugha ya nyenyekeea/tii ni lazima iachwe katika matumizi yetu leo. Kanuni inapaswa iwe moja ya kumheshimu Mungu kwa namna unavyohusiana na wenye mamlaka au uongozi mahali pa kazi na matumizi ya leo ingeleta ufanuzi kwa maneno yafuatayo: Timiza masharti ya mkataba wako kwa uwezo wako wote, hii ina maana kwa namna ambayo itamtukuzza Mungu na kuwaleta wasioamini karibu na ufalme wa Mungu.

Kuhusu nia ya ukombozi, mtazamo usiobadilika unashindwa kukabili msukumo wa maandiko kuendeleza utumwa. . . Nia ya msingi ya vifungu vya utumwa . . . kwa hakika inamtaka mwajiri nyakati fulani kwenda zaidi ya anavyotakiwa kulingana na mkataba. Pia inazingatia msukumo mkubwa wa maandiko, ikilinganishwa na ulimwengu wa kale, kwa maana kwamba inaboresha mazingira ya kazi na matibabu ya watumwa. Huu ukweli wa nia ya ukombozi hatimaye hutupeleka kwenye kukomesha kabisa utumwa. Bado, ikitumiwa katika muktadha wa leo, biblia hiyo hiyo inatoa sauti ya kuboresha hali ya mfanyakazi wa sasa. . . Inasema kuhusu mafao, mazingira mazuri kwa ajili ya familia, kuthamini watu kwanza na kutoa motisha yenye maana, vile vile na mambo ya msingi”.

(Webb 2001: 54-55)

6. Mifano ya matumizi ya tafsiri ya biblia inayozingatia mchakato/mwondoko wa kikombozi/nia ya ukombozi.

a. *Utumwa na ajira.*

(1) Ajira tafsiri ya biblia isiyobadilika na vifungu vya utumwa. Waisraeli walitakiwa kutoa mazingira salama kwa watumwa wanaokimbia kutoka nchi ya kigeni kwa ajili ya kutendewa vibaya (**Kumb 23:15-16**). Kwa hiyo, hata kama utumwa uliruhusiwa, Mtazamo wa AK kuhusu utumwa ulikuwa wa kikombozi ukilinganisha na ule wa Mashariki ya Karibu ya Kale. AJ inachukua hii nia ya ukombozi na kupeleka mbali zaidi Paulo akimweleza Philemoni ampokee mtumwa wake aliyekimbia kama “*ndugu mpandwa*” (**Philemoni 15-16**). Ingawaje AK au AJ haikueleza kuhusu kukomesha kwa utumwa. “Tafsiri ya Biblia isiyobadilika ingetumia vifungu vya ukimbizi wa kifungwa kwa kuruhusu umiliki wa watumwa siku za leo, ikizingatiwa kuwa kanisa litatoa mahali pa kuhifadhi wakimbizi wa kitumwa. . . Namna hizo za kutumia maandiko kama maneno yake yanavyosema katika vifungu—maneno hayo ya kifungu yakitafsiriwa pasipo kuzingatia maana ya nia ya kiroho ya mchakato huo wa kifungu. . . Mbaya zaidi ni kwamba kwa kuhoji au kuruhusu utumwa wa kibiblia siku ya leo, hemenutiki tuli inarudisha nyuma viwango vyetu vya haki za binadamu *nyuma* kwa hatua kadhaa. Tungeaibisha Injili inayohubiri uhuru kwa waliofungwa, Injili yenye matokeo ya mawili ya kiroho nay a kimwili.” (Webb 2001: 33-34) Katika muktadha wa ajira za leo, mtu anaweza akawahamasisha kusanyiko la leo kwamba mwajiriwa anapaswa ‘kutii’ na ‘kunyenyekeea’ waajiri wao kwa kutumia vifungu vya kitumwa” (Webb 2001: 37).

(2) Kutumia hemenutiki ya “mchakato wa kikombozi /nia ya kikombozi” kwa vifungu

nya kitumwa, Katika AK na AJ maandiko yalileta tofauti yenyeye uhuru mkubwa. Maandiko yakazidi kuendeleza nia hiyo ya ukombozi kuanzia AK hadi AJ. Kwa hiyo nia hiyo ya ukombozi inatoa tafsiri inayodai kukomesha kabisa utumwa. Hicho ndicho kilichofanyika na wakristo waliokomesha utumwa Uingereza na Amerika katika karne ya 19. Pale vinapotumika vifungu nya kitumwa katika ajira za leo, nia ya ukombozi haibakii katika kuendeleza kutumia “unyenyekevu” kwa mwajiri kwa kutumia vifungu nya kitumwa. “Matumizi hayapuuzi tu mchakato huo ili kufikia hatua kamilifu ya maadili, bali inafumbia macho misingi ya tofauti za msingi za utumwa na mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa wa siku za leo. Tofauti kubwa ni ile ya umiliki na misingi ya kimkataba kwa ajili ya mahusiano kazini. Katika mfumo wa mkataba wa siku za leo hatupaswi kuhubiri utii na unyenyekevu, lakini mwajiriwa mkristo atimize masharti ya katiba kwa uwezo wake wote kwa namna inayomtukaza Mungu na kuwezesha ushuhuda wa Injili kuwa mzuri. Kwa kuongezea, mchakato wa ukombozi wa hemenutiki inategemewa kutumia nia na mchakato kwa habari ya watumwa kwa kuzingatia tamaduni zilizopo sasa. Maandiko yanasmama upande wa watumwa, maskini na wanyonge. Maandiko ni Roho itoayo uzima, iliyoboresha hali za watumwa katika ulimwengu wa kale, ni lazima hata leo yaendeleze mchakato huo leo. Waajiri wa siku za leo, hawatakiwi kunyanyasa katika matumizi ya uwezo wao katika uzalishaji na biashara bali wawajali waajiriwa wao na kuwatendea kwa haki. Mazingira ya kazi, viwango nya mapato, na tofauti kati ya matajiri na maskini ni mambo ambayo nia ya ukombozi ni lazima izingatie kwa dhahiri katika maandiko tunayahusisha haya katika ulimwengu wetu wa leo.” (Webb 2001: 37-38) “Mchakato wa ukombozi” au “Nia ya ukombozi” wa kiblia unaonekana hivi:

X (tamaduni za asili)	=> Y (Biblia)	=> (tamaduni zetu)	=>Z (maadili makamilifu)
Utumwa wenye manyanyaso mengi	Utumwa ukiwa na hali nafuu	Kukomesha kwa utumwa na mazingira ya kazi kuboreshwa	Kukomesha utumwa; kuboreshwa kwa mazingira ya kazi; mishahara kuboreshwa kwa wote; ushirikiano, heshima na makusudi ya pamoja kati ya ngazi zote za kitaasisi.

b. *Ndoa ya jinsia moja*. “Tukiongelea ndoa ya jinsia moja kwa kutumia kanuni ya mfumo wa X=>Y=>Z , tunaona aina tofauti ya mchakato, yakiwa, ni mchakato halisi kutoka X hadi Y. Udhibitisho wa kimaandiko kuhusu nia ya ukombozi wakati inapowasogeza watu wa Mungu kuelekea kwenye kukomesha kabisa ndoa ya jinsia moja. . . Utamaduni wa siku zetu [hasa Magharibi] ungeweza kuwekwa kwenye X (sawa sawa na utamaduni wa asili ulivyokuwa) au inawezekana ikawekwa upande wa kushoto wa X ambapo itaonekana katika eneo la ‘W’. Ili kuendana na nia ya ukombozi leo, jamii ya Wakristo ni lazima waendelee na msimamo ulio kinyume na ndoa ya jinsia moja na kukataza kabisa tabia hiyo, hata kama jamii kwa kiasi kikubwa haikubaliani na wakristo katika msimamo huo.” (Webb 2001: 40) “Nia ya ukombozi” ya kibilia au “mchakato wa ukombozi” ni kama ifuatavyo:

[W] (tamaduni zetu)	=> X (utamaduni asilia)	=> Y (Biblia)	=> Z (maadili makamilifu)
kwa kiasi inakubalika na hakuna kizuizi kwa ndoa ya jinsia moja.	Mchanganyiko wa kukubaliana na hakuna kukatazwa kwa ndoa ya jinsia moja.	Mtazamo kinyume na kukatazwa kwa nguvu kwa ndoa ya jinsia moja.	Mtazamo kinyume na kuzuiwa kikamilifu kwa ndoa ya jinsia moja na ufahamu mkubwa na huruma; matumizi ya hatia iliyopo kuhusu ndoa ya jinsia moja.

### REJEA ZILIZOTUMIKA

Arthur, Kay. 1994. *How to Study Your Bible*. Eugene, OR: Harvest House.

Beale, G. K. 1999. *The Book of Revelation* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

\_\_\_\_\_. 2004. *The Temple and the Church's Mission* (NSBT 17). Downers Grove, IL: InterVarsity.

Blomberg, Craig. 1990. *Interpreting the Parables*. Downers Grove, IL: InterVarsity.

\_\_\_\_\_. 1999. *Neither Poverty nor Riches* (NSBT 7). Nottingham, England: Apollos.

Bullinger, E. W. 1968 (reprint). *Figures of Speech Used in the Bible*. Grand Rapids, MI: Baker.

- Caird, G. B. 1980. *The Language and Imagery of the Bible*. Philadelphia: Westminster.
- Carson, D. A. 1984. *Exegetical Fallacies*. Grand Rapids, MI: Baker.
- \_\_\_\_\_. 1991. *The Gospel According to John* (PNTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.
- \_\_\_\_\_. 1996. *Exegetical Fallacies*. 2<sup>nd</sup> ed. Grand Rapids, MI: BakerAcademic.
- \_\_\_\_\_. 2009. *Preaching Apocalyptic*. Audio mp3. Online:  
<http://resources.thegospelcoalition.org/library?utf8=%E2%9C%93&query=carson+preaching+apocalyptic>.
- Carson, D. A., and Douglas Moo. 2005. *An Introduction to the New Testament*, 2<sup>nd</sup> ed. Grand Rapids: Zondervan.
- Doriani, Daniel. 1996. *Getting the Message*. Philllipsburg, NJ: P&R.
- \_\_\_\_\_. 2001. *Putting the Truth to Work*. Philllipsburg, NJ: P&R.
- Fee, Gordon, and Douglas Stuart. 1982. *How to Read the Bible for All its Worth*. Grand Rapids, MI: Academie.
- Garlington, Don. Not dated. “Reigning With Christ (Revelation 20:1-6 In Its Salvation-Historical Setting).” Online:  
<http://www.mountainretreatorg.net/eschatology/reigning.html>.
- Goldsworthy, Graeme. 1991. *According to Plan: The Unfolding Revelation of God in the Bible*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Green, Joel. 1984. *How to Read Prophecy*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Grenz, Stanley. 1992. *The Millennial Maze*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Hays, J. Daniel. 2001. “Applying the Old Testament Law Today.” *Bibliotheca Sacra* 158: 21-25. Online:  
[http://www.biblicalstudies.org.uk/article\\_law\\_hays.html#top](http://www.biblicalstudies.org.uk/article_law_hays.html#top).
- Holwerda, David. 1984. “Eschatology and History: A Look at Calvin’s Eschatological Vision.” In *Readings in Calvin’s Theology*, edited by Donald Kim, 311–42. Grand Rapids: Baker.
- \_\_\_\_\_. 1995. *Jesus and Israel: One Covenant or Two?* Grand Rapids, MI: Eerdmans.
- International Council on Biblical Inerrancy. 1978. *Chicago Statement on Biblical Inerrancy with Exposition*. Online:  
<http://www.bible-researcher.com/chicago1.html>.
- \_\_\_\_\_. 1982. *Chicago Statement on Biblical Hermeneutics with Commentary by Norman L. Geisler*. Online:  
<http://www.bible-researcher.com/chicago2.html>.
- Irons, Lee. Not dated. “Prophetic Idiom.” Audio mp3. Online: [http://www.upper-register.com/mp3/TUM/55\\_TUM\\_Prophets.mp3](http://www.upper-register.com/mp3/TUM/55_TUM_Prophets.mp3).
- Jackson, Wayne. 2001. “Examining Premillennialism.” Online: <http://www.christiancourier.com/articles/322-examining-premillennialism>.
- Johnson, Dennis. 2007. *Him We Proclaim: Preaching Christ from All the Scriptures*. Phillipsburg, NJ: P&R.
- Kaiser, Walter, Peter Davids, F. F. Bruce, and Manfred Brauch, eds. 1996. *Hard Sayings of the Bible*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Kevan, E. F. 1954. “The Covenants and the Interpretation of the Old Testament.” *Evangelical Quarterly* 26: 19-28. Online:  
[www.biblicalstudies.org.uk/pdf/eq/1954-1\\_kevan.pdf](http://www.biblicalstudies.org.uk/pdf/eq/1954-1_kevan.pdf).
- Klein, William, Craig Blomberg, and Robert Hubbard. 1993. *Introduction to Biblical Interpretation*. Dallas, TX: Word.
- Knight III, George. 1992. *The Pastoral Epistles* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

- Koukl, Gregory. 2001. *Never Read a Bible Verse*. Online: <http://www.str.org/site/News2?page=NewsArticle&id=5466>.
- Ladd, George Eldon. 1972. *A Commentary On The Revelation Of John*. Grand Rapids, MI: Eerdmans.
- \_\_\_\_\_. 1977. "Historic Premillennialism." In *The Meaning of the Millennium: Four Views*, edited by Robert Clouse, 17–40. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Lehrer, Steve. 2006. *New Covenant Theology: Questions Answered*. Steve Lehrer.
- Lysaught, M. Therese. 2005. "Practicing the Order of Widows: A New Call for an Old Vocation." *Christian Bioethics* 11: 51-68.
- Metzger, Bruce, and Michael Coogan, eds. 1993. *The Oxford Companion to the Bible*. New York: Oxford University Press.
- Oropeza, B. J. 1994. *99 Reasons Why No One Knows When Christ Will Return*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- Osborne, Grant. 1991. *The Hermeneutical Spiral*. Downers Grove, IL: InterVarsity.
- \_\_\_\_\_. 2002. *Revelation*. Grand Rapids, MI: Baker Academic.
- Owen, W. Stuart, P. A. Grist, and R. Dowling. 1992. *A Dictionary of Bible Symbols*. London: Grace.
- Payne, J. Barton. 1980 (reprint). *Encyclopedia of Biblical Prophecy*. Grand Rapids, MI: Baker.
- Poythress, Vern. 1993. "Genre and Hermeneutics in Rev 20:1-6," *Journal of the Evangelical Theological Society* 36: 41-54. Online: [http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/36/36-1/JETS\\_36-1\\_041-054\\_Poythress.pdf](http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/36/36-1/JETS_36-1_041-054_Poythress.pdf).
- Ramm, Bernard. 1970. *Protestant Biblical Interpretation*, 3<sup>rd</sup> rev. ed. Grand Rapids, MI: Baker.
- Ramsay, William. 1875. "Triumphus." In *A Dictionary of Greek and Roman Antiquities*, ed. William Smith, 1163-67. London: John Murray. Online: [http://penelope.uchicago.edu/Thayer/E/Roman/Texts/secondary/SMIGRA\\*/Triumphus.html](http://penelope.uchicago.edu/Thayer/E/Roman/Texts/secondary/SMIGRA*/Triumphus.html).
- Roukema, Riemer. 2004. "The Good Samaritan in Ancient Christianity." *Vigiliae Christianae* 58: 56-74.
- Ryken, Leland. 2002. *The Word of God in English*. Wheaton, IL: Crossway.
- Stanley, Andy, and Lane Jones. 2006. *Communicating for a Change*. Colorado Springs, CO: Multnomah.
- Tegart, Brian. 1999. "Literal or Spiritual?" Accessed 5 June 2000 at: <http://www.tegart.com/brian/bibl/prophecy/spiritual.html>.
- Tiessen, Terrance. 1993. "Toward a Hermeneutic for Discerning Universal Moral Absolutes." *Journal of the Evangelical Theological Society* 36: 189-207. Online: [http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/36/36-2/JETS\\_36-2\\_189-207\\_Tiessen.pdf](http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/36/36-2/JETS_36-2_189-207_Tiessen.pdf).
- Travis, Stephen. 1982. *I Believe in the Second Coming of Jesus*. Grand Rapids, MI: Eerdmans.
- Ulfgard, Håkan. 1989. *Feast and Future: Revelation 7:9–17 and the Feast of Tabernacles*. Stockholm: Almqvist & Wiksell.
- VanGemeren, Willem. 1990. *Interpreting the Prophetic Word*. Grand Rapids, MI: Zondervan.
- Walker, P. W. L. 1996. *Jesus and the Holy City: New Testament Perspectives on Jerusalem*. Grand Rapids, MI: Eerdmans.
- Waltke, Bruce. 1988. "Kingdom Promises as Spiritual." In *Continuity and Discontinuity: Perspectives on the Relationship Between the Old and New Testaments*, ed. John Feinberg, 263-87. Westchester, IL: Crossway.
- Webb, William. 2001. *Slaves, Women & Homosexuals: Exploring the Hermeneutics of Cultural Analysis*. Downers Grove, IL: IVP Academic.

Wells, Tom, and Fred Zaspel. 2002. *New Covenant Theology*. Frederick, MD: New Covenant Media.

Willard, Dallas. 1997. *The Divine Conspiracy*. New York: HarperSanFrancisco.

Wolvaardt, Bennie. 2005. How to Interpret the Bible: A Do-It-Yourself Manual. London: Veritas College.

Young, Edward. 1952. My Servants the Prophets. Grand Rapids: Eerdmans.

### **MWANDISHI**



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipata B.A. yake katika Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, na kuibuka na daraja la juu la heshima, mwaka 1974, na kuingizwa katika jamii inayoheshimika ya Phi Beta Kappa. Kisha akapokea J.D. kutoka Cornell Law School, magna cum laude, mwaka 1977, na akawa miiongoni mwa Jamii ya Sheria inayoeshimika ya Coif. Alitumia miaka 28 inayofuata akijihuisha na shughuli za sheria, kama wakili wa sheria anayejitegemea kule Chicago na baadaye kama mdau Kitengo cha sheria cha Menn Law Firm kule Appleton, WI. Mwaka 1982 akaamini na kuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Upendo wake unaokua katika theolojia unalimfanya ahitim shahada yake ya pili katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School kule Deerfield, IL. Akahitim shahada ya pili ya theolojia kutoka TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa Mkurugenzi wa Equipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa Equipping Church Leaders-East Africa ([www.eCLEA.net](http://www.eCLEA.net)). Machapisho yake yaliyosheheni ya masomo ya Biblia yanapatatikana kwenye [www.eCLEA.net](http://www.eCLEA.net). Jonathan anaweza kuandikiwa au kuwasilana naye kupitia barua pepe hii: [jonathanmenn@yahoo.com](mailto:jonathanmenn@yahoo.com).

### **NYONGEZA A**

<http://www.str.org/site/News2?page=NewsArticle&id=5466>

#### ***“Kamwe Usisome Mstari wa Biblia”, Gregory Koukl***

Kama kungekuwa na jambo moja la hekima, sheria moja ya dole gumba, ujuzi moja ninaoweza kuuwasilisha, dokezo moja ambalo ningependa kuwaachia ili liwasaidiane kwa maisha yenu yote, ingekuwa nini? Ni ujuzi gani mmoja wa pekee ambaao nimejifunza kivitendo kama mkristo?

Ni huu hapa: *Kamwe usisome mstari wa Biblia*. Hiyo ni sahihi, kamwe usisome mstari wa Biblia, Badala yake, mara zote soma angalau aya.

#### **Ujanja wangu katika Redio**

Ninapokuwa natoa ujumbe kwenye redio, Ninatumia sheria rahisi kujibu maswali mengi ya Biblia ninayoulizwa, hata kama sijui kabisa kuhusu mstari huo. Ni njia ya ajabu sana ambayo hata wewe unaweza kutumia.

Ninasoma aya, siyo mstari tu. Ninachukua maandiko mengi yaliyopo juu ya mstari na chini ya mstari. Kwa sababu muktadha ndio unaojenga mstari na ndio unaotoa maana mahususi kwa mstari mahususi, Ninaruhusu iniambie nini kinaendelea.

Hii inafanya kazi kwa sababu ni kanuni ya msingi ya mawasiliano: Maana hutiririka kutoka juu kwenda chini, kutoka kwenye sehemu kubwa kwenda sehemu ndogo, na siyo kinyume chake. Ufunguo wa maana ya mstari wowote inatoka kwenye aya, siyo kwenye maneno pekee.

Tarakimu zilizoandikwa mbele ya sentensi inaonyesha kuwa mstari huo unajitegemea katika kutoa maana. Haikuwepo kwenye nakala za asili, ingawa namba ziliwekwa miaka mingi baadaye. Sura na mistari wakati mwengine huwekwa mahali ambapo haistahili kwa bahati mbaya, ikitenganisha maneno ambayo yangeleta maana kwa pamoja.

Kwanza, puuza namba za mistari na jaribu kupata taswira pana. Halafu anza kupunguza taswira. Ni ngumu na inachukua muda. Inachukua muda mchache na uchunguza kidogo kuhusu kifungu.

Anza na muktadha mkubwa wa kitabu. Ni aina gani ya fasihi ni historia, ushairi, methali? Aya inahu nini kwa ujumla? Ni wazo lipi linajengwa?

Tazama ukiwa nyuma ya mstari na uangalie vituo katika simulizi ambalo linafafanua sehemu za wazo. Jiulize, “Ni nini katika aya au kikundi cha aya inatoa dondo kuhusu maana ya mstari?

Kuna sababu inayofanya hili zoezi dogo kuwa na umuhimu. Maneno yana maana tofauti yakiwa katika muktadha tofauti. (hilo ndilo linalofanya maneno yenye maana mbalimbali yafanye kazi). Tukichukulia mstari kama wazo lililojitenga, maana moja inaweza kupatikana kwetu. Lakini tunajuaje ikiwa ni sahihi. Msaada hautoki kwenye kamusi. Kamusi zitafanya jambo liwe na ugumu, na kutupa uchaguzi mwingi, siyo kidogo. Msaada unaweza kutoka mahali pengine karibu kabisa, kwenye aya iliyo karibu.

Tukitazama muktadha mzima, unaweza kufinya mwono wako na kutafuta maana ya mstari peke yake. Kuyajumuisha maneno yote kwa maneno yako mwenyewe.

Mwishoni ni muhimu kuona kama hayo maneno yako mwenyewe yanaleta maana iwekwe kwenye kifungu. Je inaungana kwa uhalisia na taswira kubwa?

Hapa kuna mfano mzuri sana wa namna njia hii ya kuunda maneno binafsi inavyoweza kuwa.

### **Yesu, Muumba ambaye hajaumbwa**

Katika Yohana 1:1mwamini anaongea wazi kwamba “Neno la Mungu alikuwa Mungu” Katika mstari wa tatu anatoa uthibitisho kwa dai hili. Yohana anaandika, “Yote yalifanyika kwa Yeye, na pasipo Yeye hakuna kilichofanyika ambacho kimefanyika.”

Yohana anasema jambo hilo hilo kwa namna mbili tofauti kwa ajili ya kusisitiza na ufanuzi: Kila kitu ambacho kimefanyika kimefanyika kwa Neno, ambalo limefanya litokee. Kama Neno lilifanya kila kitu kitokee, *kwa hiyo* ni lazima Awe alikuwepo kabla ya vyote kuwepo. Kwa hiyo, Neno halikuumba, Yesu ni Muumba ambaye hakuumbwa, Mungu.

Wale wanaokana uungu wa Yesu wanatoa hoja hii, hata hivyo. “Ngoja kidogo, Greg. Hukusoma mstari vizuri. Umekosa jambo fulani katika kifungu. Angalia msemo, ‘pasipo Yeye.’ Mtume hamhusishi Yesu kwenye mazungumzo yake. Uki sema, ‘Pasipo Billy, familia yote inaenda Disneyland’ humaanishi kwamba Billy hakuwa sehemu ya familia, eti kwa sababu tu hujamhusisha kwenye mazungumzo. Kila mtu kwenye familia anaenda Disneyland *isipokuwa* Billy. Kwa njia hiyo hiyo, kila kitu kilichoumbwa kimeumbwa na Yesu *isipokuwa* Yesu mwenyewe. Yehova alimwumba Yesu kwanza, Kisha Yesu akaumba vitu vingine vyote. Yesu siyo Mungu.”

Angalia hoja hii mbadala imetokea kuondoa “pasipo Yeye” na kuingiza msemo “Isipokuwa Yesu.” Embu tuseme kuna mfanano. Sawa, tujaribu kubadilisha ili tuone. Mstari utaonekana hivi: “*Isipokuwa Yesu, hakikufanyika chochote kilichofanyika.*”

Kama ubongo wako utapata shida kuelewa jambo hili, sitashangaa. Msemo uliojitokeza hauna maana kabisa. Ukiwa makini, sentensi hiyo ina maana, Yesu ni kiumbe pekee kilichoumbwa ambacho kinaishi. Soma tena na uone mwenyewe, Kwa hakika “pasipo Yesu” haiwezi kuwa na maana ya “isipokuwa Yesu.” Misemo hii haifanani.

“Pasipo Yeye” inamaanishi kitu kingine tofauti. Ina maana “pasipo utendaji Wake” Ni sawa na kusema, “Pasipo mimi kamwe hamwezi kwenda Disneyland. Mimi nina gari.” Pasipo Yesu’ kutenda hakuna ambacho kingefanyika ambacho kimefanyika. Kwa nini? Kwa sababu Yesu ni Muumba. Yeye ni Mungu. Hiyo inaleta maana kamili katika muktadha huo.

Nitoe mifano mingine.

### **Kuwa na “amani” nayo**

Wakolosai 3:15 ni kifungu kinacholewaka vibaya na baadhi ya wakristo. Paulo anaandika, “Na amani ya Kristo iamue miyoni mwenu.” Wengine wanarejea maana ya neno “iamue” kwa kigiriki ni kuhukumu au kuamuru kwa mamlaka. Wanauona mstari huu kama chombo cha kujua mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu.

Kufikiri kirahisi kunatupa maana hii. Ukimumbana na mazingira ya kufanya maamuzi, omba. Ukipata “amani” moyoni mwako, endelea. Kama huna amani moyoni, usichukue hatua. Hii hali ya ndani ya kuhisi amani inatenda kama mwamuzi anayekusaidia kufanya maamuzi sawa sawa na mapenzi ya Mungu. Kwa maneno mengine msatari unaweza kuandikwa hivi: “Ruhusu amani moyoni mwako iwe mwamuzi kuhusu mapenzi ya Mungu kwa maisha yako binafsi.” Je, Hii ndiyo maana ya Paulo?

Huu ni mfano halisi wa jinsi ambavyo ujuzi wa lugha ya kigiriki unavyoweza kuwa hatari kama muktadha haujazingatiwa. Neno “amani” lina maana mbili. Inaweza kuwa na maana ya furaha ya ndani na kuwa vizuri kihisia. Paulo alikuwa na maana hii katika Wafilipi 4:7: “Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi miyo yenu na nia zenu katika Kristo

Yesu.” Hii ni maana ya amani ya kibinafsi.

Neno pia lina maana ya hisia baada ya kufikia lengo fulani. Ina maana pia ya kutokuwepo kwa mgongano katika pande mbili ambazo zilikuwa na mgogoro. Hii maana ndiyo ile ya Paulo katika Warumi 5:1: “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” (Angalia tofauti kati ya *amani ya Mungu* na *amani kwa Mungu* katika mistari hii miwili.)

Paulo alikuwa anamaanisha amani gani alipokuwa anaongea na Wakolosai? Kigiriki hakitupi ishara yejote maana neno hilo hilo limetumika katika mambo matatu. Mara nyingine tena, muktadha ni mfalme. Maana halisi au mahususi inaweza kufahamika kutokana na mazingira yanayozunguka mstari huo.

Katika mstari wa 11, Paulo anasema kwamba katika mwili wa Kristo hakuna migawanyiko kati ya Wayunani na Wayahudi, mtumwa na mtu huru, nk. Anasisitiza umoja katika mwili wa Kristo unaodhihirishwa kwa uwepo wa msamaha, unyenyekevu, na uungwana. Kisha anaongezea maelewano (“amani”) iwe ndiyo sheria inayoongoza mahusiano yetu.

Paulo alikuwa ana hisia ya kijumla yaani kukosekana kwa amani kati ya mkristo na mkristo na siyo kukosekana kwa amani ndani ya moyo wa mtu binafsi.

Hii inakuwa wazi tukiunganisha misemo iliyopendekezwa kwenye muktadha:

Jivikieni moyo wa rehema, ukarimu, unyenyekevu, wema na uvumilivu, mkichuliana kila mmoja na mwenzake, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake na amsamehe kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi. Na zaidi ya hayo yote, Jivikeni upendo, ambao ni kifungo cha umoja. Ruhusuni hisia ya amani miyoni mwenu iamue kuhusu mapenzi ya Mungu kwa maisha ya kila mmoja, ambayo ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; mkiwa na shukrani.

Dhidi ya.

Jivikieni moyo wa rehema, ukarimu, unyenyekevu, wema na uvumilivu, mkichuliana kila mmoja na mwenzake, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake na amsamehe kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi. Na zaidi ya hayo yote, Jivikeni upendo, ambao ni kifungo cha umoja.. Ruhusuni maelewano, siyo ugomvi, iwe sheria inayowaongoza ninyi, ambayo ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; mkiwa na shukrani.

Ya kwanza ni tofauti kabisa na muktadha; ya pili inakubaliana kabisa na kila kilichopo kabla na baada. Katika muktadha wa Wakolosai 3, hakuna dokezo linalohusu hisia ya ndani kama kukubalika kiungu kwa maamuzi yetu. Kufanya maamuzi binafsi siyo lengo la aya hiyo. Maelewano na umoja wa mwili ndiyo lengo.

### “Nikiinuliwa Juu”

Yohana 12:32 ni swala lingine ambapo mstari unaweza kuwa na maana mbili tofauti kabisa. Ni jambo ambalo siyo sawa kwa viongozi wa sifa kunukuu msemo huu wa Yesu: “Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.”

Sisi “tunamwinua juu” Bwana tunapomsifu Yeye na kutangaza Utukufu wake. Tunapojielekeza kwa Yesu na kutangaza utukufu wake, nguvu ya Kristo inaachiliwa kubadilisha miyoyo ya wasikilizaji nao wanavutwa Kwake. Hii ndiyo maana ambayo kiongozi wa ibada anayo katika ufahamu wake, lakini siyo maana aliyokuwa anasema Yesu.

Tunapotumia msemo wetu kwa kuongeza mstari unaofuata, matokeo ni kama ifuatavyo: “Na Mimi, *nikiinuliwa mbele ya watu*, nitawavuta watu wote kwangu.’ Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa” (Yohana 12:32-33).

Oh. Kumsifu Yesu kutamwua? Sidhani hivyo. Hakuna utata sasa. Katika hili, “kuinuliwa juu” ni wazi kwamba inamaanisha kusulubiwa.

Kuelewa msemo huu katika muktadha kunatoa nuru kwenye kifungu kingine kinachofahamika, Yohana 3:14-15: “Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye.

Kwa maneno yetu tunaweza kusema hivi: “Na kama vile Musa alivyomwinua nyoka jangwani, vivyo hivyo na Mwana wa Mtu atasulubiwa ili kila amwaminiye awe na uzima wa milele katika Yeye.”

Hii inaleta maana inayoelewaka. Yesu alipaswa kusulubiwa kabla wokovu haujatolewa, mwelekeo unaofaa kuelekea kwenye mstari unaofuata, mstari maarufu kwa wokovu wa ulimwengu: Yohana 3:16.

Embu tujaribu nyingine.

### **“Kondoo zangu waisikia sauti Yangu”**

Wengi wamechukulia maneno haya ya Yesu katika Yohana 10 wakimaanisha kwamba wakristo wanapewa uwezo wa “kusikia” maelekezo ya Mungu kwa ajili ya kila mtu binafsi. “Kusikia sauti ya Mungu” inachukuliwa kama ujuzi wa muhimu unayowezesha maisha yatakiwayo kwa mkristo. Wakiamini kwamba, huu ni ujuzi anaujifunza mtu na kuupata kadiri anavyokua katika Kristo. Unamweshesha yeche kumtambua mapenzi ya Yesu katika mazingira yeoyote kwa kuwa “husikia” sauti ya Yesu.

Pamoja na hayo, Yesu hakuwa na wazo hili katika ufahamu wake. Kutohakana na muktadha unaozunguka mstari na ufanuzi amba Yohana anautoa mwanzoni mwa sura. Katika mstari wa 6, Yohana anaeleza wazi wazi kwamba wakati anaongea kuhusu kondoo “wanasikia sauti yake” anatumia lugha ya ishara.

Neno “sauti,” haiwezi kwa hakika kumaanisha aina fulani ya sauti ya ndani kwa sababu jambo silo la kuonyesha ishara. Ni picha ya jambo lingine zaidi. Sikia sauti, wasilisha. Ina maana gani?

Muktadha unashimulia hadithi. Yesu anasema, Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Anaongeza, “Nami nawapa uzima wa milele” (27-28). Angalia huo mtiririko: Kondoo zake husikia sauti yake. Wanaitikia kwa kumfuata Yeye. Kisha Yeye huwapa uzima wa milele. Kusikia sauti ya Yesu’ ni lugha ya alama inayomaanisha utendaji kazi wa ndani wa Roho Mtakatifu unaotuongozwa kwenye wokovu wetu. Matokeo *yake ni wokovu; yenye siyo matokeo ya wokovu*. Hapa inatumika kwa wale wasiookoka waliokusudiwa kwa ajili ya ufalme, siyo waaminio walio ndani ya ufalme.

Hii inaleta maana kamili tukitazama muktadha wa sura nzima. Wayahudi hawakuwa na shida ya “*kusikiliza*” maneno ya Yesu. Walikuwa hawajui *anachosema* Yesu. Tatizo ni kwamba *hawaitikii kwa imani*. Kwa nini Wayahudi “*hawamsikii*” Yesu kwa kuitikia kwa imani? Yesu anatuambia waziwazi. “*Hawasikii*” kwa sababu Mungu hasemi na wao. Wao si miongoni mwa kondoo amba Baba amempa Mwana (26).

Sauti inayoongelewa hapa siyo sauti ya utulivu, ndogo ya binafsi inayomwongoza mtu ambayo hutoka kwa Mungu kwa Wakristo, bali ni wito wa Roho Mtakatifu unaotendao kazi kuwaleta wasioamini kwenye wokovu.

Kwa mara nyingine tena tukirudia kwa maneno yetu wenye tunapata msaada:

Lakini ninyi hamsadiki, kwa sababu hammo miongoni mwa kondoo wangu. Wakristo waliokomaa ni wale wenye uwezo wa kuhisi mwelekeo binafsi kwa ajili ya maisha na kutii, na matokeo yake nawapa wao uzima wa milele na kamwe hawataangamia; na hakuna atakayewapokonya katika mikono yangu. Baba yangu aliyenipa Mimi hao, ni mkuu kuliko wote....

Dhidi ya.

Lakini ninyi hamsadiki, kwa sababu hammo miongoni mwa kondoo wangu. Wale anipao Baba wawe kondoo zangu ni wale wanaoitikia kwa ujumbe wangu na huniamini, na matokeo yake nawapa uzima wa milele, nao hawataangamia kamwe; na hakuna atakayewapokonya mikononi mwangu. Baba yangu aliyenipa Mimi hao, ni mkuu kuliko wote....

Mtazamo wa kwanza hakika unafanya wokovu uwe unategemea uwezo wa kupata mawasiliano binafsi kutoka kwa Mungu. Wa pili unafanya wokovu uwe unamtegemea Baba, ambaye ni wazo la Yesu katika kifungu.

Kwa Yesu, “*kumsikia*” Mungu siyo ujuzi ulioboreka amba mtu lazima aupate ili kufungua njia za kuwasiliana na Baba. Ni alama ya lugha. Kusikia sauti ya Yesu siyo kupata mawasiliano binafsi kuhusu mwelekeo wa kuchuchua. Ni kuokolewa. Ni matokeo ya Baba kumvuta asiyemini kwenye mikono ya Yesu.

### **Mkate wa kila siku?**

Hii huibua swali la muhimu kuhusu ibada ya kila siku ambayo huwa na ujumbe mfupi kutoka kwenye mstari mmoja. Katika mtazamo wangu, nyakati hizo za utulivu husaidia zinaweza kuwa za uvuvio, lakini huja na mambo ya kutuvuta nyuma.

Kwa bahati mbaya, lakini uwezekano unaweza kuepukwa kwa kukumbuka sheria yetu: *Kamwe usisome mstari wa Biblia*. Badala yake, soma aya nzima, kwa uchache. Siku zote anagalia muktadha. Chunguza mtiririko wa mawazo. Kisha jikite

kwenye mstari.

Kumbuka, maana siku zote inashuka kutoka juu kuja chini, kutoka kwenye vipengele vikubwa kuja kwenye vipengele vidogo. Kutafakari kifungu cha Biblia kutoka kwenye ujumbe au kwa ajili ya kuabudu inaweza kujenga, kutia moyo, na kuinua. Kama siyo ujumbe wa kifungu, unakosa mamlaka ya Biblia hata kama nukuu hiyo imetoka katika Neno la Mungu.

Kama utafanya jambo hili moja, kama utasoma kwa makini katika muktadha ukitumia kanuni ya kutamka kwa maneno yako mwenyewe utaanza kuelewa Biblia kama kusudio la Mungu. Bila picha kubwa utapotea.

Pale tu unapofahamishwa vema na Neno la Mungu na namna ilivyoandikwa katika muktadha wake ndipo unawenza kubadilishwa nalo. Kila kipande kinakuwa na nguvu ikiwa kinafanya kazi katika ujumla wake.

Ni somo la muhimu sana ambalo nimewahi kujifunza kwa vitendo kwamba, .... Na kitu [sic] kimoja cha muhimu sana ambalo nimewahi kukufundisha wewe.

**Vyanzo vingine vya kujifunza zaidi:**

Russell, Walt Playing with Fire How the Bible Ignites Change in Your Soul. Colorado Springs: NavPress, 2000.

Koukl, Gregory "The Perils of Prooftexting," *Solid Ground*, Sept-Oct 1999.

Sire, James *Scripture Twisting*. Downers Grove: InterVarsity Press, 1980.

Carson, D.A. *Exegetical Fallacies*. Grand Rapids: Baker, 1984.

Fee, Gordon, & Stuart, Douglas *How to Read the Bible for All It's Worth*. Grand Rapids: Zondervan, 1982.

©2001 Gregory Koukl. Uzalishaji wa nakala hii unaruhusiwa kwa matumizi yasiyo ya kibashara tu. Kwa maeleo zaidi, wasiliana na Stand to Reason at 1438 East 33<sup>rd</sup> St., Signal Hill, CA 90755. (800) 2-REASON (562) 595-7333. www.str.org

## **NYONGEZA B**

### **Mahubiri ya Kibiblia kwa Njia ya Kujifunza kwa Maswali**

Greg Scharf, Associate Professor of Pastoral Theology,  
Trinity Evangelical Divinity School<sup>9</sup>

"Usiniulize Swali nami sitakuambia Ukweli."

**Makisio:**

- Kujifunza kifungu kwa makini ni hitaji la muhimu sana ili kuhubiri kwa uaminifu. Tunavyojifunza tunaumba jinsi tutakavyohubiri.
  - Uchunguzi sahihi unawenza ukawezeshwa na maswali yanayochambua kifungu kwa undani. Maswali mengi yatasaidia uelewa wetu wa kifungu; baadhi yatakuwa na msaada maalumu katika kuanda mahubiri ya kifungu.
  - Hatuwezi kuhubiri kwa uaminifu kifungu mpaka tufahamu zaidi ya kile kinachosemwa. Ni lazima tujitahidi kugundua ni nini kinakusudiwa kufikiwa na namna ya kukifikia.

**Maswali yaliyopendekezwa (yakihusika mawili ya msingi aliyouliza Haddon Robinson ) ili kukamilisha yale ambayo tavarì umekuwa ukijiuliza:**

**1. Tuna nini hapa? (Kifungu hiki kazi yake ni nini?)**

- amri
- taarifa ya tukio, mazungumzo, maombi
- simulizi kuhusu ukombozi wa Mungu
- onyo
- unabii, "Asema Bwana"
- maeleo ya kiungu
- mfano

<sup>9</sup> Dr. Scharf ni Mwenyekiti wa Idara ya Theolojia ya Kichungaji katika Trinity Evangelical Divinity School, Deerfield, IL. Yeye ni mwandishi wa *Jiandae Kuhubiri* (Christian Focus, 2005). Machapisho yanatumiwa kwa ruhusa ya Dr. Scharf. Mabadiliko madogo yamefanywa na Jonathan Menn kwa ruhusa ya Dr. Scharf.

- ushuhuda
- ukiri/ungamo
- dua/ombi
- pumziko
- muunganiko wa simulizi la ukombozi
- ombolezo
- kutia moyo au kusifu.
- uzao/ukoo
- salamu au Baraka
- wimbo/tenzi

## 2. Kifungu hiki kinazungumzia nini?<sup>10</sup> (*Je somo kuu la kifungu hiki ni nini?*)

Kwa mfano, kifungu kimsingi kinahusu:

- maombi
- imani
- imani
- fundisho
- uasi
- uzinzi
- hofu
- furaha
- utawala
- njia za Mungu
- au kimebeba somo lingine

## 3. Je mwandishi anasema nini kuhusu somo hili?

Ili kujibu hili swalii tuta:

- Chunguza ni nini zaidi (nje na kile ambacho tunazingatia kuhusu somo) kimetajwa kwenye kifungu.
- Fupisha muktadha wa kifungu kama unavyohusiana na somo la kifungu.
- Vumbua ni kwa jinsi gani mambo mengine yaliyotajwa kwenye kifungu yanahohusiana na kile unachotambua kwamba ndiyo somo.

## 4. Ni mwitikio gani wa imani ambao Roho Mtakatifu anahitaji kwa wasomaji wa kifungu? (Kwa nini Roho Mtakatifu ametaka kuingiza kifungu katika maandiko yanayokubalika?)

Kwa mfano, Roho Mtakatifu huenda anataka kusababisha:

- toba
- tumaini kwa Mungu
- ungamo la dhambi; kumkiri Kristo
- aina yeoyote ya utii.

## 5. Je ni kwa namna gani kifungu hiki kinamsukuma msomaji afikie mwitikio uliokusudiwa?

Hili swalii linajikita katika kuhusika kwetu na namna ambavyo kifungu kilichopo mbele kinatutaka tutimize kusudi lake. Kujivika ule ufahamu tuliuopata kutoka kwenye ujumbe wetu ili kutumia vile vipengele vya kifungu vinavyotumika kufikia kusudia ambalo kwa hilo limeandikwa. Kwa mfano tunaweza kugundua:

- lugha za alama/ishara
- mahojiano
- mifano, yote mawili chanya na hasi
- hofu ya kimungu ya matokeo ya kuhuzunishwa yaliyoorodheshwa.
- udhihirisho wa faida za imani inayotuelekeza kwenye utii.
- maoni ya mchapishaji, mf., **1 Wafalme 12:15**
- rufaa ya moja kwa moja
- matumizi ya sifa ya aina fulani ya fasihi. Hivyo kwa mfano, shairi linaweza kutumia taswira au usemi fulani wa kukumbuka ili kuvuta hisia za msikiaji, mfano **Zaburi 84:3**, inayozungumzia kuhusu mbayuwayu kutengeneza kiota chake karibu na madhabahu ya Mungu.

## 6. Ni kwa namna gani kifungu kinachangia kwenye taswira pana ya ukombozi?

- Je inatuelekezaje kwa Kristo?
- Ipo wapi katika mtiririko wa simulizi la Kibiblia?
- Je ilisababisha matokeo gani kwa wasomaji /wasikilizaji wale wa awali?

<sup>10</sup>Haddon Robinson katika *Mahubiri ya Biblia: Ukuza*.

## **Nyongeza C**

[http://www.biblicalstudies.org.uk/article\\_law\\_hays.html#top](http://www.biblicalstudies.org.uk/article_law_hays.html#top)—*Bibliotheca Sacra* 158: 629 (2001): 21-35

### **Kutumia Sheria za Agano la Kale Leo, J. Daniel Hays<sup>a</sup>**

[uk.21]

Mkristo anawezaje kutumia sheria za agano la kale? Ni hakika kwamba amri katika sheria za Musa ni za muhimu, Kwa kuwa zinafanya sehemu ya muhimu ya ufunuo wa Mungu ulioandikwa. Lakini bado kuna sheria katika Agano la Kale ambazo henzieleweki kwa wasomaji wa siku za leo (mf., “Usimtokose mwanambuzi katika maziwa ya mama yake,” Kutoka. 34:26; “Wala usivae mwilini mwako nguo ya namna mbili zilizochanganywa pamoja,” Mambo ya Walawi. 19:19; “Ujifanyizie vishada katika pembe nne za mavazi yako ya kujunika,” Kumb. 22:12).<sup>1</sup>

Wakristo hukiuka baadhi ya sheria za Agano la Kale zenye masharti fulani (mf., “Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke,” Kumb. 22:5; “Mwondokeeni mtu mwenye mvi,” Mambo ya Walawi. 19:32; “Na nguruwe, kwa kuwa amepasuliwa ukwato lakini hacheui, huyu ni najisi kwenu msile nyama zao, wala mizoga yao msiiguse,” Kumb. 14:8).

Zaidi ya hayo, wakati waumini wanaacha kufuata amri nyingi za Agano la Kale, wanashika zingine, hasa hasa amri kumi, kama maadili mema kwa wakristo (mf., “Mpende jirani yako kama nafsi yako,” Mambo ya Walawi. 19:18; “Usiue,” Kutoka. 20:13; “Usizini,” Kumb. 5:18).

Kwa nini wakristo hushika amri zingine na kupuza zingine? Zipi zinfaa na zipi hazifai? Wakristo wengi hufanya maamuzi haya kwa kutazama ikiwa sheria hiyo inafaa bila kuangalia sababu za msingi. Kwa hakika utaratibu huu usio na kanuni wa kutafsiri Sheria za Agano la Kale haukidhi haja. Basi Wakristo wanapaswa kutafsiri vipi sheria? [uk.22]

### **Mtazamo wa kawaida**

Wanazuoni wengi wa kiinjili hutafsiri sheria za Musa wakisitisiza tofauti iliyopo kati ya maadili, hali ya kijamii, na sheria za maadhisho. Wanatafsiri sheria ya maadili kwamba ni ile ambayo kweli yake haifungwi na wakati ikizingatia matarajio ya Mungu kwa habari ya tabia njema kwa mwanadamu. “Mpende jirani yako kama nafsi yako” ni mfano mzuri wa sheria ya maadili. Sheria za kijamii ni zile zinazohusika na mfumo wa kisheria wa wana wa Israeli, ikihusisha sheria za ardhi, uchumi, na jinai. Mfano wa sheria za kijamii ni Kumb. 15:1, “Kila miaka saba, mwisho wake, fanya maachilio.” Sheria za maadhisho ni zile zinazoshughulika na dhabihu, sherehe, na huduma za makuhani. Mfano ni Kumb. 16:13, inayowaelekeza wana wa Israeli hivi “Fanya sikukuu ya vibanda siku saba, utakapokwisha kuyakusanya yatokayo katika sakafu yako ya nafaka, na katika kinu chako cha diva.”<sup>2</sup>

Katika njia hii ya kawaida tofauti kati ya maadili, mambo ya kijamii na sheria za maadhisho ni muhimu sana kwa sababu ufahamu huu unamfanya mwamini kujua ikiwa sheria fulani inamhusu au la. Sheria za maadili, kwa mfumo huu wa kutafsiri ni za kila mahali na hazipitwi na wakati. Zinatumika kama sheria kwa wakristo leo. Sheria za kijamii na za maadhisho zilikuwa kwa ajili ya Israeli ya wakati ule tu. Hazitumiki kabisa kwa wakristo siku za leo.<sup>3</sup>

Hata hivyo, njia hii ya kawaida ina mapungufu kadhaa, na haziakisi kanuni za kweli za hemenutiki.<sup>4</sup> Njia hii ina mapungufu kwa sababu zifuatazo.

### **Tofauti zenyewe hazina mantiki**

Tofauti zinazoonekana katika sheria za maadili, kijamii na maadhisho si za kimantiki maana zinaingizwa kutoka nije ya kifungu chenyewe. Agano la [uk.23]Kale peke yake haionyeshi tofauti hizo. Kwa mfano “mpende jirani yako kama nafsi yako” (Mambo ya Walawi. 19:18) inafuatana kwa karibu na mstari kwa sheria isemayo “Wala usivae mwilini mwako nguo ya namna mbili zilizochanganywa pamoja” (19:19).<sup>5</sup> Je mstari wa 18 utatumika kama amri, ikiwa mstari wa 19 umekataliwa jumla? Kifungu hiki hakitupi mwelekeo kwamba kuna badiliko la kimafundisho lililotokea kati ya mstari hii miwili. Ni kwa msingi upi mmoja anaweza akaamua mstari moja kwamba unafaa kwa watu wote na haupitwi na wakati hata kwa waumini wa kikristo, wakati huo amri katika mstari unaofuata inakataliwa? Nyingi ya amri hizi zinazoitwa za maadili, za kijamii, na maadhisho huwa zinakuwa pamoja bila ya udhihirisho wa kimaudhui kwamba kuna tofauti kati yao.

Kwa kuongeza mara zote ni vigumu kujua ni katika kipengele gani sheria inaangukia.<sup>6</sup> Kwa sababu sheria za Musa zinafafanu ushirika wa agano kati ya Mungu na Israeli, kwa asili ni ya kitheolojia. Sheria zote ni za kitheolojia. Je sheria yaweza kuwa ya kitheolojia lakini isiwe ya kimaadili? Kwa mfano Mambo ya Walawi 19:19 inaagiza, “Usipande shamba lako mbegu za namna mbili pamoja; wala usivae mwilini mwako nguo ya namna mbili zilizochanganywa pamoja..” Moja

ya maudhui makuu yanayojitokeza katika Mambo ya Walawi ni Utakatifu wa Mungu. Maelezo ya Mungu katika Mambo ya Walawi 19 yametanguliwa na amri, "Iweni watakatifu kwa kuwa Mimi, Bwana Mungu wenu, ni mtakatifu." Sehemu ya maudhui haya ni kwamba vitu vitakatifu ni lazima vitengwe na vitu vichafu. Wakati kuchanganya kwa mbegu au nguo haiwezi kueleweka vizuri, ni hakika kwamba kuna uhusiano na utakatifu wa Mungu. Kwa hakika sheria zote za walawi kuhusu kujitenga inahusu kanuni ya utakatifu ya Mungu isiyobadilika na huko kutenganisha ni kwa sababu ya huo utakatifu. Je sheria hii inaachaje kuwa ya kimaadili?

[uk.24]

Hata amri kumi, mfano wa wazi kabisa wa sheria iitwayo ya maadili, linatoa changamoto la kutofautisha kimaadili, kijamii, na za maadhisho. Kwa mfano sheria ya sabato ni ya kimaadili au ya maadhisho? Kama maudhui yake ni kigezo, basi, sheria ya Sabato, amabayo kwa wazi kabisa ni sehemu ya ibada ya kiisraeli ni maadhisho, na ni sheria ya maadhisho na wala siyo ya kimaadili. Lakini kama maudhui siyo kigezo kwa ajili ya kutofautisha, basi ni nini? Ikiwa mahali ilipo katika amri kumi za Mungu ni kipimo kwa ajili ya sheria ya maadili, hivyo kuna mfumo rahisi tu wenye vipengele viwili: (a) Amri kumi za Mungu, ambazo ni kwa ajili ya wote na kwa nyakati zote zinatumika kwa wakristo leo kama sheria ya maadili, na (b) sheria zingine zinazosalia, ambazo hazitumiki leo. Kwa hakika hii haikubaliki kwa sababu hairuhusu waamini kutumia Mambo ya Walawi 19:18, "Mpende jirani yako kama nafsi yako," ambayo Yesu alisema ni amri kuu ya pili. Kuchukua Mambo ya Walawi 19:18 kutoka kwenye mistari inayozunguka inahitaji kutumia kigezo cha maudhui yake katika kutofautisha. Na kama maudhui ni kigezo, basi Sheria ya Sabato inatakiwa ihesabike mionganoni mwa sheria za maadhisho.

Zaidi ya hayo, ingawa wakristo wengi hudai kuwa Sabato ni sheria ya maadili, hakuna anayeshika amri hiyo kwa usahihi. Kwenda kanisani siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya wiki, haiwezi kuhesabika kama kushika Sabato. Musa asingekubali siku ya kwanza ya Juma kuwa ni badala ya siku ya Sabato. Pia kushika sheria za Sabato ilikuwa inazingatiwa zaidi na wala siyo mahudhurio tu ya kanisani. Katika kitabu cha Hesabu mtu aliuawa kwa sababu aliokota kuni siku ya sabato (Hesabu. 15:32–36). Kwa hiyo kutofautisha kati ya sheria ya maadili, ya kujamii, na maadhisho inaonekana kukosa mantiki na haifuati yaliyomo katika kifungu. Je wakristo watumie tofauti zisizo na mantiki katika mambo muhimu yanayohitaji utendaji?

### Maelezo sahihi katika Agano la Kale yapo katika simulizi iliyopo kwenye kifungu na ni lazima ifasiriwe ipasavyo

Maelezo halali katika Agano la Kale hayajitenga, badala yake, Sheria ya Musa imebebwa katika historia ya theolojia. Ni sehemu muhimu ya simulizi inayozanzia Mwanzo 12 hadi 2 Wafalme 25. Sheria inajieleza yenye, kama aina fulani ya mtiririko usiounzana lakini ni mfumo wa tabia wa nyakati zote na mahali pote. Na inawakilishwa kama sehemu ya simulizi la theolojia linayolezea jinsi Mungu alivyowatoa watu wake kutoka Misri hadi Nchi ya Ahadi na kuwajenga kama watu wake.

Kwa mfano mafundisho makuu katika Kutoka yameandikwa katika Kutoka sura 20-23. Sehemu hii inahusisha Amri Kumi. Hata hivyo, muktadha wa simulizi la sura hizi ni lazima uangaliwe. Sura kumi na tisa za mwanzo zinælezea habari za Israeli [uk.25] wakiwa watumwa kule Misri na ukombozi wao kupitia matendo makuu ya Mungu. Sehemu hii inaælezea wito wa Musa na kukutana kwake kwa nguvu na Farao. Inaæleza mapigo ya wamisri, ikihusisha kuuawa kwa wazaliwa wa kwanza wa Wamisri. Kisha Musa anawaongoza wana wa Israeli kupitia bahari ya Shamu. Simulizi linælezea safari yao ya jangwani, hadi mwezi wa tatu tangu kutoka kwao, Waisraeli wanafika mlima Sinai, mahali Mungu anawaingiza katika mahusiano ya kiagano (Kutoka. 19). Amri kumi katika Kutoka 20 na sheria zinazofuata katika Kutoka 21-23 ni sehemu ya simulizi hili ndefu.<sup>8</sup>

Kitabu cha Mambo ya Walawi pia imepambwa kwa simulizi kuhusu taswira ya mazingira au masharti ya kukutana na Mungu katika mlima Sinai. (Mambo ya Walawi. 26:46; 27:34). Sheria katika Mambo ya Walawi imeelezwa kama sehemu ya mazungumzo kati ya Mungu na Musa. Hayo mazungumzo ni sifa halisi ya maelekezo au ufanuzi. Kitabu kinaanza kwa kusema, "Bwana akamwita Musa na kusema naye kutoka kwenye hema ya kukutania." Msemo, "Bwana akanena na Musa unajirudia rudia katika kitabu kizima." Kwa kuongezea kitabu cha Mambo ya Walawi kinahusisha misemo ya nyakati mbalimbali,<sup>9</sup> kiashiria cha malelezo au hadithi zinazoenda na wakati, sifa nyingine ya maelezo.

Kitabu cha Hesabu kinachukua habari kutoka kitabu cha Kutoka, mwaka wa pili tangu walipotoka Misri (Hesabu. 1:1) na kuelezea safari ya Israeli na kuzunguka kwao kwa miongo minne zaidi (33:38). Kiini ni Israeli kukataa ahadi katika sura ya 13 na 14. Huku kuasi kulisababisha miaka ya kuzunguka yaliyorekodiwa kwenye kitabu. Nyakati kadhaa Mungu aliwapa Israeli amri za ziada. Kama ilivyo katika Kutoka na Mambo ya Walawi sheria katika kitabu cha Hesabu zipo katika mfumo wa kukazia simulizi.

Mfumo wa simulizi katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni katika mwezi wa kumi na moja wa mwaka wa arobaini wa Kutoka (Kumb. 1:3), punde kabla ya Israeli kuingia Kanani. Mahali pameelezwani—mashariki mwa Mto Yordani (1:1, 5). Israeli walikuwa wamemaliza [uk.26] miaka arobaini kama adhabu ya kukataa kuingia katika nchi. Sasa kizazi kipyä kimekua na Mungu akawapa maelezo ya agano alilofanya na baba zao miaka arobaini iliyopita. Kiasi kikubwa cha

Kumbukumbu la Torati ni hotuba ya Musa aliyoitoa kwa niaba ya Mungu. Hotuba hizi zina uhusiano na simulizi kwa sababu zinazeleza muda, mahali, na wahusika wakuu kama vile masimulizi yalivyo. Pia mwisho wa kitabu una baadhi ya masimulizi yasiyo sheria, kuteuliwa kwa Yoshua kama kiongozi (31:1–8), wimbo wa Musa (32:1–47), Baraka za Musa na makabila (33:1–29), na kifo cha Musa (34:1–12). Zaidi ya hayo matukio ya Kumbukumbu la Torati yanaingia hadi kitabu cha Yoshua, mahali ambapo simulizi linaendelezwa bila kukatishwa.

Kwa hiyo sheria, ni sehemu ya simulizi la vitabu vitano vya Musa na simulizi lake linahusika kwa nguvu na kutoka kwa wana wa Israeli, kuzunguka jangwani na kumiliki kwao. Namna moja ya kutafsiri sheria ni lazima izingatie wazo hili. Kuunganisha kifungu na muktadha wake ni jambo la msingi katika kanuni ya kutafsiri. Sheria ni sehemu ya hadithi, na kwa hiyo hadithi inatoa muktadha katika kupata tafsiri ya sheria hiyo. Njia ya kutafsiri sheria za Agano la Kale inatakiwa ifanane na njia za kutafsiri simulizi la Agano la Kale, kwa sababu sheria kimuktadha ni sehemu ya simulizi.

Je hii inapoteza nguvu na msukumo wa kifungu? Je wakristo wanatakiwa wajiveke chini ya sheria kabla ya kusikia wito wa kutii Maandiko? Je masimulizi katika Maandiko hayana nguvu sawa na sheria? Kutoa mamlaka makubwa kwa sheria za Musa zaidi ya maadili ya Kikristo kuliko masimulizi mengine ya Agano la Kale ni kutengeneza utaratibu ndani ya utaratibu. Vile vile kusema maelezo sahihi yanatakiwa kutafsiriwa kama maelezo ya simulizi kwa hakika hayaondoi mamlaka ya kiungu katika maandiko. Wanafunzi walipookota masuke siku ya Sabato, mafarisayo wakawahukumu kwa kukiuka sheria ya sabato (Marko 2:23–28), kwa kuwa kuvuna siku ya sabato kumekatazwa katika Kutoka 34:21. Hata hivyo, alihalalisha huku kukosewa kwa sheria ya sabato kwa kuonyesha kifungu cha simulizi katika 1Samweli 21:1–9. Kwa uhalisia mafarisayo walimpinga kwa kufanua sheria lakini Yesu aliwajibu kwa kuzingatia kanuni zilizotokana na simulizi.

### **Mtazamo wa Kawaida unapuuza Muktadha wa Sheria Kitheolojia**

Mungu alitoa sheria katika muktadha wa agano, akisema, “Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali yangu” (Kutoka 19:5). Watu walikubali kutii masharti ya agano (24:3), na Musa alitia agano muhuri kwa damu (24:8). [uk.27] Sehemu ya muhimu katika hili ni ahadi ya Mungu ya kukaa katikati ya wana wa Israeli. Hali hii iliyumbishwa mara kadhaa katika nusu iliyofuata ya kitabu cha Kutoka (25:8; 29:45; 33:14–17; 40:34–38). Ikihusishwa na uwepo wa Mungu ni maelekezo ya kujenga madhabahu na sandaku la agano, mahali ambapo Mungu angelikaa (Kutoka 25–31, 35–40). Kwa hiyo Mambo ya Nyakati ni mwendelezo wa kawaida wa nusu inayofuata ya kitabu cha Kutoka, kwa sababu kinazeleza jinsi Wana wa Israeli watakavyoishi na Mungu katikati yao. Watamwendeaje? Na jinsi gani watakavyoshughulikia dhambi ya mtu binafsi na ya taifa mbele ya Mungu mtakatifu anayeishi katikati yao? Ni kwa namna gani wataabudu na kushirikiana na Mungu Mtakatifu aliye katikati yao? Mambo ya Walawi inatoa majibu kwa maswali haya, ikitoa maelekezo ya mambo ya kufanya katika masharti ya Agano la Musa.

Baada ya wana wa Israeli kukataa kuingia nchi ya ahadi (Hesabu. 13–14), Mungu aliruhusu kizazi kikaidi kife. Kisha akawaangoza watu kuelekea Kanani. Kabla ya kuingia, hata hivyo, aliwaalika kuingia kwenye agano wa upya. Kumbukumbu la Torati linalezea huku kufanya upya kwa agano punde kabla ya kuingia kwao katika nchi ya ahadi. Kumbukumbu la Torati linafafanua masharti ambayo Wana wa Israeli watayafuata ili waishi katika Nchi ya Ahadi na kubarikiwa.

Ni dhahiri kwamba, sheria ni jambo pacha katika agano la Musa. Kwa hiyo mambo mengi tunayoona katika agano la Musa yanahitaji kujadiliwa.

*Kwanza , Agano la Musa linahusiana kwa karibu na Wana wa Israeli kuteka na kumiliki Nchi ya Ahadi.* Agano la Musa siyo la kijigraphia na wala siyo la dunia nzima. Linatoa makatazo na mambo ya kufanya na ya kuwafanya Wana wa Israeli wamiliki Nchi Ya Ahadi na kuishi ndani yake kwa mafanikio. Mwunganiko kati ya Nchi na Agano unajonyesha ukijirudia katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati.<sup>10</sup> Mwunganiko huu kati ya Sheria na Nchi unaingia kote katika kutofautisha kuanzia kwenye kile kitiwacho sheria ya kijamii, ya kimaadhimisho, na ya kimaadili. Zaidi ya hayo, kupoteza kwao nchi, mwaka 587 K.B. kunatoa tahadhari ya kuchukua kwa jinsi ambavyo sheria inatazamwa, hasa kwa sababu sheria inafafanua masharti ya kubarikiwa *kwenye nchi*. Kwa kuongezea, wakati Israeli wanachukuliwa utumwani Babeli, walipoteza uwepo wa Mungu hekaluni (Ezek. 10). Umiliki wa nchi na uwepo wa Mungu katika madhabahu na hekaluni ni mambo mawili muhimu katika agano la Musa. Wakati wakimbizi waliporudi katika nchi [uk.28] yao, hawakuweza kurudisha mambo katika hali ya awali. Baraka zilizolezwa katika Kumbukumbu la Torati 28 hazikuonekana tena kwa uwazi - uhuru wa kisiasa, kukua kwa urchumi wa mahali pao, majeshi yao kuwa na nguvu, na mengineyo-hata hakukuwa na tamko lolote kuhusu Mungu kurudi ndani ya hekalu, tofauti na vifungu vya awali vilivyoelezea uwepo wa Mungu madhababuni (Kutoka 40:34–38) na ndani ya hekalu (1 Wafalme 8:9–10; 2 Mambo ya Nyakati. 7:1–2). Kwa hakika mambo hayakuwa kama yalivyokuwa kabla ya kwenda ukimbizini.

*Pili, Baraka katika Agano la Musa zilikuwa na masharti.* Katika Kumbukumbu la Torati, Mungu aliwafahamisha Israeli

kwamba utii wa Agano ndiyo ambao ungeleta Baraka, lakini kutotii agano kungesababisha adhabu na laana. Kumbukumbu la Torati 28 kipekee inaeleza asili hasa ya masharti ya sheria. Mistari ya 1–14 inaorodhesha Baraka kwa Waisraeli ikiwa watatii masharti ya agano (sheria ya Musa), na mistari ya 15–68 inatamka mambo ya kutisha yatakayowapata ikiwa hawatatii masharti ya agano. Pia uhusiano wa agano na nchi na sehemu ya masharti ya Baraka za agano mara nyingi yameunganishwa katika Kumbukumbu la Torati (30:15–18).

*Tatu, agano la Musa halifanyi kazi leo.* Agano Jipyä linadhihirisha ukweli kwamba agano la Musa limekoma kufanya kazi sasa. Agano Jipyä linadhihirisha kuwa Agano la Musa halina uhalali na halifanyi kazi sasa. Waembrania 8–9 inaweka wazi kwamba alikuja kuwa mpatanishi akichukua nafasi ya Agano la Kale. “Kwa kule kusema, Agano jipyä, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu.” (Waeb. 8:13). Hivyo Agano la Musa halifanyi kazi tena kama agano la halali. Huu ni mtazamo wa muhimu sana kwa mtu kuelewa sheria. Agano la Kale liliweka bayana masharti ambayo kwayo mtu anapokea Baraka chini ya agano la Kale (Agano la Musa). Ikiwa Agano la Kale halina uhalali, Je inakuwaje sheria zilizofanya agano ziwe na uhalali? Ikiwa Agano la Kale ni kuukuu, siyo kwamba hata sheria katika Agano la Kale nazo ni kuukuu?

Paulo alisema kwa kurudia rudia kwamba wakristo hawapo chini ya sheria za Agano la Kale. Kwa mfano katika Wagal 2:15–16 ameandika, “Mtu hahesabiwi haki kwa kushika sheria, bali kwa imani ndani yake Kristo Yesu.” Katika Warumi 7:4 Paulo anaeleza, “Nanyi pia mliifia sheria kwa njia ya mwili wake Kristo” Katika Wagal 3:25 akatangaza, “Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi.” Paulo anapinga kwa nguvu wakristo kurudia kushika sheria za Agano la Kale. Kama kuna kutofautisha kati ya sheria za kijamii, za maadhimisho, na za maadili ingekuwa siyo sahihi kwa Paulo kuzikataa. Zaidi ya hilo, ikiwa sheria za maadili zinatakiwa kuchukuliwa kama sheria zisizopitwa na wakati, tungetegemea Paulo angezitumia kama misingi ya maadili kwa wakristo. Hata hivyo, kama Goldingay anavyolisema, [uk.29] kwamba Paulo “haegemei sheria kama msingi wake wa mafundisho ya maadili bali kwenye asili ya Injili, uongozi wa Roho, na desturi za makanisa.”<sup>11</sup>

Inakuwaje basi, maneno ya Yesu katika Mathayo 5:17 yataelewekaje? Alisema, “Msidhani nimekuja kuitangua torati na manabii; sikuju kutangua bali kuzikamilisha.” Je Yesu na Paulo walipingana? Hapana kabisa. Kwanza, msemo “sheria na manabii” hurejea kwenye Agano Jipyä lote. Kwa hiyo katika mstari Paulo alikuwa hasemei tu Sheria za Musa tu. Na pia wala kinyume siyo kati ya “kutangua” na “kushika” lakini kati ya “kutangua” na “kutimiliza” Neno *plēroō* (“kutimiliza”) linatokea mara nyingi katika Mathayo, na maana yake ni kuleta katika “maana yake iliyokusudiwa.” Yesu hakusema sheria ni makatazo ya mielele kwa waumini wa Agano Jipyä. Kama hilo lingekuwa ndilo lengo, wakristo wa leo wangetakiwa sheria za dhabihu na za maadhimisho pamoja na sheria za maadili na hilo lingepingana kabisa na maeneo mengine ya Agano Jipyä.

Yesu alikuwa anasema hakuja kuondoa matakwa ya haki ya sheria, lakini kukamilishi matakwa yake ya haki. Kama kilele cha simulizi la wokovu, Yesu alitimiza matakwa yote ya Sheria na Manabii yaliyokuwa kivuli cha yajayo. Kwa kuongezea Yesu ndiye alikuwa mtafsiri wa mwisho wa mamlaka yaliyokuwa juu ya sheria na maana yake, kama inavyoelezwa na vifungu vingine katika Injili ya Mathayo. Yesu akazisema kwa upya baadhi ya sheria za Agano la Kale (19:18–19) lakini baadhi akaziboresha (5:31–32). Baadhi akaziongezea nguvu au mkazo (5:21–22, 27–28), na zingine alizibadili kabisa (5:33–37, 38–42, 43–47). Zingine akaziacha kabisa (Marko 7:15–19). Yesu hakuwa akisisitiza mwendelezo wa namna ya kitamaduni ya Israeli kuhusu kuzishika Sheria. Lakini pia hakusisitiza sheria zitupwe kabisa. Alikuwa akitangaza kuwa sheria ni lazima zitafsiriwe katika nuru ya kuja Kwake na mwanga wa mabadilko makuu yaliyosababishwa na Agano Jipyä.<sup>12</sup>

[uk.30]

### **Hitimisho**

Sheria imefungamanishwa na Agano la Musa, ambayo imeungana na kutegemeana na maisha ya Wana wa Israeli katika Nchi na Baraka zenye masharti zinazotegemea utii wao katika Nchi. Wakristo hawahusiani na Nchi, na wala hawana uhusiano na Baraka zenye masharti katika nchi. Pia agano la Musa ni kuukuu, likiwa limeondolewa na Agano Jipyä. Kwa hiyo sheria za Musa, sehemu ya Muhimu sana ya Agano la Kale, siyo halali tena kama sheria kwa waumini wa kizazi cha kanisa.

Kwa hiyo mtazamo wa kitamaduni au wa kawaida wa Sheria ya Musa, ambao unaigawa katika sheria ya maadili, ya kijamii na maadhimisho, unakumbana na kasoro kuu tatu zifuatazo: Haifuati mantiki na haizingatii maudhui ya kifungu, Inapuuza muktadha wa simulizi, na pia inashindwa kutambua badiliko kubwa kati ya Agano la Kale la Agano Jipyä. Kwa hiyo njia hii haikidhi kanuni ya Hemenutiki ya kutafsiri na kutumia sheria.

### **Utaratibu au Njia inayoshauriwa**

Ni utaratibu gani waaminio waufuate katika kutafsiri Sheria za Agano la Kale? Ili kwenda sawa sawa na kanuni sahihi za hemenutiki, ni lazima uwepo utaratibu ambao (a) una msimamo na unachukulia Agano la Kale lote kama Neno la Mungu, (b) hautegemei vipengele visivyo na mantiki na visivyo zingatia kifungu, (c) unaakisi uhalisia wa kihistoria na muktadha wa Sheria ya Agano la Kale ikijikita katika simulizi la vitabu vitano yya sharia, (d) unaakisi muktadha wa kitheolojia wa

sheria, na (e) uendane na mafundisho ya Agano Jipy.

Utaratibu ambao unatimiza vema vigezo hivi unajulikana kama *Kanuni ya matumizi ya maadili*. Baadhi ya makanisa ya kiinjili zinatumia kanuni hii mara zote kama njia waliyoichagua kutafsiri Agano Jipy.<sup>13</sup> Faida za utaratibu huu ni kwamba unamwezesha mwanafunzi wa Biblia asibadilike badilike anapotafsiri vifungu vya Agano la Kale. Hakuna sababu ya kuchambua sheria kwenye vipengele vile vinavyotumika na visivyotumika bila kujali mantiki.

[uk.31]

Huu si utaratibu wa kinadharia, bali ni wa vitendo na unaweza kutumiwa na wanazuoni, watu wasiosoma, na wanafunzi vile vile. Uzuri wake ni kwamba ni rahisi na ni wa kutegemeka. Udhafi wake ni kwamba utatibu huu unaweza kurahisi hata mambo yale magumu. Je kuna uwezekano wa kuboresha mfumo/utaratibu huu? Kwa hakika upo. Hata hivyo ni hatua inayofuata kutoka kwenye utaratibu wa kitamaduni/kawaida wa sheria usiofuata mantiki wa kugawa sheria katika vipengele yaani sheria za maadili, za kijamii, na sheria za maadhimisho.

Kanuni ya matumizi ya maadili, kama njia mbadala ya kutumia Sheria inahusisha hatua tano.

### **Tambua sheria husika ilikuwa na maana gani kwa wale wahusika walioandikiwa mwanzoni**

Tambua muktadha wa kihistoria na kifasihi wa sheria unayotaka kutafsiri. Je sheria imetolewa wakati wana wa Israeli wapo ng'ambo ya Jordani wakitaka kuingia Nchi ya ahadi (Kumbukumbu la Torati) au walikuwa mlima Sinai mara tu baada ya Kutoka (Kutoka na Mambo ya Walawi)? Je sheria ilitolewa baada ya tukio fulani kama mwitikio kwa tukio hilo, au sheria ilikuwa inaelezea mambo wanayotakiwa kuyazingatia baada ya kuwa wameshaingia Nchi ya Ahadi? Ni sheria zipi zingine zipo kwenye muktadha ulio karibu na sheria hiyo? Je kuna mwunganiko kati ya hizo. Je sheria hiyo inahusianaje na Agano la Kale? Je inaelezea namna watu wanavyotakiwa kumwelekeea Mungu? Au inaelezea namna watu wanavyotakiwa kuhusiana wao wao? Je inahusiana na kilimo au biashara? Je inahusiana moja kwa moja na maisha katika Nchi ya ahadi. Je sheria hii ina maana gani kwa hadhira ya Agano la Kale?

### **Tafuta tofauti kati ya Hadhira iliyoandikiwa na Waumini wa leo**

Elezea tofauti iliyopo kati ya Wakristo leo na hadhira ya Agano la Kale. Kwa mfano waumini katika kanisa wapo chini agano Jipy na siyo agano la Kale. Hivyo hawapo katika sheria za Agano la Kale. Wao si wana wa Israeli wanaojiandaa kuishi katika nchi ya ahadi, wala hawamwendei Mungu kwa sadaka za wanyama. Pia Wakristo, wanaishi chini ya serikali za kawaida na wala siyo theokrasia, kama Wana wa Israeli zamani. Kwa kuongezea wakristo hawakutani na msukosuko kutoka kwa dini za wakanani lakini kutoka falsafa zisizo za kikristo na za kidunia.

### **Tengeneza Kanuni za kawaida za maisha kwa ujumla kutoka kwenye kifungu**

Nyuma ya Sheria za Musa kwa ajili ya hadhira ya wakati ule kuna kanuni ya kawaida ya jumla kwa ajili ya maisha zisizopitwa na wakati. Kila sheria ya agano la kale kwa hadhira yake ya awali zilikuwa na maana inayohusiana na Agano la kale. Lakini maana mara zote ni pana na yenye ukweli wa kijumla, kweli ambayo inatumika kwa watu wote wa Mungu bila kujali [uk.32] wanaishi wakati gani na chini ya agano lipi. Katika hatua hii unatakiwa ujiulize, “Je kanuni ipi ya jumla ya kimaisha inaakisiwa katika sheria hii? Je kanuni ipi tunapata katika upeo mpana na inayoweza kutumika leo kutokana na sheria hii?”

Kanuni ni lazima itengenezwe kwa kutumia miongozo kadhaa: (a) Ni lazima iwe inaakisiwa kwenye kifungu, (b) Isifungwe na wakati, (c) ni lazima ikubaliane na theolojia ya maandiko yote, (d) isifungwe katika utamaduni, na (e) ni lazima iwe inafaa kwa waamini wa Agano la Kale na Agano Jipy. Kanuni za Jumla mara zote zinahusiana moja kwa moja na sifa za Mungu na Utakatifu wake, asili ya dhambi, habari ya utii, au kuhusika na watu wengine.

### **Husianisha Kanuni na Mafundisho ya Agano Jipy**

Chuja kanuni kwenye mafundisho ya Agano Jipy ukizingatia ile kanuni au sheria unayojifunza.

Baadhi ya sheria za Agano la kale, kwa mfano, zimeelezwa upya katika Agano Jipy kwa ajili ya waamini wa Agano Jipy. Wakati Agano la kale lilipoachwa sheria zake zilipoteza sifa ya kuwa sheria kwa wakristo. Ingawaje, ikiwa Agano Jipy itarudia sheria, huwa sheria ya Kristo kwa ajili ya waamini kutii. Lakini kufaa kwa mamlaka kama amri huja kutoka kwenye agano Jipy na wala siyo Agano la Kale. Kwa kuongezea Agano jipy huhalalisha Sheria ya Agano la Kale, au kwa kuiboresha, au kuipanua. Kwa mfano kwa amri zilizopo katika Kutoka 20:14 “Usizini,” kanuni ya jumla ni usafi wa ndoa na hitaji la kuwa waaminifu katika ndoa. Kadiri kanuni hii ilivyochujwa katika Agano Jipy, mafundisho ya Yesu kuhusu somo hili ni lazima yaunganishwe katika kanuni hii. Yesu akasema, “Kila mtu amtazamaye mwanaamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” (Mat. 5:28), hivyo akiongeza ukubwa wa amri hii. Aliitumia si tu kwa matendo ya uzinifu bali hata mawazo ya uzinzi. Kwa hiyo amri kwa wakristo leo ikawa, “Usizini kwa tendo au kwa wazo.” Lakini

wakristo wanapaswa kushika amri hii kwa sababu inabeba kanuni ya Biblia ya jumla ambayo inakaziwa na Agano Jipy, na wala si kwa sababu ni sheria ya Agano la Kale tu.

### **Tumia Kanuni ya Jumla iliyoboresha katika maisha leo**

Katika hatua hii kanuni ya jumla iliyopatikana katika hatua iliyopita inatumika katika eneo husika la maisha ya waamini leo. Udhahirisho wa Kanuni ya matumizi ya maadili waweza kuonekana katika Agano Jipy. Kama ilvyoonekana mapema, [uk. 33] nukuuu ya Yesu katika 1Samweli 21 kuwakosoa mafarisayo ulifuata utaratibu huo huo. Katika 1 Wakor 9:9 Paulo ananukukuu Kumb. 25:4 (“Usimfunge ng’ombe kinywa apurapo nafaka”) katika kutetea haki yake ya kupokea msaada wa vitu kutoka kwa wakorintho (1 Wakor 9:4, 11–12). Katika utaratibu wa kawaida sheria hii ya Kumbukumbu la Torati isingeonkana kama sheria ya maadili, pamoja na hayo Paulo akairejea kwa matumizi. Kwa kuwa Paulo ndiye aliyesisitiza mahali fulani kwamba wakristo hawapo chini ya sheria za Agano la Kale (Warumi. 6:14–15; 7:1–6; 1 Wakor. 9:20; Wagal. 2:15–16; 5:18; Waefeso. 2:15), hakuwa ananukuu Kumbukumbu la Torati 25:4 kama sheria ambayo ni lazima kwa Kanisa la Wakor. Badala alitumia sheria akihiusisha na hali halisi ya leo.<sup>14</sup> Mitume walirejea amri ambazo kanuni zake zinaweza kutumiwa kwa mazingira tofauti na yale ya mwanzo ya kihistoria.

Mambo ya Walawi 5:2 inatoa mfano wa namna mkristo wa leo anaweza kutumia kanuni hii ili kufanya kazi kifungu cha kisheria bila ya kuwa chini ya sheria. Mstari unasomeka hivi, “Au kama mtu akigusa kitu kilicho najisi, kama ni mzoga wa mnyama wa nyikani aliye najisi, au kama ni mzoga wa mnyama wa mfugo aliyenajisi, au kama ni mzoga wa mdudu aliye najisi, naye jambo hilo linamfichamania, akapata kuwa najisi, ndipo atakapochukua uovu wake.” Tendo linalohitajika kumsahihisha mtu aliyenajisi kutokana na sheria ya maadhisho linafafanuliwa katika mistari michache inayofuata. Hivyo mstari wa 5–6 ni lazima pia ihusishwe: “Na kama mtu ye yeyote ana hatia katika kwa namna ye yeyote katika ya hizi, ni lazima aeleze kwa namna gani alitenda dhambi na kama sadaka ya dhambi aliyoenda ni lazima apeleke kondoo jike au mbuzi kama sadaka ya dhambi na kuhani atafanya utakaso kwa dhambi yake.” Utaratibu ule wa kawaida wa kutafsiri sheria za Agano la Kale huhesabu sheria hii kama ya maadhisho tu na kwamba haina matumizi leo. Hata hivyo, njia ya kutafuta kanuni iliyojificha ndani ya sheria, mmoja aweza kutafsiri sheria hii na kutumia kifungu hiki akichukulia kama ambavyo angefanya kwa simulizi.

1) *Kifungu kilikuwa na maana gani kwa wahusika wa awali?* Muktadha wa Kitabu cha Mambo ya Walawi ulielezea jinsi wana wa Israeli walivyopaswa kuishi na Mungu wa ajabu na mtakatifu aliyeishi katikati yao. Walipaswa kumkaribia Mungu kwa namna gani? Wangeshughulikaje na dhambi na vitu najisi, katika uelewa wa Mungu aliyekuwa pamoja nao? Mistari hii ni muktadha wa hali halisi ya wakati wa sura ya 4:1–5:13 ambayo inazungumzia umuhimu wa sadaka kwa dhambi isiyokusudiwa. Mambo ya Walawi sura 4 kimsingi inahusika na viongozi, sura 5 inahusu watu wa kawaida.

Mambo ya Walawi 5:2 inafahamisha [uk.34] wana wa Israeli kwamba wakigusana na kitu kinajisi(maiti za wanyama au wanyama najisi) watakuwa ni najisi kwa habari ya maadhisho. Ni hivyo hivyo hata wakigusana na kitu kilicho najisi kwa bahati mbaya. Kuwa najisi maana yake hawawezi kumkaribia Mungu na kumwabudu. Kutakaswa (kusafishwa), walitakiwa kukiri dhambi zao na kumpletea kuhani mwanakondoo au mbuzi wa dhabihu (5:5–6). Kuhani angemtoa sadaka mnyama huyo badala yao nao wangkuwa safi tena na kuwa na uwezo wa kumkaribia Mungu na kumwabudu.

2) *Kuna tofauti gani kati ya wahusika wale wa zamani za Kale na wa siku za leo?* Wakristo hawapo chini ya Agano la Kale, na dhambi zao zimefunikwa na Kifo cha Kristo. Pia kwa sababu wana fursa ya kumkaribia Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, hawahitaji tena kuhani wa kibinadamu kuwa mpatanishi.

3) *Kanuni ya jumla ni ipi katika kifungu hiki?* Kanuni ya msingi katika mistari hii inahusika na wazo kuwa Mungu ni Mtakatifu. Anapoishi katikati ya watu wake, utakatifu wake unadai wajitenge na dhambi na vitu najisi. Wakijinajisi wanatakiwa kusafishwa kwa sadaka ya damu. Kanuni hii inajumuisha theolojia nzima ya kitabu chote cha Mambo ya Walawi na Maandiko yaliyosalia kwa ujumla. Imeelezwa kwa namna ambavyo ni jambo la kila mahali na wakati wote yaani la kuzingatiwa na wote wa Agano la Kale na Agano Jipy.

4) *Je mafundisho ya Agano Jipy yanaboresha au kuhalalisha kanuni hii?* Katika na Agano Jipy, Mungu hakai hekaluni au madhababuni; sasa anakaa ndani kwa njia ya Roho akaaye ndani ya waaminio. Uwepo wake, hata hivyo, bado unahitaji utakatifu uwepo. Anawataka wasitende dhambi na kujitenga na vitu vinajisi. Hata hivyo, Agano jipy inaelezea maana ya maneno “utakaso” na “unajisi.” “Hakuna kimwingiacho mtu kutoka nje kinachoweza kumtia mtu ‘unajisi’. Bali, kimtokacho ndicho kinachoweza kumtia mtu ‘unajisi’ ... Kimtokacho mtu ndicho kiwezacho ‘kumnajisi’ mtu. Kwa kuwa kutoka ndani ya moyo wa mtu hutoka wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ujisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Maovu yote haya hutoka ndani ya mtu na kumtia ‘unajisi’” (Marko 7:15, 20–23). Waaminio katika Agano Jipy hawatiwi unajisi kwa kugusa wanyama waliokufa. Wanatiwa unajisi kwa kuwaza mabaya na kutenda matendo ambayo ni dhambi.

Agano Jipy pia limebadili namna ambayo watu wa Mungu watashughulika na dhambi na unajisi. Badala ya kuleta kondoo au mbuzi kwa ajili ya sadaka ya upatanisho, dhambi ya mwamini zinafunikwa wakati wa wokovu kwa dhabihu ya Yesu Kristo. Kifo cha Yesu kinaosha dhambi zote na kumfanya mwamini awe safi. Kuungama dhambi, hata hivyo, ni muhimu

katika Agano Jipy (1 Yohana 1:9), kama ilivyokuwa katika Agano la Kale. [uk.35] Hivyo kanuni ya jumla kwa waaminio wote kwa Agano Jipy siku hizi ingekuwa, “Epuka matendo ya dhambi na mawazo mabaya kwa sababu Mungu Mtakatifu anaishi ndani yako. Ukitenda tendo ambalo ni dhambi au ukiwaza mawazo mabaya, basi ungama dhambi hiyo upate msamaha kwa njia ya mauti ya Kristo.”

5) *Wakristo leo wnawezaje kutumia kanuni hii ya jumla iliyoboreshwa kwa maisha yao?* Kuna uwezekana mwingi au kuna njia nyingi; lakini mfano moja wa wazi ni picha za ngono kwenye mtandao. Wakristo wengi wanaweza kirahisi kupata habari au picha za ngono katika maeneo yao ya usiri manyumbani au vyumba vya bweni. Kifungu hiki kinasema utakatifu wa Mungu anayekaa ndani ya waamini unahitaji wale wanaishi maisha matakatif. Kutazama picha za ngono kwa wazi kabisa inaangukia katika kipengele cha mambo ambayo Agano Jipy linasema ni unajisi. Tendo hilo hukiuka utakatifu wa Mungu na huzuia uwezekano wa mtu kuwa na ushirika na Mungu na kumwabudu. Kwa hiyo waumini ni lazima wakae mbali na picha za ngono za mtandaoni, wakitambua kuwa inawafanya wawe najisi kiroho na kuukosea utakatifu wa Mungu na kuharibu ushirika na Mungu. Hata hivyo, mtu akianguka katika dhambi hii ni lazima aungame, na kuititia mauti ya Kristo atasamehewa na ushirika na Mungu utarejea.

### **Hitimisho**

Njia au Utaratibu wa kawaida ya kugawa sheria ya Musa katika mafungu ya sheria za maadili, za kijamii, na za kimaadhimisho hukiuka kanuni ya hemenutiki sahihi, kwa kuwa haina msimamo na haifuati mantiki na agano la Kale haitupi vidokezo kuhusu hizo tofauti. Kanuni au utaratibu huu una makosa mawili yafuatayo. Kwa upande mmoja huacha kabisa sheria zote za kijamii na za kimaadhimisho. Kwa upande mwingine hutumia sheria za maadili moja kwa moja katika kipindi hiki. Kwa kuongeza, mtazamo huu wa kawaida una tabia ya kupuuza muktadha wa simulizi na muktadha wa agano la Kale kama mafundisho halali.

Kanuni ya matumizi ya maadili, njia mbadala, inatafuta kanuni ifaayao kwa wote iliyo halali kwa Agno la Kale na inayofaa kwa matumizi kwa waamini wa Agano Jipy leo. Utaratibu huu haubadiliki badiliki kama ule wa kawaida, na unazingatia sana kanuni bora za Hemenutiki. Inamruhusu mwumini kuona maandiko yote kuwa, “yanafaa kwa mafundisho, kuonya na kuadibisha katika haki” (2 Tim. 3:16).

### **Rejea**

a J. Daniel Hays ni Associate Professor Mafunzo ya Kibiblia na Theolojia, Ouachita Baptist University, Arkadelphia, Arkansas.

<sup>1</sup> Mpaka itakapoelezwa vinginevyo, Nukuu zote zimechukuliwa kwenye New International Version.

<sup>2</sup> Christopher J. H. Wright anashauri vipengele vitano: jinai, kijamii, familia, potoshaji, na kusaidiana (*Jicho kwa jicho; Nafasi ya maadili ya Agano Jipy Leo*. [Downers Grove, IL: InterVarsity, 1983], 152-59). Wright hawekei maanani yeoyote kati ya vipenge hivi vya kimaadili kwa watu wote.

<sup>3</sup> Kwa kutumia namna hii ya kutofautisha kama mwongozo kwa ajili ya maadili inaturudisha nyuma kwa John Calvin. Anatofautisha kati ya maadili na maadhimisho, akihoji kwamba wakati injili imeziacha sheria za maadhimisho, kwa upande mwingine sheria za maadili zinatumika kama sheria zinaendelea kuwa sheria kwa wakristo. (*Institutes of the Christian Religion*, trans. Henry Beveridge [reprint, Grand Rapids: Eerdmans, 1975], 2.7-8). Kwa utetezi juu ya mtazamo huu tazama Willem A. VanGemeren, Sheria ni ukamilifu wa haki katika Kristo Yesu; Mtazamo wa urejeshaji, Kwa ajili ya Utetezi wa mtazamo huu angalia Willem A. VanGemeren, Sheria ni utimilifu wa Haki katika Kristo Yesu: Mtazamo Uliorekebishwa, Katika Sheria, *Injili, na ukristo wa siku za leo*. ed. Wayne C. Strickland (Grand Rapids: Zondervan, 1993), 1358.

<sup>4</sup> Wale wengine wa Kiinjili hawakubaliani na mtazamo /utaratibu huu wa kawaida pia. Kwa mfano, tazama, David Dorsey, Sheria ya Musa na Wakristo: Kukubaliana isivyo sawa sawa, *Jarida la Jamii ya Theolojia ya Kiinjili* 34 (1991): 321-34.

<sup>5</sup> Kutokuwa na mantiki kati ya sheria ya maadili na sheria za kijamii inatokana na mpangilio wa maandiko katika Mambo ya Walawi. Baada tu ya amri ya Upendo kwa jirani linafuata katazo la kuchanganya mbegu wakati wa kupanda; kauli mbiu ya utakatifu huja kabla ya sheria juu ya watoto waasi (19:18-19; 20:79) (Gordon J. Wenham, *Kitabu cha Mambo ya Walawi*, New International Commentary on the Old Testament [Grand Rapids: Eerdmans, 1979], 34).

<sup>6</sup> Ibid., 32.

<sup>7</sup> Sheria nyingine ambayo ni ngumu kuigawa kwa kufuata mfumo huu ipo katika Hesabu 5:11-31. Kifungu hiki kinaelezea jinsi kuhani anavyomjaribu mwanamke aliyetuhumiwa kwa uzinzi. Kwa hakika uzinzi ni suala la kimaadili. Je sheria hii

itakuwa ya nyakati zote na kutumika hata leo? Je waliothumiwa kwa uzinzi wajaribiwe Amerika kwa kufuata uratibu ulioelezwa katika kifungu hiki? Ili kujua hatia au haki yake, kuhani atampatia maji ya uchungu ayanywe. Akiugua basi alikuwa na hatia. Ikiwa hataaugua basi alikuwa hana hatia. Hili lifanyiwe kazi leo kwa utaratibu huu? Kwa hakika hapana. Kwa upande mwingine, kama haifanyiki hivi, ina maana sheria ya maadili, si jambo la kimaadili?

<sup>8</sup> Kwa mfano Amri kumi zimeorodheshwa katika Kutoka 20:1-17, lakini simulizi hilo likaendelea katika mtiririko uliokuwepo kabla katika mstari wa 18, ambao unasomeka, Watu wote wakaona umeme na ngurumo na sauti ya baragumu, na ule mlima kutoka moshi; na watu walipoona hayo wakatetemeka, wakasimama mbali. Vile vile Mungu ametoa amri nyingi kwa Waisraeli katika Kutoka 21-23, lakini hata hizi ni sehemu ya simulizi, kwa sababu ni sehemu ya mjadala kati ya Mungu na Wana wa Israeli. Watu waliitikia sheria aliyowasilisha Mungu kwa kusema, Maneno yote aliyoyanena Bwana tutayatenda (24:3).

<sup>9</sup> “Kisha Musa akachukua” (Mambo ya Walawi. 8:10), “Kisha akapeleka” (8:14), “Kisha Musa akasema” (8:31), “Siku ya nane Musa akafundisha” (9:1), “Kwa hiyo Haruni akaenda kwenye madhabahu” (9:8), “Hivyo moto ukaja kutoka kwa Bwana na kuwateketeza” (10:2), “Bwana akanena na Musa baada ya kifo cha wana wawili wa Haruni” (16:1).

<sup>10</sup> Neno la kiebrania lenye maana ya “nchi” limeandikwa mara mia mbili katika Kumbukumbu la Torati. Vifungu vilivyochaguliwa vinavyounganisha moja na moja masharti ya agano na maisha katika nchi ni pamoja na 4:1, 5, 14, 40; 5:16; 6:1, 18, 20-25; 8:1; 11:8; 12:1; 15:4-5; 26:1-2; 27:1-3; 30:5, 17-18; na 31:13.

<sup>11</sup> John Goldingay, *Mifano ya kutafsiri Maandiko* (Grand Rapids: Eerdmans, 1995), 103.

<sup>12</sup> Kwa mitazamo inayofanana kuhusu Mathayo 5:17-47 tazama D. A. Carson, “Mathayo,” katika *The Expositor’s Bible Commentary* (Grand Rapids: Zondervan, 1984), 8:142-44; R. T. France, *Mathayo: Mwinjilisti na Mwalimu* (Grand Rapids: Zondervan, 1989), 194-95; na Donald Hagner, Matthew 1-13, *Word Biblical Commentary* (Dallas: Word, 1993), 104-6.

<sup>13</sup> Tazama Roy B. Zuck, *Tafsiri ya Msingi ya Biblia* (Wheaton, IL: Victor, 1991), 286-89; Goldingay, *Mifano ya Jinsi ya Kutafsiri Maandiko*, 92; na Robert Chisholm, *Kutoka kwenye Uchambuzi hadi Uelewa: Mwonozo wa Kivitendo wa Kutumia Kiebrania cha Biblia* (Grand Rapids: Baker, 1998), 223-24, 255. Wright anatumia maneno “kielelezobora” badala ya (“Kanuni ya matumizi ya maadili) kanuni yenye hatua nne”, lakini anaelezeza utaratibu huo huo wa msingi (*Jicho kwa Jicho*, 16263). William Klein, Craig Blomberg, na Robert Hubbard Jr. anamnukuu Wright na kueleza kuwa sheria inafanya kazi kama mwongozo (kanuni bora) ya maadili yasiyopitwa na wakati, nidhamu, na kanuni za kitheolojia, na kwa hiyo anayetafsiri ni lazima ajitahidi kugundua kweli isiyopitwa na wakati iliyojificha ndani ya ngozi ya utamaduni (*Utangulizi wa wa Jinsi ya kutafsiri Biblia* [Dallas: Word, 1993], 279). Mtazamo unaofanana na huu unaonekana kwa Wenham, *Kitabu cha Mambo ya Walawi*, 3335; na John E. Hartley, *Mambo ya Walawi*, *Word Biblical Commentary* (Dallas: Word, 1992), lxxiii.

<sup>14</sup> Gordon D. Fee, *Waraka wa Kwanza kwa Wakorintho*, New International Commentary on the New Testament (Grand Rapids: Eerdmans, 1987), 408. Tazama pia mjadala kuhusu mstari huu na Zuck, *Tafsiri ya Msingi ya Biblia*, 263-65.

## **NYONGEZA D**

Jarida la Kimataifa la Frontier Missiology 31:1 Spring 2014: 5-14

[p.5] ***Utamaduni na Dhamiri: Kweli za Biblia na Tofauti za Tamaduni, T. Wayne Dye***

### ***Jambo***

Wakati kuna kutokupatana kwa tamaduni za maeneo juu ya yapi ni maadili sahihi na yapi siyo sahihi wamishenari kila mahali wamekuwa wakikutana na mambo hayo na watu kule nyumbani nao hukumbana na hali hiyo ya kutokubaliana kutokana na maswali yanayojitezea. Maswali hayo kuhusu mambo ya kimaadili husababisha kutoelewana na msuguano, na mara kadhaa huchangia dai la jamii kusema mambo yahusuyo maadili ni jambo la mtu binafsi vile anavyolichukulia.

Kama mwanamke, Sally, na mimi tumekumbana na mambo kwa miaka minge, na tumefika mahali sasa tunaamini kuna majibu ya msingi ya maandiko yanayorahisisha mengi ya migogoro hii. Katika chapisho lake katika jambo hili la IJFM (uk. 15-25) “Toafauti za tamaduni katika Dhamiri: Sehemu ya Mpango wa Mungu,” Sally ameandika namna ambavyo utamaduni na dhamiri zinaweza kuathiri namna mtu anavyohitaji kumtii Mungu. Chapisho hilo hueleza kwa nini wakristo waliokomaa vema hawatii amri za Biblia kwa namna inayofanana.

Kwa miaka tulidhani kuna njia moja tu ya kutii amri za Mungu—njia ambayo tuliyofundishwa kwa mara ya kwanza.<sup>1</sup> Kama watafsiri wa Biblia ni lazima tuwape watu Biblia nzima. Wakisha kuwa nayo, kwa hakika watatii maana wazi ya maneno yake kwa kuishi kama sisi tulivyojaribu kuishi. Ingawa wameshenari na walimu wa chuo hufundisha njia yao kana kwamba ndiyo njia pekee ya kweli (na kutegemea kila mtu atii amri kwa njia waliyofuata wao), kuna tofauti za kuzingatia katika namna amri zinatakiwa kufuatwa.

Tatizo moja ni kwamba sisi watu wa Magharibi hatutii amri zote kwa kufuata namna moja. Tunachukua maandiko mengine kama yalivyo na kuyatii kwa uangalifu sana, wakati tukipuuza vifungu vingine. Kwa uhalisia, “hatusalimiani kwa busu takatifu” (Warumi 16:16, NIV<sup>2</sup>). Hatunywi mvinyo ili kusaidia mfumo wa uyeyushaji wa chakula tumboni (1 Timotheo 5:23). Hatuombi kila siku saa 9:00 alasiri, “saa ya kuomba” (Matendo 3:1). Hatuwaoshi wengine miguu, isipokuwa mara chache na katika siku maalumu (Yohana 13:14). Mke wangu akiwa Marekani hafuniki kichwa akiwa kanisani (1 Wakor 11:2-16).<sup>3</sup>

Kwa hakika kuna amri nyingi sana za namna hii katika agano Jipyा.<sup>4</sup>

[uk.6] “Huu utii wa kuchagua baadhi ya amri” siyo kwamba ni sifa ya makanisa Ya Amerika peke yake. Wakristo wote tulioikutana nao ulimwenguni kote wanachagua kwa kiasi fulani. Hili linazaa swalii: Tunafuata kanuni ya Biblia au tunafanya kosa?

Huko kukosekana kwa msimamo kunaonekana zaidi tunapotazama Agano la Kale ambalo ni Biblia ya Kanisa la Agano Jipyा. Wakati Yesu na wanafunzi waliponukuu maandiko mara zote yalikuwa ni Agano la Kale. Agano Jipyा linaeleza kwa wazi kwamba Agano la Kale linatakiwa kutiwa. 2 Timotheo 3:16-17 inasema:

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema. Wakati Paulo anaandika hivi kuhusu Agano la Kale alikuwa anakubaliana na Agano la Kale peke yake. Amri zake zimeelezwa vizuri, na umuhimu wa kuzitii umesisitizwa sana. Kwa mfano, Kumbukumbu 10:12-13 inasema:

Na sasa, Israeli, Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda, na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote; kuzishika amri za Bwana na sheria zake, ninazokuamuru leo, upate uheri?

Kuna vifungu vingi vya namna hiyo. Na bado tunaporudi kwenye vitabu vitano vya Musa tunapata amri ambazo ni kwa ajili ya watu wote na kwa nyakati zote na kwa watu wote zikiwa zimechanganywa na amri ambazo watu wachache wanazifuata. Mambo ya Walawi 19 inatupa baadhi ya mifano. Mstari wa 13 unasema, “Usimtapeli wala kumdhulumu jirani yako.” Kwa hakika hilo linatakiwa kufuatwa leo. Mstari unaendelea kusema, “Ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi..” Hakuna shirika la kikristo linalotii amri hiyo. Mstari wa 18 unasema, “... mpende jirani yako kama nafsi yako,” kwa hakika ni amri kwa ajili ya wote. Mstari unaofuata, “Usiwaache wanyama wako wa mfugo wakazaana kwa namna mbalimbali.... Wala usivae mwilini mwako nguo ya namna mbili zilizochanganywa pamoja.” Je sisi wamishenari wa nchi za tropiki tutaisije bila nguo mchanganyiko za pamba na polista?

Mstari wa 26 unasema, “Msile kitu cho chote pamoja na damu yake; wala msifanye kuloga, wala kutumia utambuzi.” Tunahitaji kufundisha rafiki zetu wenye tabia hizo. Lakini itakuwaje wakiendelea na mstari unaofuata?

Unasema, “Msinyoe denge pembe za vichwani, wala msiharibu pembe za ndevu zenu.” Ni mara chache wamishenari wa kikristo wanatii amri hiyo. Kuna amri nyingi kama hizo, kuwabakizia mavuno maskini waokotao mabaki baada ya kuvuna, kukopesha bila riba kabisa. Kupumzisha ardhi, kumwuzia tena mwenye shamba baada ya miaka hamsini kupita; hatufuati amri hizi kama zilivyo kwa uhalisia wake leo.

***Kifungu funguo juu ya asili na utii wa Kweli***

Sasa tumefikia hatua ya kuamini mtazamo wa wakristo katika nyakati mbalimbali ulikuwa sawa kwa ajili yao na kwa nyakati hizo. Wakristo wa madhehebu mbalimbali wamesoma maandiko na wameyatafsiri kwa mtazamo wao na amri wakazitafsiri kwa namna ambayo ni sawa kwa tamaduni zao. Huu uelewa wa namna hii ulikuwa mzuri kwa wale ambao wana utamaduni mmoja. Inafeli wakati watu wa tamaduni mbalimbali wanapoingiliana. Tatizo la kimisheni ni kwa sababu hatuelewi misingi ya maamuzi ya wenyeji., na sisi mara nyingi tunatumia mafundisho ya Biblia tukidhani kwamba waamini katika tamaduni zingine ni kama sisi. Katika kurasa zinazofuata nitasaidia ili sisi tuone namna madhehebu ya kiinjilisti tunavyotafsiri Biblia kwa kufuata hali za tamaduni zetu. Tutakopofahamu mchakato, tunaweza tukaweka wazi ili kwamba wakristo katika tamaduni zingine na wasiojihusisha na tamaduni moja kwa moja waweze kutumia katika mazingira yao.

### **Je Watu wanaweza kutii amri moja kwa namna tofauti tofauti?**

Kuna vifungu viwili katika nyaraka. Paulo alionyesha kuwa wakristo waaminifu kutoka kwenye tamaduni mbalimbali wanaweza kufanya mambo tofauti kabisu. 1 Wakor 8–10 na Warumi 14 zinahitaji umakini katika kujifunza kwa ajili ya kujua jinsi ya kuwa na mwingiliano sahihi na wageni leo.

Korintho ilikuwa ni kitovu cha ibada ya sanamu. Waabuduo katika muktadha huu walitoa sadaka za wanyama, halafu wakashiriki kula nyama, Nyama zilizobaki ziliikuwa zikiuzwa au kwenye mahakama ya hekalu au sokoni. Sasa mtu wa kawaida katika jamii isiyo ya viwanda wasingeweza nyama. Kwa sababu kila siku sadaka nyingi zinatolewa, na kutoa sadaka za nyama kwa miungu ikajibu hitaji lao la nyama.

Hali hii ikawa tatizo kwa wakristo ambao walitaka kula nyama ambazo hazijahusisha na ibada ya sanamu. Waumini waliokomaa wa mataifa (au waamini kutoka kwa Wana wa Israeli) wakashauri kuwa kula hizo nyama haina shida yeoyote., hususan wale waliotoka katika mazingira ya ibada ya sanamu. Walijisikia hatia kwa kushiriki kula hizo nyama.. Kwa sababu hiyo; waamini katika Korintho walitaka aongelee jambo hilo. Jibu lake lilikuwa gumu na likafuatwa na mfumo wa mjadala ambao hautumiwi leo, kwa hiyo hatua katika kufikiri kwake wakati mwingine zinakosekana.

### **Sanamu siyo halisi kwa hiyo kula nyama ni Sawa**

Paulo akaanza kuongelea upendo kwenye maarifa ya kawaida, kisha akaendelea kusema kwamba sanamu siyo viumbe vyenye uhai.

Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa [uk.7] "Hakuna Mungu ila mmoja tu." Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama dumiani, kama vile walivyo miungu mingi na mabwana wengi; lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo. (1 Wakor 8:4-6)

Paulo alikubaliana kwamba hili limewapa uhuru wale wenye "imani yenye nguvu," wale waliokuwa wana mtazamo wa kikristo wa kilimwengu katika jambo hili. Hata akasema katika muhutasari wa barua yake kwamba vileni vyote viletwayyo sokoni au vinavyotolewa na mtu asiyeamini. Ni wazo kwa kutazama jambo hili kwamba hakuna kitu kuhusu kile chakula, hakuna kitu ambacho kingemdhuru mkristo aliokomaa.

Lakini chakula hakituhudhurishi mbele za Mungu; maana, tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila, hatuongezewi kitu. (1 Wakor 8:8) Kila kitu kiuzwacho sokoni kuleni, bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri; maana, Dunia ni mali ya Bwana na vyote vijazavyo. Na mtu asiyeamini akiwaalika, nanyi mnataka kwenda, kuleni kila kitu kiwekwachoo mbele yenu bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri. (1 Wakor 10:25-27)

### **Ikiwa Mtu Anaamini Sanamu Ni Halisi Asile**

Kuna jambo lingine la kuzingatia, ingawa. Paulo alisema ya kwamba wale wenye "dhamiri dhaifu", hawana ufahamu wa Biblia kuhusu sanamu wanatenda dhambi wakila nyama zilizotolewa sadaka kwa sanamu.

Bali ujuzi huu haumo ndani ya watu wote; ila wengine kwa kuizoelea ile sanamu hata sasa hula kana kwamba ni kitu kilichotolewa sadaka kwa sanamu; na dhamiri zao, kwa kuwa dhaifu, hunajisika. Lakini chakula hakituhudhurishi mbele za Mungu; maana, tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila, hatuongezewi kitu. Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! Dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikuwa kwa ajili yake. Hivyo, mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo.

Kwa hiyo, chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisipe nikamkwaza ndugu yangu. (1 Wakor 8:7-13)

Paulo aliona mgogoro huu kama wa muhimu sana kuzingatiwa wakristo waliokomaa wawe macho kwa kuwa wanatazamwa na matendo yanaweza kutafsiriwa tofauti. Kuwa mashahidi katika tamaduni mchanganyiko lazima izingatie mema ya wengine, na hii inahusisha kuepuwa kila tendo ambalo litawapeleke wa kufanya dhambi kama watafanya uchaguzi bila kupambanua vizuri.

"vitu vyote ni halali," bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo. Mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya mwenzake. Lakini mtu akiwaambia, Kitu hiki kimetolewa kiwe sadaka, msile, kwa ajili yake yeye aliyeonesha, na kwa ajili ya dhamiri. Nasema, dhamiri, lakini si yako, bali ya yule mwingine. Maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine? Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la

Mungu, vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa. (1 Wakor 10: 23, 28-29, 31-33)

### **Siyo Njia Moja ya Kweli bali ni Mbili**

Hapo kuna fundisho la ajabu. Jambo maalumu (kula nyama iliyotolewa kwa sanamu) ni sawa na hata imetiwa moyo kwa wale wenye mtazamo wa aina moja na wenye aina fulani ya kujua mema na mabaya. Kwa watu wenye mtazamo tofauti wa mambo ya kidunia, ingawaje, hilo jambo ni dhambi na linaweza kuharibu imani yao katika Kristo.

Zaidi ya hayo hakuna mwenye haki ya kuhukumu matendo ya wengine.

Maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine? Ikiwa mimi natumia sehemu yangu kwa shukrani, kwa nini nitukanwe, kwa ajili ya kitu nikishukuriacho? (1 Wakor 10:29b-30)

Kupata uhakika, waaminio hawapaswi kuwa “kikwazo” kwa kumfanya mwingine afanye jambo lisilo sahihi kwake. Na bado hilo linazidi kusisitiza ukweli huu; kilicho sahihi kwa mtu moja inaweza ikawa siyo sahihi kwa mwingine. Hii ndiyo maana tunaweza kuwaumiza watu wengine kwa kufanya jambo kwa nia njema. Ili kuona hili linawezekanaje, tunahitaji kuangalia kwa nini inaweza kuwa dhambi kwa baadhi ya watu. 1 Wakor 10:18-21 inatoa dokezo.

Waangalieni hao Waisraeli walivyokuwa kwa jinsi ya mwili; wale wazilao dhabihu, je! Hawana shirika na madhabahu? Basi niseme nini? Ya kwamba kile kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu? Au ya kwamba sanamu ni kitu? Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo sadaka wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani.

Kwa wayahudi na wapagani wa Mashariki ya kati utamaduni wa siku zile ni kwamba mtu anaabudu kwa kula chakula kilichotolewa sadaka. Wayahudi na mataifa walifanya ibada kwa njia moja ya kula dhabihu—lakini wanayemwabudu alikuwa tofauti. Wakati Mataifa wanaabudu sanamu walikuwa wakifanya dhambi kwa kuwa wanaabudu kitu tofauti na Mungu wa Kweli. Shetani na mapepo yake ndiyo wanaofaidi na ibada hizo za uasi.

Na bado Paulo anaeleza wazi kwamba matendo ya wakorintho wakati wanatoa sadaka kwa sanamu [uk.8] hayana maana kwao kwa sababu sanamu siyo Mungu hata kidogo. Kama hii na sehemu nyingine ya Biblia inavyositisita, sanamu siyo kitu bali mti mfu, au jiwe au dhahabu. Ni ile nia ya ndani ya anayeabudu infanya tendo analofanya liwe kuabudu. Kuabudu ni swala la kumaanisha. Ni tendo la kutoa heshima kwa uungu. Mtu asiyeamini kuwa Mungu yupo akiimba wimbo wa kuabudu haabudu Mungu hata kama mkristo aliyesimama anayeimba wimbo huo huo pembeni yake anaabudu. Watu wanaoamini kuwa sanamu ni mungu wakila nyama zilizotolewa kwa sanamu wanaabudu sanamu. Hata hivyo, wakijua sanamu siyo kitu ila mapambo tu. Kamwe hawataabudu kwa sababu wanajua hakuna mungu hapa wa kumwabudu. Wakila nyama hawatoi sadaka; wanakula tu kawaida.

Tumetumia muda katika jambo hilo kwa sababu ina matumizi ya ajabu. Waumini wa Korintho ni kipimo cha maadili ya kikristo yafaayo kwa tamaduni zote. Kwa kiwango fulani kila tendo la mtu linalezea uhusiano wake na Mungu na amri zake kwamba anazitii au hazitii; kwa hiyo ni maana yake ya kimaadili na kiroho. Watu wenye mtazamo wa kilimwengu waweza kumtii Mungu kwa matendo yao, ikiwa hawatendi kinyume na amri za Mungu. Mtu mwingine mwenye mtazamo mwingine anaweza akawa anamkosea Mungu akifanya kinachofanana na alichofanya yule mwingine kwa sababu katika nia zao kuna tofauti kubwa kati yao.

Angalia kwamba katika kisa cha Paulo ni wale wakristo waliokoma zaidi ndio walio huru kula nyama iliyotolewa sadaka. Tunatambua kwamba Mungu ni mvumilivu kwa waongofu wapya, lakini wanapokua Mungu anawapa njia nyingi na nzuri zaidi za kutii. Ni lazima tutarajie huruma za Mungu kwa waongofu wapya kuwapa maelezo ya kifungu hiki, lakini katika hali hii wale waumini wapya ambao bado wanaamini sanamu kwamba ni hai wana mipaka mingi zaidi kwa kile wanachowenza kufanya. Wale wakristo waliokoma zaidi ambao hawaamini sanamu wana uhuru mkubwa zaidi.<sup>5</sup> Warumi 14 inatoa mfano wa jumla zaidi.

### **Kufanya vizuri ukiwa Roma**

Kanisa la kwanza kule Roma ni lazima liwe na tawsira ya utamaduni mchanganyiko wa Jiji lenyewe. Wayahudi na Wakristo wa mataifa walitoka katika maeneo mbalimbali ya utawala. Walikuwa wakijaribu kwenda nao lakini kwa njia tofauti walikuwa wakiishi. Baadhi ya wakristo walikuwa mboga tu, yawezezana ni ili waepuke kula nyama zilizotolewa kwa sanamu. Wengine walikula kila kitu. Baadhi waliishi wakishika siku takatifu ya Bwana, wengine hapana. Jibu la Paulo ukifuata baadhi ya sababu au fikra ambazo pia alizitoa kwa Wakor.

Yeye aliye dhaifu wa imani, mkaribisheni, walakini msimhukumu mawazo yake. Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu hula mboga. Yeye alaye asimdhara huyo asiyekula, wala yeye asiyekula asimhukumu huyo alaye; kwa maana Mungu amemkubali. Wewe u nani unayemhukumu mtumishi wa mwingine? Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka. Naam, atasimamishwa, kwa kuwa Bwana aweza kumsimamisha. Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku, mwingine aona siku zote kuwa sawasawa. Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe. (Warumi 14:1-5)

### **Kila mtu na afanye kile ambacho anahakika ni Mungu anataka Afanye**

Kila mwamini ni lazima afuate kile anachofiliki kwamba ni sahihi, akiwa “ameshawishika sana katika ufahamu wake.” Ni lazima afanye hivyo bila ya kuhukumu wengine, siyo kuwadharau au kuwahukumu kwa kuwa na ushawishi tofauti. Hata

watu hao ni watumishi wa Mungu. Hata hao watu wengine ni watumishi wa Mungu pia, na ni maana ya matendo yao kama udhihirisho wa uhusiano wao na Mungu ndiyo wenye maana. Katika hali hiyo, "...Bwana aweza kuwafanya [wao] wasimame." Warumi14, mstari wa 6 hadi wa 9 unafafanua wazo hili.

Yeye aadhimishaye siku, huiadhimisha kwa Bwana; naye alaye, hula kwa Bwana, kwa maana amshukuru Mungu; tena asiyekula, hali kwa Bwana, naye pia amshukuru Mungu. Kwa sababu hakuna mtu mionganini mwetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake. Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, au kama tukifa, twafa kwa Bwana. Basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana. Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia. (Warumi 14:6-9)

Kwa maneno mengine, kila mmoja wetu yupo kwenye uhusiano na Mungu muda wote; hatupo peke yetu kamwe. Yeye ni "Bwana" wetu, ni mkuu wetu, ni ameri jeshi wetu, yeye aliye na haki ya kutuambia la kufanya katika kila eneo la maisha yetu. Kila tendo lina upana huu wa mahusiano, na kwa msingi huu (na siyo mwingine) jema na baya hufahamika. Paulo akaendelea kusema, chakula tulacho haina umhimu wake kama cheneyewe. Ikiwa, pengine, kuna mtu anaamini hatakiwi kula chakula fulani akila hicho chakula atakuwa anafanya dhambi kwa sababu atakuwa anakwenda kinyume na ufahamu wake kuhusu uelewa wake kwa habari ya mapenzi ya Mungu.

Najua, tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake, lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi.... Ile imani uliyo nayo uwe nayo nafsi mwako mbele za Mungu. Heri mtu yule asiyejihukumu nafsi yake katika neno lile analolikubali. Lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia, [uk.9] kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi. (Warumi 14:14, 22-23)

### **Usishawishi wengine kufanya ambacho siyo sahihi kwoo.**

Paulo aliongeza kusema kuhusu namna tunavyoingiliana na watu walio na mtazamo tofauti kuhusu kipi ni sahihi. Tunapaswa kuwa makini tuisiwahukumu wengine, "Basi ni hivyo, kila mtu mionganini mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu." (Warumi 14:12). Wakati huo huo, Hatutakiwi kufanya chochote kitakachowakosesha wengine lakini siyo sisi.

Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharaa ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Basi tusizidi kuhukumiana, bali afadhalii toeni hukumu hii, mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumwangusha. Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. Basi, huo wema wenu usitajwe kwa ubaya. Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu. Kwa kuwa yeye amtumikiaye Kristo katika mambo hayo humpendeza Mungu, tena hukubaliwa na wanadamu. Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana. Kwa ajili ya chakula usihiaribu kazi ya Mungu. Kweli, vyote ni safi; bali ni vibaya kwa mtu alaye na kujikwaza. Ni vyema kutokula nyama wala kunywa divai wala kutenda neno lo lote ambalo kwa hilo ndugu yako hukwazwa. (Warumi 14:10, 13, 15-21)

Kama wakristo wote wanetakiwa kutenda kwa namna inayofanana kuhusu kila ambacho ni jema na kuwa na utamaduni moja kwa wote tusingekuwa na tatizo hilo. Ingekuwa vigumu kuwafanya wengine kuiga na kujikwaza kwa kuwa na tabia ambayo inakubalika kwa wengine katika hali inayofanana. Jambo kubwa analowasilisha Paulo ni kwamba kuna tofauti zinazokubalika za kitabia katika hali fulani. Jambo la kuepuka kuwapotosha wengine kwa kutumia tofauti hizo.

Hoja za Paulo zinaonyesha kuwa na msimamo katika kufanya huduma pamoja na mataifa. Mungu anataka watii amri hizo hizo; hata hivyo, kwa namna fulani lakini kwa njia ya kuzingatia umuhimu utii huu, ni lazima ufanyike kwa namna tofauti kwa watu tofauti. Hii itakuwaje bila kuwa na machafuko? Kile ambacho kanuni za kibiblia kinatoa kutokana na tofauti hizi katika mipaka ya amri za Mungu kwa ajili ya watu wote mahali pote? Katika sehemu inayofuata, Nitajaribu kutengeneza kanuni hizo.

### **Jinsi ya kumtii Mungu katika kila utamaduni.**

Ikitumika pamoja kanuni za msingi nne zilizopo hapo chini zinaweza kusimamia mamlaka kamili ya Biblia na umuhimu wa tofauti za kitamaduni katika kutambua namna amri iliyotolewa inavyofanya kazi. Kanuni hizi nne inatupa hatua tatu za kutumia kifungu.

### **Kanuni ya 1. Maandiko yote, Maagano yote la Kale na Jipy, yana mamlaka juu ya watu wote, kwa kila umri na utamaduni.**

Vifungu vyote ni kwa faida yetu. Hakuna amri zinazotakiwa kuchukuliwa kirahisi; hakuna mifano inayotakiwa kupuuzwa.. Andiko ni zaidi ya mwongozo wa kutenda jambo; ni "Ni kitabu cha aliyetuumba" kituelekeze namna ya kuishi.<sup>6</sup>

### **Kanuni ya 2. Ingawa maandiko yameandikwa kwa ajili ya kila mtu, hayakuwa kwa kila mtu.**

Mwandishi wa kifungu cha Maandiko alikuwa akiwasilisha ujumbe maalumu kwa wale aliokuwa anawaandikia wakati ule na ni ujumbe huo ulio na maana ya msingi ya kifungu. Wengine wote wapo nje ya mlango na ni lazima watafute Mungu anasema nini na wao leo kupitia kile alichokuwa anawaambia wale wahusika wa awali.

Vifungu viwili nya Agano Jipy, vinavyoelezea namna waamini wa leo wanavyotakiwa kujifunza kutoka kwenye Agano la Kale, vitasaidia kufafanua kanuni hii. 1 Wakor 10:6-11 inatuambia kuhusu Agano la Kale kwamba matukio ya Agano la Kale "yaliiyowapata wao ili kutusaidia sisi mioyo yetu isielekee maovu waliyofanya wao." Waebrania 11 inaorodhesha

mifano mingi ya Agano la Kale tunayotakiwa kufuata. Waamini wa siku za leo wanatakiwa kuamua ikiwa mfano ni ule tunaotakiwa kuuepuka au ni ule wa kufuata kwa kuangalia kile alichofanya mtu katika maandiko na Biblia inasema nini kuhusu alichofanya. Baadaye tunatakiwa kutafuta matendo hayo yana maana gani kwetu leo katika mazingira yetu. Inasaidia kuangalia vile kanisa la kwanza lilivyotafsiri Agano la Kale, kwa sababu makanisa tofauti tofauti ya karne ya kwanza hayakuwa katika mazingira yanayofanana. Walikuwa maskini au matajiri, walikuwa na tamaduni tofauti tofauti, walikuwa katika mateso makali au ya kawaida, na vile vile walikuwa tofauti katika mambo mengine.

### **Kanuni ya 3. Ni ile maana ya ndani, fundisho la jumla, la kila kifungu cha Andiko ambalo linaweza kutumika kwa ulimwengu wote na kwa kila tamaduni.**

Kila amri na kila mfano una kiini ambacho kinabeba maana ambayo ilikusudiwa mwanzoni kwa ajili ya wote na hiyo ina maana inayolingana na maana ya kifungu chenyewe. “Usiibe” ina maana inayofanana kila mahali. Vifungu vingi, Hata hivyo, vinaelezea hali zisizo za kawaida ambazo si rahisi kuwa na matumizi kila mahali. Katika vifungu hivyo, maana ya kiini ni lazima itafutwe kutoka kwenye kile kilichoelezwa na kifungu chenyewe. Mafundisho ya kiini siku zote yanafaa kwa kila mwanadamu wakati wowote katika historia, ingawa matumizi yanweza kutofautiana kutokana na mazingira tofauti. Hii maana iliyopo kwenye kiini ndiyo hicho tunachokiita “kweli kuu ya kibiblia” [uk.10] Pointi hii itaeleweka vizuri wakati tunapitia zile hatua tatu za kugundua na kutumia maana ya kiini. Kwa sababu kanuni ya nne ni tofauti katika tabia, tutarudia mchakato wa kawaida wa kugundua na kutumia maana ya kifungu cha Biblia kabla ya kutambulisha. Hatua zinaelewaka na ni rahisi. Zinahitaji tu kuzifuata kwa umakini, kwa sababu tofauti za kitamaduni ndizo zinazoleta ugumu.

#### **Kanuni yeye Hatua tatu kwa ajili ya kugundua na kutumia Maana ya Kiini cha kifungu.**

**Hatua ya 1. Tambua “Ilikuwa inawaambia nini wao?”** Wasomaji waliokusudiwa walikuwa ni akina nani, “wapokeaji” wa mwanzo? Kulikuwa na mazingira gani, muktadha wao? Ni maana gani ambayo mwandishi wa kibinadamu alitaka waipate kutoka katika mawasiliano yake?

**Hatua ya 2. Vumbua “Ina maana gani?”** Kuna Nini kwa ajili ya watu wote hapa? Maana Kiini ni ipi? Je hili linaweza kusemwa kwa msemo wa jumla zaidi kwa namna gani? Kwa sababu wanadamu wanafanana kwa namna nyingi. (Dye, T. W. 1987, 42-43), hali zao ni hali ya kila mmoja kwa wakati huu au mwingine. Ni vema kutamka hii maana ya jumla kwa maneno rahisi.

**Hatua ya3. Jiulize “Ina maana gani kwangu?”** Hii maana ya jumla inatumikaje kwetu na kwa wasikiasi wetu, rafiki, na wanafunzi hapa na sasa? Hapa ndiyo mahali kiatu kinapokutana na barabara. Hatua hii ni rahisi sana ikiwa tunatumia maana kwa ajili yetu wenyewe au mwingine kama sisi.<sup>7</sup> Kama matumizi ni kwa utamaduni mwingine, hapo tutakuwa na tatizo katika kutambua namna ya kutambua jinsi ya kutumia. Wanaofanya kazi katika tamaduni tofauti inabidi wategemee wale wanaoishi kwenye tamaduni hizo wawasaidie kufanya hivyo.

Hii inatupeleka kwenye kanuni ya nne.

### **Kanuni ya 4. Amri za kibiblia zipo kutusaidia sisi kumpenda Mungu na watu.**

Kanuni hii ni muhimu sana na ndiyo ya mwisho kuitazama. Paulo anaweka mahusiano yake kwenye sheria zingine kama ifuatavyo:

Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, “Usizini”, “Usiue”, “Usiibe”, “Usitamani”; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno bayu; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria. (Warumi 13: 8-10)

Kusudi la amri hizi zote ni kwa ajili ya mahusiano ya mtu na mtu, ni kutusaidia sisi kujuu jinsi ya kuwa na upendo wa kweli. Kwa kutafakari, kuna amri mbili tu kuu zinazotawala amri zote: Mpende Mungu kwanza na jirani yako kama nafsi yako. Zingine zote zilizobaki ni maelezo ya kina ya jinsi ya kutekeleza hizi mbili.

#### **Kuelewa jinsi ya kupenda wengine ni ngumu**

Sisi wanadamu hatujui namna ya kupendana katika haki, kwa hiyo imebainishwa kwa namna nyingi katika mafundisho ya Biblia. Paulo ameweka wazi maana ya upendo katika 1Wakorintho 13. Upendo ni uvumilivu, ukarimu, hufurahi katika kweli, hulinda, huamini, hutumaini, hustahimili, na kamwe haushindwi. Upendo hauhusudu, haujivuni, haujisifu, hauna kiburi, hauna ukatili, hautafuti mambo yake wenyewe, si mwepesi wa hasira, hauhesabu mabaya, au haufurahii mabaya.

Aina hii ya upendo ni lazima iwe katika matendo kila siku katika mahusiano ya familia na katika shughuli za kijamii kwa majirani. Aina hii ya upendo siyo rahisi kamwe lakini ni lazima itoke “ndani ya moyo ulio safi na dhamiri njema na imani kamilifu.” (1 Timothy 1:5). Ni rahisi kidogo kwa mtu kumpenda mtu kwenye utamaduni wake mwenyewe kwa sababu anajua sheria za kupenda wengine; ni vigumu zaidi katika utamaduni mwingine wakati desturi ni tofauti. Kwa hakika, namna kadhaa za upendo zinachanganya na kueleweka vibaya.

### **1. Upendo kama jambo la watu wote (ulimwengu mzima) na kama fundisho lenye maelezo ya kina**

Kwa kweli, kuna aina mbili za amri kuhusu kuwapenda wengine katika maandiko: wa kiulimwengu na uliofanuliwa kwa kina. Watu wanahitaji zote mbili. Hatujidanganyi wenyewe kwamba eti tuishi kwa upendo na kupuuza mafundisho

maalumu yanahusu upendo katika maagano yote mawili (lakini kwa umuhimu zaidi Agano Jipya). Mungu alijua wanadamu wanayahitaji, ndiyo maana yamehusishwa. Sisi binadamu tunaishi kwenye dunia yenye mambo mengi na inayotuvuta; hatujui namna ya kupenda bila ya uongozi wa mafundisho mengi na mifano ya maandiko.

Wakati huo huo hatujui kutafsiri kwa usahihi haya mafundisho ya kina, kwa kanuni za Upendo lazima zitumwulikie kwa yale tunayopaswa kufanya. Wakati matumizi ya amri hizi mbili zinapopingana, au wakati tamaduni mbili zinapopingana na hivyo kushindwa kujua ipi ndiyo inafaa kanuni ya upendo itatupa njia.

## **2. Tofauti za kitamaduni kuhusu upendo halisi wa Kikristo**

Wakati watu katika jamii fulani wanaposikia Bibbia inasema, “Mpende jirani yako kama nafsi yako” wana ufahamu kuhusu ule upendo unatakiwa uweje; dhamiri zao zilizozeshwa katika tamaduni zao zinawaambia nini cha kufanya. Namna nyininge ya kusema, “wafanyie wengine yale ambayo wewe ungetaka wakufanyie” inafafanua. Inakusudia kumpa mtu wazo la kile anachohitaji mtu mwingle. Upendo unauliza, “Ningetaka mtu mwingle anifanyie nini kama ningekuwa katika hali yake?”

Sheria hii ni mwongozo kwa wale tu waliopo kwenye utamaduni mmoja, hata hivyo, wakati mtu anajaribu kuonyesha upendo [uk.11] kwa jirani ambaye ana utamaduni ulio tofauti kabisa, ile “kama nafsi yako” mara chache inawakilisha upendo. Kwa mfano, mke wangu akitoa chakula kinachohusisha nyama ya nguruwe kwa waamerika wengi, wataona tendo lake kuwa ni la upendo. Kama atatoo chakula chenye nyama ya nguruwe kwa mwislamu, au watu wasiokula nyama itakuwa chukizo sana.

Tulifikiri tunaonyesha upendo kwa Bahinemosi kwa kumsafirisha kwa mashua maili ishirini kwenda hospitalini. Ingawa maisha ya watu kadhaa yameokolewa, hospitali ilionekana kama jela kwao, hasa hasa kwa sababu ya imani yao kuhusu kifo. Wanaamini ikiwa mtu akifa mbali na nyumba, roho ile haiwezi kupata ilikotoka kwa ajili ya hatua muhimu za mazishi, na hivyo hilo litasababisha majanga kwa familia nzima.

Matendo ambayo mtu mmoja atafikiri ni upendo kwa utamaduni mmoja inaweza kumwumiza mtu mwingle aliye na utamaduni mwingle. Matendo mengine yanaweza kumfanya ajikwae na kuacha imani. Inahitaji kufanya utafiti kabla ya kujua nini wenyeji wangetaka wafanyiwe ili waone kuwa ni upendo katika mfumo wao. Mara zote inahitaji 1 Wakor 13 upendo, ambao ni uvumilivu, ukarimu, lakini siyo kiburi, siyo ukali, hautafuti mambo yake wenyewe au si mwepesi wa hasira.

Inasemekana kwamba, kuna mipaka ya kimaandiko kuhusu kwa kiwango gani mtu anatakiwa kujihuisha na tabia ya mtu mwingle na kuiga. Sisi wakristo hatufanyi tu kila kitu ambacho tunafikiri ni kupenda na kupuuza maandiko yanavyofundisha. Badala yake, ni lazima tuwapende watu kwa namna ambayo inadhihirisha upendo na huku tukitii amri zote za Biblia. Umuhimu wa kupenda kunatupa sisi njia ya kutumia zile amri: na siyo kuziondoa.

### ***Kutumia Mbinu za kutafsiri***

#### ***Hatua: Mifano miwili ya Biblia***

#### ***Kuosha Miguu***

Kabla ya Karamu ya Mwisho, Yesu aliwaosha wanafunzi miguu na kuwaambia,

Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyimwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi (Yohana 13:14-15)

Makanisa machache leo hutii hilo kivitendo. Hata hayo makanisa yanayofanya hivyo hufanya nyakati maalumu sana na ni kama tendo la ishara. Kuna sababu yenyе maana; kuosha miguu kama ilivyoamriwa mwanzoni wakati huu inaweza isiwe na umuhimu sana katika tamaduni ambazo watu huvala viatu na soksi, hutembea kwenye vibaraza, na huoga mara kwa mara.

Hii ina maana amri ipuuzwe? Kanuni ya kwanza ya kutafsiri inasema Maandiko yote ni kwa ajili ya faida yetu na ni ya kutii. Kuna maana ya wazi na inayokubalika sana kwa leo, maana ambayo inaonekana wazi kanuni zikifuatwa.

Embu tufuate hatua tatu za matumizi.

#### ***Hatua ya 1: Hii ilikuwa inawaambia nini wao?***

Kuosha miguu. Muktadha wa amri hii ilikuwa ni mji wenye yumbi usio na mfumo mzuri wa maji na mfumo wa maji taka, na wanyama wengi mitaani, na watu walitembea peku au na kanda mbili. Hata kama mtu akimtembelea mtu baada tu ya kuoga, hapo atakapofika nyumbani kwa rafiki yake miguu itakuwa imechafuka tena. Kwa hiyo mwenyeji mzuri anakuwa na mtumishi wa kuosha watu miguu kabla ya kushiriki chakula akiwa na furaha (Luka 7:44). Ilikuwa hali hii ya chini, chafu, lakin ni jukumu la kutenda ambalo Yesu aliwfundisha watendeane wao kwa wao. Hii ndiyo maana yake kwa wale walioandikiwa wasomaji na wasikiaji wa mwanzoni.

### **Hatua ya 2: Hii ina maana gani?**

Kweli ya Biblia inaweza kutamkwa hivi, “Bila kujali umuhimu wa jukumu lako katika jamii ya kikristo lilivyo, siku zote uwe tayari kufanya mambo madogo sana, yale usiyoyapenda kabisa ili kumsaidia mwamini mwenzako au mwanadamu mwenzako.”

### **Hatua ya 3: Ina maana gani kwangu?**

Ulimwengu wa leo kwa hakika unatoa fursa kubwa kuonyesha unyenyekevu, na huduma ya upendo. (Hapa ndiyo mahali kanuni ya nne ya kutafsiri inapoingia.) Kuna matumizi mengi sana kwa amri hii. Wagonjwa na wale walio katika hali ya kufa, ikwa ni pamoja na wanaoishi na VVU/UKIMWI, wanahitaji kuhudumiwa. Wafungwa wanaweza kutembelewa na walioathirika na ugaidi kusaidiwa. Huduma ya kila siku ya kupika, kusafisha, kulea watoto na wazee wanaohitaji uangalizi. Orodha inaendelea. Kanisa linaweza kuendelea kwenda kwa sababu kuna watendakazi, wafagizi, wahudumu wa watoto, pamoja na walimu na wahubiri. Wakristo wanaofanya sehemu ya kazi hizi za kujitolea na kujishusha wanatii amri hii hata kama wanashiriki au hawashiriki ile ibada ya kuoshana miguu.

### **Kumfunga kinywa Ng’ombe**

Mtume Paulo anatafsiri kifungu cha Agano la kale kwa njia hii 1 Wakor 9:9-10 na 1 Timotheo 5:17-18. Alikuwa akitoa hoja kwamba Watumishi wakristo wanatakiwa kulipwa, na akathibitisha dai lake kwa kunukuu amri katika Kumbukumbu 25:4, “Usimfunge ng’ombe kinywa apurapo nafaka.”

Kwa namna gani Paulo aliruka kutoka kwenye ng’ombe hadi watu? Fuata hatua za matumizi. (Hatua ya 1: Inasemaje?) “Usimfunge ng’ombe kinywa apurapo nafaka.” Katika kifungu cha 1 Wakor anaendelea kuuliza, “Je Mungu anahuksika na ng’ombe? Kwa hakika anasema hili kwa ajili yetu, Je hafanyi hivyo?” Jibu la hili swali ni hapana, siyo katika kifungu cha awali. Maana iliyokusudiwa ni kuwatendea vizuri wanyama.

Lakini Paulo aliona maana kiini (Hatua ya 2: Ina maana gani?) Kiini cha kifungu hicho ni kwamba kila anayefanya kazi anastahili kupata mapato kwa kazi yake. (Hatua ya 3: Ina maana gani kwangu?) Wazo hilo ina matumizi mengi. [uk.12] Alilitumia hilo kumaanisha kwamba watu katika jamii za wakristo wanapaswa kulipa wachungaji wao. Zaidi ya hayo, kwa kuwa watu ni muhimu kuliko wanyama, Paulo alieleza kuwa hii ilikuwa kusudi muhimu sana ya amri. Yesu pia alisema watu ndiyo lengo la kifungu kuhusu ng’ombe katika Agano la Kale (Luka 13:15; 14:5).

Haya siyo matumizi ya kawaida ya kifungu kumtendea ng’ombe, lakini Yesu na Paulo walifuata hatua za matumizi kwa ajili yetu.

### **Baadhi ya mifano isiyo dhahiri**

Wakati mwingine hizi kanuni nne za kutafsiri ni rahisi kuzitumia. Wakristo leo wanahisi kwamba wanatakiwa kusaidia kufanya kazi ya kusafisha na duni kwa ajili ya wakristo wengine bila kujua “wanaosha miguu.” Kwa wakati mwingine mchakato ni mgumu. Katika baadhi ya mambo matatizo hutokeea kwa kuacha moja ya hatua mionganii mwa hatua tatu za kugundua maana ya msingi. Katika mambo mengine, kikundi cha wakristo wanahisi kwamba matumizi fulani mahususi ni ya dhahiri sana. Hilo linapotokea, kanuni pamoja na matumizi yake huunganishwa katika fahamu zao, ili kwamba matumizi yaye ndiyo maana yake. Kwa maneno mengine, hawa wakristo wamechanganya matumizi mahususi ya tamaduni na ukweli kamili wa Kibiblia. Matokeo yake wanazuia matumizi tofauti tofauti wakati hali zinapobadilika.

Baadhi ya amri za kibiblia zimetajwa kuwa za mahali pote, kwa hiyo hatua ya pili haina ulazima. “Usiibe,” kwa mfano, ilikuwa amri maalumu kwa Israeli wa kale, lakini pia amri ya mahali pote kwa watu wote kila mahali. Amri za agano jipya kama vile, “kuwa mwema” au “kuwa mkarimu” wamepewa watu mahususi, lakini maelekezo ni kwa ajili ya mahali pote. . Ukarimu, wema, na wizi vyote vinafahamika katika tamaduni zote. Maelekezo hayo ya mahali pote yanawaongoza wakristo kwenye upotofu kwamba matumizi yake pia ni wazi na ya mahali pote wakati ukweli ni kwamba matumizi huathiriwa na utamaduni. Tunaweza kuliona hili kwa kuchunguza ni kwa jinsi gani baadhi ya amri zilivyotekelizwa katika Agano jipya, mfano ufuataao ukihusika.

### **Ni wakati gani inakuwa Wizi?**

Embu tuangalie wizi kwa kutumia hatua tatu za mchakato wa matumizi. (Hatua ya 1): Hii ilikuwa inasema nini kwao? “Usiibe.” Kwa sababu imetakwa kwa watu wote, kanuni ya mahali pote ni sawa na maeleo ya awali. “usichukue kitu ambacho huna haki ya kuchukua” Kwa hiyo hatua ya kwanza na ya pili zinafanana. Hata hivyo, matumizi yanatofautiana kwa sababu ya utamaduni. Kama Yesu angekuwa anaishi Amerika na kufanya kile ambacho Injili inasema alifanya, angekuwa mwizi. Alikuwa akitembea kwenye bustani za watu wengine na kula matunda, hata Mafarisayo hawakulalamika.<sup>8</sup> Lakini kama nikipita kwenye bustani ya mwamerika na kuchuma tunda ninaweza kukamatwa kwa wizi. Nikijitetea mahakamani kwa kusema Yesu alifanya hivyo, Jina langu linaweza kuandikwa kwenye gazeti lakini sitaachiwa.

Tofauti ipo kwenye matumizi. (Hatua ya 3): Ina maana gani kwangu? Yesu aliishi katika utamaduni ambao kupitia vitabu vya sheria, imetafsiri haki za umma zikihusisha kuchuma matunda, ikiwa yataliwa mahali pale yalipochumwa. Kwa sababu serikali yake ilimpa Yesu kuchuma matunda, hakuwa anaiba. Utamaduni wangu haumpi mtu haki ya kula matunda kwenye bustani ya mtu mwingine. Ni lazima niombe ruhusa ya kuchuma tunda, vinginevyo itakuwa wizi.

Baadhi ya utafiti unahitajika kuingia katika kutambua ni nini ambacho watu katika tamaduni mahususi wana haki ya kuchukua. Vikundi vya watu wengi katika Irian Jaya zina sheria tofauti kuhusu ambacho watu wana haki ya kuchukua. *Hadithi ya Nanasi* (Gothard na Koning 1978) inaelezea mgogoro wa mwingiliano wa kitamaduni kama matokeo ya sheria tofauti kuhusu umiliki wa mazao. Kama mishenari akiuliza, “Nani atakuwa na haki ya kuchuma nanasi?” Na kuamini aliambiwa, hangeepuka miaka ya kueleweka vibaya na kushusha ushuhuda wake. Wairiani katika hadithi yao wana sheria wazi, “Mtu aliyepanda hula.” Mazao ya bustani hutumika kwa ukarimu hufungua njia kwa ajili ya uongozi wa siku za mbele. Wamiliki wanatoa laana ili kulinda bustani zao kutoekana na wezi kwa kuita mamlaka iliyo juu yao, hasa hasa mizimu ya baba zao. Watu wa jamii ile hawana uzoefu au ufahamu wa kazi ya mshahara. Wamishenari walibuni itifaki ya mshahara wa kibarua, “Nikilipa kibarua, Ninamiliki chochote kinachozalishwa na kibarua.”

### **Maana ya Ukarimu kulingana na Utamaduni**

Amri ya kuwa “wakarimu kwa vitendo” (Warumi 12:13) linaeleweka kila mahali, lakini bado siyo kwa namna moja. Wakati mimi na binti yangu tangu tulipowatembéa watu wa Tboli wa Mindanao, Filipi mwaka 1974, wakristo walitupa sisi zawadi na kutukarimu vitu vyenye thamani ya mshara wa mwezi. Utamaduni wao umeweka kiwango kikubwa sana cha ukarimu, na hiki ndicho kiwango walichotaka kuonyesha kwa rafiki za mpendwa wao mtafsiri.

Kama wamishenari mara nyingi tumekuwa tukifanyiwa ukarimu katika Amerika. Watu wengi wamekuwa tayari kutupokea nyumbani mwao na kutuonyesha ukarimu mkuu, ingawa sisi ni wageni. Hata hivyo, hakuna hata mmoja aliywahi hata kukaribia kutupa mshara wa mwezi mmoja kwa njia ya ukarimu. Hatutegemei jambo kama hilo katika utamaduni wa Amerika ya Kusini. Amri kwa watu wote [uk.13] ni lazima ipatiwe maana inayoendana na utamaduni husika.

### **Viwango vya Ukarimu kulingana na Tamaduni**

Amri katika Kibiblia inasema “uve mkarimu na uwe tayari kushirikisha” (1 Timotheo 6:18). Maana ya msingi ipo wazi na inafanana na amri yenye (Hatua ya 2). Lakini matumizi yapo tofauti sana kwa mwanakiji wa Isneg aliyepo Kusini mwa Filipi na sisi tulipo hapa (Hatua ya 3). Kama Isneg akija kutoka kijijini kwake na mfuko wa mananasi kutoka kwenye bustani yake akagawa theluthi mbili kwa watu, angeonekana mchoyo. Kiwango kilichowekwa kulingana na utamaduni wao ni kugawa robo tatu kwa watu. Ikiwa hapa kwetu mimi nitaenda kwenye stoo yangu ya vinywaji na kugawa theluthi mbili ya vinywaji vyangu kwa majirani watafikiri labda nimerukwa na akili.

Tunaishi katika tamaduni tofauti, zenyе viwango na mifumo tofauti ya kushirikiana vitu. Amri ni kwa watu wote, lakini matumizi yake yanategemea utamaduni husika. Ni vizuri zaidi kutumia kanuni hizi tatu wakati wote na kuwafundisha watu kwenye tamaduni zingine wafanye hivyo.

### **Busu takatifu**

Mfano mwingine wa utii unazingatia muktadha ni namna ambayo tamaduni mbalimbali inafuata mafundisho yahusuyo (Hatua ya 1) “Salimianeni kwa busu takatifu” (Warumi 16:16, 1 Wakor 16:20, 2 Wakor 13:12, 1 Wathesalonike 5:26, 1 Petro 5:14). (Hatua ya 2) Salimianeni kwa uchamfu, na kuonyesha upendo wa kweli. Watu wa tamaduni zingine wakifuata (hatua ya 3), baadhi ya tamaduni zinakubaliana na kubusu. Zingine hukumbatia, kushikana mikono kwa uchangamfu, pamoja na kuinama, au hata sauti ya upole inayoashiria urafiki na tabasamu. Kwa namna yejote inavyofanyika upendo, heshima, na kujaliana huwasilishwa kikamilifu.

### **Kuwahudumia Wazee kwa namna ya Kimagharibi**

Chukua mfano mwingine, amri ya “kumheshimu baba yako na mama yako” (Hatua ya 1 na ya 2). Kanisa la kwanza lilijua kuheshimu wazazi inahusisha kuwahudumia pale wanakuwa wamezeeka. Kanisa lilhudumia wazee ambao hawana watoto wa kuwahudumia. Yesu alivunja moyo namna ya mafarisayo kutoa sehemu inayohusu wazazi kwa Mungu (Mathayo 15:1-9). Niliwahi kusikia kuwa Seneta mmoja Mfiji aliwahi kusema hadharani kwamba jamii za kimagharibi ni “wajima” kwa sababu tunaacha malezi yote ya wazee kwa mashirika ya kijamii. Katika mtazamo wake, wazee ni lazima walelewe na familia zao na lazima waishi nao. Kwa hakika mtazamo wake ni sawa na ilivyokuwa inafanyika katika kanisa la kwanza..

Sisi wakristo katika Amerika, pamoja na wale wazee sana tunalionia hili kwa namna tofauti (hatua ya 3:Ina maana gani kwangu). Tunaona maana ya msingi kimsingi haibadiliki, lakini tunasema hivyo tukihusisha sera za kijamii ambazo zinatoa huduma na mafao ya kijamii, kwa hakika tunatekeleza jukumu letu kwa njia hiyo. Kama waamerika wengi wanavyotazama mambo, nyumba zetu hazina vyumba kwa ajili ya mtu mwingine katika familia kukaa, na siyo kwamba wazee wanataka kujitegemea katika familia zao. Ni pale tu mambo mengine hayakidhi, la sivyo tungetegemea familia ziwatunze wazazi wao wazee. Huu ni mfano wa utii ambao unaendana na muktadha wa kitamaduni kwa baadhi ya watu katika Amerika.

### **Je Mkristo avute sigara?**

Katika mfano uliopo hapo juu, utamaduni wa kabilia umeonyesha kutambua kwa nguvu sana Amnri kuliko Waamerika. Na kabla hatujahitimisha kuwa hii ni kwa sababu Waamerika hawapo vizuri kiroho, tuangalie mfano huu tofauti. Kama ilivyo kwa waamerika wengi wa kijijilisti, mimi na mke wangu hatuvuti sigara. Tumechukua amri katika 1 Wakor 6:19-20 ikiwa na maana ni lazima tujali miili yetu. Tunajua kuwa uvutaji wa sigara kunaongeza uwezekano wa kuugua. Siku hizi waamerika wengi wanakubaliana na hili, hadi kufikia kiwango cha kuwafanya wawutaji waone kuwa maisha ni magumi lengo likiwa ni kuzuia moshi wa sigara usiwepo kwemye ofisi na katika makusanyiko.

Wakristo wa Bahinemo ambao tilikaa nao kwa muda wa miaka mingi katika Papua New Guinea walikuwa na shauku ya kutii amri za Mungu. Tuliwafundisha waende kwenye Biblia kuliko sisi ili kupata majibu kwa ajili ya maisha yao. Sisi tungewenza kuwa pale kwa muda na baadaye tungeondoka kwa hiyo tulitaka wamtegemee Yesu kwa msaada wao. Kilichotufanya tujisikie vibaya mionganoni mwa wamishenari wengine ni kwamba wabahinemo hawakuona kuwa uvutaji wa sigara ni dhambi kwa sababu hakuna amri kwenye Biblia kuhusu uvutaji wa sigara. Hili halikuwa katika muktadha wa kuona makatazo dhahiri ya Mungu kuhusu dhambi zilizopo katika mtindo wa maisha yao.

Wabahinemos walifahamu kuwa Biblia inawaamuru kutunza miili yao, lakini hawakuona uhusiano kati ya kuvuta sigara na ugonjwa. Wazo la kukua kwa tatizo kidogo kidogo na wazo la dhara kufahamika kwa njia ya kutazama takwimu ni mambo mageni katika ulimwengu wao wa kifira. Mpaka pale tulipowaonyesha uhusiano kati ya madhara na visababishi, hawakuwa tayari kukubaliana na wazo letu kwamba ugonjwa mbaya wa mapafu na vikohozini vinyowapata ni matokeo ya kuvuta sigara. Zaidi ya hilo, tumbaku iliyokuwa ikilimwa ilikuwa inawapatia moja ya vitu vinyowapata starehe katika ulimwengu uliojaa insekta na kukosa faraja. Pia ilikuwa ni njia pekee ya kukarimu wageni wanaowatembelea na ni ya thamani kubwa kubwa kwao. Ni wachache tu waliokuwa wagonjwa sana wa mapafu ndiyo walioweza kuacha kuvuta sigara kwa sababu za kiafya, pamoja na juhudhi nilizofanya kufundisha swala hili.<sup>9</sup>

Nyakati zile za kwanza za kanisa tungeliwaambia kirahisi, "Hutakiwi kuvuta sigara na muwe Wakristo." Hata hivyo, sisi ndiyo tulikuwa wainjilisti wao wa kwanza na chanzo cha kila fundisho jipywa wanalojua. Kufanya hivyo kuhusiana na mafundisho na maandiko, ingawaje, ingewashawishi wao kujua kwamba kuna mambo huhitaji kabisa kwenda kwenye Biblia kabisa. Matokeo yangekuwa kupunguza utayari wa kujitoa kutii Neno la Mungu na kuliona kama chanzo cha msingi cha kujua mapenzi ya Mungu. Kirahisi ingesababisha uwezekano [uk.14] wa kudanganyika kirahisi uongezeka kutoka kwa kila "nabii" mwenye mtindo wake binafsi anayekuja kwao.

### ***Hitimisho na muhutasari***

Chapisho hili limejaribu kuelezea kwa nini ni muhimu kwa wakristo kutafsiri na kutumia mafundisho ili kuyafanya yafae zaidi katika tamaduni zao wenyewe. Kwa karne nyingi, waminio wamefanya matumizi haya bila kujua. Kwa hakika, mtazamo wao kuhusu madai ya maandiko kwao yalitengenezwa na tamaduni zao wenyewe kwamba kanuni na matumizi ya tamaduni zao zilitegemeana. Nyaraka kipekee zinatufundisha kuwa jamii ya wakristo ni lazima wapate ufhamu wa kibinafsi wa namna ya kutumia Biblia. Hata kama waamini katika kila jamii wamekomaa kikamilifu, bado tu kutakuwa na tofauti ya jinsi wanavyotii Biblia.

Tulitoa kanuni nne za kutambua jinsi amri inavyotumika.

1. Maandiko yote, mawili Agano la Kale na Jipywa, yana mamlaka juu ya watu wote, kwa kila umri na utamaduni.
2. Kuna wasomaji na wasikiaji wa asili ambao kile kifungu kiliandikwa kwao.
3. Maana ya msingi ya kila amri ya maandiko inatumika kwa tamaduni zote, hii ni kweli kamili ya Biblia.
4. Amri ya kuwapenda wengine kama unavyojipenda mwenyewe huelezea kusudi la amri zingine, na kutoa njia ya kuchambua mambo yanayohusiana na utamaduni na mambo yanayotatiza katika kutafsiri.

Hatua tatu za mchakato wa matumizi hutusaidia kupata maana ya msingi na jinsi inavyotumika katika hali yeoyote mahususi.

- Hatua ya 1. Hii ilikuwa inawaambia nini wao? (Maana ya asili)  
Hatua ya 2. Ina maana gani? (Maana ya msingi)  
Hatua ya 3. Ina maana gani kwangu? (Maana kwangu binafsi, au kwa rafiki mwenye utamaduni mwengine)

Hizi kanuni Nne za Matumizi na hatua tatu za Mchakato wa Matumizi zinatuwezesha kujua maana ya msingi ya amri.

### ***Maelezo ya Mwisho***

<sup>1</sup> Si kwamba nilifikiri ninaishi maisha ya haki, bali nilifikiri ikiwa nitafanikiwa itakuwa ni kutenda kwa uhalisia yale ambayo nilivyofundishwa kwamba ni kuishi kwa haki na kila mtu.

<sup>2</sup> Rejea zote za Biblia katika chapisho hili yamenekuliwa kutoka New International Version.

<sup>3</sup> Wahindi na Waafrika mara kadhaa walisisitiza mwanamke anapaswa kufunika kichwa baada ya kuwafahamisha kwamba tulitaka tufanye haki.

<sup>4</sup> Kwa upande mwengine, Nov-Disemba. 1975 kwa mifano hii na mingine.

<sup>5</sup> Hata hivyo, wakristo waliokomaa, wanatakiwa waache kutumia uhuru wao kwa manufaa ya wakristo wachanga.

<sup>6</sup> Kwa mjadala zaidi wa wazo hili pamoja ugumu wake uliojificha, tazama Geisler 1989. Mtindo ninaotumia unaweza kuonekana kama njia mbadala ya "Graded Absolutism" (Geisler, 113-132).

<sup>7</sup> Kwa upande mwengine ikiwa ni sisi tumeandikiwa, na inapingana na kitu ambacho utamaduni wetu unakikubalia au kukiithamini, tutatatzika katika kuona maana kamili ya amri hiyo na kuitumia.

<sup>8</sup> Yesu alikuwa anavunja sheria ikiwa tu atafanya kazi siku ya sabato. (Mark 11:12-33). Katika jaribio hili mafarisayo hawakuleta hilo kama tatizo.

<sup>9</sup> Hivi karibuni idadi inayoongezeka ya wanakijiji wa kijiji hiki wameanza kujua uhusiano kati ya uvutaji wa sigara na afya, na matokeo yake wengi wameacha kuvuta sigara.

**Rejea**

Barrett, David.

1968. Mgawanyiko na Kufanywa upya katika Afrika: *Uchambuzi wa Michakato Elfu Sita ya Dini za Siku za Leo*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.

Biblica, Inc.

2011. *Biblia Takatifu, New International Version*. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Dye, Sally F.

1983. "Viwango vyenye mgogoro vya Wema." *Makala ya Maandiko yanayotumika* 6: 23-37.

2014. "Tofauti za kitamaduni katika Dhamiri: Sehemu ya Ubunifu wa Mungu." *Jarida la Kimataifa la Frontier Missiology*, 31:1, Spring 2014.

Dye, T. Wayne.

1976. "Kuelekea Msalabani –Maana ya dhambi kulingana na Utamaduni." *Missiology: An International Review* 4 (1): 27-41.

1987. "Hemenutiki na Mtindo wa Mawasiliano wa SMR" *Jarida la Tafsiri ya Kifungu katika Lugha*, mwanzoni ikifahamika kama *Magazeti ya Msimu ya Lugha ya Kifungu cha habari*. 1(2): 37-65.

2009. "Kutambua utendaji wa Roho Mtakatifu katika Jamii." Katika *Mitazamo wa Kuenea kwa Ukristo Ulimwenguni: A Reader*. Toleo la 4, liliofanyiwa marejeo na Ralph D. Winter na Stephen C. Hawthorne. Pasadena, CA: William Carey Library, 493-496.

Geisler, Norman L.

1989. *Maadili ya Kikristo: Chaguzi na Matokeo*. Grand Rapids, MI: Baker Book House.

Gothard, Bill and Otto Koning.

1978. *Hadithi ya Nanasi*. Oak Brook, IL: Taasisi ya Migogoro ya Msingi ya Vijana.

Henry, Carl F. H.

1957. *Maadili Binafsi ya Kikristo*. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

McQuilkin, Robertson.

1995. *Utangulizi wa Maadili ya Kibiblia*. Wheaton, IL: Tyndale House.

Murchison, William.

1994. *Kudai kurejea kwa Maadili katika Amerika*. Nashville, TN: Thomas Nelson.

Naroll, Raoul.

1983. *Sheria ya Maadili*. Beverly Hills, CA: Sage Publications.

Priest, Robert J.

1993. "Cultural Anthropology, Dhambi na Mmishenari." Katika *Mungu na Utamaduni*, imerekebishwa na Carson, D. A. na John D. Woodbridge, 85-105. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

1994. "Missionary Elenetics: Utamaduni na Dhamiri." *Umisheni* 22 (3): 291-315.

1997. "Theoloji ya Kikristo, Dhambi, na Anthropology." In *Explorations in Anthropology and Theology*, liliohaririwa na Salamone, Frank A. and Walter Randolph Adams, 23-37. Lanham, MD: University Press of America.

T. Wayne Dye sasa ni Profesa Msaidizi wa Applied Anthropology katika Taasisi ya Wahitimu ya Applied Linguistics iliyopo Dallas, Texas. Yeye, pamoja na mke wake, Sally, wametumika na Wycliffe Bible Translators na SIL kwa miaka 25 katika kutafsiri Biblia na program halisi kati ya Wabahinemo wa Papua New Guinea. Wayne ana Shahda ya Uzamili katika sayansi ya binadamu na kazi zake kutoka Chuo Kikuu cha Michigan na shahada ya Uzamivu katika Taaluma ya Mwingiliano wa Kitamaduni (Intercultural Studies) kutoka Fuller Theological Seminary. Ametumika kama mshauri na mkufunzi kwa ajili ya SIL tangu 1973, kwanza kule Papua New Guinea, kisha Kimataifa. Amefundisha zaidi ya nchi thelethini duniani kote.

## **NYONGEZA E**

Machapisho haya yametumika kwa ruhusa ya Leadership Resources

### **Chimbua Utambue Kanuni za Hamenutiki: Kanuni za Msingi**

#### ***Jifunze zaidi!***

*Leadership Resources* ni huduma inayotia moyo na kuwawezesha wachungaji na viongozi wa kanisa duniani kote. Ushirika wetu wa mafunnzo unawasaidia wachungaji katika kuhubiri Neno la Mungu na Moyo wa Mungu. Vitabu vyetu na makongamano inayatia moyo makanisa kuakisi moyo wa Baba, ili kwamba aweze kuutumia kujaza dunia kwa utukufu wake.

#### **Ungana nasi katika huduma**

- Jifunzi jinsi wewe au kanisa lako linaweza kujihusisha kuimarisha kanisa la ulimwengu kwa ajili ya huduma ya kiblia, tembelea tovuti yetu: [www.leadershipresources.org/getinvolved](http://www.leadershipresources.org/getinvolved)
- Wachungaji, chimbueni maandiko kwa pamoja na wachungaji wengine katika maeneo yenu kwa ajili ya ushirika wa kujengana na kunoana kwa vitendo kupitia ushirika wa Neno. Jifunze zaidi katika: [www.leadershipresources.org/FOW](http://www.leadershipresources.org/FOW)

#### **Tafuta vyanzo vingine**

- Leadership Resources pia inatia moyo kwa Maandiko kutoka Biblia kwa Makongamano ya kibiblia, vitabu, na kwa njia ya rekodi za sauti. Tembelea tovuti yetu katika: [www.encouragementoftheword.org](http://www.encouragementoftheword.org)

#### **Jiunge na sisi**

- Kwa habari zinazohusu jinsi Mungu anavyofanya kazi kupitia mafunzo yetu na huduma yetu, pamoja na machapisho ya muhubiri na masomo ya Biblia, uanafunzi, jiunge nasi kwenye mtandao.
  - Wasiliana nasi kwenye barua pepe: [www.leadershipresources.org/fuseline](http://www.leadershipresources.org/fuseline)
  - Blogu: [www.leadershipresources.org/blog](http://www.leadershipresources.org/blog)
  - Facebook: Leadership Resources International ([facebook.com/LRInews](http://facebook.com/LRInews))
  - Twitter: @LRI\_News ([twitter.com/lri\\_news](http://twitter.com/lri_news))
  - YouTube: Leadership Resources ([youtube.com/user/lrinews](http://youtube.com/user/lrinews))

#### **Ruhusa na Usambazaji**

Ingawa tunaomba usichapishe wala kuzalisha au kusambaza machapisho haya, hasa kwa njia ya elektroniki, Leadership Resources inatoa machapisho haya kwa ajili ya matumizi binafsi kwa kuyapakua kutoka kwenye tovuti yetu au kwa mawasiliano ya moja kwa moja na sisi.

#### ***Chimbua utambue Kanuni za Hemenutiki: Kanuni za Msingi***

Imepigwa chapa na  
Leadership Resources International  
12575 S. Ridgeland Ave.  
Palos Heights, IL 60463  
United States of America  
[www.leadershipresources.org](http://www.leadershipresources.org)  
Copyright © 2014 Leadership Resources International

Haki zote zimehifadhiwa.

## **Yaliyomo**

Karibu..... 89

## **Kanuni za Msingi**

Kaa kwenye mstari..... 90

Kifungu na Mipaka yake..... 91

Tanzu za Fasihi..... 92

Kujiuliza maswali mazuri..... 93

Mafunzo yanayosafiri..... 94

Muundo. .... 95

Kutafuta Wazo kuu na Mwitikio Tarajiwa..... 96

Theolojia ya Biblia..... 97

# Karibu!

Umeshika mkononi kitabu kiitwacho “Chimba Utambue.” Kanuni za kutafsiri Biblia inayofunzwa na Leadership Resources International kama sehemu ya pili ya TNT (Kufunza Wakufunzi wa Kitaifa) program ya mafunzo iliyoandaliwa kuwatia moyo na kuwawezesha wachungaji ulimwenguni mwote kwa moyo na kwa Neno la Mungu.

Hata kama kitabu hiki kimeandaliwa kuelezea kanuni za kutafsiri Biblia, Tunachotaka wewe uelewe zaidi ya kanuni zenyewe ni maandiko yenewe. Kumbuka kuwa kanuni za kutafsiri Biblia ni kifaa tu. Tunazielea kukusaidia wewe kusoma vema, kujifunza, na kuelewa ujumbe wa Neno la Mungu wakati ukitegemea kikamilifu kuangazwa na Roho Mtakatifu katika maombi.

Na wakati unajifunza Neno la Mungu, fahamu akilini mwako kwamba kusudi hasa na lengo la kujifunza Biblia siyo tu maarifa bali ni ibada. Shauku yetu siyo tu kujaza ufahamu wako kwa maarifa ya Biblia. Badala yake, maombi yetu ni kwamba moyo wako ubadilishwe kupitia ujumbe huu kwa Roho Mtakatifu na ufurike katika kuabudu utakapomfahamu Mungu zaidi kupitia nafsi ya Yesu Kristo.

Mungu afanye hivyo kwa uhakika katika moyo wako. Akubariki unapojifunza Neno lake akufanye umpende yeye zaidi kila siku, na akufanye uliishi Neno lake kwa shukrani na utii kwa yote kwa sifa, utukufu na heshima kwake.

# Kaa kwenye mstari

## Ina maana gani “kukaa kwenye mstari”?

- Kukaa kwenye mstari ina maana kwamba mwalimu au muhubiri anatakiwa kugundua maandiko yana maana gani na kuwa mwaminifu kwa maandiko hayo.
- Mstari unawakilisha kile hasa ambacho Mungu anasema katika Neno lake:



- Kwenda juu ya mstari ina maana kuongeza kile ambacho Mungu hajasema katika Neno lake. Inatupelekea kwenye makosa, mara zote katika muundo wa kuwa wa kisheria.
- Kwenda chini ya mstari ni kuacha kitu ambacho kilikuwepo kutokuwa mkweli na mwaminifu kwa ukamilifu kwa kile Mungu anachosema. Mara zote hutupelekea kwenye uhuru usio na mipaka na kuijhesabia haki.
- Kukaa kwenye msatari kunaweza kulinganishwa na ahadi ya ushahidi ambayo mahakama ya sheria inafanya: “[usiende nje ya mstari].” Ninaahidi kusema kweli, kweli tupu (bila kwenda chini ya mstari) na siyo kingine ila kweli tu,

## Hii ina umuhimu gani kwa Mungu?

- Tangu enzi za Musa, Mungu ameweka wazi wasemaji wake wanatakiwa kusema kile asemacho yeye na siyo kuongeza wala kupunguza. (Kutoka 4:10-16; Kumb 4:1-2; 1 Samw. 3:1-4:1; Mithali 30:5-6; Ezekiel 3:1-11; Yeremia 1:4-19; 23:9-40; Yohana 7:16ff; 8:28-29; 12:29-50; Ufunuo 22:18-19).

## Hii ina umuhimu gani kwa mahubiri yetu?

- Neno la Mungu halilinganishwi. Katika Biblia yote, tunaona maneno yake yana nguvu, ni kweli, ni mazuri, ni neno lake linawenza kutoa uzima. Tunataka watu wasikie sauti ya Mungu kuliko sauti zetu. Kweli yake kuliko maoni na mawazo yetu ya wanadamu. Tunahitaji kupata uzoefu wa nguvu za Mungu zinazokuja kupitia Neno lake.

## Kukaa kwenye mstari kunahitaji nini?

- Kujitoa wenyewe kwa Mungu.
- Kujua kwa makini na kuelewa kile Mungu anasema kwa hakika.
- Kuwasilisha kwa uaminifu katika mafundisho yetu, mahubiri yetu na maisha yetu.

# Kifungu na mipaka

**Kanuni:** Ni lazima turuhusu Biblia ituwekee mitazamo kuliko kufanya mitazamo yetu ielekeze namna tunavyotafsiri Biblia.<sup>1</sup>

## Tunamaanisha nini Kwa “Kifungu” na “Mitazamo au mipaka”?

- Kifungu ni aya kutoka kutoka Biblia ambacho tunajifunza na kuhubiri au kufundisha.
- Mtazamo au mipaka ni namna ya msingi tunayotumia kuelewa mambo. Inaathiri namna tunavyosoma na kuelewa kifungu.

## Zaidi “Nini maana ya Mtazamo/mipaka?”

- Mtazamo au mipaka Ni ufahamu wa msingi wa mtu kuhusu vitu. Ni msingi wa muundo wa mawazo unaounda uelewa wetu kuhusu vitu vyote. Mtazamo/mipaka yetu inaunganisha mawazo yetu na fikra zetu kuzifungamanisha pamoja kwa namna ambayo inatupa kuelewa mambo.
- Kila mtu ana mtazamo wake. Umejengeka kwa muda mrefu kutoka kwa wazazi wetu, mafundisho, elimu yetu, utamaduni, uzoefu binafsi, na sehermu yetu katika historia-hata kusoma Biblia.
- Katika maisha yetu tunakutana na taarifa mpya. Tunatakiwa kujuja jinsi inavyoingiliana na uelewa wetu wa mwanzo wa vitu. Mwishoni, au tunaamua kupuza au kukataa taarifa mpya, au tunapokea na kuruhusu kuumbika kwa mtazamo mpya.


## Mipaka/Mtazamo huathiri jinsi tunavyosoma Biblia.

- Tunapoketi kusoma Biblia, tunakuja na mitazamo yetu-ikihusisha namna tunavyomwelewa Mungu, mtu, dhambi, Kristo, mateso, ukombozi, na vitu vingine vingi.
- Mipaka/Mtazamo ya ndani peke yake siyo lazima iwe mibaya. Ingawa kwenye mchakato wa kusoma, kuelewa, na kuwasilisha Biblia. Pamoja na hayo inaweza kuathiri vibaya namna tunavyoelewa kifungu.


## Kifungu ni lazima itawale na kuumba mtazamo wetu.

- Tunaamini kwamba Biblia inatoka kwa Mungu (2 Petro 1:21), imevuviwa na Mungu (2 Timotheo 3:16a), ya kweli na ya kutegemewa (Mathayo 5:17-18), inatosha kwa imani yetu na uzoefu (2 Timotheo 3:16b). Mara nyingi hatuwezi kutambua ni lini mitazamo yetu inaathiri jinsi tunavyoelewa kifungu, na wakati mwingine, hata tunapokuwa tumetambua, haturuhusu kuachilia mitazamo yetu na kufuata maandiko yanavyosema.
- Ili kuelewa Neno la Mungu na kulihubiri kwa uaminifu, ni lazima turuhusu kifungu kitawale na kuunda mtazamo wetu.
- Kunapokuwa na tofauti kati ya kifungu na mtazamo, tunapaswa kumwomba Mungu atusaidie kutambua na kuruhusu kifungu kiumbe upya mtazamo wetu.

*Mara zote  
kinachotokea:  
Mtazamo  
wetu  
unapoathiri  
na kuumba  
upya kifungu.*



*Nini kitatokea:  
Kifungu  
kinapotawala na  
kuumba mtazamo  
wetu.*



\* Kwa kuzingatia machapisho ya msingi © The Proclamation Trust with kind permission. www.proctrust.org.uk

1 The Charles Simeon Trust, "Kanuni za Ufafanuzi," <http://www.simeontrust.org/media/wbe-principles.pdf>

# Tanzu

## Tanzu ni nini ?

“Tanzu” ni neno ambalo linalezea aina, au mfumo wa fasihi, maandishi yaliyoandikwa, tunayopata kwenye Biblia. Tunatambua aina za tanzu kwa tofauti zilizopo katika sifa za kifasihi kama vile mtindo wa uandishi, muundo, yaliyomo, na kusudi la kuandikwa.

## Ni kwa namna gani kuelewa Tanzu inatusaidia ?

- Kuelewa tanzu kunatusaidia sisi kuelewa sifa za aina ya fasihi tunayosoma. Na uelewa wa sifa za fasihi kunatusaidia kusoma na kuelewa kwa usahihi-kuelewa kusudi la mwandishi na kile alichotaka kuwasilisha..

## Kwa nini tanzu ni muhimu?


- “Tanzu ni ufunguo wa kuelewa aina ya taarifa ambavyo mwandishi wa Biblia anajaribu kuwasilisha.”<sup>2</sup>
- “Mpaka pale utakapoelewa kusudi na aina ya kifungu, kinachokusudiwa kuwasilishwa ndipo utaweza kusoma kwa usahihi” (C. S. Lewis).<sup>3</sup>
- Kuelewa tanzu na sifa za kifungu kunatupa mwanga fulani, hata kuelewa sheria na jinsi ya kusoma na kutafsiri maana ya kifungu.

## Aina tofauti za Tanzu katika Biblia

Kuna aina tofauti za tanzu za fasihi katika Biblia. Hapa chini kuna Tanzu kuu katika Biblia. Ingawa vitabu vyote vya Biblia mara zote vinahusiana na tanzu fulani, kitabu kimoja katika Biblia kinawezwa kuwa na aina tofauti za tanzu au tanzu mchanganyiko-kwa mchanganuo wa undani zaidi wa fasihi.

## Namna tofauti ya matumizi ya lugha:

Tofauti moja ya muhimu tunayoona katika tanzu ni namna ambavyo kila mmoja inavyotumia lugha kuelezea ujumbe. Hapa chini ni mwonekano unaoliganisha aina tofauti za tanzu na sifa za aina za lugha na matumizi ya kila mmoja.




2 Ufupisho wa Ben Witherington wa sehemu ya kitabu kilichofanyiwa marudio katika “Neno la Mungu lililohai (kwenye kizazi cha Mmomonyoko wa Kweli)” (Oktoba 31, 2007) kwenye <http://benwitherington.blogspot.com>.

3 Ukinukunuliwa moja kwa moja na Ben Witherington, “Hemenutiki – Mwongozo wa wasomaji wa Biblia Wanaoshindwa kuelewa” (August 21, 2007) kwenye <http://benwitherington.blogspot.com>

# Kuuliza Maswali mazuri

## Umuhimu wa kuuliza maswali mazuri:

Kuuliza maswali mazuri kutatusaidia sisi, kwanza kuelewa Biblia inavyosema. Kisha, maswali mazuri hutusaidia kuchimbua kwa undani kutambua moyo wa ujumbe wa Neno la Mungu ili kwamba tuwe waaminifu kwake na kubadilishwa nayo.



## Swali zuri ni lipi?

- Swali zuri huuliza kitu ambacho si wazi kwenye kifungu lakini inatusaidia kuelewa alichokusudia mwandishi.
- Swali zuri ni lile linalotupeleka kwenye uelekeo ambaa mwandishi anatutaka twende.

## Tunawezaje kuuliza swali zuri?

Anza kujiuliza maswali ya msingi ya uchunguzi. Kisha, ingia ndani kwa maswali yanayotusaidia kuelewa kusudi na maana ya mwandishi.

### ➤ **Maswali ya msingi ya Uchunguzi.**

Anza na maswali yanayofungua ufahamu kuhusu kile kinachosemwa na kifungu:

- Kifungu kinasemaje? (Endelea kujiuliza swali la uchunguzi na la msingi sana.)
- Hii ilitokea lini? Wahusika waliohusishwa ni akina nani? Maeneo gani yametajwa?
- Ni maneno gani ya muhimu sana yanayounganisha au yanayohamisha?
- Je kuna ulinganifu wowote au kupingana?
- Kuna maneno yaliyorudiwa au mawazo?

### ➤ **Maswali ya muhimu sana yanayoingia ndani zaidi:**


Nenda zaidi ya maswali ya msingi jiulize maswali yanayosaidia kuelewa kwa nini mwandishi aliandika alichoandika.

- **Mwandishi anasemaje?**
- Mwandishi alisema kwa namna gani?
- Alisema kwa sauti ya namna gani?
- Kwa nini amekisema hapa? Kwa nini ni kwa njia hii?
- Nini kinashangaza kuhusu hiki?
- Kinazungumza au kuelekeza nini kuhusu Yesu?
- Kwa ujumla nini kinasemwa?
- Kwa nini mwandishi amesema hivi? Alitegemea mwitikio gani toka kwa wasomaji wake?
- Ni mwitiko gani Mungu anataka kwetu miyoni mwetu na maisha yetu leo?

## Hali ya moyo wakati unajiuliza maswali:

Hali tatu za moyo ni muhimu wakati tunatafuta kufahamu nini Neno la Mungu linasema katika kutusaidia sisi kukuza ujuzi wa kujiuliza maswali mazuri.

- **Shauku.** Uliza maswali kwa shauku ya mtoto:
- **Ufunuo.** Jifunze kuuliza maswali yanayoenda zaidi ya majibu ya kawaida.
- **Uvumilivu.** Endelea kufanya kazi na kuuliza maswali ili kuelewa.



### Kanuni:


- Ili sisi tuelewe namna ya kutumia Neno la Mungu kwa maisha yetu leo, ni lazima turejee nyuma kuelewa kwenye ujumbe uliowasilishwa na mwandishi katika muktadha ule wa asili.

### Jinsi mafunzo yanayosafiri yanavyotenda kazi?

- (1) **Bila kuchukua mwelekeo wa moja kwa moja.** Mara nyingi tunajaribiwa kutumiwa Neno la Mungu moja kwa moja katika maisha yetu. Lakini kwanza Mungu aliongea kupitia moyo wa mwandishi kwa wasomaji kwa nyakati na mahali tofauti tofauti, Na kwa hiyo badala ya kuchukua mwelekeo wa moja kwa moja kutoka kwenye Neno la Mungu hadi kwenye maisha yetu leo, kwanza tunahitajika kusafiri kutoka kwenye Neno la Mungu lilivyosema kwa wasomaji wa mwanzo, tunahitaji kujua nini alikuwa anasema mwandishi kwa wasomaji wake wa asili, na kwa nini.
- (2) **Kusikiliza kusudi la mwandishi.** Ni lazima turudi nyuma kusikiliza nini Mungu alikuwa anasema kupitia mwandishi katika muktadha wa wakati ule.—muktadha halisi wa ujumbe wa kitabu, muktadha wa kihistoria wa mazingira ya ujumbe, na hata muktadha wa kibiblia wa habari kw aujumla na ujumbe wa Biblia. Na wakati kuna muktadha mbalimbali wa kuangalia, tunataka kujikita kwenye yale ambayo yatatusaidia kuelewa anachosema mwandishi, kwa nini alisema hili kwa watu hawa, na ni mwitikio gani ulistahili kutohana na ujumbe huu.
- (3) **Kutumia ujumbe kwetu leo.** Mwishoni lengo la mafunzo yanayosafiri ni matumizi. Baada ya kugundua mwitikio alioutaka mwandishi kwa ujumbe wake tunasafiri tena hadi kwetu leo na kujiuliza mwitikio ule ungeonekanaje leo kwenye maisha yetu leo, mahali tunaishi na kuhudumu.

### Kwa nini mafunzo yanayosafiri ni ya muhimu?

- Ikiwa tutachukua njia ya mkato na kujaribu kutumia Neno la Mungu kwa maisha yetu, tunakuwa kwenye hatari ya kutafsiri vibaya kile anachosema katika Neno lake, tukikosa njia ambayo Mungu anataka kuona mwitikio wetu, na kuwapotosha watu tunaowahudumia.
- Hata hivyo, ikiwa tutachukua muda kutembea kwa usahihi, tutagundua maajabu ya moyo wa Mungu unaofafanuliwa katika muktadha ule wa asili na nguvu inayobadilisha ya Neno lake kwa maisha yetu leo.



## Muundo ni nini?

- Muundo wa kifungu (au kitabu) inahusisha: (1) sehemu za kifungu – vipengele vya mawazo na fikra zilizo na mawazo makuu ya kifungu na
- (2) muunganiko wa fikra, ambazo zinabeba visehemu au mawazo makuu na fikra kuu za kifungu.

## Kwa nini muundo ni muhimu?

- Kutazama muundo kunatusaidia kuvumbua mawazo makuu ya kifungu na kuona jinsi ambavyo mwandishi amejenga mawazo yake. Kutazama muundo kunasaidia kwenda kwenye mawazo ya mwandishi.
- Muundo ni muhimu kwa ajili ya mahubiri na mafundisho kwa sababu tunataka kuhakikisha kuwa vile tunavyopanga mawazo katika mafundisho yetu inaanishi namna ambavyo mwandishi ameweka mawazo yake katika kifungu cha maandiko. Uelewa wa muundo katika Biblia unaleta ufanuzi wa nguvu katika mahubiri yetu.

## Unapataje muundo wa kifungu?

1. Tazama mpangilio na awamu katika fikra. Unaposoma kifungu, unaona mpangilo wa aina gani unaona unalenga mawazo ambayo mwandishi anataka kuyatoa? Pia wakati unasoma, angalia jinsi mwandishi anavyohama kutoka wazo moja kwenda lingine au anavyobadili mwelekeo. Hii inaweza kuonekeana kwenye mabadiliko ya mpangilio.
 

Kipekee angalia: <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kurudiwa kwa mawazo</li> <li>• Mwendelezo</li> <li>• Kulinganishwa kwa mawazo au kupingana.</li> <li>• Jinsi kifungu kinavyoanza na kinavyoishia</li> <li>• Kuhamia wazo lingine au maeleo kwa muhutasari</li> </ul>	Pia tazama: <ul style="list-style-type: none"> <li>• Maagizo/amri</li> <li>• Kilele cha simulizi na suluhisho</li> <li>• Maswali yaliyoulizwa na kujibowi</li> </ul>
--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------	----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
2. **Gawa kifungu.** Baada ya kuona mpangilio na jinsi mwandishi alivyokuwa akihama toka wazo moja hadi jingine, gawa kifungu katika sehemu zenye mawazo makuu. Andika idadi ya mistari kwa kila sehemu.
3. **Elezea mawazo makuu.** Elezea mawazo makuu kwa kila sehemu katika sentensi moja kamili.
4. **Tafuta jinsi fikra zilivyounganika katika mawazo makuu.** Ni kwa namna gani wazo linaungana na lingine au linavyohamia kwenye wazo lingine? Je mawazo yanaungana vipi ili kutoa mwelekeo wa mawazo ya mwandishi?  
(Kwa kutazama muundo tunaongozwa kwenye ugunduzi wa wazo kuu. Kwa mwangaza wa muundo, jiuilize nini kusudi au wazo kuu la mwandishi?"")

# Tafuta wazo kuu na mwitikio tarajiwa

## Wazo kuu ni nini?

- Wazo kuu ni dokezo kuu au maudhui ya kifungu (au kitabu).

## Kwa nini kutafuta wazo kuu ni muhimu?

Katika Maandiko:

- Inatusaidia sisi kufahamu ujumbe ambao Mungu anakusudia kutupa kupitia kifungu cha maandiko.
- Inatusaidia sisi kuona dokezo la msingi ambalo mawazo mengine yamejenga juu yake.

Katika mahubiri na mafundisho:

- Inatusaidia kubakia waaminifu kwa kile Mungu alichosema katika Neno lake.
- Ni maudhui ambayo kila kitu katika ujumbe kinahusika nacho na kupangiliwa.

## Kutafuta wazo kuu kunahusisha...

- Chunguza vidokezo katika kifungu. Angalia yafuatayo:
  - Muunganiko kati ya mwanzo na mwisho wa kifungu.
  - Kujirudia kwa maneno muhimu au mawazo.
  - Mstari wa muhutasari
  - Hitimisho au maelezo ya kusudi (ni yale yanayoanza na maneno kama (kwa hiyo, au ili kwamba)
- Kutafuta muundo wa kifungu.
  - Zingatia jinsi ambavyo mpangilio wa mawazo yanavyojielekeza kwenye wazo kuu.
- Kujiuliza maswali mawili ya muhutasari kuhusu kifungu.
  1. Nini wazo la jumla ambalo mwandishi anaongelea?
  2. Anasema nini ambacho ni mahususi kuhusu wazo hilo?

## Kutafuta mwitikio tarajiwa

- Kutafuta wazo kuu kunatufanya tujiulize, "Mwandishi amesemaje? Tukiwa tunatafuta mwitikio tarajiwa tutajiuliza, "Kwa nini mwandishi alisema vile?"
- Kirahisi jiulize: Katika nuru ya kifungu hiki, mwandishi alitamani kuona mwitikio gani kwa hadhira yake? Kwa maneno mengine, Ni mabadiliko gani ambayo Mungu anataka kutimiza kwa njia ya Neno katika maisha ya msikiaji?..... Mwitikio tarajiwa ni upi?

## Tunatamkaje wazo kuu?

Wazo kuu linaweza kutamkwa kwa namna mbili tofauti :

- "Maelezo" wazo kuu – kwa maana ya kile kilichoelezwa kwenye kifungu
- "Mafundisho" wazo kuu – kwa maana ya kanuni isiyopitwa na wakati ambayo inaanishi ujumbe mahususi wa kifungu lakini pia ina nguvu ya kubadilisha na mwitikio uliotarajiwa kwa maisha yetu leo.

Maelezo ya Wazo kuu yatakuwa:

- Kamili-siyo kichwa cha somo, bali sentensi kamili (yenye muhusika na tendo)
- Iliyofupishwa-Fupi ya kutosha ili msikiaji aweze kukumbuka
- Mahususi-ikihuhsisha baadhi ya mawazo ya kipekee ya kifungu

## Mstari wa melodi




*Wazo kuu na mwitikio  
tarajiwa wa kifungu  
au kitabu  
linalinganishwa na  
melodi ya wimbo  
ulioandaliwa na  
mtunzi ambao  
tunaimba au  
tunaitikia kwa namna  
alivyokusudia*

# Theolojia ya Biblia

## Theolojia ya Biblia ni nini?

- Theolojia ya Biblia ni namna ya kutazama Biblia ambayo itatusaidia kuona ...
  - (1) picha kubwa ya simulizi iliyofungamana ya Biblia na jinsi  
kila kipengele kidogo (kifungu binafsi au kitabu tunachojifunza)  
kinavyoweza kuingia ndani ya simulizi zima.
  - (2) Jinsi kila sehemu ya simulizi inavyomhusu Kristo, na namna simulizi  
iliyofungamana kuhusu Mungu na Mpango wake ulivyotimia katika Kristo.



### (1) Simulizi iliyofungamana

- Kwanza, theolojia ya Biblia inatusaidia kuona mwunganiko kati ya kila kipengele kidogo (kifungu au kitabu tunachojifunza) na simulizi kwa ujumla.

#### Kamba



Biblia ni kamba. Kamba ina nyuzi nyingi, lakini kuna kamba moja.  
Biblia ina maudhui mengi, theolojia ya Biblia inatusaidia kuunganisha  
maudhui hayo pamoja na kutupa simulizi moja lenye ujumbe mmoja.

# Theolojia ya Biblia


- Theolojia ya Biblia inatusaidia sisi pia tuone mwendelezo wa simulizi na ujumbe wa Biblia mpaka kutimizwa kwa yote ndani ya Kristo na kwa njia yake.

## (2) Kutimizwa ndani ya Kristo

- Theolojia pia inatusaidia tufahamu kwa namna gani kila sehemu ya Biblia – siyo tu Agano Jipya, bali na Agano la Kale lilivyobainisha kutimizwa kwake ndani ya Kristo
- **Agano la Kale linamnyoshea kidole Kristo**
  - Katika Luka 24, Yesu alieleza kwamba “Kila kitu nilichoandikiwa mimi katika sheria ya Musa na manabii na Zaburi lazima yatimie”(24:44). Kwa hiyo tunapohubiri kutoka Agano la Kale, tunaweza kumhubiri Kristo kwa sababu Agano la Kale kwa ujumla linamnyoshea kidole Kristo.

### Njia kuu kwenye ramani

Tunaweza kufikiria Biblia kama ramani, na kwenye ramani hiyo tunaona barabara zote katika Agano la Kale zinalekeea kwa Kristo. Siyo njia zote ni njia kuu. Njia kuu ni vile vifungu ambavyo vinaonyesha kwa wazi mwunganiko wa moja kwa moja na Kristo. Lakini kuna njia za miguu, barabara ndogo, uchochoro, na barabara nyinginezo nyingi ambazo si njia kuu ingawa zinaweza hatimaye kuungana nayo.



Tunaweza tukawa tunajifunza kifungu ambacho kipo kando ya njia kuu. Swali la muhimu kujiliza ni: *Ni kwa jinsi gani kifungu hiki kitanifikisha njia kuu?* Au, Ni kwa jinsi gani kifungu hiki kitanunganishaa na maudhui makuu yanayonielekeza kwa Kristo? Ni kwa namna gani kifungu hiki kinasaidia kuongeza ufahamu wangu kuhusu Kristo na kile alichofanya? Maswali kama haya yatasaidia kuelewa jinsi maandiko yanavyomwonyesha Kristo.

## ➤ Agano Jipya linamweleza Kristo

- Wakati Agano la Kale linaandaa njia na kutuelekeza kwa Kristo, Agano Jipya linamweleza Yeye ni nani.
- Jilize: Je mwandishi wa Agano Jipya anatazama nyuma kwenye ahadi ya Agano la Kale inayomhusu Kristo? Kama ndivyo, mwandishi anaielewa? Mwandishi anatazamaje matokeo ya ujio wa Kristo na huduma yake katika upande huu wa misalaba na kufufuka? Je mwandishi anatuelekeza kwenye ahadi ya kurudi kwa Kristo na ufalme wake ujao? Kama ndivyo, anasema nini juu yake?